BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini – Tarehe 14 Juni, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu!

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

MHE. ZAYTUN S. SWAI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/2022 na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021 pamoja na Mapendekezo ya Serikali Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge; Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti makofi hayo yanakuhusu kwa malezi mazuri ya vijana walio kwenye Kamati yako. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Katibu. *(Makofi)*

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 410

Wawekezaji Waliomilikishwa Ardhi na Kituo cha Uwekezaji – TIC

MHE. COSATO D. CHUMI aliuliza:

Je, mpaka sasa ni wawekezaji wangapi wamemilikishwa ardhi na kupata Hati kupitia Kituo cha Uwekezaji *TIC?*

NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, wawekezaji wa kigeni wanamiliki ardhi kwa ajili ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kwa utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999. Kifungu cha 20 cha Sheria hiyo kinaelekeza kwamba, Kamishna wa Ardhi atatoa hati ya umiliki wa ardhi *(Certificate of Right of Occupancy)* kwa jina la Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kwa ajili ya uwekezaji endapo uwekezaji huo unafanywa na mwekezaji wa kigeni. Kwa kutumia hati hiyo, *TIC* hutoa Hati ya Umiliki Isiyo Asili (*Derivative Right*) kwa mwekezaji wa kigeni aliyewasilisha maombi ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mwekezaji kupewa Hati ya Umiliki Isiyo Asili na *TIC*, hati hiyo inasajiliwa na Msajili wa Hati *(Registrar of Titles)* ambaye anatoa hati ya umiliki wa ardhi hiyo *(Derivative Title)* kwa jina la mwekezaji wa kigeni kulingana na masharti ya uwekezaji husika kama yalivyoainishwa kwenye mkataba wake na *TIC.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia utaratibu huo, tangu mwaka 1999 hadi mwezi Mei, mwaka huu, Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* kimewezesha upatikanaji wa Hati za Umiliki Zisizo Asili (*Derivative Rights*) 401 kwa wawekezaji wa kigeni.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chumi, swali la nyongeza.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza, nitakuwa tu na swali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa za Benki ya Dunia za Easy *Way of Doing Business* moja wapo ya kikwazo kwa wawekezaji ni uchelewaji wa kupatikana hati kwa wakati na utaratibu uliopo ni kwamba ile Kamati ya Kugawa Ardhi ya Kitaifa inakaa mara nne tu kwa mwaka. Je, Serikali ipo tayari kurahisisha walau hiyo Kamati ikakaa hata kila mwezi ili wawekezaji wapate hati kwa wakati? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, majibu.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kwa niaba ya Wizara hiyo, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kanuni zilikuwa zinataka Kamati hii ikutane mara nne kwa mwaka na ndivyo walivyokuwa wanafanya lakini kutokana na ripoti hiyo na *outcry* ya wawekezaji na umuhimu wa kuharakisha uwekezaji, kwa sababu Kamati hii inaundwa na mimi, nimeelekeza sasa Kamati hii ikutane kila mwezi badala ya miezi minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuanzia Awamu hii ya Sita wameshaanza kukutana mara moja kila mwezi na mwezi

uliopita wamekutana kila wiki na ndio maana imewezesha katika maombi 174 yaliyowasilishwa katika Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Samia, tayari maombi 173 yameshapata vibali na yameshaandikiwa hati za uwekezaji na tayari zimeshakabidhiwa kwa *EPZA* na *TIC* kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, tunaendelea na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 411

Upungufu wa Watumishi wa Afya Nchini

MHE. MWANTUMU M. ZODO aliuliza:-

Sekta ya Afya nchini ina upungufu wa Watumishi wapatao 16,000:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na changamoto hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Sekta ya Afya nchini ina upungufu wa watumishi ambapo hadi mwezi Mei 2021 watumishi waliokuwepo ni asilimia 41 ya mahitaji halisi. Upungufu huo unatokana na sababu mbalimbali ikiwemo kustaafu kazi, kufariki na kuongezeka kwa idadi ya Vituo vya kutolea huduma za afya nchini kutokana na utekelezaji wa

Programu ya Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya kutolea huduma za Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2017 hadi 2020 Serikali kwa kushirikiana na wadau imeajiri watumishi 12,868 wa Sekta ya Afya ambao wamepangwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Adha, Serikali inakamilisha taratibu za ajira 2,726 za watumishi wa kada mbalimbali za afya zilizotangazwa Mwezi Mei 2021. Watumishi hao watapangwa kwenye Vituo vya kutolea huduma za afya vyenye uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ili kukabiliana na changamoto hii, mpango wa Serikali ni kuendelea kuajiri watumishi wa kada za afya kwa awamu, nashukuru.

MHE. MWAMTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa moja ya changamoto ambazo zinasababisha kukosekana kwa watumishi kwenye sekta yetu ya afya ni pamoja na vifo, kustaafu na ujenzi wa vituo vya afya pamoja na zahanati. Na kwa kwakuwa bado tunaendelea na ujenzi wa vituo vya afya, je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kasi ya ujenzi wa vituo vya afya inaendana na kasi ya kuajiri watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau mwaka 2017/2020 wameajiri watumishi 12,868 na wadau hao ni kama Benjamin Mkapa, *AMREF* na *MDH*. Je, ni upi mchango wa wadau hao katika ajira kwa sekta hii ya afya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri swali la pili linahitaji takwimu kwa hiyo utamjibu kwa wakati wako, jibu swali la nyongeza la kwanza.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi ni kweli kwamba Serikali kwa kujali na kuthamini afya za wananchi imeendelea kujenga, kukarabati na kutanua vituo vya huduma za afya ili kusogeza huduma bora za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuzingatia hilo, Serikali pia imeweka mkakati wa kuhakikisha kasi ya ujenzi wa vituo vya huduma za afya kote nchini inaendana na kasi ya ajira za watumishi ili kuviwezesha vituo hivyo kuanza kutoa huduma za afya katika vituo vyote vinavyojengwa na kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana katika kipindi cha mwaka 2017 hadi 2020 jumla ya watumishi takribani 12,868, wastani ya watumishi 4,200 kila mwaka wameajiriwa lakini hivi sasa Serikali inaendelea na ajira za watumishi 2,726 ambazo pia zitakwenda kupunguza upungufu wa watumishi katika vituo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba tunaajiri watumishi katika vituo hivyo, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, kabla sijaruhusu maswali ya nyongeza Waheshimiwa Wabunge wenye maswali tuzingatie matakwa ya Kanuni ya 49 inayoeleza jinsi ya kuuliza swali; ukienda kinyume na hii Kanuni leo mtakaa humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa George Mwenisongole swali la nyongeza.

MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Napenda kuuliza swali langu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na upungufu huo wa watumishi wa afya kwenye hivi vituo kwa nini Serikali isitoe vibali maalum kwa hizi zahanati na vituo vya afya kuajiri watumishi wa kujitolea kwa kutumia mapato yao ya ndani, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba pamoja na jitihada za Serikali Kuu kuajiri watumishi katika Sekta ya Afya lakini mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu pia wa kuajiri watumishi hawa kwa mikataba kupitia mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hili naomba nimhakikishie kwamba Serikali ilikwishatoa kibali kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia zahanati, vituo vya afya na hospitali wale ambao mapato yao yanaruhusu kuajiri watumishi kwa mikataba, waajiri na Serikali imeendelea kufanya hivyo; kuna vituo vingi ambavyo vina watumishi wa mkataba wanaolipwa na Halmashauri ili kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, naomba nimhakikishie kwamba suala hilo lipo hivyo na niwaelekeze Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa vile vituo ambavyo vina uwezo wa kuajiri watumishi wenye sifa kwa kufuata taratibu, waajiriwe kuhakikisha kwamba tunaboresha huduma za afya katika vituo vyetu, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 412

Hitaji la Bandari ya Uvuvi na Meli ya Uvuvi - Mtwara

MHE. TUNZA I. MALAPO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Bandari ya Uvuvi na kununua Meli ya uvuvi katika Mkoa wa Mtwara?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo Mbunge wa Mtwara Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 Ibara 43(a) ambazo zimeainisha kujenga Bandari ya Uvuvi katika Ukanda wa Pwani ambayo itawezesha meli zinazovua Bahari Kuu kutia nanga kwa lengo la kushusha samaki na mazao ya uvuvi, kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi na huduma nyinginezo ikiwemo kujaza mafuta, vyakula na matengenezo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza Mpango huo, Serikali iliingia mkataba na mshauri elekezi ili kubaini eneo linalofaa kwa ujenzi wa bandari. Baada ya uchambuzi huo, mshauri elekezi alipendekeza bandari ijengwe katika eneo la Mbegani – Bagamoyo, na kazi hiyo itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na mahitaji na uwepo wa bajeti Serikali itaendelea kutazama uwezekano wa kujenga Bandari za Uvuvi katika maeneo mengine ikiwemo Mkoa wa Mtwara kwa siku za usoni ikiwa ni pamoja na kuboresha mialo, kuimarisha vikundi wa usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi na kuanzisha Vyama Vya Ushirika wa Wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji na ujenzi wa Bandari za Uvuvi utawezesha kukua kwa biashara na shughuli za uvuvi Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi ikiwemo Mkoa wa Mtwara.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa majibu haya Mheshimiwa Waziri ni wazi kwamba suala la ujenzi wa bandari na ununuzi wa meli katika Mkoa wa Mtwara bado. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza; kwa kuwa wavuvi ili waweze kutengeneza vyombo vyao, wanahitaji kununua miti ama mbao kutoka kwa wauza mbao ambao *TFS* wanatoa kibali kwao. Nataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inawapa vibali wavuvi ili waweze kukata ile miti na kutengeneza vyombo kuepusha gharama inayopatikana kwa kwenda kununua kule kwa wauza mbao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa hakuna uelekeo wa sasa hivi wa kuonekana kutajengwa Bandari ya Uvuvi pamoja na ununuzi wa meli katika Mkoa wa Mtwara, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inawawezesha wavuvi wa Mtwara kupata vyombo vya kisasa vile vya *fibbers* nakushukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Ulega, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni upatikanaji wa mbao na kwa kuwa vibali vinatoka *TFS*, Wizara ya Maliasili na Utalii, naomba nichukue rai hii ya Mheshimiwa Mbunge na nataka nimhakikishie yeye na wavuvi wote ya kwamba ndani ya Serikali tutalizungumza jambo hili ili kuweza kuona unafuu wa hao wavuvi ambao wanahitaji mbao 10 hadi 15 waweze kuzipata kwa urahisi kwa ajili ya ku-*repair* au kutengeneza vyombo vipya kwa kuwa ikizingatiwa wao hawaendi kufanya biashara bali wanakwenda kutengeneza

vyombo kwa ajili ya matumizi yao. Kwa hivyo, hili ni jambo jema na nalichukua kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni suala la upatikanaji wa *fibbers.* Tunaanzisha upya Shirika letu la *TAFICO* na moja ya hadidu za rejea za kuhakikisha *TAFICO* mpya iweze kufanya vyema ni kuingia ubia kwa maana ya *PPP* na Sekta Binafasi na moja ya jambo tutakalokwenda kulikazania kwa huyo mtu atakayekuja kwa ajili ya *PPP* ya ubia ni kuhakikisha atuoneshe dalili na matumaini ya pamoja na kuvua lakini upatikanaji wa vyombo kuanzia katika ukanda wetu wote wa bahari hata na visiwani pia vilevile kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa samaki kwa kutumia vyombo vipya vya kisasa na hii ni pamoja na Mkoa wa Mtwara.

Na. 413

Uvunaji wa Mikoko katika maeneo ya Delta

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakamilisha mpango wa uvunaji wa mikoko kwa wananchi wanaoishi maeneo ya Delta wanaotegemea zao hilo kuendesha shughuli zao za kimaisha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mpembenwe unayo Kanuni ya 49 hapo? Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba ama napenda kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, misitu ya mikoko ina umuhimu mkubwa katika nyanja za kiuchumi na kimazingira, kutokana na kuvamiwa kwa misitu hii kwa kufanya shughuli zisizokubalika kiuhifadhi kama vile kilimo, ufugaji utayarishaji wa chumvi, Serikali ilisimamisha uvunaji wa mikoko yote kote nchini ili kutoa fursa ya kuweka mipango na mikakati ya matumizi endelevu. Hivyo, Wizara inaandaa mpango na mwongozo wa usimamizi wa matumizi endelevu ya misitu ya mikoko utakaotoa utaratibu wa uvunaji. Mipango na miongozo hiyo ipo katika hatua za mwisho za maandalizi na inatarajiwa kukamilika robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022 na baada ya kukamilika utaanza kutumika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Twaha Mpembenwe swali la nyongeza.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Serikali, mimi sina swali la nyongeza isipokuwa nilikuwa ninaomba ikimpendeza Mheshimiwa Naibu Waziri tutakapokuwa tumemaliza *session* hii ya bajeti basi twende kule Kibiti tukazungumze na wananchi ili aweze kwenda kujionea mwenyewe hali halisi ya wananchi wale inayowakabili. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Twaha Mpembenwe bila shaka unataka kuambatana na Waziri wa Maliasili na Utalii na siyo Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 414

Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Ziwa Madunga

MHE. DANIEL B. SILLO aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza upembuzi yakinifu na ujenzi wa miundombinu ya maji katika Ziwa Madunga ili kutatua

tatizo sugu la maji katika Kata ambazo hazina maji Jimbo la Babati Vijijini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Ulega kwa niaba ya Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa Babati Vijijini ni asilimia 74. Kwa lengo la kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Serikali inaendelea na utafiti wa ubora na uwingi wa maji katika chanzo cha Ziwa Madunga. Utafiti huo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2021 na usanifu wa miundombinu ya maji utakamilika katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sillo Daniel Baran swali la nyongeza.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina swali la nyongeza ila ninaipongeza sana Serikali kwa majibu yake yanayotia moyo naomba tu wajielekeze katika utekelezaji, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 415

Mradi wa Maji wa Mji mdogo wa Chala

MHE. VINCENT P. MBOGO aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi wa maji wa Mji Mdogo wa Chala ambayo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za mwaka 2020?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Abdallah Ulega kwa niaba ya Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI K.n.y. WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Paul Mbogo Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji mdogo wa Chala unapata maji kutoka Mto Kauzike na Bwawa la Ntanganyika na hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika Mji huo ni asilimia 56. Aidha, katika kuhakikisha huduma ya maji katika mji wa Chala inaboreshwa mwaka 2020/2021 ulitekelezwa mradi wa maji ambao umehusisha kuchimba kisima kirefu chenye uwezo wa kuzalisha lita 153,600 kwa siku na kiasi hiki kimeongeza upatikanaji wa maji zaidi ya lita 300,000 kwa siku. Hivyo kazi itakayofanyika kuanzia mwezi Julai, 2021 ni ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji, ujenzi wa nyumba ya mtambo wa maji, ufungaji wa pampu na ulazaji wa bomba mita 500 kwenda kwenye tanki lililopo la lita 150,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji wakati wote, hivyo mpango wa muda mrefu katika mji wa Chala ni kutumia mabwawa madogo na ya ukubwa wa kati ambapo kwa sasa utafiti wa kubainisha maeneo yanayofaa kwa ajili

ya ujenzi wa mabwawa mawili (2) katika Mji Mdogo wa Chala unaendelea na unatarajiwa kukamilika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vincent Mbogo swali la nyongeza.

MHE. VINCENT P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkasi ina kadiriwa na changamoto kubwa sana ya maji, ni lini Seikali itatoa maji Ziwa Tanganyika ambacho ndiko chanzo kikuu cha uhakika kuweza kutatua changamoto Wilayani Nkasi?

Swali la pili; Wilaya ya Nkasi katika Tarafa ya Nkate upo mradi wa maji ambao umekaa muda mrefu sana Tarafa ya Nkate ambao unahudumia vijiji vya Ntuchi, Ntemba, Siriofu na Ifundwa, mradi huu Mkandarasi hajalipwa ili aweze kumaliza mradi huu na ipo kesi ambayo anatuhumiwa mahakamani, naomba Wizara hii iweze kushughulikia kesi ya Mheshimiwa Felix Mkandarasi atoke ili aweze kumalizia mradi huu umekaa muda mrefu wananchi wanahangaika na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbogo Mbunge wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lini Serikali itatumia maji ya Ziwa Tanganyika kwa ajili ya kulisha katika Mji wa Nkasi wote. Serikali ya Awamu ya Sita katika vipaumbele vyake cha kwanza ni kuhakikisha kumtua ndoo kichwani mwanamama, kwa hivyo nataka nimhakikishie kazi kubwa imefanyika katika

maji eneo la Ziwa Victoria kuyatoa na kuyapeleka Mikoa mbalimbali ikiwemo Tabora na kwingineko, kwa sasa kwenye bajeti hii ya 2021/2022 Serikali inaendelea kutafuta fursa ya kuona namna ya kuweza kusaidia na kwa hivyo hili la Ziwa Victoria naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge linaweza kuwa ni moja ya sababu ya kuweza kulifanyia kazi ili kuondosha hii adha inayowapata wananchi wa Nkasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili juu ya mradi uliokwama wa Kata ya Nkate jambo hili naomba nilichukue na mara baada ya kikao hiki kuisha tuje tulizungumze tulielewe tatizo lake ni nini na baadaye tuweze kulitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba sasa aulize swali lake.

Na. 416

Ujenzi wa Barabara ya Mnivata – Newala - Masasi

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza: -

Je, ni lini ujenzi wa barabara kutoka Mnivata hadi Masasi kupitia Newala kwa kiwango cha lami utaanza?

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nimewakumbusha Kanuni ya 49, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara Mnivata, Newala, Masasi yenye urefu wa kilometa 160 ni sehemu ya barabara ya Mtwara, Nanyamba, Tandahimba, Newala hadi Masasi yenye urefu wa kilometa 210.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mtwara, Nanyamba, Tandahimba, Newala hadi Masasi yenye urefu wa kilometa 210 umekamilika. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo awamu ya kwanza ya sehemu ya Mtwara hadi Mnivata yenye urefu wa kilometa 50 imekamilika.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga shilingi milioni 3,000 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Mnivata, Newala, Masasi yenye urefu wa kilometa 160.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia kwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* inaendelea kuifanyika matengenezo mbalimbali barabara hii ili kuhakikisha kuwa inapitika majira yote ya mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya Shilingi Milioni 1,017.33 zimetengwa. Ahsante

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa, barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya usafirishaji wa zao la korosho na kwa kuwa bajeti ya mwaka jana zilitengwa kiasi cha fedha na mwaka huu imetengwa bilioni tatu, naomba sasa nijue Je, ni lini Serikali itatangaza barabara hii ili apatikane Mkandarasi wa kuanza kipande kilichobaki cha kilometa 110.

Pili, kwakuwa kilometa 50 ambazo zimeshajengwa kwa awamu ya kwanza bado kuna kazi chache zimebaki

Serikali inatuhakikishia mpaka lini kipande hiki kitakuwa kimekamilika kwa asilimia 100? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Injinia Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imetengewa fedha ambayo mara tu fedha itakapoanza kutumika za bajeti ambayo imepitishwa na Bunge lako barabara hii itatangazwa ili ianze kuendelea kipande cha Mnivata Tandahimba kwenda Newala, ameuliza barabara ambayo imejengwa ya Mtwara hadi Mnivata yenye kilometa 50 ni kweli haijakamilika kabisa lakini tumetenga shilingi bilioni Tatu kwa ajili ya kukamilisha barabara hiyo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Esther Midimu swali la nyongeza.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa barabara ya Mwigumbi Maswa imejengwa chini ya kiwango na imeanza kubomoka bomoka. Je, ni lini Serikali itarudia ujenzi huo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Injinia Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kawaida barabara zikishajengwa baada ya muda hasa muda wake unapokuwa umekwisha zinachakaa na hivyo kufanyiwa mategenezo kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo itaingizwa kwenye mpango wa ujenzi mara tu fedha itakapopatikana hasa katika awamu tunazoziendea, kwa sababu ni taratibu kwamba tunafanya tathmini kuangalia gharama halafu barabara hiyo itafanyiwa *rehabilitation* kubwa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri barabara kuchakaa nadhani ni tofauti na kujengwa chini ya kiwango cha lami, ni kama hii barabara ya kutoka hapa kuelekea Iringa inavyotoboka kila siku ni tofauti na barabara ambayo imekaa muda mrefu, kwa hiyo inahitaji kujengwa upya zinazojengwa chini ya kiwango wataalam mtusaidie kwa sababu fedha za Serikali zinapotea. Mheshimiwa Ally Mchungahela swali la nyongeza.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara ya Tandahimba ni barabara ya muda mrefu sana imeahidiwa kwa muda mrefu sana tangu wakati wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Serikali itakuwa imeamua lini kufanya kwa vitendo kutimiza ahadi zake kwa sababu barabara hii ni ya muda mrefu sana? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Injinia Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mchungahela Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii imeahidiwa muda mrefu lakini Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba barabara hii tayari Serikali imeshaanza kutekeleza kwa vitendo ambapo kilometa 50 zimeshajengwa na katika bajeti tunayoenda, bado tunaendelea tumetenga Billioni tatu kwa ajili ya kuanza

barabara hii ya Mnivata kwenda Tandahimba. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara bajeti itakapoanza kutekelezwa barabara hii itatangazwa na itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya kujenga barabara katika Mji Mdogo wa Karatu kwa kiwango cha lami toka Serikali ya Awamu ya Nne na Awamu ya Tano.

Je, ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa kujenga kilometa 10 za lami katika mji dogo wa Karatu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Injinia Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za Mjini Karatu zitajengwa kulingana na upatikanaji wa fedha kadri Serikali itakavyopata fedha. Kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu ya Ujenzi na Uchukuzi ikisaidiana na Wizara ya TAMISEMI tutahakikisha kwamba barabara hizi ambazo ni ahadi za viongozi na zipo kwenye Ilani zinajengwa kwa kiwango cha lami kama zilivyoahidiwa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fredy Mwakibete swali la nyongeza.

MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niulize swali moja la nyongeza.

Barabara ya kutoka Katumba - Suma – Mwakareli - Luwanga - Mbambo mpaka Tukuyu yenye urefu wa Kilometa 82, imeanza kujengwa kipande cha kutoka Luhangwa – Mbambo – Tukuyu.

Je, ni lini kipande cha kutoka Luhangwa - Mwakareli - Suma - Katumba kitajengwa? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakibete kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni mwendelezo wa ujenzi ambao unaendelea, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti hii kuna fedha ambayo imetengwa ambapo barabara hii ya Katumba hadi Luhangwa itaendelea kujengwa, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Busokelo pamoja na wananchi wa Busokelo kwamba barabara hii itaendelea kujengwa kadri fedha itakapokuwa inapatikana na tayari imeshaanza kwa hiyo Serikali itaendelea kuijenga barabara hii. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oliver Semuguruka swali la nyongeza.

MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Barabara ya Bugene, Karagwe kupitia pori la Kimisi hadi Ngara Mheshimiwa Hayati Magufuli akiwa Karagwe mwaka huu mwezi wa Januari alitangaza ianzwe kuwekwa lami naomba kujua utekelezaji wake umefikia wapi? Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo ni kweli barabara hii iliahidiwa na ilikuwa ni agizo la Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli barabara hii imetengewa fedha katika bajeti iliyopitishwa kwa hiyo itakuwa ni kati ya barabara ambazo zitaanza kutekelezwa kujengwa kwa kiwango cha lami mara bajeti itakavyoanza kutumika ahsante. *(Makofi*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Jafar Wambura Chege Mbunge wa Rorya.

Na. 417

Ujenzi wa Bandari ya Sota

MHE. JAFARI W. CHEGE aliuliza:-

Je, ni lini Bandari ya Sota eneo la Shirati itaanza kurekebishwa ili kuinua uchumi, lakini pia kuboresha shughuli za kibiashara eneo la mpakani mwa Tanzania na Kenya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Sota ni miongoni mwa Bandari za kati na ndogo 693 zilizoainishwa na Serikali

kupitia Mamlaka ya Bandari (TPA) ili kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa lengo la kuzirasimisha. Aidha, mpango huo wa urasimishaji unakwenda sambamba na zoezi la kuhuisha Mpango Mkuu wa TPA wa kuendeleza Bandari zote nchini unaojumuisha Bandari ya Sota.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa mpango huo unafanyiwa mapitio na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, mwaka huu 2021. Baada ya mpango huo kukamilika, orodha ya bandari kwa ajili ya uendelezaji ikiwemo Bandari ya Sota eneo la Shirati itatolewa kwenye tangazo la Serikali ili zihuishwe, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jafari Chege swali la nyongeza

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ambayo yana matumaini. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nje ya shughuli za kiuchumi na kibiashara ambazo wananchi wa Jimbo la Rorya watafaidika kutokana na urekebishwaji wa bandari hii, lakini pia ni pamoja na shughuli za kiusalama, hasa ukizingatia bandari hii iko mpakani kati ya nchi mbili.

Nilitaka nijue tu, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini sasa bandari hii itaweza kutengewa fedha ili ianze kurekebishwa kama vile ambavyo swali la msingi limekuwa hasa ukizingatia bado hatujafanya hata ule upembuzi yakinifu kujua gharama za ujenzi wa bandari hii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Msongwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda

kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jafari Chege Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jibu langu la msingi nilisema kuwa Bandari ya Sota ni kati ya bandari ambazo bado hazijawa rasmi lakini zimetambuliwa na Serikali ili ziweze kurasimishwa. Kwa hiyo isingekuwa rahisi kutenga fedha kupeleka kwenye bandari ambayo bado haijarasimishwa; na ndiyo maana tumesema kwaajili urasimishaji tathmini inafanyika ili hadi mwezi Agosti mwaka huu bandari hizo baada ya kuainishwa na kuona zina sifa zitarasimishwa na baada ya hapo fedha itatengwa kwa ajili ya kuzijenga ili ziweze kuwa rasmi ahsante.

NAIBU SPIKA: Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, swali ni la Mheshimiwa Dkt Thea Medard Ntara Mbunge wa Viti Maalum.

MHE. DKT THEA M. NTARE: Mheshimiwa Naibu Spika, niombe swali langu namba 418 lijibiwe kwa niaba ya vyuo vikuu vyote.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Thea Ntara pia wewe usome Kanuni ya 49, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga majibu.

Na. 418

Kusomesha Waahadhiri Wengi Zaidi Katika Shahada ya Uzamivu (Ph.D)

MHE. DKT. THEA M. NTARA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusomesha Wahadhiri wengi zaidi katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (Ph.D) kwani waliopo sasa ni wachache?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mpango mkakati wa kuongeza rasilimaliwatu katika taasisi za elimu ya juu ikijumuisha wahadhiri, wakutubi na wataalamu wa maabara na karakana ili kukidhi mahitaji ya viwango na ubora wa Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwezi Julai, 2021 Serikali kupitia mradi wa *Higher Education for Economic Transformation (HEET)* ina mpango wa kusomesha jumla ya wahadhiri 430 katika kipindi cha miaka mitano (2021-2026) ili kukabiliana na upungufu huu katika fani za kipaumbele (*Priority Programs*) katika vyuo vikuu vya Serikali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na mpango huo mahsusi, vyuo vikuu navyo vinaendelea kusomesha wahadhiri wao kupitia vyanzo vingine, ikiwemo mikataba ya kitaalam ya utafiti (*collaborative research projects*) na *scholarship* mbalimbali tunazopokea kutoka nchi rafiki ambapo wahadhiri hupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mipango hiyo, Jumla ya wahadhiri 621 katika ngazi ya shahada ya Uzamivu *(PhD)* na 241 katika Shahada ya Umahiri wanaendelea na masomo. Aidha kwa mwaka wa masomo 2021/2022 jumla ya wahadhiri 48 wanaendelea na masomo katika nchi mbalimbali. Kwa mfano katika nchi ya China wapo wanafunzi au wahadhiri 30, Uingereza 12 na Hangaria wahadhiri sita. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ntara swali la nyongeza

MHE. DKT THEA M. NTARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa mara ya kwanza mimi naona amelitendea haki sana swali hilo, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; ili kuendelea kupunguza uhaba wa wahadhiri;

Je, Serikali haiwezi kurudisha utaratibu wa kuwafanya wahadhiri hao wafundishe hata baada ya miaka 65 kama nchi nyingine za Marekani na Ujerumani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, majibu kwa swali hilo.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ntara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wahadhiri wetu kufundisha zaidi ya miaka 65 ni suala la kiutumishi kwenye kanuni zetu za kiutumishi. Nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalichukua suala hili, tutakwenda kukaa na wenzetu wa Wizara ya Utumishi ili tuweze kuangalia namna gani ya kurekebisha sheria zetu zile ili ziendane sasa na mahitaji haya muhimu ya soko letu la wahadhiri nchini. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kabisa hayo. Kama ulivyosema, mkalitazame, kwasababu mtu anayekuwa amefikia miaka 65 ndipo anabobea kwenye eneo lake. Sasa ukimuondoa huyo ukasema unatengeneza ajira mpya hakuna uhalisia, kwasababu unayemuajiri hawezi kuwa kama huyo mwenye miaka 65. Kwa hiyo kuna maprofesa wengine hawana kazi ya kufanya lakini wamestaafu na vichwa vyao viko sawasawa wanaweza kuendelea kufanyakazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo hilo mlitazame kwa ujumla wake kwa sababu miaka yote hiyo anakuwa anafanya machapicho kwa hiyo akifika umri huo, na nadhani *Professor* hapa atakubaliana na mimi, ndipo anakuwa amebobea hasa kwenye eneo lake.

Waheshimiwa Wabunge Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Martha Festo Mariki Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 419

Upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa

MHE. MARTHA F. MARIKI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha zoezi la utoaji wa Vitambulisho vya Taifa kwa wananchi kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya upatikanaji wa vitambulisho hivyo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Festo Mariki Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa inaendelea kutekeleza mpango kazi wa kuzalisha vitambulisho, na inatarajiwa ifikapo Agosti, 2021 wananchi wote waliotambuliwa na kupewa namba za usajili watakuwa wamepatiwa vitambulisho. Aidha, mpango huu unalenga kuzalisha vitambulisho kwa awamu kwa kila wilaya, ambapo kwa kipindi cha kuanzia tarehe 14 Januari 2021 hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2021 Mamlaka imefanikiwa kuzalisha na kusambaza vitambulisho 7,148,971 katika wilaya 73 nchini. Tanzania bara wilaya 63 na Zanzibar wilaya 10, na kazi ya uzalishaji inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Mei, 2021 Mamlaka imefanikiwa kugawa namba za utambulisho kwa wananchi 11,737,021 Kutokana na mfumo wa *NIDA* kuunganishwa na mifumo mingine ya taasisi za Serikali na binafsi. Aidha, wananchi wanaendelea kupata huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi kama vile huduma za

kifedha, kufungua biashara, kupata namba ya mlipa kodi *(TIN),* kupata hati za kusafiria, umilikishaji ardhi na kusajili laini za simu kwa kutumia namba za utambulisho wakati wakisubiri kupatiwa vitambulisho vyao vya taifa. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Martha Mariki swali la nyongeza.

MHE. MARTHA F. MARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa vigezo vinavyowakwamisha vijana wetu wa Kitanzania hususan waliopo katika mikoa inayopakana na nchi jirani ikiwemo Mikoa ya Katavi, Kigoma na mingineyo ni pamoja na ucheleweshwaji na upatikanaji wa namba za *NIDA*.

Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kutokutumia kigezo hiki wakati vijana wanapokuwa wanatumia ajira ili kuwawezesha vijana wetu waweze kupata ajira kwa kuwa mchakato huo bado haujakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali langu la pili; ni kwanini sasa mfumo wa *NIDA* usiunganishwe na mfumo wa *RITA* wa vyeti vya kuzaliwa ili kuwawezesha Watanzania pale tu mtoto anapozaliwa aweze kupata cheti kimoja kinachounganisha kuonyesha kwamba huyu ni raia kwa kuzaliwa? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Hamis Hamis majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nichukue fursa hii nimpongeze sana Mheshimiwa kwa kuwa umefika

wakati ameona umuhimu wa wananchi hasa wa mkoa wake kufanyiwa haraka katika kupata vitambulisho huku akiwa anajua kwamba vitambulisho kwa sasa *NIDA* ndiyo kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba sasa nianze kujibu swali la kwanza, kwamba, je, Serikali sasa haioni haja ya kuondosha hiki kigezo cha *NIDA* ili sasa mambo mengine yaweze kuenda yakiwemo ya vijana kuweza kupata ajira?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba tumeamua kuweka kigezo hiki ili kuweza kuwajua ni nani wenye sifa na nani wasiokuwa na sifa; na tumeamua kukiweka kigezo hiki ili kuona kwamba nani ambao wana Utanzania na nani ambao hawana Utanzania. Sasa kwa kusema moja kwa moja kigezo hiki kukitoa basi ni jambo ambalo linahitaji *procedure,* twende tukakae na watu wa utumishi na taasisi nyingine. Nimwambie tu Mheshimiwa kwamba jambo hili tunalichukua na tutakwenda kuona namna ya kulifikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kikubwa kingine ninachotaka niseme ni kwamba, na hapa nataka nitoe agizo lakini pia nitoe wito kwa mamlaka hii inayosimamia; kwamba kwa sasa tuone namna ya kuwapa zaidi kipaumbele vijana ambao wanakwenda kutafuta ajira ili waweze kupatiwa hivi vitambulisho kwasababu tumeona na tumegundua kwamba kweli hii imekuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na yote hayo nichukue fursa hii niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba bado kuna wilaya vitambulisho vipo wenyewe hawajaenda kuvichukua, sasa matokeo yake tunaendelea kupata lawama. Tunataka tutoe wito tuwaambie Waheshimiwa Wabunge kwa kushirikiana na viongozi wengine huko wa Chama na Serikali muwaambie watu waende wakachukue vitambulisho vyao. Yapo maeneo vitambulisho vipo lakini hawajaenda kuvichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba, kwanini sasa tusiunganishe *RITA* na *NIDA*. Lengo na azma ya Serikali siku

zote ni kuhakikisha kwamba wanatengeneza muunganiko wa mfumo ili wananchi waweze kupata huduma kwa urahisi zaidi. Sasa kuunganisha *RITA* na *NIDA* si tatizo, Serikali ipo tayari kuunganisha mifumo lakini kuziunganisha taasisi nadhani ni jambo ambalo tunahitaji tukae sasa tufikirie tuone namna bora ya kuziunganisha hizi. Ni kweli zote ni taasisi za Serikali lakini zinao utofauti katika muundo na katika majukumu yake. Kwa hiyo nalo hili pia tutalichukua tuone namna ambavyo tunaweza tukaenda tukasaidia wananchi. Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kutoka upande wa Serikali.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lemburis nimesimama Wabunge huwa inabidi wote wawe wamenyamaza wananisikiliza ninachotaka kusema. Kwahiyo nitakapokaa ndiyo utapata fursa ya kusema hivyo.

Wageni waliopo jukwaa la Spika; kwanza ni wageni 52 wa kwangu ambao ni Madiwani kutoka Jijini Mbeya, na hawa wameongozwa na Meya wa Jiji Mheshimiwa Dourmohamed Rahmat, wameongozana pia na Naibu Meya Mheshimiwa Agnes Mangasila. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani kutoka Jiji la Mbeya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hawa wote wanatoka Chama cha Mapinduzi, mnaweza kukaa sasa. Wameongozana pia na wataalamu, kwa maana ya watumishi wanne; wanaweza kusimama kwa pamoja; karibuni sana. Kwa hiyo tukiwaambia jamani kata ziko nyingi Mbeya Mjini muwe mnatuelewa, mmewaona madiwani hapo walivyo wengi wanatoka kata 36 hao. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa George Simbachawene ambaye ni Waziri

wa Mambo ya Ndani ya Nchi wakiongozwa na ndugu Maria Mazengo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia Wageni 50 wa Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor ambaye ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni wanachuo na watumishi wa Chuo cha Diplomasia wakiongozwa na Mkurugenzi wa Chuo hicho Balozi Dkt. Abdulrahman Kaniki; karibuni sana. Dkt. Abdulrahman Kaniki sijui amekaa sehemu gani? Ahaa yuko upande ule. Ahsante sana Mheshimiwa Balozi karibu sana. Huyu nakumbuka kama alikuwa mwanafunzi wangu hivi! au mimi ndiyo nilikuwa mwanafunzi wake!? karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 32 wa Mheshimiwa David Kihenzile ambao ni viongozi wa CCM na Serikali ya wanafunzi Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino cha Jijini Mwanza wakiongozwa na Wema Somba, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa David Kihenzile.

Tunao wageni 23 wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Chalinze wakiongozwa na Diwani wa kata ya Vigwaza Mheshimiwa Mussa Gama, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani kutoka Chalinze, karibuni sana. Sijui wamemuona Mheshimiwa Ridhiwani au hawajamuona! yuko humu ndani jamani Mbunge wenu. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Ghati Chomete ambao ni madiwani wa viti maalum kutoka Manispaa ya Musoma Mkoani Mara wakiongozwa na katibu wao Mheshimiwa Naima Minga, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani. Leo naona tuna madiwani wengi sana humu ndani. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni wanafunzi wa kozi ya lugha ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, na hawa ni ndugu Roselinda Mrase na ndugu Rosseta Maganga. Siwaoni pengine hawakupata fursa ya kuingia asubuhi hii. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kagera ambao ni Masheikh wa Mkoa wa Kagera wakiongozwa na Sheikh Mkuu wa mkoa huo Sheikh Haruna Kichwabuta, karibuni sana viongozi wetu wa dini, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu ambao ni wapiga kura wake wanaosoma Chuo cha St. John's na Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Ikungi Mkoani Singida wakiongozwa na ndugu Nashon Sylivester, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 29 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambao ni viongozi wa Serikali ya wanafunzi wa Chuo cha Afya cha *DECOHAS* Kampasi ya Dodoma wakiongozwa na kiongozi wao ndugu Elia Mtani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 15 wa Mheshimiwa Simoni Songe ambao ni wapiga kura wake kutoka Busega Mkoa wa Simiyu wakiongozwa na ndugu Kulwa Stephano, Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 60 wa Mheshimiwa Mrisho Gambo ambao ni Wanafunzi Walimu, Wafanyakazi na Wajumbe wa bodi ya Shule ya St. Jude kutoka Jijini Arusha wakiongozwa na Mwanzilishi wa shule hiyo Ndugu Gemma Sisia, shule hii inafadhili masomo kwa wanafunzi wapata 2,000 katika elimu ya msingi, sekondari, na vyuo vikuu ndani na nje ya nchi. Karibuni sana wageni kutoka St. Jude. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Neema Lugangila ambao ni ndugu Mansoor Amri, Judith John na kaka yake Ndugu Bushira Jumanne, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ester Bulaya ambao ni mdogo wake Ndugu Godfrey Mkangala na mtoto wake Ndugu Brighton Gustavous Babile, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, huyu mtoto wa Mheshimiwa Ester Bulaya, Brighton kuna kipindi alisema anataka kusoma sheria, sijui bado ana lengo hilo ama amebadilisha. Alikuwa anataka kuwa kama Tulia hivi, sasa sijui kama amebadilisha. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambaye ni rafiki yake kutoka Jimbo la Sikonge na huyu ni Mwalimu Castory Mhangwa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 15 wa Mheshimiwa Deo Sanga ambao ni Waandishi wa Habari na wadau wa Habari kutoka Mkoa wa Njombe wakiongozwa na Ndugu Pili Nyenje. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo nao ni wageni 34 ambao ni Wanachama wa Chama cha Mapinduzi kutoka Chuo Kikuu cha Jordan cha Morogoro Mjini, ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Hawa wameongozwa na ndugu Mwita Nyamuhanga. Karibuni sana wageni wetu kutoka Morogoro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao leo, lakini bado matangazo yanaendelea. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa na Katibu wa Bunge kwamba bendera za Wabunge zimekwishafika. Kwa hiyo, kila Mbunge atagawiwa bendera hizo kuanzia saa saba mchana, eneo la mapokezi, Jengo la Utawala. Kila Mbunge bendera yake iko pale wataanza kugawa saa saba, mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo lingine la michezo. Kwanza wako Wabunge wanatembea, wengine wanaongea na mimi nimesimama sijui wana hamu ya kutajwa hivi majina kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo linalohusu michezo linatoka kwa Mheshimiwa Abbas Tariba ambaye ni Mwenyekiti wa *Bunge* la *Sport Club*. Mnatangaziwa matokeo

ya michezo mbalimbali ya *bonanza* ambalo lilidhaminiwa na Benki ya *CRDB*, iliyochezwa Jumamosi tarehe 12 Juni, 2021. Kwa upande wa mpira wa miguu Bunge lilipoteza ushindi kwa tabu sana kwa kufungwa goli moja kwa *penalty. (Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa walitoshana nguvu, lakini kwa sababu mshindi lazima apatikane ndiyo maana wakapiga *penalty* halafu mambo yakawa hayako upande wa Bunge. Kwa hiyo, tuwapongeze jamani walijitahidi. *(Makofi)*

Kwa upande wa mpira wa *netball*, Bunge *Queens* walishika nafasi ya pili. Msisikitike Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu huu mchezo tulikuwa tulikuwa tunacheza na watu ambao wanacheza ligi kuu ya *netball.* Kwa hiyo, kimsingi Bunge ndiyo tulishinda na siyo watu wa TAMISEMI kwa sababu wale wanacheza *netball* kila siku, sasa sisi siku nyingine tuko humu ndani kama sasa hivi tunaendelea na kazi nyingine. Kwa hiyo wapongezeni *netball* walifanya vizuri. *(Makofi)*

Hapa nakumbushwa kwamba na mimi mnipongeze maana nilikaba magoli tukaingia *finally*. *(Makofi)*

Haya *basketball* Bunge walishinda nafasi ya kwanza, kwa hiyo walileta kombe. Pia kuvuta Kamba wanawake walishinda nafasi ya kwanza, wanaume kuvuta kamba walishinda nafasi ya kwanza, Wabunge pia. Mchezo wa kufukuza kuku, Bunge walishinda. Hapa Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, ndiyo aliyekamata kuku. *(Makofi)*

Ahsante sana, kwa hiyo yule kuku kwa sababu ni mmoja tukawa tumeomba wawakilishi ndiyo wakanywe supu na kuku akanywewa supu msije mkaanza kumfuata Mheshimiwa Saada kwenda kuomba vipande vya kuku. Kwa matokeo hayo tuliyoyasema kwa ujumla wake *Bunge Sport Club* walishinda kombe la Ujumla la *Bonanza*, kwa hiyo Bunge liliibuka washindi.

Nichukue fursa hii kuwapongeza sana Wabunge wote walioshiriki michezo hiyo, lakini niwaombe Wabunge wengine mwendelee kujitokeza kufanya mazoezi ili tuendelee kushinda vizuri. Mnaweza kuona ushindi huu jamani ulichangiwa na uwepo wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye michezo ile na Waziri Mkuu alianza na mbio hapa nje ya Bunge mpaka alipofika Jamhuri, wengine waliishia njiani huku, lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika mpaka Jamhuri akikimbia. Kwa hiyo, nimpongeze sana anaonyesha mfano mzuri kwa vitendo na mpaka amefika pale akawa anauliza jamani tunaishia hapa au bado kidogo, kwa hiyo yuko vizuri. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kushiriki pamoja na sisi. *(Makofi)*

Nimeletewa tangazo hapa kwamba, kuna wageni wa Mheshimiwa Oran Njeza ambao hawakutangazwa na hawa ni watoto na ndugu zake ambao wako humu Bungeni. Wageni wa Mheshimiwa Oran Njeza pengine hawakupata nafasi ya kuingia, wataingia baada ya hawa wageni wengine kutoka nje na tutawatangaza wakati huo.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Noah Lemburis.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 54, naomba kutoa hoja kuhusiana na masuala ya usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui utaniruhusu nisome kanuni au niendelee moja kwa moja kwenye hoja.

NAIBU SPIKA: Endelea nilishaisoma hiyo kanuni.

MHE. NOAH L. S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kuanzia nadhani mwaka huu kumekuwepo ya hali ya wasiwasi ya majambazi kuvamia maeneo mbalimbali katika nchi yetu na kusababisha hofu na taharuki kubwa sana katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na tukio la hivi karibu la tarehe 7 Juni, 2021, majambazi waliteka basi Kaprikoni na T146 BHD katika eneo la Kambi ya Nduta Kigoma na kupora wananchi vitu vyao mbalimbali. Haikutosha, tarehe 25 Mei, majambazi pia walivamia eneo la Mbezi na kumpiga mtu risasi na kupora pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo halikutosha, tarehe 26 Mei, walivamia tena eneo la Mabibo na kumpiga mfanyabiashara risasi, lakini hawakufanikiwa kupora. Tarehe 7 Mei, Mabwepande walivamia Kituo cha Mafuta Makeson wakampora mfanyabiashara shilingi milioni mbili wakaiba na *shortgun* yenye risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Mei, walivamia baa ya Himbizo Mikocheni wakamkamata mlinzi na kuiba vitu mbalimbali na *Television,* vingamuzi na kadhalika. Tarehe 23 Mei, 2021, majambazi pia walivamia duka la Daudi wakaiba vitu mbalimbali ikiwemo laptop na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hiyo, Serikali inasema nini kuhusiana na matukio haya ambayo yanakwenda mfululizo bila kukoma na hatimaye kuleta wasiwasi na taharuki kwa wananchi wetu Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Umetoa hoja, kwanza hoja haijaungwa mkono, lakini umeitoa sehemu siyo.

MBUNGE FULANI: Aah!

NAIBU SPIKA: Kuna Mbunge anasema aah wakati hata yeye hakusimama wakati unasema natoa hoja. Kwa

hiyo, hakuna Mbunge aliyekuunga mkono, lakini hata hivyo Waheshimiwa Wabunge jambo hili alilolizungumzia Mheshimiwa Noah Lemburis. Kasema amesimama kwa kanuni 54 inayozungumzia kuhairisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura, kwa hivyo amezitaja tarehe hapo na matukio yaliyotokea ni dhahiri kwamba matukio yako mengi. Kanuni yetu ya 55 inaweka masharti kuhusu jambo linaloweza kukidhi matakwa ya kuwa jambo la dharura.

Kanuni ya 55(4) inasema jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi ya kwa umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake. Waheshimiwa Wabunge hili jambo lihesabike kwamba ni jambo la dharura kwanza; liwe la dharura kwa maana ya kwamba limetokea hivi karibuni, lakini pia liwe na maslahi mapana ya Taifa kwa ujumla, maslahi ya umma. Kwa muktadha huo ni kweli lina maslahi ya umma na yamekuwa yakitokea hivi karibuni.

Hata hivyo, halikidhi hili takwa ya kwamba halina uwezo wa kushughulikiwa katika utaratibu uliopo wa kawaida. Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa na ninamuona na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, niwaombe myafatilie mambo hayo ili wananchi wawe na utulivu wakijua Serikali inafuatilia kwa karibu matukio hayo ili yaweze kukomeshwa kabisa.

Waheshimiwa Wabunge, tumeshamsikia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akilizungumzia hilo na kwamba viongozi wetu wa Jeshi la Polisi wachukue hatua zinazostahili kwa watu ambao wanahusika kwenye matukio kama haya. Kwa hiyo na ninyi tunaomba mtusaidie kufuatilia ili kuwe na utulivu katika nchi watu waendelee na shughuli zao za maendeleo.

Katibu!

NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

(Majadiliano Yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka siku ya tarehe 10 Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alitusomea mpango kwanza asubuhi halafu, mchana akatusomea bajeti kwa maana ya makadirio ya mapato na matumizi, lakini Mwenyekiti kwa niaba ya Bunge alikuwa hajasoma kwa hiyo kwa utaratibu wetu yeye ndiyo anaanza kusoma leo kabla hatujaanza michango.

Kwa hivyo nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, atusomee kwa niaba ya Kamati ya Bajeti.

MHE. DANIEL B. SILLO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 124(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, pamoja na Sheria ya Bajeti, Sura 439.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kutoa pole kwa wananchi wote kwa kumpoteza aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyeiongoza nchi kwa uadilifu mkubwa. Aidha, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa kwanza Mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidory Mpango kwa kuteuliwa na kuidhinishwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile Kamati inampongeza, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia shughuli zote za Serikali kikamilifu. Aidha, Kamati inampongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri uliojaa weledi na uzoefu wa kutosha katika kuliendesha Bunge letu. Vile vile, nikupongeze wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika kwa kazi nzuri unayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati inapotekeleza majukumu yake. Aidha, Kamati inawashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Gavana wa Benki Kuu, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Watumishi wa Idara na Taasisi za Serikali kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kuangalia viashiria

mbalimbali vya uchumi, miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali pamoja na mwenendo wa mapato na matumizi. Pia, Taarifa hii imeainisha maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu nane kama ilivyoainishwa kwenye taarifa ya Kamati iliyowasilishwa mezani. Naomba taarifa yote iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi Jumla kwa Mwaka 2020; deni la Serikali; kwa kuwa nchi yetu imeingia katika kundi la nchi lenye kipato cha kati cha chini *(Lower MiddleIncome Country-LMIC)*; na kwa kuwa deni letu ni himilivu kwa viashiria vyote muhimu vya kimataifa. Hivyo basi, kutakuwa na changamoto ya upatikanaji wa mikopo nafuu ambayo Serikali imekuwa ikiitumia kutekeleza miradi yake. Hatua hii itasababisha Serikali kutumia mikopo ya kibiashara kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kuangalia uwezekano wa kujipima uhimilivu wa deni kwa kutumia uwiano wa malipo ya deni ya kukusanya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa tathmini ya uwezo wa ukopaji na ulipaji *(credit rating)* ili kuiwezesha Serikali kupata mikopo nafuu na kwa urahisi;

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, mikopo yenye masharti ya kibiashara ielekezwa katika miradi yenye sura ya kibiashara ili miradi hii ikamilike kwa wakati na kuanza kurejesha gharama za mikopo hiyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Serikali kutafuta mikopo yenye masharti ya kati ambayo masharti yake ni nafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathimini ya hali ya umaskini nchini; Kamati inatambua kuwa mojawapo ya hatua kubwa ya maendeleo sio tu kukua kiuchumi, lakini pia kuhakikisha umaskini wa mahitaji ya msingi na umaskini wa chakula unapungua. Hivyo, Serikali iendelee kusimamia vema Sera yake ya Elimu Msingi bila ada na kutekeleza Sera ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992 ambayo inaelekeza wananchi kuzaa watoto wanaoweza kuwahudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kielelezo Na.1 kinaonyesha kiwango cha umaskini kwa idadi ya wanakaya. Kielelezo Na.2 kinaonyesha kiwango cha umaskini kwa kiwango cha elimu ya mkuu wa kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inashauri Serikali iwekeze zaidi katika sekta ambazo zinahusisha wananchi wengi kama vile kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwakwamua kutoka kwenye umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka fedha 2020/2021; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya Shilingi trilioni 34.88 kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa shilingi trilioni 24.07, sawa na asilimia 69; Mapato ya kikodi yalikadiriwa kuwa shilingi trilioni 20.33 sawa na asilimia 84.5; Mapato yasiyo ya kikodi yalikadiriwa kuwa ni shilingi trilioni 2.92 sawa na asilimia 12.1; na mapato ya Halmashauri ni shilingi bilioni 814.96 sawa na asilimia 3.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 22.1 sawa na asilimia 63.4 zilielekezwa kwenye matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 12.78 sawa na asilimia 36.6 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2021, shilingi trilioni 24.53 zilipatikana sawa na asilimia 70.3 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kielelekezo Na.2 kinaonyesha mgawanyo wa bajeti wa Serikali ya Mwaka 2020/2021 kisekta, mchanganuo wa makusanyo kutoka

vyanzo vyote pamoja na mwenendo na matumizi ni kama ilivyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2020/2021 na mapendekezo ya Mpango wa maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2021/2022; Mpango wa Maendeleo ya Mwaka mmoja wa 2022 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano yaani mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026, dhima ya mpango huu ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu Mpango huu wa Mwaka 2020/2021 na mapendekezo ya Mpango wa 2021/2022 na ingependa kutoa ushauri na maoni katika maoni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, dhima ya Mpango huu ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu Mpango wa Mwaka 2020/2021 na Mapendekezo ya Mpango wa 2021/2022 na ingependa kutoa ushauri na maoni katika maoni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Afya, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya afya, huduma za kibingwa, upatikanaji wa vifaatiba, kinga, dawa na vitendanishi. Kamati inaunga mkono pia hatua madhubuti zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza ukiwemo ugonjwa wa UVIKO 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa zake, Serikali imeeleza kuwa mwezi Februari, 2021 imeingiza nchini mitambo saba yenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 ya hewa ya oksijeni kwa siku. Mitambo hiyo itasimikwa kwenye Hospitali ya Amana na Mikoa ya Dodoma, Geita, Manyara, Mbeya, Mtwara na Ruvuma ambapo kila mtambo mmoja kwenye hospitali hizo utakuwa na uwezo wa kusambaza gesi

ya oksijeni katika vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 18. Serikali imeeleza pia kwamba katika mwaka 2021/2022, itaongeza mitambo mingine ya aina hiyo 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na mkakati mpya wa upatikanaji wa fedha ili kuweza kukamilisha maboma 8,004 ya Zahanati na maboma 1,500 ya Vituo vya Afya ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa nia yake kuhakikisha kwamba zinapatikana shilingi bilioni 149 kwa mwaka wa mwanzo kwa ajili ya kugharamia Bima ya Afya kwa wote *(Universal Health Care)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi zitapunguza changamoto nyingi katika sekta ya afya. Ni vyema Serikali ikahakikisha fedha hizo zinapatikana ili mipango hii mizuri iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua juhudi zilizofanywa na Serikali katika kuboresha sekta ya kilimo nchini kwa kuanzisha *program* mbalimbali za kilimo kama vile *ASDP I* na sasa *ASDP II,* kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakulima. Hatua hizi zimesaidia kuongeza uzalishaji wa baadhi ya mazao nchini. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo, bado kilimo kinakabiliwa na changamoto nyingi zinazopelekea kilimo chetu kutokuwa na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa masoko endelevu ya uhakika kwa mazao ya kilimo, miundombinu hafifu katika maeneo ya uzalishaji, huduma duni za Ugani, kutozingatia kanuni bora za kilimo, matumizi hafifu ya pembejeo na zana za kilimo, uwekezaji mdogo wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zifuatazo zinapendekezwa ili kutatua changamoto za kilimo kwa lengo la kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakuwa na tija:-

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo, zana za kilimo na mbegu bora kwa wakati na kwa gharama nafuu;

(ii) Kuweka mazingira wezeshi katika uwekezaji kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo;

(iii) Kuhamasisha kilimo cha mkataba na kilimo kitalu;

(iv) Kuboresha mifumo ya upatikanaji wa taarifa za masoko ya mazao;

(v) Kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo. Hii ni pamoja na kuimarisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB);*

(vi) Kuboresha miundombinu na teknolojia katika kilimo cha umwagiliaji kwa kusimamia hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na mazingira;

(vii) Kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo,

(viii) Ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na nishati ya umeme ya uhakika unaovutia wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo;

(ix) Kuimarisha mifumo ya teknolojia, habari na mawasiliano; na Utashi wa kujitosheleza kwa bidhaa za ndani ikiwemo sukari, mafuta ya kula na ngano;

(x) Kuboresha miundombinu ya kilimo, kwa mfano kujenga maabara zenye uwezo wa kutoa ithibati za mazao ya kilimo Kitaifa na Kimataifa na miundombinu ya baridi *(Cold chains);*

(xi) Serikali ihakikishe inadhibiti magonjwa mbalimbali katika kilimo; na

(xii) Serikali itenge ne kupima ardhi ya kilimo pamoja na kuongeza bajeti ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pampja na mafanikio na hatua ambayo Serikali imechechukuwa katika sekta ya uvuvi, Kamati bado inapendekeza masuala yafuatayo:-

(i) Kuweka vivutio maalum kwa wawekazi wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi;

(ii) Kuweka mazingira bora na kuhamasisha wananchi kufuga samaki;

(iii) Kuhakikisha kwamba vifaranga vya samaki, chakula cha samaki na vifaa vya uvuvi vinapatikana kwa bei nafuu; na

(iv) Kuendeleza mapambano dhidi ya uvuvi haramu na kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo inakabiriwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kutokuwapo kwa masoko ya uhakika ya mifugo na mazao yake, magonjwa ya mifugo, migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, uvamizi wa maeneo ya malisho, kutotumia kikamilifu ranchi za Taifa, uingizwaji holela wa mazao ya mifugo toka nje ya nchi pamoja na uuzaji wa madawa bandia ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza tija katika sekta ya mifugo, Kamati inapendekeza Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Iwezesha upatikanaji wa maeneo ya malisho, chakula na maji kwa ajili ya mifugo;

(ii) Kutenga na kupima maeneo ya malisho katika maeneo mbalimbali nchini;

(iii) Kuimarisha huduma za utafiti wa mifugo, huduma za ugani na mafunzo kwa wafugaji na Maafisa Ugani;

(iv) Serikali ifanye uhakiki wa mipaka ili kutatua changamoto kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi;

(v) Kuanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya mazao ya mifugo;

(vi) Serikali iongeze ulinzi wa viwanda vya ndani vya mazao ya mifugo na pembejeo; na

(vii) Serikali iagize mitamba nje ya nchi na kuwauzia wananchi kwa ruzuku pamoja na kuboresha mitamba katika ranchi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya maziwa inakabiliwa na changamto kuu mbili ambazo ni utegemezi zaidi ya asilimia 90 ya maziwa yanayozalishwa nchini yanategemea ng'ombe wa asili wanaofugwa na wafugaji wanaohamahama pamoja na gharama za uzalishaji. Changamoto hizi mbili zimepeleka sekta ya maziwa kutokuwa ya ushindaji ukiinganisha na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua changamoto hizo, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Kuwepo na mfumo wa uzalishaji maziwa utakaopunguza gharama za uzalishaji. Kwa mfano, uanzishwaji wa mashamba madogo ya ng'ombe wa maziwa;

(ii) Kuhakikisha kwamba kunakuwa na upatikanaji wa vyakula vya ziada vya mifugo kwa kuanzisha vituo vya kuuzia vyakula vya mifugo. Hatua hii itapunguza gharama za ufugaji na bei ya maziwa;

(iii) Serikali kuwawekea mazingira wezeshi ya ufanyaji kazi kwa Maafisa Mifugo ili waweze kuzungukia mashamba ya mifugo ya wananchi na kutoa ushauri kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo zimekumbwa na

changamoto za ukuaji katika kipindi cha mwaka 2020/2021 kutokana na janga la Homa Kali ya Mapafu lililoikumba dunia kuanzia mwishoni mwa mwaka 2019. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Mataifa mbalimbali duniani katika kujikinga na janga hilo ikiwemo kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege na kuwafungia watu ndani, zilichangia kutokukua vizuri kwa sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa mwaka 2021/2022 kwa kuendelea kuimarisha sekta ya utalii na usalama wa watalii wanaoingia nchini, kuongeza kasi zaidi ya kutangaza vivutio vya utalii kama vile Mlima Kilimanjaro, hifadhi ya Serengeti, Ngorongoro na maeneo mengine ya kihistoria ndani na nje kwa kutumia balozi zetu, tovuti na sekta ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kuweka mazingira bora yatakayowezesha kuongezeka kwa shughuli za utalii kanda ya kusini na nyanda za juu kusini kwa kukamilisha haraka ujenzi wa viwanja vya ndege, kujenga miundombinu ya barabara, kuhamasisha ujenzi wa hoteli na kisha kuanzisha *package* za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa bajeti za mifuko na mapitio ya utendaji kazi wa baadhi ya mashirika ya Umma pamoja na utekelezaji wa Bajeti za Mashirika ya Umma. Kamati ilikutana na kufanya tathmini ya utendaji kazi wa mifuko maalumu na Mashirika ya Umma ili kutekeleza takwa hili la kisheria. Masuala yafuatayo yalibainika:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko Maalumu *(Ring-fenced Funds);* Mfuko wa maji una vyanzo vikuu viwili vya fedha; fedha zinazotokana na tozo za mafuta ya petroll na dizeli na fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Kamati imebaini kwamba utolewaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maji kwa miaka miwili mfululizo imekuwa ikitegemea zaidi chanzo cha tozo ya mafuta ya petroli na dizeli kuliko fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 fedha zilizotolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni asilimia 37 tu ya lengo la mwaka na fedha zilizotolewa kutoka kwenye tozo ya mafuta kwenda kwenye Mfuko wa Maji ni asilimia 87 tu ya lengo la mwaka. Mwenendo wa utolewaji wa fedha hafifu kama huu umejitokeza pia kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo tozo ya mafuta kwenda kwenye Mfuko wa Maji ilikuwa ni asilimia 74 na fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ilikuwa ni asilimia 30 tu. jedwali Na. 5 linaonesha Mwenendo wa Bajeti ya Utekelezaji wa Bajeti ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kufanya mabadiliko katika Sheria ya **"***The Road and Fuel Toll Act, Cap 220"* Kifungu cha 4A na kuongeza Kifungu kidogo cha (c) ili kuhakikisha kwamba bei za mafuta zinaposhuka tofauti ya bei iliyopo na iliyoshuka itumike kutunisha mfuko wa maji kwa sababu uzoefu unaonyesha, hata bei za mafuta zinaposhuka bei ya huduma na bidhaa zinazotegemea mafuta huwa hazishuki kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati imebaini kwamba *RUWASA* haina chanzo mahsusi cha mapato na badala yake mapato ya mfuko huu hulazimika kugawanywa mijini na vijijini. Hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa fedha hizi zikipatikana zielekezwe moja kwa moja *RUWASA*. Hatua hii itasaidia katika kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji vijijini ukizingatia kuwa katika mwaka huu wa fedha Serikali imejielekeza katika kuongeza fedha za kugharamia miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha Mfuko wa Barabara kinatokana na fedha kutoka Serikali kuu pamoja na Tozo ya mafuta. Kamati imebaini kwamba chanzo kutoka tozo za mafuta kimekuwa kikifanya vizuri tofauti na kile kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta kwa kuongeza ushuru wa barabara kwa shilingi 100/= kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli kwa

ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini kupitia *TARURA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii itasaidia kuongeza upatikanaji wa fedha kwa *TARURA* tofauti na ilivyokuwa awali ambapo *TARURA* walikuwa wakigawana mapato hayo hayo na *TANROADS.* Jedwali Na. 6 linaonyesha bajeti na mgao wa fedha za Mfuko wa Barabara katika Shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa matumizi ya Mfuko wa Reli, Kamati imebaini kwamba kwa kiasi kikubwa cha matumizi ya mfuko huu yameelekezwa katika reli ya kisasa *ya SGR.* Ni vyema miundombinu mingine ya reli ya kati nayo ikawa inapata mgao ili kuendelea kuhakikisha inatoa huduma kwa sababu reli ya *SGR* haifiki katika maeneo hayo. Mfano ni reli ya Tabora – Kaliua – Kigoma, Dar es Salaam – Tanga – Moshi hadi Arusha na Tabora – Kaliua – Mpanda. Endapo fedha zote zitaelekezwa katika *SGR* na kusahau maeneo haya tutapoteza manufaa ambayo yanapatikana hivi sasa hasa ya usafirishaji wa mizigo. Jedwali Na. 7 linaonyesha mwenendo wa makusanyo ya fedha inayotolewa kwa mfuko wa reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapitio ya utendaji kazi kwa baadhi ya mashirika ya Umma Pamoja na utekelezaji wa Bajeti za Mashirika ya Umma, hususan Shirika la Wakala wa Meli Tanzania *(TASAC);* kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Sheria ya *TASAC* majukumu yake ni pamoja na kufanya kazi za uwakala wa meli, uhakiki wa shehena, uhudumiaji wa nyaraka za uwakala wa meli na uwakala wa forodha kwa shehena na maeneo yenye maslahi kwa Taifa. Majukumu haya yameleta taharuki kubwa kwenye tasnia ya uwakala wa forodha nchini kwa sababu *TASAC* ambaYe ni msimamizi *(Regulator)* wa masuala ya uwakala wa forodha naye anafanya kazi za uwakala wa forodha kwa misingi ya utawala bora, suala ambalo Kamati inaona siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba kufanya mabadiliko kwenye Kifungu cha 7 (1), cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415, kwa lengo la

kuweka ukomo kwa *TASAC* kujishughulisha tu na mizigo na bidhaa nyeti za Serikali kama vile silaha, nyara za Serikali, madini, na mitambo inayohusiana na madini katika uchimbaji na uandaaji wa shughuli nyingine za masuala za uwakala wa forodha, ziendelee kwa sekta binafsi na *TASAC* aendelee na shughuli zake za usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kukutana kwa pamoja na Mashirika ya *TIRDO*, *TEMDO* na *CAMARTEC* na kubaini masuala yafuatayo:-

(i) Taasisi zote hizi ni muhimu kwenye kuendeleza uchumi wa viwanda;

(ii) Kuna uhaba mkubwa sana wa fedha kwa ajili ya utafiti na kuendeleza teknolojia zinazogunduliwa ambazo nyingi ni za bei nafuu na zinaendana na mazingira ya Taifa letu;

(iii) Ugunduzi unaofanyika unakosa viwanda vya ndani vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa kwa wingi ili ziwafikie wananchi; na

(iv) Taasisi hizi hazijulikani kwa wananchi pamoja na umuhimu wake katika Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kubaini masuala hayo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: -

(i) Kuangalia uwezekano wa kuyaunganisha mashirika hayo ili liwe shirika moja lenye nguvu na litakalotengewa bajeti ya kutosha kwa maendeleo ya viwanda;

(ii) Ziandaliwe ajenda za utafiti za Kitaifa mahsusi kwa ajili ya kuendeleza viwanda nchini; na

(iii) Kulinda ugunduzi na kuhakikisha kwamba ugunduzi huu unatumiwa na Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022, kati ya vipaumbele iliyojiwekea ni pamoja na kuimarisha uzalishaji viwandani kwa kuimarisha taasisi za tafiti na maendeleo ya viwanda na kilimo zikiwemo taasisi hizi. Aidha, ili nia hii njema iweze kufanikiwa, Serikali ione haja ya kuzisaidia taasisi hizi kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 taasisi za utafiti zimetengewa fedha za ndani shilingi bilioni 3.5 tu, kiwango ambacho Kamati inaona hakijitoshelezi hasa ukizingatia kazi kubwa na majukumu iliyonazo taasisi hizi. Kamati inaamini endapo mapendekezo haya yatafanyiwa kazi Taifa litaona umuhimu na manufaa ya mashirika haya ambapo hivi sasa hauonekani kwa kiwango kilichokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022; katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 36.33 ikiwa ni sawa na ongezeko la 4% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/2021 ya shilingi trilioni 34.88. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 23.00 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni asilimia 63 ya bajeti yote na shilingi trilioni 13.33 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 37 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo inajumuisha shilingi trilioni 10.37 fedha za ndani na shilingi trilioni 2.96 fedha za nje. Uchambuzi wa sera na mapato na sera za matumizi ni kama inavyoonekana kwenye taarifa ya kamati. Hatua za kikodi zinazopendekezwa na Serikali; kwanza kabisa nianze kwa kutoa pongezi kwa Serikali ambapo kwa kiasi kikubwa imechukua na kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyoguswa na hatua mbalimbali za Kodi na Usimamizi wake; Kamati imefanya uchambuzi wa hatua mbalimbali za kikodi zinazopendekekezwa na Serikali na kubaini kwamba hatua

hizo zimegawanyika katika makundi makuu saba kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Waziri wa Fedha na Mipango akiwasilisha hotuba yake alitoa rai kwa Watanzania kwamba tujifunge mikanda ili kuchangia zaidi mapato ya Serikali. Kamati inakubaliana na kauli mbiu hiyo. Hata hivyo, kila hatua ya kikodi iliyopendekezwa itachambuliwa kikamilifu na Kamati na kutoa mapendekezo kwa Bunge lako Tukufu pindi Serikali itakapoleta mbele ya Bunge lakp Tukufu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2021 *(The Finance Bill, 2021)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua pia kwamba baadhi ya vyanzo vipya vya mapato vilivyopendekezwa vinaenda kuongeza gharama za baadhi ya huduma na bidhaa nchini. Ongezeko hilo litachambuliwa kwa undani ili kuhakikisha kwamba Serikali inaongeza mapato yake bila kuathiri shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, pamoja na kwamba Muswada wa Fedha bado haujawasilishwa, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo kwa hatua za kikodi zilizopendekezwa na Serikali:-

(i) Serikali lazima ifuate utaratibu wa kikanuni kwamba inapowasilisha Bajeti ya Serikali Bungeni, iwasilishe sambamba na Muswada wa Sheria ya Fedha ili Kamati ipate muda wa kutosha wa kuupitia na kuuchambua pamoja na kuwaita wadau ili kupokea maoni yao;

(ii) Pili Serikali kuweka utaratibu wa kutoa ufafanuzi wa *HS Code* zilizoguswa katika Bajeti ya Serikali zinahusisha bidhaa na malighafi zipi ili Waheshimiwa Wabunge na wananchi wajue ni bidhaa zipi na malighafi zipi zinagusa? Utaratibu ulipo hivi sasa hauleti uwazi kwa jambo ambalo Bunge linataka kuidhinisha;

(iii) Serikali kuangalia upya ushirikishwaji wa wafanyabiashara na wazalishaji wa ndani kwa hatua za kikodi ambazo zinapendekezwa katika Sheria ya Forodha ya

Afrika Mashariki. Utaratibu uliopo hivi sasa hautoi fursa ya kutosha kwa sekta binafsi nchini kushiriki kikamilifu;

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maoni ya ujumla ya kamati kuhusu hatua mbalimbali za kikodi, Kamati ina maoni yafuatayo katika baadhi ya Dheria za Kodi ambazo zimependekezwa kufanyiwa mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332, Serikali inapendekeza kuweka kodi ya zuio kwa kiwango cha 2% kwenye mauzo ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi yanapouzwa kwenye kampuni na mashirika yote yanayojihusisha na usindikaji na ununuzi wa mazao. Hatua hii itakuwa na madhara makubwa sana kwenye bei ambazo wakulima watalipwa na makampuni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima Serikali ikafikiria upya uamuzi huu kwa sababu bado kilimo chetu kina changamoto ya kuwa duni hivyo kutokuwa na tija inayotakiwa, yaani mavuno madogo ukilinganisha na gharama zilizotumika. Changamoto ya upatikanaji wa masoko ya uhakika wa mazao, mfano zao la mahindi msimu uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo haileti maana hata kidogo mkulima ambaye siku zote tumesema hajaweza kufaidika na kilimo chake tunataka kumtwika mzigo mwingine mpya. Jambo hili linaweza kusababisha mazao yao yakawa yananunuliwa au kuuzwa kwa bei ya chini kwa kisingizio cha kodi hii ya zuio.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya Kodi ya Majengo Ssura 289; Serikali inapendekeza kuanza kutoza kodi ya majengo kupitia mashine za *LUKU.* Ubunifu huu una lengo la kupanua wigo wa mapato ya Serikali na kufanya ukusanyaji wa kodi hii kuwa rahisi. Uamuzi huu unaenda na Tamko la Serikali la awali la kurejesha ukusanyaji wa kodi hii kwa Serikali za Mitaa ambazo zina rasilimali watu katika ngazi zote za kukusanya kodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ubunifu huu kuwa mzuri, unaenda kinyume na Sheria ya Kodi ya Majengo ambayo inaangalia majengo ambayo yako kwenye maeneo yanayotakiwa kulipa kodi hiyo *(rateable areas)*. Mapendekezo haya yanachukulia nyumba zote zenye umeme hata zile ambazo ziko vijijini zinapaswa kulipa kodi. Hii ni kinyume na utaratibu uliowekwa kwenye Sheria ya Kodi ya Majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya hayatoi msamaha kwa Taasisi za Umma na Majengo mengine ya Umma ambayo yanatumia Umeme, lakini kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Majengo yamesamehewa kodi hiyo. Aidha, kuweka kiwango mfuto kwa nyumba zilizoko mjini na vijijini ni kuwaumiza wananchi ambao wanaishi vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kwamba ubunifu huu uende sambamba na kufanya uthamini wa nyumba na kutumia *Luku* kama namba ya mlipa kodi na kila Luku itozwe kulingana na nyumba ambayo Luku hiyo ipo. Utaratibu maalumu uwekwe kwa majengo ya maghorofa ambayo yana mkazi zaidi ya mmoja kama *apartments*. Hatua hii italeta mapato zaidi kuliko utaratibu huu unaopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hotuba ya Bajeti ya Serikali imeonyesha kwamba kuna kanuni mbalimbali ambazo zinaenda kufanyiwa mabadiliko. Ieleweke wazi kwamba kanuni hazitabadilishwa kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 kwa sababu Muswada unagusa Sheria mama tu. Hivyo, ni wazi kwamba Kamati ya Sheria Ndogo ambayo ndiyo hupitia kanuni hizo, inatakiwa kuzipata mapema iwezekanavyo ili kutekeleza masharti ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1, ambacho kinataka Kanuni zote zinazobadilishwa kuwasilishwa Bungeni mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ndani ya siku sita katika Mkutano wa Bunge unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Bajeti

ya Serikali kwa mwaka 2021/2022, hususani katika utaratibu wa uibuaji na ugharamiaji wa miradi ya kuongeza mapato ya Halmashauri, Kamati imefanya upembuzi kwenye mchakato wa uibuaji, uidhinishaji na utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya kimkakati ya Halmashauri ili ijitegemee kimapato na kubaini kwamba:-

(i) Utaratibu uliopo japo ulikuwa na nia ya kuziwezesha Halmashauri ambazo zinajiweza tayari ili zijitegemee, umekuwa unaumiza sana Halmashauri ambazo ukusanyaji wake wa mapato ni duni. Hali hii inatokana na ukweli kwamba wakati wa kuzipima zote zinawekwa kwenye kundi moja;

(ii) Pia, kwa Halmashauri zinazoonekana kuwa na wigo mdogo wa ukusanyaji wa mapato, viongozi wake huwajibishwa ilhali hakuna uwezeshaji wowote wa kuongeza mapato uliofanywa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ni vyema utaratibu huu ukabadilishwa na badala yake zikaangaliwa kwanza Halmashauri zenye hali mbaya na zenye uwezo wa kati kutokana na wigo mdogo wa mapato, kisha ndiyo zikaangaliwa zile zenye hali nzuri ya ukusanyaji wa mapato ili kuleta usawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo ya *TANAPA* na hali ya Sekta ya Utalii, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuwa inatoa fedha za matumizi mengineyo kwa Mamlaka za *TANAPA, NCAA* na Ngorongoro kwa miezi miwili unapoanza mwaka wa fedha na kuendelea kutoa kwa mwezi mmoja mmoja kila mwezi. Hatua hii itaziwezesha taasisi hizi kuwa na akiba ya fedha ya kukidhi mahitaji ya mwezi unaofuata katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, fedha za Mamlaka hizo zilipitia Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina ambapo hadi mwezi Aprili, 2021 jumla ya shilingi 227,519,349,953.48 zilitolewa kwa Taasisi hizo. Kati ya

fedha hizo shilingi 68,440,922,181.36 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi 139,287,122,765.62 kwa ajili ya uendeshaji wa na *TAWA* na shilingi 19,791,305,006.50 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugharamiaji wa miradi ya maendeleo ya *TANAPA* na hali ya sekta ya utalii. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuwa inatoa fedha za matumizi mengine kwa Mamlaka za *TANAPA, NCAA* na *TAWA* kwa miezi miwili unapoanza mwaka wa fedha na kuendelea kutoa kwa mwezi mmojammoja kila mwezi. Hatua hii itaziwezesha taasisi hizi kuwa na akiba ya fedha kwa kukidhi mahitaji ya mwezi unaofuata katika kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, fedha za Mamlaka hizo zilipitia Fungu 7 – Ofisi ya Msajili wa Hazina ambapo hadi mwezi Aprili, 2021 jumla ya shilingi bilioni 227.5 zilitolewa kwa Taasisi hizo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 68.4 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 139.3 ni kwa ajili ya uendeshaji wa *TAWA* na shilingi bilioni 19.8 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, imebainika kwamba ulipaji wa fedha za *WMA* ambao ni walinzi wa hiari wa hifadhi pamoja na miundombinu ya barabara zimekuwa hazilipwi kwa wakati. Aidha, miundombinu katika baadhi ya Hifadhi ambazo zinaliingizia Taifa mapato kama vile Serengati na Ngorongoro imeharibika na hazipitiki kwenye baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima itambue kwamba matumizi katika masuala ya uhifadhi wakati mwingine hayatabiriki. Kwa mfano changamoto za ujangili, magonjwa ya wanyama, uvamizi wa wananchi kwenye maeneo ya hifadhi na uvamizi wa wanyama kwenye makazi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maduka ya kubadilisha Fedha za Kigeni; kufuatia udhibiti wa biashara ya maduka

ya ubadilishaji fedha nchini uliofanywa na Benki Kuu mwaka 2019 iliyopelekea kufungwa kwa baadhi ya maduka hayo. Hatua hii ilikua na lengo la kuhakikisha kwamba biashara hiyo inafanywa kwa mujibu wa sheria na kanuni za Benki Kuu. Aidha, hatua hii ilisababisha uhaba wa upatikanaji wa huduma ya ubadilishaji wa fedha za kigeni nchini kutokana na huduma hiyo kutolewa kwa kiasi kikubwa na mabenki na maduka binafsi machache. Adha hiyo ilisababishwa na: -

(i) Mabenki kutokufanya kazi kwa masaa 24 na kutokufunguliwa siku za Jumapili suala ambalo linasababisha usumbufu kwa wahitaji; *(Makofi)*

(ii) Mabenki kuwa na matawi machache ambayo yako mbali na maeneo ambayo huduma hiyo inahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia changamoto hizo Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Kanuni ya Uendeshaji wa Maduka ya Kubadilisha Fedha ya 2019 ili kurahisisha ufunguaji na uendeshaji wa maduka hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki *(Electronic Tax Stamp);* Kamati inatambua faida za mfumo wa Kodi za Kieletroniki. Faida hizo ni pamoja na kupata taarifa sahihi za uzalishaji wa viwandani na hivyo kukusanya kodi stahiki ya ushuru wa bidhaa pamoja na kodi ya makampuni, uwezo wa utambuzi wa bidhaa halisi na zisizo halisi, kuondoa udanganyifu wa baadhi ya wazalishaji na wafanyabiashara wasio waaminifu. Changamoto kubwa ya mfumo huu ni gharama zinazotozwa kwa stempu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

(i) Ni kuangalia uwezekano wa mfumo huo kutumika katika bidhaa nyingine ambazo zinazalishwa na kupitia *conveyer belt* ili kupanua wigo wa ukusanyaji wa taarifa na inaweza kupunguza gharama za stempu, bidhaa zinazopendekezwa ni pamoja na saruji, mafuta ya kula na mabati.

(ii) Ni Serikali kukaa na mkandarasi na kufanya marejeo ya gharama za stempu ili zisiwe mzigo kwa wazalishaji; na

(iii) Ni kuwa na mkakati wa wataalamu wa ndani kuendesha mfumo huo pindi mkataba na mkandarasi wa sasa utakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa uwasilishaji wa maoni ya Kamati za Bunge na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati ya Bajeti imebaini kwamba utaratibu uliopo wa uwasilishaji wa mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki haushirikishi wafanyabiashara wa ndani kama walivyo wenzao wa nchi jirani kabla ya Serikali kupeleka mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati imebaini kwamba baadhi ya maamuzi ambayo Serikali inaridhia katika Jumuiya yanakuwa na athari hasi kwa wafanyabiashara na wazalishaji wa ndani na yanatoa manufaa kwa wazalishaji wa nchi nyingine wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu maalumu utakaojulikana na wafanyabiashara wote ili washiriki kikamilifu katika mapendekezo ya Tanzania yanayoenda katika Jumuiya na yale ya nchi wanachama yanayopelekwa katika Jumuiya. Aidha, Ofisi ya Bunge ione haja ya kuandaa utaratibu wa ndani na Kikanuni utakao toa fursa kwa Kamati za Bunge kuyapitia na kupata maoni ya umma kupitia *Public Hearing* ili maoni hayo yanaporidhiwa na nchi yawe yameshirikisha wadau kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti *(Compliance Report).* Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura ya 438 kifungu cha 56(1), Serikali inatakiwa kuandaa na kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti Kila baada ya miezi sita. Kifungu hiki kilifanyiwa mabadiliko mwaka 2017 na kubadilisha uwasilishaji wa Ripoti ya

Utekelezaji wa Bajeti kutoka miezi 3 iliyokuwepo hadi miezi 6 ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko haya yamekuwa na changamoto kubwa sana katika utekelezaji wake katika maeneo makuu mawili. Kwanza ni kuchelewa kufuatilia utekelezaji wa bajeti kwa miezi sita na pili ni kushindwa kutoa maoni na mapendekezo katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka husika ili kurekebisha kasoro ambazo zinaweza kuwa zimejitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe kwanza kwa kunipa fursa na kuniamini kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Aidha, napenda kumshukuru, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa *Eng.* Hamad Yussuf Masauni, Mbunge, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za majadiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Omari Kigua, Makamu Mwenyekiti wa Kamati, na Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipa wakati wote wa kupitia na kuchambua Bajeti Kuu ya Serikali na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa yangu yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndg. Nenelwa Mwihambi pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake kwa wakati bila kukwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo na Makatibu

wa Kamati hii Ndg. Godfrey Godwin, Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala na Wilfred Akasi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru watendaji wote wa Idara na Vitengo husika vya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2020, MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2021/22, TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2020/21 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 124(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/22 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/21 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni 2020, pamoja na Sheria ya Bajeti Sura 439. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imekuwa ikitoa ushirikiano wa kutosha kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kutoa pole kwa wananchi wote kwa kumpoteza aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyeiongoza nchi kwa uadilifu mkubwa na kuhakikisha nchi inaendelea kusimama imara na kukua kiuchumi. Aidha, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa kwanza Mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidory Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile Kamati inampongeza, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kusimamia shughuli zote za Serikali kikamilifu. Aidha, Kamati inakupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako mahiri uliojaa weledi na uzoefu wa kutosha katika kuliendesha Bunge hili la Kumi na Mbili (12) la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi Kamati ya Bajeti tunakushukuru kwa miongozo yako na ushirikiano uliotupa katika kutekeleza majukumu yetu. Vilevile nimpongeze Mheshimiwa Dkt Tulia Ackson Naibu Spika wa Bunge kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni, (Mb) Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati wote tulipowahitaji kwenye Kamati ili kuhakikisha Kamati inafanya kazi zake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inawashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango Ndg. Emmanuel Tutuba na Manaibu wake, Gavana wa Benki Kuu Prof. Frolence Luoga, na Manaibu Gavana, Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Ndg. Alphayo Kidata na Wakuu wa Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ushirikiano wao kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa tathmini ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 na uchambuzi wa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa

Mwaka wa fedha 2021/22 kwa kuangalia viashiria mbalimbali vya uchumi, miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali pamoja na mwenendo wa mapato na matumizi. Pia, Taarifa hii imeainisha maeneo mbalimbali ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Taarifa hii imegawanyika katika maeneo makuu nane (9). Eneo la kwanza ni Utangulizi; Eneo la pili ni Tathmini ya Mwenendo wa viashiria vya uchumi jumla; Eneo la tatu ni Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/21; Eneo la nne ni Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2020/21 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2021/22; Eneo la Tano linahusu Mapitio ya Utendaji Kazi wa Baadhi ya Mashirika ya Umma pamoja na Utekelezaji wa Bajeti za Mashirika ya Umma; Eneo la Sita linahusu Sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22; Eneo la Saba linahusu Hatua za Kikodi zinazopendekezwa na Serikali; Eneo la Nane ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati na mwisho ni Hitimisho.

2.0. TATHMINI YA MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA KWA MWAKA 2020

2.1. Hali ya Uchumi wa Dunia

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ilionyesha kuwa kufuatia Janga la UVIKO-19, uchumi wa dunia kwa mwaka 2020 ulitarajiwa kuwa na ukuaji hasi wa **asilimia 3.3.** Na kwa zile Nchi ambazo uchumi wao unategemea zaidi utalii na uuzaji wa mafuta nje, zilikadiriwa kuwa na mdororo mkubwa zaidi wa kiuchumi ikilinganishwa na mataifa mengine. Pamoja na hali ya uchumi kuanza kuimarika baadhi ya nchi zimeanza kurejesha njia za awali za kuzuia kusambaa kwa ugonjwa wa UVIKO-19, ikiwemo kufunga mipaka na kusimamisha baadhi ya shughuli za kiuchumi kutokana na maambukizi mapya ya ugonjwa huo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa Mwezi Aprili, 2021 (World Economic Outlook Report,

April 2021), uchumi wa dunia kwa mwaka 2021 unatarajiwa kukua kwa **asilimia 6** na kushuka hadi **asilimia 4.4** mwaka 2022. Kuimarika kwa uchumi kutahusisha kulegezwa kwa hatua zilizochukuliwa na serikali mbalimbali katika kudhibiti kusambaa kwa homa kali ya mapafu na mategemeo ya kupata suluhisho la vihatarishi vya maambukizi ya virusi vya UVIKO-19. Hivyo ni dhahiri kuwa uimarikaji wa uchumi wa dunia utategemea zaidi kupatikana kwa chanjo ya janga hili lakini vilevile ubora na uimara wa sera zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa kwa kila nchi kulingana na chumi zao.

2.2. Hali ya Ukuaji wa Uchumi kwa Mwaka 2020

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zilizokuwa na ukuaji chanya wa uchumi kwa mwaka 2020 na kuepuka ukuaji hasi uliozikumba nchi nyingi duniani kutokana janga la UVIKO-19. Kabla ya UVIKO-19, Uchumi wa Tanzania ulikuwa unakua kwa wastani wa **asilimia 6.9.** ukuaji huu uliweza kupunguza hali ya umaskini kutoka **asilimia 28.2** hadi **asilimia 26.4** hivyo kuliwezesha taifa kuingia katika Uchumi wa kati wa chini Julai 2020. Uchumi umeendelea kuwa imara licha ya athari za janga la UVIKO-19 zilizoikumba Dunia. Ukuaji huu umetokana na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na janga hili ikiwemo kutowafungia watu ndani (lock down) na kuwaruhusu waendelee na shughuli za kiuchumi na kijamii wakati wa mlipuko wa homa kali ya mapafu. Hatua nyingine ni pamoja na hatua mbalimbali za kisera zilizochukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2020, Pato la Taifa lilikua kwa **asilimia 4.8** ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 7** mwaka 2019. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi, kilimo, uchukuzi na uchimbaji madini. Kiasi hiki ni kikubwa zaidi ya kile kilichokuwa kimekadiriwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) la **asilimia 2.5** ikiwa chini ya lengo la nchi la kukua kwa **asilimia 5.5**. Kupungua kwa kasi ya ukuaji katika kipindi husika kumechangiwa na mvua zilizozidi wastani zilizosababisha mafuriko ambayo yaliharibu miundombinu ya uchukuzi na uhifadhi wa mizigo nchini na kuchelewesha

utekelezaji wa baadhi ya miradi pamoja na athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu ulioenea katika nchi nyingi ambazo ni washirika wetu wakubwa wa biashara.

Mheshimiwa Spika, athari kubwa za kiuchumi zilijitokeza zaidi katika robo ya pili ya mwaka 2020 (Aprili hadi Juni) ambapo shughuli za kiuchumi za hoteli, utalii, biashara na elimu zilikuwa na ukuaji hasi. Ukuaji huu ulichangiwa na hatua zilizochukuliwa kwa muda na Serikali za kusitisha baadhi ya shughuli za kiuchumi hasa mikusanyiko ikiwemo kufungwa kwa safari za anga pamoja na kusitishwa kwa shughuli zote za sanaa na burudani ikiwemo michezo. Kwa kipindi cha mwaka 2020, sekta zilizochangia ukuaji huu ni pamoja na Sekta ya Ujenzi **(asilimia 9.1**); Madini na Mawe (**asilimia 6.7**); Habari na Mawasiliano (**asilimia 8.4**); Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo **(asilimia 8.4);** na Shughuli za kitaalamu,Sayansi na Ufundi (**asilimia 7.3**).

Mheshimiwa Spika, pamoja na sekta nyingine za uchumi kudorora, sekta ya kilimo ilikua kwa wastani wa **asilimia 4.9** mwaka 2020 ikilinganishwa na **asilimia 4.4** mwaka 2019 na hivyo kusaidia katika kuimarisha mfumuko wa bei. Sekta ya Kilimo ni kati ya sekta pekee ambayo pamoja na uwepo wa ugonjwa wa UVIKO-19 imeweza kukua na kuongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya kilimo na sekta nyingine kama vile utalii wa ndani ili zichangie katika uchumi na hivyo kuwa na uchumi usiotegemea sekta chache.

2.3. **Mfumuko wa Bei**

Mheshimiwa Spika, Mfumuko wa bei umeendelea kushuka na kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo ulifikia wastani wa **asilimia 3.3** mwaka 2020, ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 3.4** mwaka 2019. Mwenendo huu uko ndani ya lengo la muda wa kati la **asilimia 5.0** na ndani ya wigo uliowekwa kwa mujibu wa vigezo vya mtangamano wa kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kiwango ambacho hakizidi **asilimia 8.0** na wigo uliowekwa

na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) wa kati ya **asilimia 3.0** na **7.0**.

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki cha mfumuko wa bei kilitokana na upatikanaji wa chakula cha kutosha, bei ndogo ya mafuta kwenye soko la dunia, utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani, na sera madhubuti ya fedha na sera ya bajeti. Hata hivyo, hali ya upungufu wa chakula katika baadhi ya nchi jirani, iliyosababishwa na nchi hizo kufunga baadhi ya shughuli za kiuchumi kufuatia mlipuko wa UVIKO-19, inaweza kusababisha mfumuko wa bei kuongezeka kwa kiasi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuchukua tahadhari ya suala hili ili kuondokana na adha ambayo inaweza kujitokeza hapo baadae ikiwa ni pamoja na kuwa na hifadhi ya kutosha hasa ikizingatiwa sasa Wananchi wameruhusiwa kuuza mazao yao nje ya nchi.

2.4. Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji fedha

Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine za washirika wakuu wa biashara ulimwenguni imeendelea kuwa tulivu. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na mfumuko mdogo wa bei, utekelezaji thabiti wa sera ya fedha, usimamizi imara katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni, kuimarika kwa urari wa biashara, pamoja na bei ndogo ya mafuta katika soko la dunia. Katika kipindi cha Desemba 2020, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa **shilingi 2,309.19** ikilinganishwa na **shilingi 2,300.62** kipindi kama hicho mwaka 2019 sawa na kushuka kwa **asilimia 0.37**. Njia pekee na ya uhakika ya kuhakiksha kwamba thamani ya shilingi ina imarika dhidi ya dola ni kuwekeza katika maeneo ambayo yataongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

2.5. Akiba ya Fedha za Kigeni

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Desemba 2020, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za

kimarekani **milioni 4,767.7, k**iwango kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha **miezi 5.6**. Aidha, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu katika usimamizi wa masoko ya ubadilishaji fedha nchini hatua ambayo sio tu imepelekea utulivu wa thamani ya shilingi lakini na nchi kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kwamba moja ya kigezo muhimu Duniani cha kupima uwezo wa nchi kukabiliana na majanga au msukosuko wa kiuchumi kama janga la UVIKO-19 ni akiba ya fedha za Kigeni. Kamati inaishauri Serikali kufikiria kuhifadhi dhahabu kama akiba mbadala wa fedha za kigeni.

Jedwali Na. 1. Mwenendo wa Akiba ya Fedha za Kigeni kwa mwezi Desemba kuanzia mwaka 2015 hadi 2020

	2015	2016	2017	2018	2019	2020
Kiasi (USD million)	4,093.7	4,325.6	5,900.3	5,044.6	5,554.4	4,767.7
Uwezo (miezi)	5.1	5.0	6.6	4.9	6.4	5.6

Chanzo: *Benki Kuu ya Tanzania*

2.6. **Deni la Serikali**

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba, 2020, Deni la Serikali lilifikia **shilingi trilioni 59.01**, sawa na ongezeko la **asilimia 7.6** ikilinganishwa na **shilingi trilioni 54.85** kipindi kama hicho mwaka 2019. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni **shilingi trilioni 42.83** na deni la ndani ni **shilingi trilioni 16.18.** Ongezeko la deni limetokana na: Ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo na malimbikizo ya riba ya deni la nje, hususan nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris (Non Paris Club members) ambazo Serikali inaendelea kujadiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu imeingia katika kundi la nchi lenye kipato cha kati cha chini (Lower Middle Income Country-LMIC). Na kwa kuwa deni letu ni himilivu kwa viashiria

vyote muhimu vya kimataifa. Hivyo basi, kutakuwa na changamoto ya upatikanaji wa mikopo nafuu ambayo Serikali imekuwa ikiitumia kutekeleza miradi yake. Hatua hii itasababisha Serikali kutumia mikopo ya kibiashara kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:

i. Kuangalia uwezekano wa kujipima uhimilivu wa deni kwa kutumia kiashiria cha makusanyo ya mapato ya ndani kwa ulipaji wa deni. Hii ni kwa sababu deni la Taifa hulipwa na makusanyo ya ndani na ni malipo ya lazima (first charge) katika matumizi ya Serikali;

ii. kukamilisha haraka mchakato wa nchi yetu kufanyiwa tathmini ya uwezo wa ukopaji na ulipaji (credit rating) ili kuiwezesha Serikali kupata mikopo nafuu na kwa urahisi;

iii. Mikopo yenye masharti ya kibiashara ielekezwa katika miradi yenye sura ya kibiashara ili miradi hii ikamilike kwa wakati na kuanza kurejesha gharama za mikopo hiyo;

iv. Kuboresha mikakati ya kukusanya kodi ili kuhakikisha sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa na mapato ya ndani pamoja na kupunguza matumizi yanayoweza kuepukika; na

v. Serikali kutafuta mikopo yenye masharti ya kati (Semi concessional loans) ambayo masharti yake ni nafuu ikilinganishwa na mikopo ya kibiashara.

2.7. **Mwenendo wa Viwango vya Riba na Huduma za Kibenki**

Mheshimiwa Spika, Viwango vya riba za mikopo ya mabenki ulipungua kwa kasi ndogo, hadi kufikia **asilimia 16.58** katika kipindi cha mwezi Julai hadi mwezi Aprili 2021 kutoka wastani wa **asilimia 16.91** katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Katika kipindi hicho hicho, wastani wa riba za amana kwa ujumla uliongezeka kutoka **asilimia 6.69** hadi **asilimia 6.95**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali katika kuyaongezea mabenki yetu nchini ukwasi viwango vya

mikopo ya riba vimeendelea kuwa juu na riba za amana zimeendelea kuwa chini, na hivyo kufanya tofauti ya riba za mikopo na amana kwa mwaka mmoja (interest rate spread) kuwa ni kubwa ambayo kwa sasa ni **asilimia 7.28**. Ikumbukwe kuwa Sekta ya benki ni injini ya shughuli za kiuchumi na hivyo huchukua sehemu muhimu sana katika kusaidia ukuaji wa uchumi kupitia mgawanyo mzuri wa rasilimali fedha. Hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutafuta mwarobaini utakaopelekea kushuka kwa viwango vya riba za mikopo ukichukulia maanani mfumuko wa bei wa **asilimia 3.3** na kuongeza viwango vya amana. Aidha, Serikali ifikirie kuweka utaratibu na riba rafiki kwa watumishi wa umma wanaokopa hasa ikizingatiwa kuwa urejeshaji wake ni wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utekelezaji wa sera wezeshi ya fedha, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia wastani wa **asilimia 5.1** mwezi Julai hadi Desemba mwaka 2020, ikilinganishwa na **asilimia 9.3** katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba mwaka 2019. Ukuaji huu hasi umechangiwa na kupungua kwa shughuli za uchumi zilizosababishwa na changamoto za janga la UVIKO-19. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuja na mkakati wa kusaidia kutatua changamoto za upatikanaji wa mikopo nafuu kwa sekta binafsi ili kuendana na mahitaji ya shughuli za uchumi hasa katika kipindi hiki cha janga la UVIKO-19.

2.8. Tathmini ya Hali ya Umaskini Nchini

Mheshimiwa Spika, viashiria vya kupima hali ya umaskini nchini hupatikana kwa kutumia taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi *(Household Budget Survey - HBS)* utafiti unaofanyika kila baada ya miaka mitano. Matokeo ya Utafiti ya mwaka 2017/18 yanaonyesha kuwa kaya zenye wanakaya wachache wana kiwango kidogo cha umaskini kuliko kaya zenye wanakaya wengi. Na kiwango cha umaskini wa mahitaji ya chakula na ya msingi ni kikubwa kwa kaya zinazoongozwa na wakuu wa kaya wenye elimu ndogo. Kamati inatambua kuwa mojawapo ya hatua kubwa ya maendeleo sio tu kukua kiuchumi lakini pia kuhakikisha umaskini wa mahitaji ya msingi na umaskini wa chakula

unapungua. Hivyo, Serikali iendelee kusimamia vema Sera yake ya Elimu Msingi bila ada na kutekeleza Sera ya Idadi ya Watu yam waka 1992 ambayo inaelekeza wananchi kuzaa watoto wanaoweza kuwahudumia. Kamati inaendelea kusisitiza kwamba Serikali iwekeze zaidi katika sekta ambazo zinahusisha wananchi wengi kama vile kilimo, mifugo na uvuvi ili kuwakwamua kutoka kwenye umaskini.

Kielelezo Na. 1: Kiwango cha Umaskini kwa Idadi ya Wanakaya, HBS 2017/18



Jedwali Na. 2: Kiwango cha Umaskini kwa Kiwango cha Elimu ya Mkuu wa Kaya, HBS 2017/18

Kiwango cha Elimu ya Mkuu wa Kaya	Umaskini wa Chakula	Umaskini wa Mahitaji ya Msingi
Hana Elimu	11.0	35.7
Elimu ya Watu Wazima	19.2	31.0
Elimu ya Msingi (isiyokamilika)	10.8	35.0
Elimu ya Msingi	7.9	25.9
Elimu ya Sekondari au zaidi	1.0	5.9
Tanzania Bara	**8.0**	**26.4**

3.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21 Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 34.88** kutoka katika vyanzo vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo mapato ya ndani yalikadiriwa kuwa **shilingi trilioni 24.07** sawa na **asilimia 69**, mapato ya kikodi yalikadiriwa kuwa **shilingi trilioni 20.33** sawa na **asilimia 84.5**; mapato yasiyo ya kikodi yalikadiriwa kuwa ni **shilingi trilioni 2.92** sawa na **asilimia 12.1** na mapato ya Halmashauri ni **shilingi bilioni 814.96** sawa na **asilimia 3.4**. Kati ya kiasi hicho **shilingi trilioni 22.1** sawa na **asilimia 63.4** zilielekezwa kwenye matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 12.78** sawa na **asilimia 36.6** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Aprili, 2021 **shilingi trilioni 24.53** zilipatikana sawa na **asilimia 70.3** ya lengo la mwaka.

Kielelezo Na. 2: Mgawanyo wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2020/21 Kisekta



Chanzo: *Wizara ya Fedha na Mipango*

3.1. Mwenendo wa Mapato.

a) Mapato ya Kodi

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Serikali iliweza kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 14.54** dhidi ya malengo ya kukusanya **shilingi trilioni 20.33** sawa ana **asilimia 71.51** ya lengo la mwaka. Mapato ya kodi kwa mwaka 2020/21 yamepungua kwa **asilimia 0.68** ukilinganisha na **shilingi trilioni 14.64** kwa mwaka wa fedha 2019/20. Hii ni sawa na upungufu wa **shilingi bilioni 100**, hivyo kamati inaishauri Serikali kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na kusimamia ulipaji wa kodi kikamilifu ili fedha za kuendesha Serikali zipatikane na utekelezaji wa miradi ya maendeleo uweze kuendelea.

Jedwali Na. 3. Ulinganisho wa Makusanyo ya Kodi kuanzia JulaiHadi Aprili kwa mwaka 2019/20 na 2020/21

Mwezi	Makusanyo Halisi 2019/20	Makusanyo Halisi 2020/21	Asilimia za Ukuaji
Julai-20	1,232,189.51	1,267,684.7	2.8%
Agosti-20	1,315,495.03	1,376,040.8	4.4%
Septemba-20	1,708,501.52	1,681,596.0	-1.6%
Oktoba-20	1,445,098.98	1,314,921.7	-9.9%
Novemba-20	1,446,408.00	1,317,311.5	-9.8%
Disemba-20	1,906,284.26	2,087,934.6	8.7%
Januari-21	1,476,474.76	1,288,372.4	-14.6%
Februari-21	1,303,475.53	1,296,990.6	-0.5%
Machi-21	1,539,061.34	1,625,196.8	5.3%
Aprili-21	1,167,545.20	1,258,130.6	7.2%
JUMLA	**14,540,534.13**	**14,514,179.6**	**-8.0%**

***Chanzo**: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*

b) Mapato yasiyo ya Kodi

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia Aprili, 2021 Mapato yasiyo ya Kodi yalifikia **shilingi trilioni 1.80**, sawa na **asilimia 61.6** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 2.92** kwa mwaka. Kamati ilibaini kwamba Wizara ya Madini imeendelea kufanya vizuri katika

ukusanyaji wa mapato kutokana na kuimarishwa kwa usimamizi unaofanywa na Serikali kwenye masoko ya madini. Maduhuli yaliyokusanywa katika sekta ya madini kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21 ni **shilingi bilioni 317.5** sawa na **asilimia 120.6** ya lengo la kukusanya **shilingi bilioni 263.4** kwa kipindi hicho. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Wizara na Idara zote zinazo kusanya Maduhuli ya Serikali inafanya hivyo kwa kutumia mifumo ya kieletroniki ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta za uchumi nchini ambazo zinatoa mchango mkubwa katika ukusanyaji wa mapato na kuendeleza maisha ya Watanzania wengi ikiwepo fursa za ajira. Mathalan, Sekta hii ya Utalii kupitia vivutio mbalimbali inachangia zaidi ya **asilimia 17** ya pato la Taifa, **asilimia 25** ya fedha zote za kigeni na kuajiri zaidi ya watu **milioni 5.5.** Aidha, Sekta utalii ilichangia **asilimia 3.1** ya mapato yasiyo ya kodi kutokana na sekta hii kuathiriwa na ugonjwa wa UVIKO-19. Jedwali na 4 linaonyesha mchango wa sekta hii kwenye mapato yasiyo ya kodi. Hivyo [illegible] za haraka kuinusuru sekta hii ambayo na mchango mkubwa katika pato la taifa.

Mamlaka	Makadirio	Mapato Halisi	Asilimia
TANAPA	168,595.59	44,299.14	26.3
NCAA	35,937.74	21,685.59	60.3
TAWA	27,365.08	13,949.13	51.0
JUMLA	**231,898.4**	**79,933.9**	**34.5**

Jedwali Na. 4 Makusanyo yasiyo ya Kikodi sekta ya utalii kuanzia Julai, 2020 Hadi Februari, 2021

Chanzo: *Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)*

c) Mapato ya Serikali za Mitaa

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili 2021 Mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani vya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia **shilingi bilioni 607.4** sawa na **asilimia 88.5** ya lengo. Kamati ilibaini kwamba kutokufikiwa kwa lengo la makusanyo ya Serikali za mitaa ni kutokana na baadhi ya

serikali za mitaa kutegemea tozo ya mazao (Crop cess), inayotegemea msimu wa mavuno. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa serikali za mitaa nchini na kuimarisha ukusanyaji wake ili kuongeza mapato, hatua hii itazisaidia serikali za mitaa uwezo wa kujitegemea kimapato.

d) Misaada na Mikopo ya Masharti Nafuu kutoka Nje

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21 Serikali ilitarajia kupokea jumla ya **shilingi trilioni 2.4** ambapo kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 949.3** ilikuwa ni Misaada na **shilingi trilioni 1.93** ilikuwa ni Mikopo ya masharti nafuu. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021 Misaada na mikopo nafuu iliyopokelewa ilikuwa **shilingi trilioni 1.89** sawa na **asilimia 70.4** ya lengo. Mchanganuo wa fedha zilizopokelewa unajumuisha misaada **shilingi bilioni 327.3** sawa na **asilimia 66.2** ya lengo la **shilingi bilioni 494.6** na mikopo nafuu **shilingi bilioni 643.9** sawa na **asilimia 61.7** ya lengo la kipindi husika la **shilingi trilioni 1.044. Mheshimiwa Spika**, Hali hii inaonyesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2020/21 wahisani wanapendelea zaidi kutoa mikopo nafuu kuliko kutoa misaada ya kibajeti. Hii imetokana na Janga la UVIKO-19 ambalo limezikumba nchi nyingi duniani. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kwa kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano (Development Cooperation Framework-DCF) ambao umeonyesha matumaini makubwa kimaendeleo katika kipindi kifupi.

e) Mikopo ya ndani

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 Serikali ilikusudia kukopa jumla ya **shilingi trilioni 4.92.** Kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2020/21, Serikali ilipanga kukopa katika soko la ndani jumla ya **shilingi trilioni 2.55.** Hadi Desemba 2020, **shilingi trillion 2.41** zilipatikana sawa na **asilimia 94.6** ya lengo la kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, **shilingi trillion 1.44** zimetumika kulipia mikopo ya ndani iliyoiva na **shilingi bilioni 942.6** zimetumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021

Mikopo ya ndani ikijumuisha mikopo ya kulipa dhamana za Serikali zilizoiva ilifikia **shilingi trilioni 3.99**, sawa na **asilimia 95.7** ya lengo. Kamati inaishauri Serikali iangalie uwiano wa kiasi inachokopa ndani na nje ili kuhakikisha kwamba sekta binafsi ya ndani nayo inapata mikopo kutoka kwenye Taasisi za fedha za ndani kwa riba nafuu.

3.2. Mwenendo wa Matumizi

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya matumizi kwa mwaka 2020/21 yalikuwa **shilingi trilioni 34.88** ambapo **shilingi trilioni 22.1** ni matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 12.78** ni matumizi ya maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, jumla ya **shilingi trilioni 24.74** zimetolewa sawa na **asilimia 86.8** ya lengo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 17.42** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambazo zinajumuisha **shilingi trilioni 6.09** kwa ajili ya mishahara, **shilingi trilioni 4.49** Matumizi Mengineyo na **shilingi trilioni 6.84** kugharamia deni la Serikali.Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia Sera za Matumizi kwa mwaka 2020/21.

3.3. Matumizi ya Serikali kwa ujumla

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini kuwa ridhaa ya matumizi iliyotolewa na Serikali katika katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, ni kama ifuatavyo: Ulipaji wa deni la Serikali ni **shilingi trilioni 6.84;** Ulipaji wa mishahara ya watumishi ni **shilingi trilioni 6.09;** Miradi ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme ikiwemo mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere na mradi wa kusambaza umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) **shilingi trilioni 1.02;** Ujenzi na ukarabati wa Reli ikiwemo ujenzi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR) **shilingi trilioni 1.49;** Ujenzi wa barabara, madaraja, na viwanja vya ndege **shilingi trilioni 1.15;** Ulipaji wa madeni yaliyohakikiwa ya Watumishi, Wazabuni na Watoa Huduma, Wakandarasi na Washauri Elekezi shilingi **bilioni 965.1;** Mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, elimumsingi bila ada, uimarishaji wa vyuo vya VETA, kukuza ujuzi kwa vijana na ujenzi wa miundombinu ya elimu **shilingi bilioni 406.6**;

Ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya afya **shilingi bilioni 265.8**; na Miradi ya maji mijini na vijijini **shilingi bilioni 207.5**.

Mheshimiwa Spika, Hatua hii ni ishara nzuri kwa Serikali katika kutekeleza mikakati yake ya kibajeti. Aidha, kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika ulipaji wa malimbikizo ya madeni hasa kwa watumishi na wakandarasi ili kuondoa lawama katika makundi haya, na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

4.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2020/21 NA MAPENDEKEOZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2021/22

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja wa 2021/22 ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2021/22 – 2025/26. Dhima ya Mpango huu ni *Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*. Mpango huu utakuwa na maeneo makuu matano ya kipaumbele ambayo ni: (i) kuchochea uchumi shindani na shirikishi; (ii) kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma; (iii) kukuza biashara; (iv) kuchochea maendeleo ya watu; na (v) kuendeleza rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya utangulizi hapo juu, Kamati ingependa kutoa maelezo, ushauri na maoni yake katika maeneo yafuatayo: -

4.1. Tathmini ya Utekelezaji

4.1.1. Sekta ya Afya

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya afya, huduma za kibingwa, upatikanaji wa vifaa tiba, kinga, dawa na vitendanishi. Hatua hizi zimesaidia; kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka wastani wa vifo 67 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2014/15 hadi vifo 50.3 mwaka 2019/20; kupungua kwa vifo vya akina mama

wajawazito wakati wa kujifungua kutoka vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi vifo 321 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019/20; na kuongezeka kwa watoto wanaozaliwa kwa kuhudumiwa na wahudumu wa afya wenye ujuzi kutoka asilimia 51 mwaka 2015/16 hadi asilimia 80 mwaka 2019/20 pamoja na kupunguza athari kutokana na magonjwa yanayoambukiza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono pia hatua madhubuti zilizochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza ukiwemo ugonjwa wa Uviko 19. Katika Taarifa zake, Serikali imeeleza kuwa mwezi Februari 2021, imeingiza nchini mitambo saba yenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 ya hewa ya oksijeni kwa siku. Mitambo hiyo itasimikwa kwenye hospitali ya Amana na Mikoa ya Dodoma, Geita, Manyara, Mbeya, Mtwara na Ruvuma ambapo kila mtambo mmoja kwenye hospitali hizo utakuwa na uwezo wa kusambaza gesi ya oksijeni katika vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 18. Serikali imeeleza pia kwamba Katika mwaka 2021/22, itaongeza mitambo mingine ya aina hiyo 12.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na mkakati mpya wa upatikanaji wa fedha ili kuweza kukamilisha maboma 8,004 ya Zahanati na maboma 1,500 ya vituo vya afya ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, kamati inaipongeza serikali kwa nia yake kuhakikisha kwamba zinapatikana **shilingi Bilioni 149** kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji kwa ajili ya kugharamia Bima ya Afya kwa wote (Universal Health Care). Hatua hizi zitapunguza changamoto nyingi katika Sekta ya afya. Ni vema Serikali ikahakikisha fedha hizo zinapatikana ili mipango hii mizuri iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa ufanisi.

4.1.2. Sekta ya Elimu

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi kubwa ambazo Serikali inazichukua katika kuboresha miundombinu ya kutolea elimu na kuongeza Bajeti ya Elimu mwaka hadi mwaka. Mwaka 2020/21, Serikali imetekeleza mpango wa

Elimumsingi Bila Ada pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu nchini kwa shule za msingi, shule za sekondari za wanafunzi wenye mahitaji maalum. Hatua hizi zimewezesha kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya msingi kutoka **asilimia 93.3** mwaka 2015 hadi **asilimia 110.6** mwaka 2020; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 196,091 mwaka 2015/16 hadi 320,143 mwaka 2019/20 na elimu ya ufundi kutoka 117,067 mwaka 2015/16 hadi 151,379 mwaka 2019/20; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu nchini kutoka 65,064 mwaka 2015/16 hadi kufikia 87,813 mwaka 2019/20.
Aidha, Serikali imeongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya juu kwa kutoa mikopo ya **shilingi bilioni 464** kwa wanafunzi 142,179 kwa mwaka wa masomo 2020/21 ukilinganisha na **shilingi bilioni 450** zilizotumika kwa wanafunzi 130,883 mwaka 2019/20.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ubora wa miundombinu na ongezeko la idadi ya wahitimu wa elimu ya msingi, sekondari na vyuo vikuu ni dhahiri bado kuna changamoto ya aina na ubora wa elimu yetu. Hata hivyo, Elimu inayotolewa sasa haitoi fursa ya kumjenga mwanafunzi kuweza kujiajiri. Kamati ina maoni yafuatayo;

i. Serikali ikajielekeza zaidi katika kutoa elimu ya ufundi (Technical Education) na ujasiliamali (Enterprenuership);

ii. Kupitia upya mitaala yote na kuiboresha ili kuwawezesha wanafunzi kuanzia ngazi ya elimu ya msingi na sekondari kupata mafunzo ya stadi za kazi katika taaluma mbalimbali ili kuweza kuwajengea uwezo wa kujiajiri wenyewe na kuajiriwa katika viwanda kwa kada ambazo zinahitaji watumishi wengi; na

iii. Serikali iongeze na kuboresha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia hasa vifaa vya ufundi na maabara.

4.1.3. Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

4.1.3.1. Kilimo

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina ikolojia pana yenye ardhi nzuri na yenye rutuba ya kutosha kukidhi uzalishaji wa mazao bora ya chakula na biashara, pia nchi yetu ina nafasi nzuri ya kimasoko kutokana na kuzungukwa na nchi nane (8). Na hivyo kuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata masoko ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Aidha, kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuboresha sekta ya Kilimo nchini kwa kuanzisha Programu mbalimbali za kilimo kama vile ASDP I na sasa ASDP II, kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakulima. Hatua hizi zimesaidia kuongeza uzalishaji wa baadhi ya mazao nchini. Hata hivyo pamoja na mafanikio hayo bado kilimo kinakabiliwa na changamoto nyingi zinazopelekea kilimo chetu kutokuwa na tija. changamoto hizo ni pamoja na; uhaba wa masoko endelevu ya uhakika kwa mazao ya kilimo, miundombinu hafifu katika maeneo ya uzalishaji, huduma duni za Ugani, kutozingatia kanuni bora za kilimo, matumizi hafifu ya pembejeo na zana za kilimo, uwekezaji mdogo wa viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mabadiliko ya tabianchi.

Hatua zifuatazo zinapendekezwa ili kutatua changamoto za kilimo kwa lengo la kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakuwa na tija;

i. Kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo, zana za kilimo na mbegu bora kwa wakati na kwa gharama nafuu, kudhibiti ubora wa pembejeo za kilimo na kuimarisha masoko ya mazao;

ii. Kuweka Mazingira wezeshi katika uwekezaji kwenye mnyororo wa thamani.

iii. kuhamasisha kilimo cha mkataba (Contract farming) na kilimo kitalu (block farming);

iv. Kuboresha Upatikanaji na mifumo endelevu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa Kuboresha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo;

v. Kuboresha mifumo ya upatikanaji wa taarifa za masoko ya mazao; na Kuongeza mauzo ya mazao na bidhaa za kilimo ndani na nje ya nchi

vi. Kuhakikisha kunakuwa na Upatikanaji wa mitaji kwaajili ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo hii ni pamoja na kuimarisha benki ya maendeleo ya kilimo TADB.

vii. Kuboresha miundombinu na teknolojia katika kilimo cha umwagiliaji kwa kusimamia hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na mazingira

viii. kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo, vyuo vya mafunzo ya kilimo, ufundi stadi, udhibiti wa ubora wa pembejeo na zana za kilimo; Kuanzisha Programu za kitaifa, kikanda na kimataifa za kuendeleza Sekta ya Kilimo; Ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na nishati ya umeme ya uhakika unaovutia wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo; Kuimarisha mifumo ya teknolojia, habari na mawasiliano; na Utashi wa kujitosheleza kwa bidhaa za ndani ikiwemo sukari, mafuta ya kula na ngano.

ix. Kuboresha miundombinu ya kilimo kwa mfano kujenga maabara zenye uwezo wa kutoa ithibati za mazao ya kilimo kitaifa na kimataifa na miundombinu ya baridi (Cold chains)

x. Serikali ihakikishe inadhibiti magonjwa mbalimbali katika kilimo

xi. Serikali itenge ne kupima ardhi ya kilimo pamoja na kuongeza bajeti ya Serikali ya kilimo.

4.1.3.2. Uvuvi

Mheshimiwa Spika, Serikali ilieleza kuwa katika mwaka 2020/21 imeanza kulifufua Shirika la Uvuvi Tanzania (Tanzania

Fisheries Corporation - TAFICO). Hatua hizo za kulifufua shirika hilo zinaenda sambamba na ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Mbegani pamoja na ununuzi wa meli tisa (9) za uvuvi. Pamoja na hatua hizo nzuri za Serikali, Kamati bado inapendekeza masuala yafuatayo;

i. Kuweka vivutio maalumu kwa wawekezaji wa viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi

ii. Kuweka mazingira bora na kuhamasisha wananchi kufuga samaki;

iii. Kuhakikisha kwamba vifaranga vya samaki, chakula cha samaki na vifaa vya uvuvi vinapatikana kwa bei nafuu;

iv. Kuweka mazingira bora yatakayowezesha usafirishaji wa mazao ya Samaki.

v. Serikali iendeleze mapambano dhidi ya uvuvi haramu na kudhibiti utoroshaji wa mazao ya uvuvi.

vi. Serikali ihakikishe kuwa vifaa vya uvuvi vinapatikana kwa gharama nafuu na hivyo kuweza kusaidia kukuza uchumi wa bluu.

4.1.3.3. Mifugo

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya 2020 katika Mwaka 2020/21 idadi ya mifugo hapa nchini inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019/20 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka **milioni 33.4** hadi **milioni 33.9,** mbuzi kutoka **milioni 21.29** hadi **milioni 24.5** na kondoo kutoka **milioni 5.65** hadi **milioni 8.5.** Pamoja na kuwa na idadi hii kubwa ya mifugo Mchango wa sekta ya mifugo ni mdogo ukilinganishwa na rasilimali ya mifugo iliyopo Nchini. Kwa sasa Sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo; kutokuwepo kwa masoko ya uhakika ya mifugo na mazao yake, magonjwa ya mifugo, biashara ya mifugo kufanyika bila kuzingatia taratibu zote, migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na

watumiaji wengine wa ardhi, uvamizi wa maeneo ya malisho, kutotumia kikamilifu ranchi za Taifa, uingizwaji holela wa mazao ya mifugo toka nje ya nchi pamoja na uuzaji wa madawa bandia ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza tija katika sekta ya mifugo Kamati inapendekeza mambo yafuatayo yafanyiwe kazi;

(i) Kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya malisho, chakula na maji kwa ajili ya mifugo;

(ii) Kutenga na kupima maeneo ya malisho katika maeneo mbalimbali nchini

(iii) Kuimarisha huduma za utafiti wa mifugo, huduma za ugani na mafunzo kwa wafugaji na maafisa ugani;

(iv) Serikali ifanye uhakiki wa mipaka ili kutatua changamoto kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi;

(v) Kuanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya mazao ya mifugo;

(vi) Serikali iongeze ulinzi wa viwanda vya ndani vya mazao ya mifugo na pembejeo;

(vii) Serikali iagize Mitamba nje ya nchi na kuwauzia wananchi kwa ruzuku pamoja na kuboresha Mitamba katika ranchi za taifa

Mheshimiwa Spika, kuhusu sekta ya maziwa, kati ya Viwanda 99 vya usindikaji maziwa vilivyopo nchini, kuna viwanda 5 vikubwa vyenye uwezo uliosimikwa (Instaled Capacity) wa kusindika maziwa yatakayodumu kwa muda mrefu (UHT) jumla ya lita takribani 350,000 kwa siku. Hata hivyo kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo; Uzalishaji mdogo wa maziwa ghafi na uchache wa miundombnu ya ukusanyaji maziwa kutoka kwa wafugaji; uzalishaji wa viwanda hivyo ni chini ya asilimia 35% ya uwezo uliosimikwa. Zaidi ya asilimia 90% ya maziwa yanayozalishwa Nchini yanategemea

ng'ombe wa asili wanaofugwa na wafugaji wanao hamahama. Mfumo huu wa ufugaji pamoja na kuongeza gharama ya ukusanyaji maziwa, pia hautoi uhakika wa upatikanaji maziwa hayo muda wote. Hivyo kuwa ni sehemu ya changamoto katika uwekezaji wa viwanda vya usindikaji wa bidhaa za maziwa. Aidha, gharama ya uzalishaji wa lita moja ya maziwa kwa ng'ombe wa kisasa Nchini Tanzania ni kati ya **Shilingi 540** hadi **Shilingi 600**. Gharama hiyo ni zaidi ya mara mbili hadi tatu ya gharama za uzalishaji wa maziwa ukilinganisha na Nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi mbili za gharama za uzalishaji na mfumo wa ufugaji zimepelekea sekta ya maziwa kutokuwa ya ushindani ukiinganisha na nchi jirani, hivyo kupunguza ushindani wa bidhaa za maziwa zinazozalishwa Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kutatua changamoto hizo, Kamati inashauri yafuatayo: -

i. Kuwepo na mfumo wa uzalishaji maziwa utakaopunguza gharama za uzalishaji; Kwa mfano uanzishwaji wa mashamba madogo ya ng'ombe wa maziwa (Small Scale commercial dairy Farms).

ii. Kuhakikisha kwamba kunakuwa na upatikanaji wa vyakula vya ziada vya mifugo kwa kuanzisha vituo vya kuuzia vyakula vya mifugo (animal feeds resource centers). Hatua hii itapunguza gharama za ufugaji na bei ya maziwa.

iii. Serikali kuwawekea mazingira wezeshi ya ufanyaji kazi kwa maafisa mifugo ili waweze kuzungukia mashamba ya mifugo ya wananchi na kutoa ushauri kwa wafugaji.

4.1.4. Sekta ya Maji

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji na hivyo kuona ipo haja ya kuongeza fedha za kugharamia miradi ya maji kwa kubuni vyanzo mbadala vya mapato

hususani katika maeneo ambayo yana uhaba mkubwa wa maji. Kwa hatua hii ni dhahiri miradi ya maji ambayo imekwama muda mrefu sasa itakamilika na maeneo ambayo hayajafikiwa na maji yatafikiwa kwa wakati. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizi ni vema Serikali ikaongeza usimamizi katika miradi yake inayoitekeleza ili ilete tija inayotazamiwa kwa kujengwa kwa ubora na kwa kuzingatia thamani ya fedha.

4.1.5. Sekta ya Miundombinu

4.1.5.1. Barabara

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha chanzo maalumu kupitia tozo ya mafuta ili fedha zitakazopatikana zielekezwe TARURA kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara. Hatua hii itasaidia kuimarisha mtandao wa barabara zinazosimamiwa na TARURA unaokadiriwa kufikia **kilometa 108,946.2.** Jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa barabara zitakazojengwa ziwe na ubora unaotakiwa kwa kuzingatia thamani ya fedha. Aidha, ni vema Serikali ikatoa kipaumbele kwa barabara ambazo zinaunganisha maeneo yenye fursa za kiuchumi.

4.1.5.2. Reli

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kukarabati na kujenga miundombinu ya reli nchini. Taarifa za Serikali zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021, Serikali imeendelea kusimamia ujenzi wa reli ya Dar es Salaam hadi Mwanza kwa kiwango cha Standard Gauge (SGR). Ujenzi wa reli ya Kati kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) umekamilika kwa **asilimia 91** na kutoka Morogoro hadi Makutupora (km 422), ujenzi umekamilika kwa **asilimia 60.2**. Serikali pia kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeendelea kusimamia, kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za usafiri wa reli yenye jumla ya urefu wa Kilometa 2,706 kwa ajili ya kuhudumia nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kutambua juhudi hizi za Serikali, Kamati inaishauri Serikali kutafuta fedha ili iweze kujenga kwa

wakati mmoja na kwa haraka reli ya kati kwa kiwango cha Standard Gauge kwa vipande vya Makutupora – Tabora (km 294) na Tabora – Isaka (km 133). Maeneo mengine yanayoendelea kutafutiwa fedha za ujenzi ni pamoja na Tabora – Kigoma (km 411), Keza - Ruvubu (km 36), Uvinza-Musongati (km 200), Kaliua – Mpanda - Karema (km 321) na Isaka - Rusumo (km 371).

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua umuhimu wa Reli ya TAZARA katika uchumi wa nchi yetu. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa Reli hii bado haijaleta manufaa kwa kiwango kikubwa kinachotakiwa. Reli hii ambayo ni ya kiwango cha kimataifa *(standard gauge)* ina umuhimu mkubwa sana kwa uchumi wa Tanzania hasa ikitumiwa ipasavyo na nchi za Malawi, Zambia na Congo DRC ya kusini. Hivyo, Kamati inaishauri tena Serikali mambo yafuatayo;

i. Serikali ikamilishe haraka mapitio ya Mkataba na Sheria inayosimamia Reli ya TAZARA ili kutatua changamoto zilizopo na kuiwezesha Tanzania kuisimamia na kuiendesha reli hiyo pamoja na miundombinu yake kwa upande wa Tanzania;

ii. Serikali itatue haraka changamoto za kimenejimenti zinazoikabili TAZARA; na

iii. Serikali ione uwezekano wa kuiunganisha Reli ya TAZARA na reli nyingine ili kuwa na mtandao mmoja wa Reli nchi nzima.

4.1.5.3. Usafiri wa Anga

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuboresha miundombinu ya usafiri wa anga kwa kununua ndege zinazotumiwa na Shirika letu la ATCL, kurekebisha menejimenti ya ATCL pamoja na kujenga na kukarabati viwanja vya ndege. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia TANROADS imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege vya Kigoma, Mpanda, Songwe, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga, Mwanza, Arusha na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Kufuatia changamoto ya kushuka kwa idadi ya watalii wanaokuja nchini, Kamati inalishauri Shirika la Ndege kuongeza safari zake za ndani ili kuongeza idadi ya miruko na hivyo kupunguza hasara kwa kusimamisha ndege. Aidha, ATCL itumie fursa ya kusafirisha mizigo hasa matunda, mbogamboga, maua na samaki kutoka hapa nchini kwenda nchi za nje badala ya kuachia ndege za mashirika mengine.

4.1.5.4. Bandari

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua juhudi za Serikali katika kuboresha bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga pamoja na bandari zilizopo katika maziwa makuu. Kamati ilielezwa kwamba kwa sasa TPA inasimamia jumla ya Bandari rasmi 89 zinazotambuliwa na Sheria ya Bandari na Bandari nyingine 23 zinazohudumiwa na TPA lakini hazijaainishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bandari Sura 166. Vilevile ilielezwa kwamba, hadi Juni 2020, jumla ya Bandari 693 zisizohudumiwa na TPA zilikuwa zimetambuliwa. Bandari hizi ziko katika mwambao wa bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Taratibu za kuidhinisha bandari hizo kwa mujibu wa sheria zinaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliieleza Kamati kuwa TPA imeanza kuhudumia baadhi ya Bandari hizo 693 kwa kuweka miundombinu muhimu za shughuli za kijamii na kibiashara kwani zilikuwa zinapitisha shehena kubwa bila kutambuliwa na baadhi kukosesha mapato na kuhatarisha usalama mipakani. Kamati bado inaona eneo hili linaweza kuwa ni uchochoro mkubwa wa kupoteza mapato ya Serikali lakini pia haijakaa sawa kwa usalama wa nchi yetu hivyo Kamati inaishauri Serikali kufanya haraka mchakato wa kurasimisha Bandari hizi na nyingine kuzifunga kabisa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kuliibuka mjadala mkubwa baada ya Serikali kufanikiwa kubaini wizi mkubwa wa mafuta yaliyokuwa yakisafirishwa kwa bomba kutoka Bandrini kwenda kwa Makampuni ya mafuta. Ni vema Serikali ikatafuta suluhisho la kudumu ili kutatua changamoto ya

upotevu wa mafuta Bandarini na kwenye bomba linalosafirisha mafuta kutoka bandari kwa kukamilisha haraka matengenezo ya *Flow Meter* bandarini na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa bomba linalosafirisha mafuta ili kubaini endapo kuna hujuma zozote zimefanyika. Kamati pia inaishauri Serikali kukamilisha haraka mpango wake wa kuanzisha utaratibu wa kutunza mafuta kwenye kila kanda mfano Dar es salaam, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Mtwara, Mbeya na Tanga. Mafuta haya yatanunuliwa kwa utaratibu wa sasa wa pamoja (Bulk Procurement) hivyo kuipa nchi yetu usalama pale kunapotokea mtikisiko wa bei au majanga yatakayopelekea kushindwa kupata mafuta kwa wakati kutoka nje ya nchi.

4.1.6. Sekta ya Viwanda na Biashara

Mheshimiwa Spika, Ili kulinda viwanda vyetu na kulinda mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya Viwanda ni vema Serikali ikaja na mkakati utakaoviwezesha Viwanda vyetu vya ndani kuwa shindani na kuzalisha zaidi. Hili linaweza kufanikiwa kwa kuzuia uingizaji wa bidhaa kwa wingi (Dumping) pamoja na kuzuia kuingiza bidhaa zisizo na ubora. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kukamisha haraka mchakato wa kuleta Bungeni Sheria ya Kujilinda Dhidi ya Athari za Biashara (Trade Remedies Act) pamoja na kuweka mazingira bora yatakayowezesha biashara ya ndani.

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya Mipakani yanatoa mchango mkubwa sana wa uchumi kupitia biashara, mfano halisi ni Mipaka ya Namanga na Tunduma. Hata hivyo, baadhi ya maeneo ya mipaka yetu na nchi jirani bado hayajaleta mchango unaostahili wa manufaa ya kibiashara na kiuchumi. Kamati inaishauri Serikali ifanye tathmini ya maeneo hayo katika mipaka yetu yote ili kuweka mazingira yatakayowezesha kufanyika biashara katika maeneo hayo. Kwa mfano kwa kujenga vituo katika mipaka na masoko mbalimbali.

4.1.7. Sekta ya Utalii

Mheshimiwa Spika, Sekta ya utalii ni miongoni mwa sekta za kiuchumi ambazo zilikumbwa na changamoto za ukuaji katika kipindi cha mwaka 2020/21 kutokana na janga la Homa Kali ya Mapafu lililoikumba dunia kuanzia mwishoni mwa mwaka 2019. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa na mataifa mbalimbali duniani katika kujikinga na janga hilo ikiwemo kufunga mipaka, kusitisha safari za ndege na kuwafungia watu ndani zilichangia kutokukua vizuri kwa sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono mpango wa Serikali wa mwaka 2021/22, kwa kuendelea kuimarisha sekta ya utalii na usalama wa watalii wanaoingia nchini, kuongeza kasi zaidi ya kutangaza vivutio vya utalii kama vile Mlima Kilimanjaro, Hifadhi ya Serengeti, Ngorongoro na maeneo mengine ya kihistoria ndani na nje kwa kutumia balozi zetu, tovuti na sekta ya michezo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kuweka mazingira bora yatakayowezesha kuongezeka kwa shughuli za utalii kanda ya kusini na nyanda za juu kusini kwa kukamilisha haraka ujenzi wa viwanja vya ndege, kujenga miundombinu ya barabara, kuhamasisha ujenzi wa hoteli na kisha kuanzisha *package* za utalii.

4.1.8. Sekta ya Ardhi na Mazingira

4.1.8.1. Ardhi

Mheshimiwa Spika, Ardhi ni maliasili isiyoongezeka, hivyo, ni muhimu kuwa na mipango thabiti ya kuhakikisha kwamba tunapanga matumizi bora ya ardhi kwa vizazi vya sasa na Vizazi vijavyo. Endapo hatutapanga matumizi bora ya ardhi kwa kuangalia ongezeko la watu ni wazi kwamba vizazi vijavyo havitakuwa na maeneo ya hifadhi za misitu, makazi na maeneo ya shughuli za kiuchumi. Hivyo, ni lazima maamuzi yafanyike sasa ya kulinda misitu, mabonde na rasilimali maji ambazo zitaimarisha ustawi wa mazingira ambayo ni kiungo muhimu katika maendeleo endelevu. Vilevile, Serikali ione umuhimu wa kuingiza kilimo na uhifadhi wa misitu katika miji (urban agriculture and urban forestry).

4.1.8.2. Mazingira

Mheshimiwa Spika, Karibu **asilimia sabini (70%)** ya Wat anzania wanaishi **vijijini** wakitegemea Kilimo na maliasili za asili katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Kutokana na utegemezi mkubwa wa shughuli hizi, wameanza kuharibu mazingira ikiwa ni pamoja na vyanzo vya maji, misitu na uoto wa asili. Uharibufu huu usipodhibitiwa utahatarisha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mazingira unaweza kuwa suluhisho la kukabiliana na uharibifu huu. Hivyo ni vema Serikali ikaifanyia marekebisho Sheria ya Mazingira sura ya 191 iliyoanzisha mfuko huu ili kuuwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kutafuta vyanzo vya fedha za kufadhili miradi ya kutunza na kuboresha mazingira. Vilevile, ili kulinda mazingira yetu Kamati inaishauri Serikali iendelee kuhamasisha kilimo bora pamoja na kuendeleza programu za upandaji miti nchi nzima kila mwaka; na kuongeze usimamizi na ulinzi katika vyanzo vya maji na misitu.

5.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA MIFUKO NA MAPITIO YA UTENDAJI KAZI WA BAADHI YA MASHIRIKA YA UMMA PAMOJA NA UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA MASHIRIKA YA UMMA

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura 439 kifungu cha 9 (f) kinaipa mamlaka Kamati kukutana na Mashirika ya Umma ili kuangalia mizania yao ya fedha pamoja na kuangalia endapo mashirika hayo yanafuata misingi ya fedha za umma na ya sheria nyingine za Nchi. Kutokana na takwa hilo la kisheria Kamati ilikutana na kufanya Tathimini ya utendaji kazi wa mifuko maalumu na Mashirika ya Umma ili kutekeleza takwa hilo la kisheria. Masuala yafuatayo yalibainika:-

5.1. Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mifuko Maalumu (Ring-fenced Funds)

5.1.1. Mfuko wa Maji

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa maji una vyanzo vikuu viwili vya fedha, fedha zinazotokana na tozo za mafuta ya petroll na

dizeli na fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali. Kamati imebaini kwamba utolewaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maji kwa miaka miwili mfululizo imekuwa ikitegemea zaidi chanzo cha tozo ya Mafuta ya petroli na Dizeli kuliko fedha kutoka Mfuko mkuu wa Serikali kwa sababu fedha hizo zimekuwa hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Hadi kufikia mwezi Aprili 2021 fedha zilizotolewa kutoka mfuko mkuu wa Serikali ni **asilimia 37** tu ya lengo la mwaka na fedha zilizotolewa kutoka kwenye tozo ya mafuta kwenda kwenye mfuko wa maji ni **asilimia 87** tu ya lengo la mwaka. Mwenendo wa utolewaji wa fedha hafifu kama huu umejitokeza pia kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambapo Tozo ya mafuta kwenda kwenye Mfuko wa maji ilikuwa ni **asilimia 74** na fedha kutoka Mfuko mkuu wa Serikali ilikuwa ni **asilimia 30** tu. (Rejea Jedwali Na.5 Hapo chini linaonyesha mwenendo huu.)

Jedwali Na.5 - Mwenendo wa Bajeti ya Utekelezaji wa Bajeti ya Maji

	Bajeti	Fedha zilizotolewa	Asilimia
Chanzo	**2019/20**	**2019/20**	**%**
Tozo ya mafuta	175,912,837,000.00	153,177,713,491.37	**87**
Mfuko-Serikali	173,586,163,000.00	64,144,612,334.05	**37**
Ndani	**349,499,000,000.00**	**217,322,325,825.42**	**62**
	2020/21	**2020/21**	
Tozo ya mafuta	175,912,837,000.00	131,742,995,737.13	**74.9**
Mfuko-Serikali	173,536,163,000.00	52,511,380,538.39	**30.3**
Ndani	**349,449,000,000.00**	**184,254,376,275.52**	**52.7**

Chanzo: Wizara ya Maji

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kufanya mabadiliko katika sheria ya ***"The road and fuel toll Act Cap 220" kifungu cha 4.A na kuongeza kifungu kidogo cha (c)*** ili kuhakikisha kwamba bei za mafuta zinaposhuka tofauti ya bei iliyopo na iliyoshuka itumike kutunisha mfuko wa maji kwa sababu uzoefu umeonyesha hata bei za mafuta zinaposhuka bei ya huduma na bidhaa zinazotegemea mafuta huwa hazishuki kwa kiasi kikubwa. Aidha, kamati imebaini kwamba RUWASA haina chanzo mahsusi cha mapato na badala yake mapato ya mfuko huu hulazimika kugawanywa mijini na vijijini. Hivyo, ni maoni ya

Kamati kuwa fedha hizi zikipatikana zielekezwe moja kwa moja RUWASA. Hatua hii itasaidia katika kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji vijijini ukizingatia kuwa katika mwaka huu wa fedha Serikali imejielekeza katika kuongeza fedha za kugharamia miradi ya maji.

5.1.2. Mfuko wa Barabara

Mheshimiwa Spika, Chanzo cha Mfuko wa barabara kinatokana na fedha kutoka Serikali kuu pamoja na Tozo ya mafuta. Kamati imebaini kwamba chanzo kutoka Tozo za mafuta kimekuwa kikifanya vizuri tofauti na kile kutoka Mfuko mkuu wa Serikali Aidha, kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta kwa kuongeza ushuru wa barabara kwa shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini kupitia **TARURA**. Hatua hii itasaidia kuongeza upatikanaji wa fedha kwa **TARURA** tofauti na ilivyokuwa awali ambapo **TARURA** walikuwa wakigawana mapato hayo hayo na **TANROADS**.

Jedwali Na. 6: Bajeti na Mgawo wa Fedha za Mfuko wa Barabara (Shilingi)

	Bajeti	Mgawo	Mafanikio
2018/19			
Tanroads	567,625,475,160	476,468,798,639	83.9%
Tarura	243,267,550,920	204,200,485,720	83.9%
Mowtc	63,069,497,240	52,940,977,627	83.9%
Po-Ralg	27,029,727,880	22,688,942,858	83.9%
Rf Admin.	7,815,748,800	6,560,594,273	83.9%
Jumla	**908,808,000,000**	**762,859,799,116**	**83.9%**
2019/20			
Tanroads	524,103,709,140	486,423,490,626	92.8%
Tarura	224,615,747,880	208,467,099,069	92.8%
Mowtc	58,233,745,460	54,047,054,514	92.8%
Po-Ralg	24,957,305,320	23,163,011,008	92.8%
Rf Admin.	7,216,492,200	6,697,660,547	92.8%
Jumla	**839,127,000,000**	**778,798,315,764**	**92.8%**
2020/21			
Tanroads	572,604,616,096	479,674,550,423	83.8%
Tarura	245,401,978,709	205,638,414,102	83.8%
Mowtc	63,622,735,122	53,297,172,542	83.8%
Po-Ralg	27,266,886,523	22,805,340,200	83.8%
Rf Admin.	7,884,312,549	6,763,066,167	83.8%
Jumla	**916,780,529,000**	**768,178,543,434**	**83.8%**

Chanzo: Road Fund Board

5.1.3. Mfuko wa Maendeleo ya Reli

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa matumizi ya mfuko wa reli Kamati imebaini kwamba kwa kiasi kikubwa matumizi

ya mfuko huu yameelekezwa katika Reli ya kisasa ya SGR jambo ambalo kamati haina shida nalo, ila inaona ni vyema miundombinu mingine ya Reli ya Kati nayo ikawa inapata mgao ili kuendelea kuhakikisha inatoa huduma kwa sababu Reli ya SGR haifiki katika maeneo hayo. Mfano Reli ya Tabora-Kaliua-Kigoma, Dar-es-Salaam-Tanga-Moshi-Arusha na Tabora-Kaliua- Mpanda. Endapo fedha zote zitaelekezwa katika SGR na kusahau maeneo haya tutapoteza manufaa ambayo yanapatikana hivi sasa hasa ya usafirishaji wa mizigo. Jedwali Na.7 Linaonyesha mwenendo wa makusanyo ya Mfuko wa Reli.

Jedwali Na.7: Mwenendo wa makusanyo na fedha zilizotolewa kwa Mfuko wa Reli

	Bajeti	Fedha zilizotolewa	Asilimia %
Mwaka wa Fedha	**2018/19**	**2018/19**	
Jumla ya Fedha	252,639,947,853	247,848,863,445.23	98.1
Mwaka wa Fedha	**2019/20**	**2019/20**	
Jumla ya Fedha	255,700,000,000	249,888,462,566.57	97.73
Mwaka wa Fedha	**2020/21**	**2020/21(Hadi/Aprili)**	
Jumla ya Fedha	289,678,923,000	202,869,754,564.00	70.03

Chanzo: *Taarifa ya TRC*

5.2. **Mapitio ya Utendaji Kazi wa Baadhi ya Mashirika ya Umma pamoja na Utekelezaji wa Bajeti za Mashirika ya Umma.**

5.2.1. Shirika la Bima la Taifa (National Insurance Cooperation-NIC)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba pamoja na Serikali kufanya uamuzi wa kulipa shirika hili kazi ya kutoa Bima kwa miradi mikubwa na ya Kimkakati Shirika hili halina mtaji wa kutosha na hivyo kulazimika kutoa Bima hizo kwa njia ya mtawanyo. Aidha, Kamati imebaini Shirika linaidai Serikali jumla ya **Shilingi bilioni 40.3** ambazo hazijalipwa na hivyo kuharibu mizania ya Shirika. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kuliongezea shirika hili mtaji

na kulipa madeni yote ambayo linaidai Serikali ili lijiimarishe na kufanya kazi kwa ufanisi**.** Aidha, Kamati inashauri NIC vilevile iweze kutoa bima kwa mikopo inayotolewa na mabenki ili iweze kupanua biashara yake.

5.2.2. Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation-TASAC).

Mheshimiwa Spika, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation – TASAC) lilianzishwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415. TASAC ilianza rasmi kutekeleza majukumu yake tarehe 23 Februari, 2018 baada ya Tangazo la Serikali Na 53 la Mwaka 2018. Mara tu TASAC ilipoanza, ilitekeleza majukumu ya udhibiti wa usafiri majini na usimamizi wa ulinzi na usalama wa usafiri majini na kuzuia uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za usafiri majini. Majukumu hayo awali yalikuwa chini ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) na yalihamishiwa TASAC kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 68 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya TASAC majukumu yake ni pamoja na kufanya kazi za uwakala wa meli, uhakiki wa shehena, uhudumiaji wa nyaraka za uwakala wa meli na uwakala wa forodha kwa shehena na maeneo yenye maslahi kwa Taifa (Shipping Business Functions). Majukumu haya yameleta taharuki kubwa kwenye tasnia ya uwakala wa forodha nchini kwa sababu TASAC ambae ni msimamizi (Regulator) wa masuala ya uwakala wa forodha naye anafanya kazi za uwakala wa forodha kwa misingi ya utawala bora suala ambalo kamati inaona si sawa. Kamati inaishauri Serikali kwamba kufanya mabadiliko kwenye kifungu cha 7 (1), a cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415. Kwa lengo la kuweka ukomo kwa TASAC kujishughulisha tu na mizigo na bidhaa nyeti za Serikali kama vile Silaha, Nyara za Serikali, Madini, na Mitambo inayohusiana na Madini katika Uchimbaji na Uandaaji. Shughuli nyingine za masuala za uwakala wa

forodha ziendelee kwa sekta binafsi na TASAC aendelee na shughuli zake za usimamizi.

5.2.3. Mamlaka ya Bandari Tanzania (Tanzania Ports Authority-TPA)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba katika kipindi cha Julai-Desemba 2020, TPA ilfanikiwa kuhudumia tani za uzito (DWT) **milioni 8.955** sawa na **asilimia 95** ya lengo la kuhudumia tani za uzito **milioni 9.430**. Idadi ya meli za mwambao zilizohudumiwa zilikua **asilimia 76** ya lengo la kuhudumia meli 1,098 na uzito wa meli hizo (GRTs) ulifikia **asilimia 82.8** ya lengo. Utendaji huo umeiwezesha Mamlaka kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 453.686** ikilinganishwa na lengo la kukusanya **shilingi bilioni 582.203**. Mapato haya ni sawa na **asilimia 78** ya lengo la kipindi hicho. Aidha, matumizi yalikuwa **shilingi bilioni 144.206** sawa na **asilimia 39** ya lengo la kutumia **shilingi bilioni 367.637**.

Mheshimiwa Spika, ukitizama ulinganisho wa mapato na matumizi hapo juu utagundua kwamba Mamlaka ya Bandari wametumia **asilimia 39** tu ya mapato yao na hii ndio sababu kubwa ya ucheleweshaji wa upakuaji wa mizigo bandarini. Sababu kuu ikiwa ni kwamba Serikali haiwekezi katika bandari hasa katika vifaa vya mfumo wa *Electronics Data Interchange System* na vifaa vya kupakia na kupakulia shehena ya mizigo na badala yake inachukua mapato yote. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuwekeza katika Bandari ya Dar es salaam na bandari nyingine kama vile Tanga na Mtwara kwa kuweka vifaa vya kisasa vya kupakia na kupakulia shehena ya mizigo pamoja na ujenzi wa matanki ya kuhifadhia mafuta kwa bandari ya Tanga na Mtwara.

5.2.4. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (Tanzania Communication Regulatory Authority)

Mheshimiwa Spika, Kamati imepitia ukusanyaji wa mapato kupitia mfumo wa TTMS na kujiridhisha kwamba mfumo huo unafanya kazi kwa ufanisi. Hata hivyo, kamati imegundua kwamba kwa sasa mfumo huo hauna uwezo wa kukusanya

mapato yatokanayo na simu zinazotumia data mfano kupitia whatsapp, twitter, we chat, zoom na mingineyo. Hivyo, kupelekea Serikali kupoteza mapato kwa njia hii. Kutokana na kuwa hivi sasa mfumo huu haujaweza kukuksanya mapato hayo na kwa kuwa ni vigumu kuboresha mfumo ili uendane na mahitaji hayo ya sasa, Kamati inaishauri Serikali kulifanyia tafiti pendekezo la kuweka tozo maalum kwenye bei za data hasa ukizingatia ni eneo ambalo Serikali halijaweza kukusanya mapato yoyote. kuangalia uwezekano wa kuweka tozo maalumu kwenye bei za data (*mb)* ili fedha zitakazopatikana zipelekwe katika kugharamia Bima ya Afya kwa wote.

5.2.5. Utendaji Kazi pamoja na Majukumu ya TIRDO, TEMDO na CAMARTEC

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kukutana kwa pamoja na Mashirika ya TIRDO, TEMDO na CAMARTEC na kubaini masuala yafuatayo :-

i. Mashirika haya yote ni muhimu kwenye kuendeleza uchumi wa viwanda;

ii. Kuna uhaba mkubwa sana wa fedha kwa ajili ya utafiti na kuendeleza teknolojia zinazogunduliwa ambazo nyingi ni za bei nafuu na zinaendana na mazingira ya Taifa letu;

iii. Ugunduzi unaofanyika unakosa viwanda vya ndani vyenye uwezo wa kuzalisha bidhaa kwa wingi (Mass Production) ili ziwafikie wananchi; na

iv. Mashirika haya hayajulikani kwa wananchi pamoja na umuhimu wake katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini masuala hayo kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: -

i. Kuangalia uwezekano wa kuyaunganisha mashirika hayo ili liwe shirika moja lenye nguvu na litakalotengewa bajeti ya kutosha kwa maendeleo ya viwanda;

ii. Ziandaliwe ajenda za utafiti za kitaifa mahsusi kwa ajili ya kuendeleza viwanda nchini; na

iii. Kulinda ugunduzi na kuhakikisha kwamba ugunduzi huu unatumiwa na watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/22 kati ya vipaumbele ilivyojiwekea ni pamoja na kuimarisha uzalishaji viwandani kwa kuimarisha taasisi za tafiti na maendeleo ya viwanda na kilimo zikiwemo taasisi hizi. Aidha, ili nia hii njema iweze kufanikiwa Serikali ione haja ya kuzisaidia taasisi hizi kifedha. Katika mwaka wa fedha 2021/22 taasisi za utafiti zimetengewa fedha za ndani **shilingi 3,500,000,000** tu kiwango ambacho Kamati inaona hakijitoshelezi hasa ukizingatia kazi kubwa na majukumu ilizo nazo taasisi hizi. Kamati inaamini endapo mapendekezo haya yatafanyika kikamilifu taifa litaona umuhimu na manufaa ya mashirika haya ambao hivi sasa hauonekani kwa kiwango kilichokusudiwa.

6.0. SURA YA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti ya Serikali inatoa hali halisi ya mwelekeo wa Bajeti ya Serikali pamoja na utekelezaji wa malengo ya Bajeti yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, bajeti ya Serikali ya mwaka 2021/22 ni bajeti ya kwanza kutekelezwa ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 2021/22 - 2025/26 ambayo ndio itajenga misingi ya utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Tatu na Dira ya Maendeleo ya Taifa. Hivyo, ufanisi wa utekelezaji wa bajeti hii inayopendekezwa itatoa taswira ya mwenendo wa nchi kufikia malengo na shabaha ya uchumi jumla ifikapo 2025/26.

Mheshimiwa Spika, uandaaji wa kiwango cha ukomo wa bajeti umezingatia matumizi ya miradi inayoendelea; yaliyolindwa; vibali vya miradi mipya; miradi yenye vyanzo maalum; vibali vya ajira mpya na upandishwaji wa madaraja

kwa watumishi pamoja na mahitaji ya Mamlaka ya Uhifadhi zilizoathiriwa nakushuka kwa biashara katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali imepanga kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 36.33** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 4** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/21 ya **shilingi trilioni 34.88** Kati ya fedha hizo, **shilingi trilioni 23.00** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni **asilimia 63** ya bajeti yote na **shilingi trilioni 13.33** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na **asilimia 37** ya bajeti yote. Bajeti ya maendeleo inajumuisha **shilingi trilioni 10.37** fedha za ndani na **shilingi trilioni 2.96** fedha za nje.

a) Sera za Mapato

Mheshimiwa Spika, Serikali inalenga kukusanya kiasi cha **shilingi trilioni 25.17**. Kati ya fedha hizo, Mapato ya kodi (TRA) ni **shilingi trilioni 22.18**; Mapato yasiyo ya kodi **shilingi trilioni 2.99**; na Mapato ya Halmashauri **shilingi bilioni 863.86**. Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio 2015 kwa mwaka 2021/22 unatarajiwa kuwa **shilingi trilioni 129.1.** Kati ya kiasi hicho Mamlaka ya Mapato pamoja na Serikali za mitaa zitaweza kukusanya **asilimia 17.84** tu. Ili Serikali iweze kufikia malengo hayo ni lazima ijizatiti kikamilifu ili kufikia ukusanyaji wa mapato unaokusudiwa kwa kuboresha taratibu za kiutawala, mifumo ya ukusanyaji sambamba na kupanua wigo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Serikali inategemea kupata kiasi cha **shilingi trilioni 2.96**. Kati ya fedha hizo Serikali haitegemei kupokea kiasi chochote kutokana na Misaada ya kibajeti (GBS) kutokana na kufika ukomo wa Mkataba wa Programu ya GBS katika sekta ya Fedha na Uchumi kutoka Jumuiya ya Ulaya iliyojumuisha nchi za Denmark na Sweden, badala yake fedha hizo zitakuwa zinapelekewa moja kwa moja kwenye Miradi; misaada na mikopo ya masharti nafuu ya Miradi ni **shilingi trilioni 2.67**; misaada na mikopo nafuu ya kisekta ni **shilingi bilioni 282.31.** Hivyo, Kamati inashauri Serikali

kuendelea kufanya mazungumzo na Washirika na kushawishi kuendelea na utaratibu wa awali wa GBS.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuondokana kabisa na utegemezi wa kibajeti hasa kipindi hiki ambapo hali ya uchumi ya Nchi za wahisani zimetetereka kutokana na ugonjwa wa Uviko – 19 na hivyo kuwepo na uwezekano mkubwa wa nchi hizo kushindwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mikopo ya ndani na nje, Serikali imepanga kukopa katika soko la ndani kiasi cha **shilingi trilioni 1.84,** mikopo ya nje **shilingi trilioni 2.35** na mikopo ya ndani kwa ajili ya *rollover* **shilingi trilioni 3.15**. Kwa takwimu hizi inaonyesha wazi ni kwa jinsi gani Serikali kwa asilimia kubwa inakopa katika vyanzo vya ndani suala ambalo linapelekea kukosekana kwa mikopo yakutosha kwa Sekta Binafsi. Hivyo, Kamati inapenda kuishauri Serikali kuliangalia suala hili ambalo litasababisha kukosekana kwa mikopo kwa sekta binafsi itakayopelekea kupungua kwa ushiriki wao katika kutekeleza mipango ya Serikali. Aidha, Serikali ifikirie kuanza kutafuta mikopo yenye masharti ya kati ili kuondokana na ile yaenye masharti ya kibiashara.

b) Sera za Matumizi

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali imepanga kutumia kiasi cha **shilingi trilioni 36.33** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizi kiasi cha **shilingi trilioni 23.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 63** ya bajeti yote na **shilingi trilioni 13.33** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na **asilimia 37**. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa mapato ya ndani yanazidi matumizi ya kawaida kwa kiasi cha **shilingi trilioni 3.03.** Hii maana yake ni kwamba mapato yote ya ndani yanaweza kugharamia matumizi ya kawaida peke yake na **asilimia 8.3** tu ya miradi yote ya maendeleo. Kufuatia uchambuzi huu Serikali haina budi ikahakikisha inasimamia vizuri mapato ili kuongeza ufanisi wa matumizi kupitia mapato

yake ya ndani baadalla ya kutegemea misaada na mikopo kutoka kwa wahisani na washirika wa maendeleo.

Jedwali Namba 8: Ulinganisho wa Sura ya Bajeti ya Serikali kati ya Mwaka 2020/21 na 2021/22

NA.		2020/21	2021/22	TOFAUTI	ASILIMIA		
	MAPATO	C1	C2	C2-C1	(C2-C1)/C1*100		
1.	**Mapato ya Ndani**	**23,250,582.3**	**25,168,718**	**1,918,135.7**	**8.25**		
	• Mapato ya Kodi (TRA)	20,325,779.9	22,178,721	1,852,941.1	9.12		
	• Mapato yasiyo ya Kodi (TRA)	2,924,802.4	2,989,998	65,195.6	2.23		
2.	**Mapato ya Halmashauri**	**814,961**	**863,858**	**48,897.0**	**6.00**		
.	**Mikopo/Misaada kutoka Nje**	**2,874,372.2**	**2,955,923**	**81,550.8**	**2.84**		
	• Mikopo ya Masharti Nafuu -GBS	138,323.3	0	-138,323.3	-100.00		
	• Msaada na Mikopo ya Miradi	2,460,506.1	2,673,617	213,110.9	8.66		
	• Msaada na Mikopo ya Kisekta	275,542.8	282,306	6,763.2	2.45		
.	**Mikopo ya Ndani na Nje**	**7,939,877.5**	**7,341,240**	**-598,637.5**	**-7.54**		
	• Mikopo ya Nje	3,035,630.0	2,352,107	-683,523.0	-22.52		
	• Mikopo ya Ndani	1,588,169.2	1,838,796	250,626.8	15.78		
	• Mikopo ya Ndani - Rollover	3,316,078.3	3,150,337	-165,741.3	-5.00		
	JUMLA YA MAPATO YOTE	**34,879,793.0**	**36,329,740**	**1,449,947.0**	**4.16**		
	MATUMIZI	**C1**	**C2**	**C2-C1**			
.					**4.08**		
	•				1.78		
	•				5.00		
	•				5.43		
	• Mahitaji ya TANAPA, NCAA na TAWA	-	245,000	**Matumizi ya Kawaida**	**22,100,538.0**	**23,002,951**	**902,413.0**
.	**Matumizi ya Maendeleo**	**12,899,433.8**	**13,326,788**	Mfuko Mkuu wa Serikali	10,476,832.4	10,663,278	186,445.6
	• Fedha za Ndani	10,043,206.1	10,370,865	Mishahara	7,762,389.5	8,150,509	388,119.5
	• Fedha za Nje	2,736,048.9	2,955,923	Matumizi Mengineyo (OC)	3,741,137.2	3,944,164	203,026.8
	JUMLA YA MATUMIZI YOTE	**34,879,793.0**	**36,329,740**	**1,449,947.0**	**4.16**		
	NAKISI YA BAJETI (% OF GDP)	**2.6%**	**1.8%**				

Chanzo: *Wizara ya Fedha na Mipango*

7.0. HATUA ZA KIKODI ZINAZOPENDEKEZWA NA SERIKALI

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kutoa pongezi kwa Serikali ambayo kwa kiasi kikubwa imechukua na kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Bajeti. Hatua hii inaonyesha utayari wa Serikali kupokea mapendekezo na kuyafanyia kazi, tunaamini hii ni kutokana na Uongozi bora wa Rais Wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

7.1. **Maeneo yaliyoguswa na Hatua mbalimbali za Kodi na Usimamizi wake.**

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa hatua mbalimbali za kikodi zinazopendekekezwa na Serikali na

kubaini kwamba hatua hizo zimegawanyika katika makundi makuu yafuatayo: -

i. Kuchochea uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi kama vile kilimo na viwanda;

ii. Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji na Ufanyaji Biashara Nchini yaani "Blueprint for Regulatory Reforms to Improve Bussiness Enviroment"

iii. Kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa vyanzo vilivyopo na kuongeza vyanzo vipya vya mapato;

iv. Kurahisisha ulipaji kodi pamoja na usimamizi wake;

v. Kulinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani usio sawa ili viweze kushindana na uzalishaji kwa ufanisi na tija;

vi. Kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata kiasi chake stahiki; pamoja na

vii. Utaratibu wa kushughulikia misamaha ya kodi kwa miradi ya Serikali na ile ya wahisani.

7.2. **Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu hatua za Kikodi**

Mheshimiwa Spika, Wakati Waziri wa Fedha na Mipango akiwasilisha Hotuba yake alitoa rai kwa watanzania kwamba tujifunge mikanda ili kuchangia zaidi mapato ya Serikali. Kamati inakubaliana na kauli mbiu hiyo. Hata hivyo, kila hatua ya kikodi iliyopendekezwa itachambuliwa kikamilifu na Kamati na kutoa mapendekezo pindi Serikali itakapoleta mbele ya Bunge lako tukufu muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2021 *"The Finance Bill 2021*. Kamati inatambua pia kwamba baadhi ya vyanzo vipya vya mapato vilivyopendekezwa vinaenda kuongeza gharama za baadhi ya huduma na bidhaa nchini, ongezeko hilo litachambuliwa kwa undani ili kuhakikisha kwamba Serikali inaongeza mapato

yake bila kuathiri shughuli za kiuchumi. Pamoja na kwamba Muswada wa Fedha bado haujawasilishwa kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo kwa hatua za Kikodi zilizopendekezwa na Serikali: -

(iv) Serikali lazima ifuate utaratibu wa kikanuni kwamba inapowasilisha Bajeti ya Serikali Bungeni iwasilishe sambamba na Muswada wa Sheria ya Fedha ili kamati ipate muda wa kutosha wa kuupitia na kuuchambua pamoja na kuwaita wadau ili kupokea maoni yao;

(v) Serikali kuweka utaratibu wa kutoa ufafanuzi wa HS Code (Harmonized system code) zilizoguswa katika Bajeti ya Serikali zinahusisha bidhaa na malighafi zipi ili zijulikane kwa wote;

(vi) Serikali kuweka mizania ya Kodi zinazosamehewa na mapato yanayokusudiwa kupatikana ili ifahamike wazi hatua zinazochukuliwa katika kupunguza mapato na zile za kuongeza mapato mwisho wa siku zinakuwa na athari hasi au chanya kwa mapato ya Serikali; na

(vii) Serikali kuangalia upya ushirikishwaji wa wafanyabiashara na wazalishaji wa ndani kwa hatua za kikodi ambazo zinapendekezwa katika Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki. Utaratibu uliopo hivi sasa hautoi fursa ya kutosha kwa sekta Binafsi nchini kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na maoni ya ujumla ya Kamati kuhusu Hatua mbalimbali za Kikodi kamati ina maoni yafuatayo katika baadhi ya sheria za Kodi ambazo zimependekezwa kufanyiwa mabadiliko.

7.2.1. Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kuweka kodi ya zuio kwa kiwango cha **asilimia 2** kwenye mauzo ya mazao ya Kilimo, mifugo na uvuvi yanapouzwa kwenye kampuni na mashirika yote yanayojihusisha na usindikaji na ununuzi wa mazao. Hatua hii itakuwa na madhara makubwa sana kwenye bei ambazo wakulima watalipwa na makampuni

hayo. Ni lazima Serikali ikafikiria upya uamuzi huu kwa sababu bado Kilimo chetu kina changamoto ya kuwa duni hivyo kutokuwa na tija inayotakiwa (mavuno madogo ukilinganisha na gharama zilizotumika), changamoto ya upatikanaji wa masoko ya uhakika wa mazao (Mfano zao la mahindi msimu uliopita 2020). Hivyo, haileti maana hata kidogo mkulima ambaye siku zote tumesema hajaweza kufaidika na kilimo chake tunataka kumtwika mzigo mwingine mpya. Jambo hili linaweza kupelekea/kusababisha mazao yao yakawa yananunuliwa/kuuzwa kwa bei ya chini kwa kisingizio cha kodi hii ya zuio.

7.2.2. Sheria ya Kodi ya Majengo SURA 289.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kuanza kutoza kodi ya majengo kupitia mashine za LUKU. Ubunifu huu una lengo la kupanua wigo wa mapato ya Serikali na kufanya ukusanyaji wa kodi hii kuwa rahisi. Uamuzi huu unaenda na Tamko la Serikali la awali la kurejesha ukusanyaji wa kodi hii kwa Serikali za Mitaa ambazo zina rasilimali watu katika ngazi zote za kukusanya kodi hii. Pamoja na ubunifu huu kuwa mzuri unaenda kinyume na Sheria ya Kodi ya Majengo ambayo inaangalia majengo ambayo yako kwenye maeneo yanayotakiwa kulipa kodi hiyo (rateable areas). Mapendekezo haya yanachukulia nyumba zote zenye umeme hata zile ambazo ziko vijijini lakini hazipo kwenye maeneo ambayo kwa mujibu wa sheria hazina sifa ya kutozwa kodi.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo haya hayatoi msamaha kwa Taasisi za Umma na Majengo mengine ya Umma ambayo yanatumia Umeme lakini kwa mujibu wa Sheria ya kodi ya majengo yamesamehewa kodi hiyo. Aidha, kuweka kiwango mfuto kwa nyumba zilizoko mjini na vijijini ni kuwaumiza Wananchi ambao wanaishi vijijini. Kamati inaishauri Serikali kwamba ubunifu huu uende sambamba na kufanya uthamini wa nyumba na kutumia LUKU kama namba ya mlipa kodi na kila luku itozwe kulingana na nyumba ambayo luku hiyo ipo. Utaratibu maalumu uwekwe kwa majengo ya maghorofa ambayo yana mkazi zaidi ya mmoja

(Apartments). Hatua hii italeta mapato zaidi kuliko utaratibu huu unaopendekezwa.

7.2.3. Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na mabadiliko ya viwango vya matangazo kwenye mabango ambavyo vimekuwa ni kilio cha muda mrefu. Gharama za mabango zilipelekea wafanyabiashara kusitisha kabisa kufanya matangazo kupitia mabango na hivyo kupelekea Serikali kukosa kodi hii na kupunguza wigo wa mapato ya Halmashauri.

7.2.4. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 124(2) cha Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Serikali inaruhusiwa kufanya mabadiliko ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwa kuzingatia matarajio ya mfumuko wa bei. Uamuzi wa kutofanya mabadiliko kwa mujibu wa sheria umetokana na ukweli kwamba biashara za bidhaa hizi zimezorota kutokana na athari za kiuchumi zilizosababishwa na ugonjwa wa UVIKO-19. Hatua hii ina lengo la kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa hizi ambazo tayari zinatozwa gharama kubwa kupitia mfumo wa kodi za kielektroniki. Uamuzi huu utaongeza uzalishaji na uuzaji wa bidhaa hizo na hivyo kupekelekea ongezeko la mapato ya Serikali. Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza ushuru kwenye bia zinazotumia shayiri inayozalishwa nchini itakayolenga kuongeza uzalishaji wa zao hili.

7.2.5. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kikodi ilizozichukua hasa katika sekta ya kilimo zitakazoenda kuchochea ukuaji wa sekta hii kama vile;- Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye vyumba vya ubaridi, hatua hii inaenda kuinua sekta ya kilimo hasa cha maua na mbogamboga (horticulture) ambayo imekuwa inaiingizia Serikali mapato ya kigeni; Kufuta msamaha wa Kodi

ya Ongezeko la Thamani kwenye mikebe ya kuhifadhia maziwa (Canes) ambayo itasaidia ukusanyaji wa maziwa ya wafugaji na kuyapeleka kwa wazalishaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani katika miradi inayotekelezwa na taasisi husika na kubadilisha utaratibu wa kuombea msamaha wa kodi kwa miradi hii. Hatua hizi ikiwa zitasimamiwa vizuri zitapelekea ukamilikaji wa miradi kwa wakati.

7.3. Mabadiliko ya Kanuni mbalimbali yaliyojitokeza katika Hotuba ya Bajeti

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Bajeti ya Serikali imeonyesha kwamba kuna kanuni mbalimbali ambazo zinaenda kufanyiwa mabadiliko. Ieleweke wazi kwamba kanuni hazitabadilishwa kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021 kwa sababu Muswada unagusa Sheria mama tu. Hivyo, ni wazi kwamba Kamati ya Sheria ndogo ambayo ndio hupitia kanuni hizo inatakiwa kuzipata mapema iwezekanavyo ili kutekeleza masharti ya Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1, ambacho kinataka Kanuni zote zinazobadilishwa kuwasilishwa Bungeni mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali ndani ya Siku 6 katika Mkutano wa Bunge unaofuata.

8.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/22

8.1. Utunzaji wa dhahabu

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura 197 inaruhusu Benki hiyo kuhifadhi hazina ya fedha za kigeni kwa dhahabu na kutumia sarafu zinazotambulika duniani. Dhahabu inayotakiwa kuhifadhiwa ni ile iliyosafishwa hadi kufikia ubora wa **asilimia 99.5.** Thamani ya dhahabu ilidhihirika wazi katika kipindi hiki cha Uviko- 19 ambapo iliongoza katika mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ikinunuliwa kama *safe haven*. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali ianze kutekeleza takwa hilo la kisheria.

8.2. **Utaratibu wa Uibuaji na Ugharamiaji wa Miradi ya kuongeza Mapato ya Halmashauri**

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya upembuzi kwenye mchakato wa uibuaji, uidhinishaji, na utolewaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya kimkakati ya Halmashauri ili ijitegemee kimapato na kubaini kwamba;

i) Utaratibu uliopo japo ulikuwa na nia ya kuziwezesha Halmashauri ambazo zinajiweza tayari ili zijitegemee umekuwa unaumiza sana Halmashauri ambazo ukusanyaji wake wa mapato ni Duni. Hali hii inatokana na ukweli kwamba wakati wa kuzipima zote zinawekwa kwenye kundi moja.

ii) Pia, kwa Halmashauri zinazoonekana kuwa na wigo mdogo wa ukusanyaji wa mapato Viongozi wake huwajibishwa ilihali hakuna uwezeshaji wowote wa kuongeza mapato uliofanywa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Hivyo, ni vyema utaratibu huu ukabadilishwa na badala yake zikaangaliwa kwanza Halmashauri zenye hali mbaya na zenye uwezo wa kati kutokana na wigo mdogo wa mapato, kisha ndio zikaangaliwa zile zenye hali nzuri ya ukusanyaji wa mapato ili kuleta usawa.

8.3. **Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo ya TANAPA na hali ya Sekta ya Utalii**

Mheshimiwa Spika. Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuwa inatoa fedha za matumizi mengineyo kwa Mamlaka za TANAPA, NCAA na Ngorongoro kwa miezi miwili unapoanza mwaka wa fedha na kuendelea kutoa kwa mwezi mmoja mmoja kila mwezi. Hatua hii itaziwezesha taasisi hizi kuwa na akiba ya fedha ya kukidhi mahitaji ya mwezi unaofuata katika kipindi chote cha mwaka. Katika mwaka wa fedha 2020/21, fedha za Mamlaka hizo zilipitia Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina ambapo hadi mwezi Aprili, 2021 jumla ya **Shilingi 227,519,349,953.48** zilitolewa kwa Taasisi hizo.

Kati ya fedha hizo **Shilingi 68,440,922,181.36** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 139,287,122,765.62** kwa ajili ya uendeshaji wa na TAWA na **shilingi 19,791,305,006.50** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, imebainika kwamba ulipaji wa fedha za WMA ambao ni walinzi wa hiari wa hifadhi pamoja na miundombinu ya barabara zimekuwa hazilipwi kwa wakati. Aidha, miundombinu katika baadhi ya Hifadhi ambazo zinaliingizia Taifa mapato kama vile Serengati na Ngorongoro imeharibika na hazipitiki kwenye baadhi ya maeneo. Serikali lazima itambue kwamba matumizi katika masuala ya uhifadhi wakati mwingine hayatabiriki. Kwa mfano changamoto za ujangiri, magonjwa ya wanyama, uvamizi wa wananchi kwenye maeneo ya hifadhi na uvamizi wa wanyama kwenye makazi ya watu.

8.4. **Maduka ya kubadilisha Fedha za Kigeni**

Mheshimiwa Spika, kufuatia udhibiti wa biashara ya maduka ya ubadilishaji fedha nchini uliofanywa na Benki Kuu mwaka 2019 iliyopelekea kufungwa kwa baadhi ya maduka hayo. Hatua hii ilikua na lengo la kuhakikisha kwamba biashara hiyo inafanywa kwa mujibu wa sheria na kanuni za Benki Kuu. Aidha, hatua hii ilisababisha uhaba wa upatikanaji wa huduma ya ubadilishaji wa fedha za kigeni nchini kutokana na huduma hiyo kutolewa kwa kiasi kikubwa na Mabenki na maduka binafsi machache. Adha hiyo ilisababishwa na:-

i. Mabenki kutokufanya kazi kwa masaa 24 na kutokufunguliwa siku za Jumapili suala ambalo linasababisha usumbufu kwa wahitaji;

ii. Mabenki kuwa na matawi machache ambayo yako mbali na maeneo ambayo huduma hiyo inahitajika.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya kanuni ya uendeshaji wa maduka ya kubadilisha fedha ya 2019 ili kurahisisha ufunguaji na uendeshaji wa maduka hayo.

8.5. **Kutumia Taarifa za Hali ya Uchumi, Fursa za Uwezekezaji Pamoja na changamoto katika Mikoa na Halmashauri katika ugawaji wa Rasilimali.**

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kuwa Serikali imekuwa ikifanya Tafiti za Hali ya Uchumi pamoja na Fursa za Uwekezaji kwenye mikoa na halimashauri zote nchini. Tafiti hizo zina lengo la kutoa taswira ya mikoa na halmashauri zote nchini ili kuisaidia Serikali kuu inapokuwa inafanya mgawo wa rasilimali watu na fedha. Kamati inaamini kwamba taarifa hizi zikitumika vizuri zitasaidia katika kuleta usawa katika ugawaji wa rasilimali za nchi.

8.6. **Tathmini na Ufuatiliaji (Monitoring & Evaluation)**

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Mpango wa Maendeleo waTaifa wa mwaka 2021/22 umeongelea kuhusu kufanyika kwa tathmini na ufuatiliaji wa masuala mbalimbali ikiwemo miradi ya maendeleo. Mpango haujasema chochote juu ya nchi kuwa na Sera na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/22 Serikali inaenda kuandaa Mwongozo wa Tathmini na Ufuatiliaji. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa Mwongozo huo bado hautaweza kujumuisha mfumo mzima wa Tathmini na Ufuatiliaji. Hivyo, Kamati bado inaona haja ya Serikali kuwa na Sera na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji itakayoongoza Mwongozo huo kwa lengo la kuhakikisha inafikia malengo tarajiwa, hususan kuwa na ubora na thamani ya fedha za umma kwa ajili ya kuimarisha maisha na ustawi wa
wananchi.

8.7. **Mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki (Electronic Tax Stamp).**

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua faida za mfumo wa Kodi za Kieletroniki ETS. Faida hizo ni pamoja na kupata taarifa sahihi za uzalishaji wa viwandani na hivyo kukusanya kodi stahiki ya ushuru wa bidhaa pamoja na kodi ya Makampuni, uwezo wa utambuzi wa bidhaa halisi na zisizo halisi, kuondoa udanganyifu wa baadhi ya wazalishaji na wafanyabiashara

wasio waaminifu. Changamoto kubwa ya mfumo huu ni gharama zinazotozwa kwa stempu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri mambo yafuatayo;

i. **Kwanza** ni kuangalia uwezekano wa mfumo huo kutumika katika bidhaa nyingine ambazo zinazalishwa na kupitia *conveyer belt* ili kupanua wigo wa ukusanyaji wa Taarifa na inaweza kupunguza gharama za stempu, bidhaa zinazopendekezwa ni pamoja na saruji, mafuta ya kula na mabati.

ii. **Pili** ni Serikali kukaa na Mkandarasi na kufanya marejeo ya gharama za stempu ili zisiwe mzigo kwa wazalishaji; na

iii. **Tatu** ni kuwa na mkakati wa Wataalamu wa Ndani kuendesha mfumo huo pindi Mkataba na Mkandarasi wa sasa utakapokamilika**.**

8.8. **Utaratibu wa Uwasilishaji wa Maoni ya Kamati za Bunge na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imebaini kwamba utaratibu uliopo wa uwasilishaji wa mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki *(East Africa Customs Management Act 2004)* haushirikishi wafanyabiashara wa ndani kama walivyo wenzao wa nchi jirani kabla ya Serikali kupeleka mapendekezo hayo. Aidha, kamati imebaini kwamba baadhi ya maamuzi ambayo Serikali inaridhia katika jumuiya yanakuwa na athari hasi kwa wafanyabiashara na wazalishaji wa ndani na yanatoa manufaa kwa wazalishaji wa nchi nyingine wanachama.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu maalumu utakaojulikana na wafanyabiashara wote ili washiriki kikamilifu katika mapendekezo ya Tanzania yanayoenda katika Jumuiya na yale ya nchi wanachama yanayopelekwa katika jumuiya. Aidha, Ofisi ya Bunge ione haja ya kuandaa utaratibu wa ndani na kikanuni utakao toa fursa kwa Kamati za Bunge kuyapitia na kupata maoni ya

umma kupitia *"Public Hearing"* ili maoni hayo yanaporidhiwa na nchi yawe yameshirikisha wadau kwa kiasi kikubwa.

8.9. **Vyanzo vya Mapato vinavyopendekezwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba kuna mapendekezo mengi ya vyanzo vya mapato hutolewa na Kamati za Bunge katika ngazi ya Kamati na Katika ngazi ya Mijadala ya Bunge zima. Vyanzo hivyo huwa havina mrejesho kutoka Serikalini na badala yake Bunge limekuwa likiridhia vyanzo vinavyoletwa na Serikali kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha. Kamati inashauri utengenezwe utaratibu kikanuni wa Serikali kuwa inawasilisha Bungeni Taarifa ya vyanzo vya mapato vinavyokuwa vimependekezwa na Bunge. Hatua hii itaondoa dhana kwamba Bunge lako tukufu linajadili matumizi tu bila kuangalia vyanzo vya mapato.

8.10. **Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti (Compliance Report)**

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti Sura ya 438 kifungu cha 56(1), Serikali inatakiwa kuandaa na kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti Kila baada ya miezi sita. Kifungu hiki kilifanyiwa mabadiliko mwaka 2017 na kubadilisha uwasilishaji wa Ripoti ya Utekelezaji wa Bajeti kutoka miezi 3 iliyokuwepo hadi miezi 6 ya sasa. Mabadiliko haya yamekuwa na changamoto kubwa sana katika utekelezaji wake katika maeneo makuu mawili. Kwanza ni kuchelewa kufuatilia utekelezaji wa Bajeti kwa miezi sita na Pili ni kushindwa kutoa maoni na mapendekezo katika utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka husika ili kurekebisha kasoro ambazo zinaweza kuwa zimejitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuleta mabadiliko ya sheria ya bajeti kifungu cha 56 (1) ili kurejesha utaratibu wa Serikali wa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti (Compliance Report) kila baada ya miezi mitatu badala ya miezi sita ya sasa. Hatua hii italiwezesha Bunge kuweza kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Aidha,

Serikali iwe inaleta Bungeni Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka mzima katika Bunge la mwezi wa Tisa kama sheria ya Bajeti inavyoitaka.

8.11. **Changamoto na fursa zilizopo katika uchumi wa Kidijiti (Digital Economy)**

Mheshimiwa Spika, Uchumi wa Kidijiti umeleta changamoto kubwa sana kwa mataifa yanayoendelea na yaliyoendelea ambapo makampuni yameweza kukwepa ulipaji wa kodi kwa kufanya Biashara kwenye nchi na kupata faida bila makampuni hayo kuwa na Ofisi au makampuni katika nchi husika. Kamati inaitaka Serikali kuangalia sheria zetu zinazosimamia biashara za Kitaifa na Kimataifa ili kuhakikisha kwamba tunadhibiti kwa kiasi kikubwa upotevu huu wa mapato. Juhudi hizi lazima ziendane na kuchochea ugunduzi katika sekta ya TEHAMA. Aidha, mamlaka zinazohusika kama TCRA ziangalie namna ya kuendeleza sekta ya mawasiliano na teknolojia badala ya kuwa wadhibiti tu.

8.12. **Mapendekezo ya marekebisho ya sheria za fedha ili kurahisisha utekelezaji wa maamuzi ya kamati ya taifa ya uwekezaji rasilimali (NISC-National Investment Steering Committee)**

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Taifa ya Uwekezaji ni kamati maalumu iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji Sura ya 38 na lengo lake ni kupitia na kutatua changamoto zote za kikodi na zisizo za kikodi kwa lengo la kuchochea miradi ya uwekezaji nchini kwa wawekezaji mahiri *(Strategic Investors).* Kamati hiyo inaundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambae ndie Mwenyekiti, Waziri wa Fedha na Mipango, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC ambaye ndie Katibu na Mawaziri wa Sekta na wataalamu ambao jambo lao litakuwa likijadiliwa. Muda mrefu sasa umepita kwa kamati hiyo kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea kutokana na sheria mbalimbali za fedha kushindwa kutambua maamuzi ya kamati hiyo**.**

Mheshimiwa Spika Mfano mzuri ni pindi ambapo kamati (NISC) **inaporidhia** vivutio vya kikodi Sheria ya Uwekezaji

Tanzania, Sura 38, Kifungu cha 20(8) kinamtaka Waziri wa Fedha na Mipango kuridhia Mapendekezo ya vivutio vya ziada kwa wawekezaji mahiri maalum kama vilivyopendekezwa na NISC wakati vifungu vya Sheria ya Mapato, Sura 332 Kifungu cha 10(3) , Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura 148 Kifungu cha 6 na Kifungu cha 11; havimpi Mamlaka Waziri wa Fedha na Mipango kuidhinisha vivutio hivyo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhuisha Sheria zinazotoa misamaha ya kodi kwa wawekezaji mahiri.

8.13. **Hali ya Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kutokushirikishwa kikamilifu kwa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini. **Hali** hii imepelekea kuwa na changamoto kubwa katika upatikanaji wa takwimu za uchangiaji wa fedha za miradi ya maendeleo kutoka kwa Sekta Binafsi. Serikali lazima itambue mchango wa Sekta binafsi katika kusukuma gurudumu la maendeleo. Kwa mfano katika Mpango wa Pili wa Taifa wa miaka mitano; jumla ya **Shilingi trilioni 107** zilitakiwa kugharamia mpango huo. Mpango huo ulitegemea Serikali kutoa jumla ya **shilingi Trilioni 59** na Sekta Binafsi **Shilingi trilioni 48**.

Mheshimiwa Spika, Aidha kamati imebaini kutokuwepo kwa takwimu sahihi na za kujitosheleza juu ya mchango wa sekta binafsi katika miradi ya maendeleo nchini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutumia utaratibu wa wawekezaji wenyewe kutoa taarifa zao kwa hiari (Self declaration) za uchangiaji wa miradi ya maendeleo ili kupata takwimu za uwekezaji uliofanywa na Sekta Binafsi kwenye Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba suala la kutilia mkazo sekta binafsi liende sanjari na suala la miradi ya ubia baina ya Serikali na Sekta binafsi (PPP). Kamati imebaini kwamba licha ya uwepo wa Sera na Sheria ya PPP tangu mwaka 2010, mpaka sasa hakujawa na mradi hata mmoja ambao umetekelezwa kwa njia ya ubia. Aidha, pamoja na

mabadiliko ya Sheria ya mwaka 2018 bado hakuna mradi uliotekelezwa, miradi iliyopo ipo kwenye hatua mbalimbali za maandalizi. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kutilia mkazo suala la miradi ya ubia ili kuvutia wawekezaji nchini na kujipatia unafuu wa kuendesha miradi mikubwa ya maendeleo.

8.14. **Mfuko wa Kuwasaidia Wakulima kustahimili kushuka kwa Bei za Mazao ya Kilimo (Price stabilization Fund)**

Mheshimiwa Spika, Ukisoma Taarifa ya Hali ya Uchumi utagundua kwamba katika mwaka 2019 mazao yetu ya biashara kama kahawa, pamba, katani na chai yote yalishuka na kwa mwaka 2020 mazao yaliyofanya vizuri ni tumbaku na karafuu tu. Hali hii inasababisha kuwepo na sera mahsusi za kuangalia wakulima pindi bei za mazao na uuzaji wa mazao yao unapoanguka kwa kiwango cha kusababisha kushindwa hata kurejesha gharama za kulima na kukidhi mahitaji yao ya msingi. Kamati inashauri Serikali kuanzisha mfuko maalumu wa kuwalinda wakulima dhidi ya kuporomoka kwa bei ya mazao yao ili kuleta tija katika kilimo na kutowakatisha tamaa wakulima ambao wamekuwa wakipambana mashambani ili kuliletea Taifa mapato ya kigeni.

Jedwali Na 10. Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao ya Kibiashara kwa mwaka 2020

Na	Zao	Asilimia
1.	Kahawa	-4.6
2.	Pamba	-4.6
3.	Katani	-8.9
4.	Chai	-29.1
5.	Tumbaku	1.5
6.	Korosho	1.8
7	Karafuu	87.9

8.15. **Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara (BLUEPRINT)**

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua hatua nzuri zilizochukuliwa na Serikali ni dhahiri nchi yetu bado inakabiliwa na mazingira yasiyoridhisha ya Biashara nchini. Na ndiyo maana Ripoti ya Dunia ya Ufanyaji Biashara (World Doing Business Report) inayoandaliwa na *UNCTAD* imetuweka katika Nafasi ya 141 kati ya nchi 189 Duniani kwa mazingira bora ya Biashara. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa BLUEPRINT ili nchi yetu iwe kati ya nchi 100 zenye mazingira bora ya kufanya biashara duniani ifikapo mwaka 2025.

8.16. **Utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo (Flagship Projects)**

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Miradi ya Kielelezo iliyoainishwa katika Mpango wa Pili wa mwaka 2015/16 -2020/21 bado kuna baadhi ya miradi haikutekelezwa kikamilifu. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inakamilisha miradi ya kimkakati iliyokuwa kwenye Mpango wa pili wa maendeleo kabla ya kuanzisha Miradi mipya.

9.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe kwanza kwa kunipa fursa na kuniamini kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Aidha, napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Eng. Hamad Yussuf Masauni, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu na wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za majadiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na

kuchambua Bajeti Kuu ya Serikali na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard) :-**

1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, **Ndg. Nenelwa Mwihambi** pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo na Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo husika vya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Sillo Daniel Baran, (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI
14 Juni, 2021

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa mawasilisho hayo.

Waheshimiwa Wabunge, kama ulivyo utaratibu wetu, tutaanza na wachangiaji mbalimbali ambao wanahitaji kuchangia bajeti hii. Tutaanza na Mheshimiwa Jerry William Silaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ajiandae.

Lakini kabla uchangiaji haujaanza, nirekebishe tangazo moja; wageni wa Mheshimiwa David Kihenzile hawatoki Mwanza, wanatoka Chuo cha *SAUT* Arusha. Kwa hiyo, Taarifa Rasmi za Bunge Makatibu, zinadikwe sawasawa; wanatokea Jijini Arusha na siyo Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Jerry William Silaa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 iliyowasilishwa hapa Bungeni na Waziri wa Fedha tarehe 10, Juni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kidhati kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuja na bajeti iliyobeba matumaini mapya kwa Watanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee maeneo mawili makubwa ambayo bajeti hii imekuja na matumaini mapya. Mosi; bajeti hii imekuja kujibu lile swali

ambalo Watanzania wamekuwa wakijiuliza kuhusiana na uendelezaji wa miradi yetu ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiisoma bajeti hii – naomba kunukuu – inasema hakuna mradi hata mmoja utakaokwama bila kusimama hata kwa mwezi mmoja. Na maneno haya yanachukua uhalali wake kwenye maneno aliyoyasema Rais wetu tarehe 06, Aprili, pale Ikulu, Dar es Salaam akiapisha Makatibu Wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alisema, naomba kunukuu;

"Tuna urithi aliyotuachia marehemu Rais wetu; miradi mikubwa miwili" – akimaanisha Mradi wa Bwawa la Nyerere na Mradi wa *Standard Gauge* – *"na miradi mingine midogomidogo."(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anaendelea kusema; wanasema ukifanya vibaya kwenye urithi, Mungu anakulaani. Aliyekuachia urithi hana radhi na wewe, na Mungu atakulaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa siyo maneno ya Mheshimiwa Rais, lakini naamini neno urithi unaweza ukaliondoa ukaweka neno wosia. Kwa maana yako maneno aliwahi kuyasema mwendazake. Naomba kunukuu;

Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliwahi kusema, akizungumzia miradi hii mikubwa ya kimkakati, alisema;

"Mimi ni dereva tu, lakini pia najiuliza, ikiwa siku moja Mungu atanichukua hawa wanaokuja watakuja kuyamaliza kweli?"(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu tarehe 06, April wakati Mheshimiwa Rais anaelezea ule urithi, alikuwa anazungumzia kauli hii. Na ukisoma sentensi hizi, maneno aliyoyasema Hayati Magufuli, liko neno ikiwa siku Mungu

atanichukua. Hakuelezea kwamba ikiwa atafika mwisho wa ukomo wa utawala wake kwa mujibu wa Katiba; ni maneno mazito sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema bajeti hii imekuja kujibu kiu ya Watanzania, imekuja kujibu wosia aliotuachia Hayati Magufuli na imekuja kutekeleza kauli ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha miradi yote ya kimkakati inakwenda kutekelezwa na kukamilika kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili; bajeti hii imekwenda kutoa majibu ya kero zilizosemwa hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge. Ukiangalia mijadala yote, kuanzia tunajadili Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, mjadala wa bajeti mbalimbali, siamini kuna Mbunge yeyote alisimama hapa hakuzungumzia barabara zetu zinazotekelezwa kwa kusimamiwa na *TARURA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge hapa waliongea kwa hisia kubwa. Na mimi nilikuwa mmoja wao na nilikuwa nasubiri bajeti hii niangalie Serikali imejipangaje kuongeza fedha kwa *TARURA.* Ukurasa wa 72 zimetengwa shilingi bilioni 322,158,000,000 kwa ajili ya barabara zetu za *TARURA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku hapa hakukosi swali la Wizara ya Maji. Na hisia za Wabunge zilijionesha sana kwenye bajeti ya Wizara ya Maji. Bajeti hii imekuja kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la afya; kwenye majimbo yetu wananchi wamejenga maboma, Serikali imeshindwa kumalizia. Pamoja na ujenzi mkubwa wa miundombinu ya afya, vituo vya afya, vifaatiba, wataalam, dawa; bajeti hii imekuja na mwarobaini wa kutatua kero hizi za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo mengi ambayo bajeti hii imeyagusa. Lakini naomba niseme; ili

kufadhili miradi ya maendeleo – wataalam wa uchumi wanafahamu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ni mtaalam wa uchumi – ziko njia nne. Njia ya kwanza ni mikopo, ya pili ni misaada, ya tatu ni fedha zetu za ndani, na ya nne ni *venture capital* ama *PPP* ama miradi inayosajiliwa na sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo hii tunayoikopa tukisema tutatekeleza miradi yetu kwa mikopo tunabebesha Taifa letu mzigo wa uchumi wa sasa, watoto wetu na wajukuu zetu. Leo kwenye bajeti hii deni la Taifa ni himilivu kwa mujibu wa *international standards* ambazo zinataka deni la nje lisizidi asilimia 50; deni la Taifa letu ni asilimia 17. Deni la nje na ndani ukichanganya kwa pamoja kwa vigezo vya kimataifa halipaswi kuvuka asilimia 70; leo sisi tuko asilimia 27, tunafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ziko nchi za majirani zetu, takwimu hizi zipo, zimekopa mpaka sasa ziko nje ya vigezo hivi. Lakini maeneo mawili salama, ukiacha eneo la misaada ambalo wote mnafahamu misaada hii inakuja na masharti, na masharti mengine ni magumu, hatuwezi hata kuyataja humu kwenye Bunge hili, tunabaki na maeneo mawili salama zaidi ya ku-*finance* miradi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo kwanza ni kodi zetu sisi wenyewe. Naomba ninukuu maneno ya Hayati Dkt. Magufuli aliyoyasema kule Kyela; alisema tunajenga vituo vya afya, barabara kwa fedha zetu. Alisema Tanzania inatakiwa iwe mfano kiuchumi katika dunia, yale mawazo ya kufikiri kuna mtu ataleta misaada tuyapoteze kichwani, ule ni ugonjwa mkubwa. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema; Serikali isiyokusanya kodi ni Serikali ya wala rushwa. Lakini pamoja na *TRA* na Serikali kupambana kuongeza wigo wa kodi, mpaka sasa walipa kodi walioko kwenye *tax base* ya *TRA* ni watu milioni mbili na laki saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini? Kwa sababu tulikuwa kwenye semina pale Ijumaa; sekta kubwa ya Watanzania iko kwenye sekta isiyo rasmi. Kwa hiyo, ukisema unapanua wigo wa kodi utabaki palepale kwa watumishi, palepale kwa walimu wetu, palepale kwa wafanyakazi wetu, palepale kwa kuwaumiza wafanyakazi kwa kodi za mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upande wa pili...

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa Silaa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, siyo ya kwanza?

NAIBU SPIKA: Ya pili. Ahsante.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa dakika moja.

NAIBU SPIKA: Sekunde 30.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini upande wa pili, tunao mtandao mkubwa wa watumiaji wa simu za mkononi kwa laini zisizopungua milioni 52; hawa ndi Watanzania wanaoteseka kukosa dawa. Tunayo miamala ya fedha kwa Januari mpaka Desemba, 2020 ya jumla ya trilioni 201; hapa wako wanaotuma miamala tukiwemo wale tunaotuma na ya kutolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Watanzania tukubaliane kugharamia bajeti yetu sisi wenyewe. Waziri wa Fedha ameupiga mwingi sana tarehe 10, ametoa hotuba nzito sana, ameupiga kama Bernard Morrison, siyo Morrion huyu, Morrison yule aliyekuwa *Dar Young Africans. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hoja ya mawasilisho matatu yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu Hali ya Uchumi wa Mwaka 2020, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Fedha na taasisi zake zote kwa kutuandalia bajeti nzuri ya kimkakati kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba kumuita kwa jina hili; *the Tanzanite super woman of our time. (Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wetu ameanza vizuri uongozi ndani ya Taifa letu kama Rais wa Serikali ya Awamu ya Sita. Bajeti iliyowasilishwa siku ya tarehe 10, Juni, 2021 inadhihirisha umakini, ujasiri na weledi wake katika eneo la uchumi wa Taifa letu; pongezi nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia bajeti hii inathibitisha msemo wa wahenga unaosema mama ni nguzo na mlezi wa familia. Nayasema haya kwa sababu kuu mbili kwa siku hii ya leo kwa sababu ya muda; sisi sote Watanzania

ni mashahidi kwamba chini ya uongozi thabiti wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli na msaidizi wake namba moja mama Samia Suluhu Hassan, Taifa letu limehimili mtikisiko na mdororo wa uchumi wa athari ya Ugonjwa wa Korona (UVIKO-19) kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hili kwa sababu katika taarifa iliyowasilishwa, Taifa letu ni miongoni mwa mataifa 11 tu kati ya Mataifa 45 yaliyo Chini mwa Jangwa la Sahara ambayo uchumi wetu umekuwa kwa ukuaji chanya wa asilimia 4.8. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mataifa 43 yaliyo chini ya Jangwa la Sahara ukuaji wao wa uchumi umekuwa kwa ukuaji hasi, na mataifa mawili yameona ukuaji wao wa uchumi ni sifuri. Hakika tunastahili kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuweza kuhimili mtikisiko huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhimilivu huo wa uchumi wetu haujaletwa na jambo jingine bali ni ujasiri, uthubutu wa viongozi wetu wakuu na sasa tukiongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alipotuambia Watanzania tufanye kazi wapo wenzetu walitukimbia humu Bungeni tuache kupitisha bajeti, lakini kwa umakini wa viongozi wetu tulisimama imara bajeti tuliyoipitisha ndiyo hii leo inatueleza zile mbinu zote na mikakati mbalimbali tuliyoitekeleza imewezesha Taifa letu kuwa moja ya nchi chache zilizoweza kuhimili mtikisiko huu wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo limesababisha nimsifu Mheshimiwa Rais wetu, katikati ya kipindi hiki kigumu cha *Corona* mwaka 2020 tuliona Taifa letu likiingia katika kundi la nchi zenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati, miaka mitano kabla ya kipindi tulichojiwekea Watanzania kwenye Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa. Hili nalo jambo tunasema ni jambo ambalo limeishangaza dunia

tumewezaje kama Taifa, tumeweza kwa sababu tuna viongozi jasiri na sasa tuna mwanamama shupavu anayetupa miongozo ya kutenda yaliyo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu moja kubwa iliyofanikisha Taifa letu tuweze kuingia katika nchi zenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati ni uwekezaji kwenye miradi mikubwa ya kielelezo. Ukisoma bajeti iliyowasilishwa pamoja na Mpango wa Pili wa Maendeleo, tunaona *commitment* kubwa ya Serikali yetu ya kwenda kuikamilisha miradi hii ya kielelezo ambayo itaendelea kutuwezesha kufanya uchumi wetu uendelee kuwa imara. Pongezi nyingi sana kwa Rais wetu na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *commitment* hii ya Mheshimiwa Rais inadhihirisha nadharia ya uwekezaji kwenye miundombinu *(theory of economics of infrastructure investment)* inayotuambia kwamba uwekezaji kwenye miradi mikubwa hasa ya miundombinu lazima ifanywe na Serikali yenyewe. Jambo ambalo tulisimama imara Serikali ya Chama Cha Mapinduzi tukasema tunakwenda kuwekeza kama Serikali kwa sababu tunahitaji kuona matokeo chanya ya uwekezaji wetu huu ambao tunaufanya na ambao tayari tumeshaona matumaini makubwa ndani ya uchumi wetu ulio imara kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo naomba sasa niishauri Serikali yangu. Nianze kwa kupongeza kwa kupeleka asilimia zaidi ya 37 ya bajeti nzima kwenda kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka huu 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili thamani halisi ya fedha zetu asilimia 37 zaidi ya trilioni 13 tunazozipeleka kwenye Miradi ya Maendeleo iweze kuonekana kwenye maisha halisi ya wananchi wetu naomba kushauri mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba Serikali yetu sikivu iimarishe Idara ya Mipango ya Kitaifa; Idara ya Mipango ya Kitaifa iwezeshwe ili iweze kufanya kazi yake ya

tathmini na ufuatiliaji wenye tija kwa ajili ya Taifa letu. Idara hii inapendekeza iwezeshwe katika maeneo makuu matatu; eneo la kwanza iwezeshwe kwenye eneo la Rasilimali fedha, eneo la pili iwezeshwe kwenye eneo la Rasilimali watu na eneo la tatu iwezeshwe kwenye eneo la rasilimali teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu tukiiwezesha Idara hii ya Mipango ya Taifa inaweza kufanya kazi kubwa ya kufuatilia miradi mbalimbali ya maendeleo na fedha nyingi zinazowekezwa na Serikali yetu kwenye miradi ya maendeleo. Tatizo kubwa la ndani ya Taifa letu siyo upelekaji wa fedha bali ni usimamizi, ufuatiliaji na kufanya tathimini ya fedha zile tunazozipeleka kwenye miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kushauri katika idara hii, pia niombe sana tunahitaji kufanya kubadilisha mfumo wa kitaasisi wa jinsi kazi ya ufuatiliaji na tathimini inayofanyika ndani ya Serikali yetu. Wizara ya Fedha na Mipango naomba sana muweke nguvu kwenye neno Mipango ndani ya Wizara yenu hapa ndipo kwenye kupanga mipango kwenye ufuatiliaji kuhakikisha kwamba tunahakikisha tunapata thamani halisi ya fedha inayopelekwa kwenye eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni eneo muhimu sana kwa sababu mara nyingi tumeona tukifanya ufuatiliaji baada ya miradi kukamilika. Hili jambo linapelekea fedha nyingi za Serikali kupotea, nipendekeze ikiwapendeza Serikali yetu tuwe na *real time monitoring and evaluation* ya miradi yote tunayopeleka fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa tuanze kufuatilia...

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sekunde thelathini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba kabla fedha haijapelekwa idara hii ya mipango ya kitaifa ikajiridhishe na eneo ambalo tunakwenda kuwekeza, lakini mchakato mzima wa manunuzi ukoje kwa sababu miradi mingi tunaona wanachelewesha katika eneo la manunuzi, fedha nyingi za Serikali zinapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya pia ufuatiliaji wakati wa utekelezaji naamini alichokisema Mheshimiwa Rais jana pale wakati anazindua jengo la Benki Kuu pale Mwanza, kwamba pesa iliyowekezwa ni kubwa kuliko jengo linaloonekana hatutoweza kusikia kauli hizi tena kwa sababu idara hii itafanya kazi yake inayotakiwa na thamani halisi ya fedha itaonekana.

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. DKT. ASHATU K. KIJAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma atafuatiwa na Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza ajiandae.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya, pia kwa usikivu ambao sisi wabunge tumekuwa na mambo mengi tumelalamika kwa muda mfupi lakini kwa muda mchache aliokaa madarakani tumeona ameanza kutekeleza kila Mbunge hapa amepata milioni mia tano kwenye jimbo, hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hongera sana Mheshimiwa Waziri umeanza vizuri na mimi kama Mbunge mzoefu kidogo nadhani mishale mikubwa tutakupiga Bunge lijalo, hakuna Mbunge ambaye hajaridhia na hajaridhika na

Mpango huu wa Bajeti uliowasilisha kwetu. Tunaimani kama sasa utausimamia na kuyatekeleza yale ambayo umeyazungumza kwa kauli yako utakuwa umetubeba sana sisi Wabunge ambao bado tunahitaji kuendelea kuwa kwenye Bunge hili kipindi cha mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana katika suala la kupandisha na kuwachukua Waheshimiwa Madiwani kuwaweka kwenye bajeti ya Serikali. Mheshimiwa Waziri mimi ni zao la Diwani, mimi kuingia humu nimefanya kazi nzuri na ya mateso nikiwa kama Diwani, lakini baadaye nimepanda kuja huku Mheshimiwa Waziri umefanya kazi kubwa sana Diwani awe na mshahara unaotambulika na Serikali siyo hisani za Wakurugenzi, umetuheshimisha hata mizinga kule kwenye Baraza la Madiwani kwa Madiwani wetu na ninakushukuru leo Serikali imewatambua na kuwaweka kwenye mpango sasa mtalipwa mshahara kama mtumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ulitekeleze na ikikupendeza sitaki kutamka kiwango bado mshahara wa madiwani ni mdogo sana ukilinganisha na majukumu yao kwa hiyo ukafikirie sitaki utamke ni shilingi ngapi kwenye *windup,* lakini...

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Msukuma kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. CECILIA DANIEL PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nataka nimpe taarifa mchangiaji kwamba kilichoridhiwa siyo mshahara ni posho badala ya kulipwa na halmashauri sasa inalipwa na Serikali Kuu, ukiongea habari ya mshahara ni habari nyingine ambayo ina utaratibu wake itakuja kuwa na makato yake, itakuja kuwa na *pension* na mambo mengi. Kwa hiyo kinacholipwa ni posho siyo mshahara. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Hilo moja, labda lingine ni kwamba, kwa sababu umetawaja wale wa kwangu, wale wakwangu hawahusiki kwenye mpango huo maana sisi ni jiji na tunaweza kujilipa wenyewe. Kwa hiyo, wale wapo vizuri Mheshimiwa Musukuma usiwe na wasiwasi.*(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, watanisaidia kuwaambia wale ambao wapo jirani na Jiji la Mbeya *message* yangu itafika. Mheshimiwa nilindie muda wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru iwavyo vyovyote vile kama taarifa ilivyotolewa, lakini naishukuru Serikali iwe posho, iwe mshahara iwavyo vyovyote ni jambo la msingi Mheshimiwa endelea kuchapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwenye faini ya bodaboda, nataka nikuambie katika kitu ambacho Mungu atakukumbuka kukuongezea hata siku zako za uhai wako ni suala la faini ya bodaboda. Mimi nilikuwa najiuliza wachumi wetu mpo namna gani inawezekanaje faini ya bodaboda anayebeba watu wawili unamlinganisha faini na basi la watu 65. Mimi nilikuwa nashauri Mheshimiwa Waziri hata hiyo elfu kumi bado ni nyingi, tungeweka hata elfu mbili, lengo letu siyo faini!

WABUNGE FULANI: Aaah!

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mnabisha nini Waheshimiwa Wabunge.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilindie muda wangu, lengo siyo *faini* lengo letu ni kuwawezesha watu watoke kwenye bodaboda wanunue magari, hakuna mtu anapenda kuendesha bodaboda miaka mitano, miaka kumi anaumia kifua, kwa hiyo mimi nadhani bado mimi kama Mbunge nashauri hata hiyo elfu kumi umeanza vizuri, lakini tufikirie kwenda hata kwenye elfu mbili hata buku kwani kuna shida gani nchi ina pesa nyingi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia kuhusiana na suala la machinga, Mheshimiwa Waziri katika jambo ambalo nakuomba sana Mheshimiwa Waziri hamna tajiri yeyote anaanza kuwa tajiri bila kuhangaika huku chini. Machinga ni mtu muhimu sana Mheshimiwa Waziri na mimi niliona Dar es Salaam ni sehemu ambayo Watanzania wote tunaitegemea nilienda tu hizi siku mbili tatu nikazungukia kule Kariakoo baada ya kuona Mkuu wa Mkoa mmoja anasema tunaondoa machinga, nyinyi Waheshimwa Wabunge kama mnakumbuka Wabunge wenzangu wa CCM katika raha tuliyoipata kwenye uchaguzi wa 2020 ni pamoja na machinga kutuunga mkono, kwa sababu tuliwawezesha walikuwa *busy* na kazi zao hawakusikiliza mambo ya kudanganywa danganywa na wanasiasa ambao hawana mwelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo anasimama mtu mmoja anasema tuondoe machinga tuwarudishe vijijini, nendeni mkafanye *research* Dar es Salaam machinga wengi sasa hivi waliopo huko mitaani wengi wana *degree* moja na wengine *degree* mbili wameamua kujiajiri, pili, unapom-*disturb* machinga usidhani unamuharibia maisha yeye watu wengi waliopo kule kwanza tuliwaambia wanunue vitambulisho ili wafanye biashara yao kwa uhuru na Serikali imechuma bilioni 43 halafu leo gafla mtu mmoja anasema tuwatoe machinga unapomuharibia mtu biashara mnaharibia taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wapo pale tayari wana mikopo, wamekopa, wamekopeshwa wanafanya biashara yao wanamarejesho eti tunathamini magari, kwani Mheshimiwa Waziri tuna shida gani tukisema magari yasiingie Kariakoo ili iwe *center* ya biashara watu wafanye biashara yao kwa uhuru wasibugudhiwe. Hii kitu Mheshimiwa Waziri mimi huwa najiuliza hivi mnaona faida gani magari yaingie elfu moja ambayo hayalipii au kuachia machinga wafanye biashara kwa uhuru kama tulivyowaahidi halafu nyie mkusanye kodi. Machinga ndiyo anafanya *research* ya biashara Tanzania nzima nyie wote wenye *degree* hapa

hakuna mtu anafanya *research* ya biashara machinga hauzi kitu ambacho hakinunuliwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara ndiyo watu wanaowategemea leo mtu mmoja anasimama ndiyo maana huwa najiuliza tunao Wachumi nchi hii au tuna vicheche tu, maana siwaelewi kabisa. Kwa hiyo niwaombe sana mliangalie wasisumbuliwe hawa watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Musukuma hebu usiwaite watalaam wetu vicheche tafadhali, ondoa hilo neno kwa sababu wamesoma ili watusaidie na haya yote tunayoipongeza Serikali wachumi wamefanya kazi nzuri.*(Makofi)*

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaliondoa, lakini wafanyekazi kwa ufasaha wadhihirishe yale waliyoyasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nimeona kwenye kodi za wachimbaji wadogo unapendekeza kuongeza kodi Mheshimiwa Waziri nikushauri kumbuka kabla hatujarekebisha kodi za wachimbaji wadogo Serikali ilikuwa inakusanya bilioni 168 baada ya marekebisho ya sheria tupo bilioni 544. Ukiongeza kodi ukiwanyima faida wafanyabiashara ya elfu mbili, elfu tatu utaongeza utoroshaji hutapata hela hii, nikuombe sana ondoa hayo mawazo ya kuongeza hiyo asilimia tatu sijui asilimia saba tufikirie zaidi kupunguza kwa sababu tunaona tunawekeza mpaka viwanda vikubwa hapa halafu tunaongeza masuala ya kodi siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nazungumza kwa upole sana kwa sababu Mheshimiwa Ndumbaro ni Waziri ambaye ni rafiki yangu kuhusu suala la Ng'ombe. Mimi nipo humu Bungeni nimeshuhudia mawaziri wawili Mzee Magembe alikaa pale na rafiki yangu ndugu yangu Mpina na juzi amelizungumza kwa uchungu kuisumbua Ng'ombe

sidhani kama tunafanya sahihi hata kutuchaji tu elfu hamsini Ng'ombe ikikamatwa kwenye maliasili kule mbugani haifai, kwa sababu Ng'ombe haina uharibifu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tufanye ulinganisho, tembo akienda kula mahindi hana faini Ng'ombe akienda kula majani anafaini kwa sababu gani? tufikirie kuondoa hii faini Ng'ombe anaenda kula majani na hii ni roho mbaya kwa wataalam Ng'ombe akiingia kula majani aharibu miti na mwisho wa siku majani mnayachoma moto sasa sielewi mnajenga viwanda vya kuchinja wapi kule Dar es Salaam na sehemu zingine machinjio za kimataifa halafu Ng'ombe mnazipiga vita mnataka kuchinja fisi au mnachinja vituo gani.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana Mhehimiwa Waziri tuondoe faini haiwezekani twende hata kitaalam tu kwamba kama ni sahihi kumkamata mtu ana Ng'ombe ukaichaji laki moja au elfu hamsini wakati thamani ya Ng'ombe ni laki mbili hebu tujaribu ma-*traffic* wakikamata *VX* wakuchaji milioni mia nusu ya bei uliyonunulia mbona tutayakimbia magari. Nifikirie sana Waziri kukushauri kwamba tuondoe hizi kodi ambazo zinaonea watu na tuache Ng'ombe ya Mtanzania itembee na uhuru popote ambapo itataka kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho nimemsikia Mheshimiwa Rais jana ameelekeza kwa uzuri tu, kwamba dhahabu ziingine kutoka Kongo na sehemu zingine, ni kweli, lakini Mheshimiwa Waziri naujua udhaifu tulionao naomba uzungumze na watu wako wa *TRA* wasisumbue wafanyabiashara. Wafanyabiashara wanapeana taarifa kuliko hata mitandao ya simu akikamatwa mmoja tu, wanaambizana wote hawaji na tunafungua viwanda tunategemea *material* kutoka Kongo ambapo kuna dhahabu ambazo hazina utaratibu. Kwa hiyo nikuombe sana tuwape uhuru wafanyabiashara na wasisumbuliwe na mambo ya polisi na mambo ya *TRA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Musukuma alikuwa anasema ng'ombe waende popote wanapotaka kwenda nikaanza kuwaza hivi wanautashi wakuamua wapi wanataka kwenda kumbe. Siku tukipishana nao humu ndani tusije kuanza kutafuta nani aliyewaleta jamani atakuwa ni Mheshimiwa Musukuma.

Lakini Mheshimiwa Waziri wale wakusanya kodi wakati mwingine kwa sababu siyo wote, lakini wengine hawajawahi kufanya biashara, kwa hiyo ile lugha ya kibiashara wakati mwingine hawaelewi kabisa, yaani mtu akiwaambia sijauza hawamwelewi kwamba sijauza, lakini muangalie utaratibu mzuri kwa sababu ya maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wetu ameliweka vizuri sana hilo la makusanyo ya kodi.

Mheshimiwa Charles John Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mheshimiwa Juma Hamad Omar, ajiandae.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Bajeti Kuu, Bajeti ya Serikali. Awali ya yote naunga mkono bajeti hii, mimi naiita bajeti ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Bunge inayoshughulikia bajeti, lakini nijitendee haki naunga mkono mchango wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba alipozungumzia Idara ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika mchango wangu nitazungumzia zaidi namna ya kupata mapato. Najua waswahili wanasema kulea mimba siyo kazi, kazi ni kulea mwana, tumehangaika tupo hapa miezi yote hii tangia mwezi wa kumi, vijijini huko tunatengeneza bajeti mtoto huyu Mwigulu Nchemba ameshamtoa sasa tutengeneze mapato, mimi najikita kwenye mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti yetu tumeongeza shilingi mia.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

T A A R I F A

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kumpa taarifa ndogo tu kwamba kulea mimba ni kazi sana na kuna kipindi hata wamama tunapata *bed rest* kwa miezi tisa yote ukilea mimba. Kwa hiyo kulea mimba ni kazi na kulea mwana pia ni kazi vyote kwa pamoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage, nadhani hiyo inamaanisha misemo mingi ya Kiswahili itabidi ibadilishwe, maana wanawake tuko kazini safari hii. Tunataka kurekebisha mambo yote ambayo kwake yeye hayajakaa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Mwijage.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naikubali sana taarifa hiyo. Kazi ya mwenzio ambayo hujawahi kuifanya usiizungumzie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niizungumzie ongezeko la shilingi 100 kwenye mafuta. Ongezeko la shilingi 100 kwenye mafuta, ile tozo si hoja, hoja ni mzigo mzito sasa utakaokuwa unabebwa na kila lita ya mafuta. Kwa ongezeko la shilingi 100 petroli sasa itatozwa shilingi 892, dizeli shilingi 768 na mafuta ya taa shilingi 765. Si hoja na hiyo, hoja ni kuwa sasa mafuta haya kwa kiasi kinachotozwa italeta ushawishi na kivutio cha watu kukwepa kodi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiweza kutoa *depot* malori 27 ya mafuta utaweza kukwepa shilingi bilioni moja. Kwa

viwango vya Mheshimiwa Ummy Mwalimu, hizo ni sekondari mbili kabisa kabisa za Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachotaka kuzungumza, katika kuboresha mapato lazima Serikali tujiandae na tujiimarishe katika kuimarisha vitengo vyetu vya upimaji, sina wasiwasi na *ways and measure,* lakini lazima tujiimarishe. Tujiimarishe na kitengo kinachopewa kazi ya kuangalia kwamba mafuta hayatoki kundi moja kwenda kundi lingine pale tunapozungumzia suala la vinasaba. Lakini tunalo tatizo la miundombinu ya cha wote. Kuna miundombinu muhimu ya mafuta ambayo hakuna yeyote anayewajibika nayo, ambapo mafuta yanapotea na huwezi kumuwajibisha yeyote. Serikali inapaswa kudhibiti maeneo hayo na kumuwajibisha mmojawapo. Lazima ichukuliwa taasisi moja ya Serikali ipewe jukumu la kulinda miundombinu hiyo ambako ndipo mafuta mengi yanaweza kuwa yanapotelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jumla ya yote, nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba kitengo cha *TRA* kiimarishwe upya kwa kuongezewa watu na kupewa mafunzo ya kudhibiti sekta hii. Kwa sababu utakuja kuona kwamba, katika kuuza lita bilioni 3.14 kwa mwaka kwa kiwango cha wastani wa shilingi 700 kwa lita ni fedha nyingi tutakuwa tunazikusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hiyo, mimi napenda niishauri Serikali, hayo ni mafuta yatakayouzwa ndani, tunapaswa kufanya utaratibu wa kuchochea mafuta mengi yauzwe. Na hapa nazungumzia mafuta ambayo yakiuzwa humu ndani hayatatubebesha mzigo. Kwa sababu kumbuka mafuta haya unayoyatoza tozo utawajibika kutafuta dola kusudi uyanunue; lakini kuna mafuta unaweza kuyatoza pasipo kutafuta dola kusudi kuyanunua. Haya ni mafuta yanayowezesha mizigo kupita Tanzania kwenda nchi za Jirani *(transits)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, ya sheria zetu na uendeshaji wa shughuli tumekuwa *tuki-discourage transit*

cargo, na ndiyo maana mizigo inakwenda Durban, Beira pamoja na Mombasa. Sasa tunapaswa kuangalia udhibiti na usimamiaji wa mizigo yetu ili mingi ipite kusudi tuweze kupata mafuta ambayo tutayatoza tozo kwa ili tuweze kuongeza pato letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hiyo niishauri Serikali, kwamba muangalie sasa, wakati umefika wa kuweza kuitumia Dar es Salaam kuwa *trading hub*. Yaani mafuta yawe *traded* Dar es Salaam yaweze kuuzwa nje. Lita bilioni 2.5 zinapita Dar es Salaam zikiwa *transit* kwenda *land locked countries.* Sasa tukigeuza *re-export* Tanzania ikiwa *trading hub* ina maana takriban asilimia 30 zinaweza kuwa zinauzwa kutokea hapa, na kila yanapouzwa, unapata *mark-up* na ile *mark-up* inaweza kuchangia kwenye mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la uchumi wa nchi. Nimeona mapendekezo katika sekta ulivyopendekeza. Niombe sasa, kwa kila sekta tuanze kuweka vigezo *KPI*, kwamba kila sekta inaleta nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tunauza nje ya nchi kwenye *re-export,* tunauza mazao yenye thamani ya dola bilioni 2.9. Katika hiyo theluthi mbili ni dhahabu, lakini ukiangalia *potential* ya *export* ni trilioni 2.36 bila kuweka dhahabu. Sasa tunapaswa kuwekeza katika maeneo hayo kusudi tuuze zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema hapa kwamba katika fursa ya nyama Tanzania *hatu-export* chochote ilhali wenzetu Uganda na Botswana wanauza dola milioni 100, dola 135 mtawalia, Uganda anauza maziwa dola milioni 100 kwa mwaka, sisi hatupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna fursa ya ma-*avocado* ambayo yanapendwa dunia nzima, na soko la *avocado* linaendelea kuongezeka duniani. Hata hivyo Tanzania pamoja kuwa na nafasi ya tatu katika Afrika bado kiasi tunachosukuma kwenye soko hili soko kubwa halijaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuja fursa ya *soya beans.* Ukihesabu tani milioni 42 tunazopewa na China kuuza kule ni *revenue* kubwa sana kuliko mazao yote *tunayo-export.* Sasa, Wizara isaidie sekta hizo kusudi tuweze kutengeneza kipato kikubwa na kuweza *ku-supply* kwenye i*International markets*. Hiyo ni sekta ya *re-export*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye mchango wa Mheshimiwa Waziri alipozungumzia matumizi ya *LUKU* katika kuweza kukusanya *Property Tax*. Nakubaliana na wazo hilo kwa kuwa lina ubunifu ndani yake, hata hivyo kuna angalizo. kuna mtu ana nyumba ya ghorofa vyumba viwili juu kimoja chini analipa shilingi 5,000. Je, yule mwenye vyumba vitano chini kwa nini umlipishe shilingi 1,000?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mtu ana vyumba saba, ana wapangaji watatu kila mpangaji ana mita yake atalipa shilingi 3,000. Sasa kwa nini huyu unamlipisha shilingi 3,000 badala ya shilingi 1,000 na ni vyumba 31 vile vile? Lakini kuna mtu ni mstaafu, kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati, kwanini huyo unampa adhabu hiyo? Suala la msingi kuna watu wako tayari kulipa hawajapewa umeme. Kwa hiyo napendekeza Serikali iongeze fedha kwenye *REA* kusudi wale wanaotaka umeme wapewe umeme. Vilevile Serikali iwekeze katika huo mfumo wa *LUKU;* na nashauri ikiwezekana tusubiri. Huu utaratibu usije ukashindwa kama ule wa *TRA* ulivyoshindwa au wa *local government* ulivyoshindwa katika kuweza kukusanya mapato haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Hamad Omar, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ajiandae.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kutoa maoni yangu katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nataka nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha kwa bajeti yake hii ambayo ameiwakilisha, bajeti ambayo kimsingi ni ya kimkakati na imejikita kweli kweli kwenye kutatua changamoto za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana mama yetu mpendwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa bajeti hii nzuri, ambayo moja kwa moja inaonyesha nini ambacho amekusudia kuwatendea Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itoshe kusema kwamba, hii ni bajeti ya wananchi; na ziko sababu nyingi sana ambazo zinaonesha na kuthibitisha kwamba bajeti hii ni bajeti ya wananchi wa Tanzania. Ikizingatiwa kwamba, ndiyo bajeti yake ya kwanza tangu alipoingia madarakani, lakini ndani ya muda mfupi huo amefanikiwa kwa asilimia 100 kuonesha nini ambacho amepanga kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania. Vilevile ameonesha vipaumbele vyake vizito alivyonavyo katika kufikia maono hayo. Ni wazi kwamba Rais wetu Samia Suluhu Hassan, amebeba maono makubwa sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kana kwamba haitoshi, ukifuatilia hii bajeti imegusa makundi mbalimbali katika jamii yetu. Sisi sote ni mashahidi, tumekuwa tukizungumza humu Bungeni changamoto kubwa ya watumishi. Kilio kikubwa cha watumishi ilikuwa ni kupandishwa madaraja. Kupitia kwenye bajeti hii, mama yetu ameweza kutenga zaidi ya bilioni 449, kwa ajili ya kupandisha madaraja watumishi. Jambo hilo lina tija kubwa sana. Kwa sababu, kwanza litasaidia sana kuweza kuongeza motisha kwa watumishi wetu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama haitoshi, tunafahamu, ilikuwepo tozo ya asilimia sita ya ongezeko la thamani. Tozo ile ilikuwa inasababisha deni lilikuwa haliishi; unalipa lakini bado deni linaendelea kuongezeka. Watumishi wamefurahi sana kwa kuondokewa kwa tozo hiyo, kwa sababu sasa ni wazi moja kwa moja, itasaidia kuweza kukuza uchumi wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu changamoto ambazo zipo kwenye barabara zetu, na barabara nyingi ambazo zinachangamoto kubwa ni zile barabara za vijijini. Lakini kupitia bajeti hii fedha zimetengwa za Kimarekani milioni 300 kwa ajili ya kwenda kusaidia barabara za vijijini, na hizo fedha zinatoka kwenye mkopo wa Benki ya Dunia. Vilevile, dola za kimarekani milioni 50, kwa ajili ya kwenda kuhudumia barabara zetu za vijijini *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kilichonifurahisha zaidi ni kwa sababu huu mkopo moja kwa moja utapelekwa kwenye yale maeneo ambayo yana tija kubwa ya uzalishaji, na hicho ndicho kilichokuwa kilio cha Bunge hili, kwamba sehemu nyingi ambazo zinatumika kwa ajili ya uzalishaji barabara zake zilikuwa zina changamoto kubwa sana. Mimi kama Mbunge wa wanawake wa Mkoa wa Songwe nimefurahi sana kwa sababu sote tunafahamu wazalishaji wakubwa ni wanawake. Kwa hiyo moja kwa moja fedha hizi zitasaidia sana kuweza kukuza uchumi wa wananchi, hususani uchumi wa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ipo tozo ambayo imewekwa kutoka kwenye mafuta. Mimi nasema Bunge lililopita Waheshimiwa Wabunge wote humu Bungeni tulikuwa tukisimama tunaiomba Serikali. Kwamba Serikali tunaomba iongeze tozo kwenye mafuta ili kwenda kushughulikia changamoto zetu. Na leo tumeshuhudia Serikali imesikia kilio hicho na tozo hiyo imeongezeka, kwa lengo ambalo ni jema la kwenda kukarabati barabara zetu za kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wanawake tunajua namna ambavyo tulikuwa tunapata shida sana inapokuja suala la hizi barabara. Wanawake wengi walikuwa wanajifungulia barabarani, wanajifungulia njiani kutokana na ubovu wa hizi barabara. Sisi wanawake tunamshukuru sana Rais wetu kwa sababu sasa suala la wanawake kujifungulia barabarani linafikia kikomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi ambayo nikianza kuyaeleza ni mambo mazuri ambayo yapo

kwenye bajeti yetu. Lakini ni wazi kwamba, ili mambo hayo yote yaweze kutekelezwa itakuwa si sawa kwamba mzigo huu wote ukaachiwa Serikali. Ni lazima wananchi tuweze kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kwamba haya mambo mazur, ambayo Rais wetu ameyakusudia kwa Watanzania yanapatiwa ufumbuzi. Na namna pekee ya kuwashirikisha wananchi ni kupitia kodi. Mwalimu Nyerere alisema wakati wa Azimio la Arusha; naomba ninukuu kwamba:-

"kila mtu anataka mendeleo, lakini si kila mtu anaelewa na kukubali mahitaji ya msingi, kwa ajili ya maendeleo". (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya msingi kwa ajili ya maendeleo ni pamoja na kuwa na Serikali nzuri, kufanya kazi kwa bidii, wananchi kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo yao pamoja na Serikali kusimama kidete katika ukusanyaji wa kodi. Ni wazi kwamba Serikali isiyokusanya kodi ni Serikali ambayo ni mfu. Ni Serikali ambayo ni mfu kwa sababu daima haiwezi kuwapelekea maendeleo wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia kwenye bajeti hii, kwamba Serikali imeleta kodi aina mbalimbali. Sasa mimi nataka nizungumzie kodi ya *Property Tax* kwa sababu, ni kodi ambayo ilikuwepo miaka mingi, si kitu ambacho ni kipya. Hata hivyo changamoto yake ilikuwa ni kwamba, kodi hiyo wananchi tulikuwa hatulipi nikiwemo mimi mwenyewe Juliana Shonza, sijawahi kulipa kodi ya majengo. Hii ni kutokana na usumbufu ambao mtu ukifikiria, utoke, uende ukapange foleni *TRA*, ilikuwa ni usumbufu mkubwa sana. Sasa Serikali imekuja na ubunifu wa kukusanya kodi, na imetumia akili kwamba sasa kodi hii itakusanywa kwa akili kuliko kutumia nguvu na mabavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie changamoto chache ambazo zipo kwenye hii kodi. Niishauri Serikali, kwamba tunatambua wazo ni jema na ubunifu ambao umefanyika ni mzuri. Ni lazima sasa Serikali iweze kusimamia, ili basi, katika utekelezaji wa agizo hili la Serikali kusije kukaibuka sintofahamu na changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya majengo ya awali inasema kabisa kwamba suala la kulipa kodi ya majengo ni suala la mwenye nyumba si suala la mpangaji. Kwa hiyo kwenye agizo hili nataka nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, atakaposimama hapa kuja *ku-windup* bajeti yake atuambie Serikali imejipangaje, ina mkakati gani wa kuondoa sintofahamu kati ya mwenye nyumba pamoja na mpangaji? Kwa sababu ni kweli mmiliki wa nyumba ni mwenye nyumba, lakini kwa kuwa kodi inakatwa kwenye *LUKU* maana yake atakayekuwa anakatwa ni mpangaji na si mwenye nyumba. Kwa hiyo nilikuwa naomba Serikali ilete utaratibu mzuri ambao imejipanga kuhusiana na kodi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunafahamu katika sheria ya kodi wazee wa miaka 60 walikuwa *exempted* kwenye kulipa kodi hii. Sasa sijajua, kwenye sheria hii haijazungumza kwa sababu sheria hii imesema kwamba agizo hili kwenye bajeti, kwamba ni nyumba yoyote ambayo ina umeme. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja *ku-windup* atuambie kuhusu kwa wale wazee ambao wana miaka 60 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kuna zile nyumba ambazo inakuwa ni nyumba moja lakini kila mtu anakuwa na LUKU yake, utaratibu utakuwa vipi? Kama haitoshi kuna yale maeneo ambayo yalikuwa nje ya wigo wa kodi; kuna maeneo ambayo kodi hii ilikuwa haiwagusi, je, Serikali imejipangaje kuweza kuhakikisha kwamba kodi hiyo wakati wa kuanza kuikusanya haitaleta mgongano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema kwamba, bajeti hii ni nzuri sana. Ni kwa sababu ni takwa tu la kisheria kwamba ijailiwe, lakini ilipaswa ilipomalizwa kusomwa pale Wabunge wote tuipitishe iweze kupita kwa kishindo kwa sababu imebeba mambo mazuri sana. Rais wetu ni sawa na mama ambaye ameandaa chakula kazi yetu imebaki ni kuweza kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tuiunge mkono bajeti hii kwa

sababu, imekusudia kuweza kutatua changamoto mbalimbali kwa wananchi. Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Juma Hamad Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, ajiandae.

MHE. JUMA HAMAD OMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue fursa hii kukupongeza sana wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Naibu Spika na kumpongeza Mheshimiwa Job Ndugai kuchaguliwa kwake kuwa Spika wa Jamhuri ya Muungano. Nawapongeza kwa sababu Mheshimiwa Spika, Job Ndugai *ali-participate* sana katika kuandaa kanuni ambazo zina mawanda mapana; zinatufanya tufanye kazi zetu katika Bunge hili ndani na nje kwa urahisi zaidi. Na wewe ninakupongeza kwa sababu umekuwa *dictionary* wa kutekeleza kanuni hizi. Lakini baada ya hayo, najua itifaki inazingatiwa, nataka niende kumpongeza Rais wetu wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan. Ninampongeza kwa sababu ameingia katika *record* ya dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa nini, sasa hivi katika viongozi wa dunia wanawake *heads of states* tunao 26 na sita katika hao wanatoka Bara la Europe, watano wanatoka Afrika na mama Samia akiwa mmojawapo. Nchi ambazo zilikuwa zina viongozi wanawake katika Afrika kama ninavyosema ni watano. Tunaye kiongozi wa Namibia, Saara Kuugongelwa, tunaye kiongozi wa Ethiopia Sahle-Work Zewde, tunaye kiongozi wa Togo, Victoire Tomegah Dogbe Dogbe na tuna Garbon kiongozi wake anaitwa Rose Francine Rogombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kutoa pongezi hizo kwa Mheshimiwa Rais sasa nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu wake pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Bajeti kwa hivyo, sina sababu ya kutounga mkono hoja hii. Nakupongeza sana, umeleta bajeti ambayo nataka niseme wazi, katika maisha yangu ya kuwa Bungeni, sijapata kuona bajeti ambayo imeleta mapinduzi makubwa kama bajeti ya mara hii. Nimekuwa hapa vipindi vinne, kipindi cha Mzee Mwinyi nikiwa Waziri wake na kipindi cha Mheshimiwa Magufuli na sasa hivi Mheshimiwa Samia. Lakini nataka nikuhakikishie bajeti yako ni ya aina yake. Nasema ni ya aina yake kwanini, nitakuja nitaeleza vizuri. Lakini, ili hii nchi ipate maendeleo na ihitajike kuna mambo matatu makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nchi lazima iwe na *Prudent Physically and Monetary Policy*, la pili nchi iwe na *Budgetary Policy* ambayo ni imara. Yote hayo yawe katika *backet*/katika kapu ambalo ni la *good governance,* tunayo. Tumemchagua Rais wetu juzi, kwa kishindo kikubwa tu. Kwa hiyo, tunayo *good governance*, kama vile hii *transition* ya madaraka kutoka Hayati Mheshimiwa Magufuli mpaka kuja Samia, ilikuwa ni ya salama kwa hivyo, tunayo *good governance*. Sasa sitazungumzia *Physically Monetary Policy* sasa hivi, lakini zaidi kwa sababu muda wenyewe hautoshi nitajikita kwenye *Budgetary Policy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna nchi yoyote duniani inayoweza kufanya kazi zake bila la kodi, Kodi ndiyo inayoendesha Serikali. Marekani ni nchi ambayo imeendelea lakini haiwezi kwenda bila kukusanya kodi. Katika *City of* New York kuna *road tolls* pale, kuna *road toll station* inatozwa kodi ya barabara na kadhalika. Kwa hivyo kodi ni muhimu na siri moja ya kukusanya kodi ni kukusanya kodi *with minimum inconvenience to taxpayer*. Huyu *taxpayer* ikusanywe kodi yake bila ya kusumbuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hizi *indirect taxes* zinazopita kwenye mafuta, zinazopita kwenye simu hazinipi matatizo, hizi haziumizi hata kidogo na bajeti yetu kwa kiasi kikubwa imejikuta na *indirect taxes.* Katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri mara zote, mara zote, nasema tena au

mara nyingi amekuwa akipunguza kodi katika Sekta ya Kilimo, Sekta ya Uvuvi, Sekta ya Madini na Sekta ya Mifugo. Hayo ni mambo yanayogusa wananchi, maana asilimia 65 ya wananchi wa nchi hii ni hao. Kwa hivyo nasema ni mkombozi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweze ku-*refer* maneno mazuri sana ya Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwanza twendeni Ukurasa wa, kama sikosei, Ukurasa wa 127. Ukurasa wa 127, Kifungu cha 105. Mheshimiwa Mwigulu anasema:

"Amekuwa wazi kuwa Rais wetu hataki kodi ya dhuluma. Hataki kodi ya dhuluma. Hataki kuendesha Serikali kwa Mapato ya dhuluma. Ameweka wazi kusimama imara kwenye masuala ya mapato na matumizi ya Serikali. Ameweka wazi kuwa atakuwa imara kwenye vita dhidi ya rushwa."

Hayo ni maneno ya Mama Samia Suluhu Hassan tunataka Rais wa namna gani kama si Mama Samia?

WABUNGE FULANI: Mama Samia.

MHE. JUMA HAMAD OMARI: Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukienda ukurasa wa 136, Mheshimiwa Mwigulu ana-*windup* kwa kusema:

"Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amenituma, niwahakikishie Watanzania kupitia hotuba hii kuwa, tutaendelea kujenga nchi. Ije mvua, lije jua tutaendelea kujenga nchi. Uwe usiku na mchana tutaendelea kujenga nchi. Kazi inaendelea."

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka maneno gani ya busara kama hayo? Kwa hiyo nadhani tuna kila hali ya kumpongeza Rais wetu mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hiyo naomba nijikite zaidi kwenye mambo haya ya *budgetary policy*. Nchi

hii naifananisha na Nchi ya Malaysia, Malaysia ilipopata uhuru kutoka Uingereza mwaka 1957 ilikuwa ni nchi ya *low income, basically* nchi ile ilikuwa ya kilimo, walikuwa wanauza haya mazao ya kilimo ndipo ulikuwa uchumi wao. Akaja Mwanamapinduzi mmoja Mohamad Mahathir akaifanya Malaysia ikatoka kwenye *low income* ikaja kwenye *middle income* jambo ambalo kuwa na sisi Tanzania tumefanya hivyo. Tumetoka kwenye *low income* tumekuja kwenye *middle income* kiwango cha chini. Nani kafanya hayo? Ni Mama Samia na akishirikiana na Mheshimiwa Hayati marehemu Magufuli. Kwa hivyo tumetoka kwenye *low* income tumekuja kwenye *middle income* kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa vigezo vya Benki ya Dunia ili u-*qualify* kuwa uchumi wa kati kigezo cha chini unatakiwa uwe *per capital income* ya dola 1,036, sisi tunakwenda zaidi. Malaysia sasa hivi hawapo tena kwenye *low income*, kigezo cha chini, wao wapo hawapo kwenye *middle income* kigezo cha juu ambao wameshafika uchumi wao *per capital income* ya dola 4,045. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inachukua muda mrefu sana kutoka *middle income* ngazi ya chini kwenda kwenye *middle income* ngazi ya juu. *Kwenye high income* itachukua muda mrefu zaidi kwa sababu *you're talking per capital high income of* 12,000 *dollars* ambayo hiyo siyo rahisi kufika kwa muda wa karibuni. Kwa hivyo, tutakuwa hapa kwa muda mrefu najua, lakini kwa jitihada hizi, ambazo Serikali yetu inafanya, nina hakika hatuna muda tutakwenda uchumi wa kati kigezo cha juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ninavyosema hii mimi ni bajeti yangu ya kipindi cha nne; sijapata kuona bajeti nzuri kama hii. Kwa mfano, bajeti inakwenda inapunguza kodi kwenye *horticulture*, wenzetu wa Kenya *horticulture* peke yake *per annum* wanapata kama *two billion dollars*. Sasa sisi *foreign exchange* yetu imeongezeka sasa hivi tunakwenda kwenye 5,000 *dollars*. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba kwa sababu kuna upunguzaji wa kodi kwa vifaa vya *horticulture* kama vile majokofu ambayo yatajengwa

Airport, nina hakika inawezekana kabisa tunaweza kuvuka dola 5,000 kwa muda mdogo sana. katika kipindi kinachokuja kidogo tu sisi tutavuka zaidi ya hiyo. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

MHE. JUMA HAMAD OMARI: Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema, tuna mengi sana lakini kwa sababu muda mdogo, namalizia kwa kusema tu, naiunga mkono bajeti hii na nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu hatuna sababu ya kutounga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshiwa Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe na Mheshimiwa Luhaga Mpina ajiandae.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii. Kimsingi kwa sababu Rais sasa ni mgeni na hii ndio bajeti yake ya kwanza, niseme tu tunatoa ushauri kwa Serikali, yale ambaye yalikuwa yakikosewa awamu zilizopita, tunaomba bajeti hii wasiendelee kuyakosea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wengi walivyosema, tunazungumzia *TRA* ambayo sisi kama Watanzania tumeipa jukumu la kuweza kukusanya kodi kwa niaba ya wananchi wote. Leo hii *TRA*, imeshindwa kukusanya kodi sawasawa na malengo ambayo sisi tuliwapangia wakusanye kodi. Tunafahamu kabisa bajeti yetu ni ya kukusanya kodi na kutumia. Kwa hiyo wanapokosea na wanapofanya chini ya kiwango cha ukusanyaji kimsingi inachelewesha maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* wana uhaba wa wafanyakazi na mtu anayesimamia *TRA*, kwa *TRA* iliyopita kuna wakati tuliona walichukua hata vyombo vya usalama kusaidia kukusanya kodi. Watu wa *TRA* wanatakiwa wasomee na ndio maana kuna Chuo cha Ukusanyaji wa Kodi. Tunaomba sana, *TRA* iwajengee uweze wafanyakazi wake wa ukusanyaji wa kodi na hasa hasa kupata mafunzo ya mara kwa mara ili wawe makini na wawe na weledi katika ukusanyaji wa kodi. Mlipakodi ni mtu namba moja anayefanya nchi hii iendelee, ukimwendea kibabe, ukamwendea kwa hali za vitisho, walipakodi wengi wanajificha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado *TRA* haijaweza kufanikiwa walipa kodi ni akina nani, wachache wanaowafahamu hao ndio wanao wabana zaidi. Namwomba Mheshimiwa Waziri tuhakikishe *TRA* inafanya *identification* ya walipakodi wa Nchi nzima ili kodi iweze kulipwa kwa usahihi na ufasaha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa *CAG* wa mwaka 2019/2020, *CAG* anasema katika wale watu ambao wamekwepa kodi na Baraza ya Kodi tunadai kodi zaidi ya trilioni 360. Hii ni nini? Ni kwamba bajeti ya nchi hii zaidi ya miaka mitano inaweza ikajengewa uwezo kutokana na fedha hii ambayo inapotea kwa wale watu ambao hawalipi kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mabaraza ya Kodi ambao wao wanatakiwa wafanye kazi kesi kwa sisi tunaowadai, *TRA* haijafanya kwa ukamilifu. Pesa hii trilioni 360 na Mheshimiwa Rais anisikilize, tunahitaji kuhakikisha *TRA* inasimamia fedha hizi ili ziende kuongeza maendeleo ya nchi hii; kwa sababu leo hii tunakusanya fedha kidogo, bajeti yetu ya mwaka mmoja ukijumlisha hizi trilioni 360 ni miaka kumi takriban tunaweza tukakaa tunakula pesa ambayo ipo mikononi kwa watu haijakusanywa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini tufanye? Kwanza kabisa nimesema lazima wafanyakazi wajengewe uwezo,

hicho ni cha msingi. Pia Ikama ya *TRA* ina wafanyakazi wachache sana ambao hawajaweza kuajiriwa na kutusaidia kukusanya kodi. Ni aibu sana watu wanaokusanya kodi eti wana uhaba wa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kabisa kwenye ile Mamlaka ya Rufani ambayo ndiyo nimesema wao wanao wajibu wa kufanya hizo kesi lazima tuwaongezee nguvu waweze kufanya kesi za ukusanyaji wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie wafanyabiashara. Leo hii kwenye biashara ili ufungue biashara kuna tozo nyingi sana na ziko *scattered*. Lazima tuwe na *one stop center* ambayo mfanyabiashara akitaka kufungua biashara yake ahakikishe anakwenda anakutana na *OSHA* sehemu moja, akutane na watu wa mamlaka ya halmashauri sehemu moja, sio kwamba anakaa mwezi mzima kwenye dirisha moja akifuatilia namna gani afunguliwe biashara. Akimaliza hapo tena unamtuma aende *OSHA*, akitoka *OSHA* anakwenda kwenye halmashauri anakutana napo kuna tozo, hii inaleta usumbufu kwa wafanyabiashara. Tunaomba wawe na eneo moja, mtu akiamua kufungua biashara isiwe ni mateso, kazi yake iwe kutafuta mtaji wala siyo kuhangaika namna ya kufungua biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la kilimo. Asilimia 65 ya Watanzania wanategemea kilimo, lakini leo hii nikizungumzia Nyanda za Juu Kusini ambayo ipo kwenye *big five* ambayo inalisha Taifa hili, leo hii hatuna mkakati makini kwenye kilimo hususan kwenye utafiti. Leo ukienda Mbeya kuna Chuo cha Uyole, huu ni mwaka wa tatu hawajapata fedha za utafiti. Huwezi kuwa na kilimo bila ya utafiti. Ni lazima uwekeze kwenye utafiti ili ujue udongo huu unafaa mbegu gani, ili ujue mazao haya yanafaa maeneo gani, lazima watafiti watutangulie. Kama kilimo kinachukua asilimia 65 ya Watanzania, tunahaja ya kuwekeza maeneo hayo ili tuweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii bajeti ya kilimo inakwenda chini ya asilimia 30. Huwezi kupitisha bajeti

kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utekelezaji wake ambao Wizara ya Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Waziri haipeleki fedha kwa wakati na inapeleka chini ya kiwango. Hatuwezi kufanikiwa, kwani kilimo ndio kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukizungumzia kilimo, tunazungumzia masoko, vitu hivi vinakwenda sambamba. Leo hii katika Nyanda za Juu za Kusini tumekuwa wakulima wazuri wa parachichi. Tunaita ni zao la kijani, zabibu ya kijani, lakini leo hatujajua yakini wanunuzi wa parachichi waliowekeza huko Iringa, Njombe, Rungwe, na maeneo kama haya wanauza kiasi gani nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wananunua kwa kilo moja 1,500 sisi unafahamu tulikuwa tunauza maparachichi 10 kwa buku, lakini leo wanachukua kwa 1,500 kwa kilo, lakini bado kuna haja ya kuchunguza, kama mwekezaji ananunua parachichi, amesafirisha zaidi ya *container* 100 yeye kapata kiasi gani? Kwa maana ukienda nje, unakuta parachichi moja unaweza ukapata kwa dola 1.9 ambayo hiyo ni karibu Sh.3,000 kwa nini mkulima asiuze kwa bei kubwa 1,500 bado naona ni ndogo, naomba Mheshimiwa Waziri Mwigulu asimamie hilo ili wakulima wetu wapate fedha sahihi na sawasawa na thamani ya zao lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia masoko nikija suala la chai. Nimekuwa nikizungumza sana suala la chai katika Bunge hili. Hii leo, chai inanunuliwa dunia nzima na kwenye soko la dunia bado ina soko. Katika nchi hii, ukienda Rungwe chai ni Sh.320 baada ya kupiga kelele. Ukienda Njombe chai Sh.500, ukienda Lushoto chai iko juu, mimi nataka kujua Mheshimiwa, Bodi ya Chai ni moja, nchi ni moja na CCM ndio wanaongoza nchi hii, kwa nini kunakuwa na bei tofauti wala hakuna usawa wa bei katika zao moja? Naomba suala la chai lipatiwe jibu makini wakati Mheshimiwa Waziri anapokuja kujibu masuala yake hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la maji. Maji ni uhai, tunafahamu kabisa kwamba maji ndio kila kitu,

lakini leo hii, tuna vyanzo vingi vya maji na nijikite kwetu Nyanda za Juu Kusini. Leo hii ni aibu kubwa sana miaka 59 kwenda 60 ya Uhuru hatuna maji ndani ya nyumba za watu tunachota maji mitoni na vyanzo vya maji. Ziwa Nyasa lipo kama ambavyo Ziwa Victoria lipo. Niiombe Serikali iweze kuwekeza kwenye Ziwa hili na tuweze kupata maji katika Mkoa wa Mbeya wote, tupate maji kwa sababu uwezekano wa kupata maji upo na fedha zipo za kuweka maji. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa ahsante sana. Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei ajiandae.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili kuweza kuchangia bajeti hii, bajeti ya kihistoria kabisa. Kabla sijaanza kuichangia bajeti hii nilikuwa naomba tu kwanza nimtoe shaka Mheshimiwa Waziri na kumpongeza yeye pamoja na timu yake. Siku ya tarehe 10 Juni, 2021, wakati ana *windup* bajeti alisema bajeti hii inaweza kumfanya yeye awe *very unpopular Finance Minister* kwa sababu yupo tayari kupendwa tu na washabiki wa Yanga na wale Wapiga Kura wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimtoe wasiwasi, nimwambie tu bajeti hii imekufanya kuwa *very popular Finance Minister,* kwa sababu amekwenda kugusa maisha halisi ya wananchi na amekwenda kujibu maswali ambayo wananchi walikuwa wanahitaji. Kwa tafsiri hiyo hiyo, maana yake ni nini? Amekuwa *very popular* kuliko alivyokuwa *popular* kuwa mshabiki wa timu ya Yanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kwa kusema kwamba, naomba sasa nichukue nafasi hii, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo makubwa na mazuri ambayo ameanza kuyafanya tangu alivyoweza

kuingia madarakani. Kabla sijaichangia bajeti hii nataka niguse matatu, manne tu ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kuyafanya yameweza kutupa matumaini na vile vile kuwapa ladha nzuri sana wananchi kujua kwamba sasa tunakwenda katika kazi yenye kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja la msingi ambalo Mheshimiwa Rais ambalo ameweza kufanya ameweza kutupa fedha za takriban shilingi bilioni 172, zimekwenda katika majimbo ya Wabunge wote ambao wapo ndani humu katika Bunge hili. Ikiwemo kule Mtwara Kusini pamoja na Nkasi vile vile zimekwenda katika maeneo ya Tarime na maeneo mengine. Tumepewa fedha hizo ili kwenda kusaidia katika masuala mazima ya *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, Mheshimiwa Rais jambo lingine la msingi ambalo ameweza kulifanya; ameweza kuweka jiwe la msingi katika kuhakikisha kwamba barabara ile *Standard Gauge* inaanza kujengwa kuanzia Mwanza kwenda kule Isaka na bilioni 300 tayari zimeshatoka. Nani Kama mama? *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo haitoshi, Mheshimiwa Rais katika jambo lingine la msingi ambalo ameweza kutufanyia sisi Wabunge, ametupa heshima kubwa sana kwani ameweza kuhakikisha kwamba kila Mbunge ambaye yupo ndani humu katika Jimbo lake imechaguliwa kata moja kwenda kujengwa shule ya sekondari. Nani kama mama? *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Hakuna.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya machache, naomba sasa nijikite katika bajeti ambayo bajeti hii imekwenda kutengeneza taswira nzima na kujibu maswali ambayo wananchi wetu wengi sana walikuwa wanajiuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja la msingi ambalo limeweza kufanyika katika bajeti hii ni suala zima la kuweza ku-*reduce* ile *tax* ambayo wanaenda kukatwa wale wafanyakazi wetu. Imetoka kwenye asilimia tisa sasa inakwenda kwenye asilimia nane. Mheshimiwa Waziri wa fedha naomba tu nimwambie, yuko *very popular* kwa sababu alichokifanya amekwenda kuwafanya wafanyakazi waendelee kuwa na *disposable income* ambayo inakwenda kuwasaidia kwa namna moja ama nyingine waendeane na kasi ya kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo haitoshi, jambo lingine la msingi ambalo limefanyika katika bajeti hii na hili ni la msingi kweli kweli. Naomba tu niseme kwamba kuna katozo kameweza kutozwa kale kanachohusiana na mambo mazima ya mafuta Sh.100. Naomba niseme tu fedha hii ambayo inatozwa ni fedha ya msingi kwa sababu inakwenda kutatua kero za wananchi kule vijijini. Kwa kusema hivyo tafsiri yake ni kwamba, naomba niungane na Mheshimiwa Juliana Shonza yale aliyokuwa ameyasema, akinamama walikuwa wanapata adha kubwa sana. Mazao yetu yalikuwa hayawezi yakaenda katika masoko kwa wakati. Mheshimiwa Waziri, katika jambo la msingi ambalo ameweza kulifanya, hili ni mojawapo. Tunamshukuru sana na tunampongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, katika jambo la msingi ambalo ameweza kulifanya, hili ni mojawapo. Tunamshukuru sana na tunampongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme tu, bajeti hii tunapoenda kuiunga mkono mpaka wale rafiki zetu ambao tumewafunga *speed governor* watakwenda kuunga mkono bajeti hii, kwa sababu ni bajeti ambayo kwa namna moja ama nyingine imekwenda kugusa maisha ya wananchi kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, naomba tu niseme *TARURA* ni sehemu ambayo ilikuwa ina kero kubwa sana. Wakati tunachangia hapa Bajeti ya Wizara

ya Ujenzi, kwa mara ya kwanza niliweza kupokea shikamoo ya Mheshimiwa Waziri wakati anataka tuipitishe bajeti ile. Mambo yalikuwa magumu sana humu ndani. Mheshimiwa Rais ameliona hilo. Fedha zinaoenda kupatikana takribani shilingi bilioni 332, tunaweza kuziongeza kule. Hizo tunaenda kuongeza na shilingi bilioni 172 ambazo Mheshimiwa Rais tayari ameshatupa. Haya ni mambo ya msingi kabisa. Nani kama mama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee mbele. Katika mambo mengine mazuri ambayo bajeti hii imeenda kugusa wananchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, wewe utaendelea kuwa *popular,* ondoka kule katika Yanga, njoo Simba. Moja la msingi umeweza kulifanya, umekwenda kuwasaidia wananchi wanyonge, bajeti imekwenda kuongezeka shilingi bilioni 500 sasa, tunakwenda kutoa mikopo kwa wanafunzi. Nani kama mama? *(Kicheko/Makofi)*

WABUNGE FULANI: Hakuna. *(Makofi)*

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niendelee kusema tu, kule kwangu katika maeneo ya Kibiti na maeneo ya kule Mbeya na maeneo mengine yote, kuna wanafunzi wengi sana ambao wapo katika maisha ya kawaida sana. Bajeti hii imekwenda kuongeza shilingi bilioni 500, sasa wanafunzi wanakwenda kukopa na wanakwenda vyuoni. Nani kama mama? *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Hakuna. *(Makofi)*

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee mbele. Mama huyu mambo makubwa sana ameyafanya. Naomba tu niweke rekodi sawa sawa kwenye *Hansard,* ninaposema mama, nakusudia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Amiri Jeshi Mkuu, mama yetu Mheshimiwa Nama Samia Suluhu Hassan. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya, naomba niishauri Serikali katika jambo moja la msingi, hasa

katika suala zima la kukusanya mapato. Tozo tulizokuwa tumetoza, shilingi moja, bado haitoshi kwa sababu *TARURA* mtandao wa barabara waliokuwa nao ni sawasawa na kilometa 108,449.19. Fedha ambazo tulikuwa tumewapa mwaka jana, 2020 zilikuwa ni shilingi bilioni 245. Ili *TARURA* waweze kufanya kazi kwa usahihi wanahitaji shilingi trilioni moja ili sasa kwa namna moja ama nyingine waende kutatua kero zote. Naomba nitoe ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwezekana tuangalie suala zima la *TV License.* Hili jambo liko wazi. Mimi nilipata bahati ya kwenda kutembea kwa Wandengereko kule. Wao walichokuwa wanakifanya, kuna kitu kinaitwa *TV License* pale Uingereza. Nasi siyo vibaya tukifanya hivyo. Ukienda katika *database* ya Azam utakuta watu waliopo. Tuna Azam, *Zuku, DSTV, Star TV; in totality,* Mheshimiwa Waziri chukua tu kwamba *viwers* wako 1,000,000, ambao wana-*own TV.* Wanapokwenda ku-*subscribe* pale, sisi tuchaji shilingi 1,000 tu kwa kila mwezi. Tafsiri yake ni nini? Tunakwenda kukusanya shilingi bilioni 120. Tukifanya hivyo, tunakwenda kuupanua wigo huu ili sasa tuweze kumsaidia mama, twende tusonge mbele ili sasa hii bajeti ambayo inakwenda kujibu maswali ya wananchi, iweze kukamilika na wananchi hawa wafurahie kuwa na Mama Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kama Amiri Jeshi Mkuu wa nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hivyo haitoshi, eneo lingine ambalo naomba nilikazie vizuri ni katika suala zima la kufanya *projects* hizi kubwa kubwa. Mnajua tumefanya utaratibu. Mheshimiwa Waziri amekuja hapa, ana taswira nzuri sana ya kusema kwamba tunakwenda kuitengeneza miradi mikubwa mikubwa kwa kupitia mambo mengine kama vile *infrastructure bond.* Nina ombi vile vile Serikali tuweze kuangalia suala zima la *PPP. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *PPP* tunapaswa tuitumie kwa namna moja ama nyingine. Siyo vyema kweli kuitumia katika *infrastructure* kwa sababu najua hilo ni eneo liko *very sensitive,* lakini tunayo miradi mingine. Kwa mfano, tuna mradi

ambao tunakusudia katika Wizara yetu hii ya Uvuvi kwenda kule katika *deep sea* kuvua samaki. Tunakusudia vile vile kwenda kujenga bandari. Haya hatuwezi kuyafanya kama hatuwezi kwenda katika suala zima la *PPP. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda huu hautoshi, lakini kule kwetu sisi Wandengereko huwa tunasema, mtu akifanya vizuri sana, huwa tuna ngoma ya kuicheza. Tuna ngoma inaitwa Kinyantindili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiniruhusu nicheze tu kidogo nidemke. Kama utaniruhusu ili tuweze kumpongeza mama. Unaniruhusu? *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Hapana Mheshimiwa Twaha. Hapana, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Naibu Spika, kama huniruhusu basi mimi nitakachokifanya niseme tu nitakwenda kuandika *paper* na hii tutaiita *concept note. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mama yangu, nakushukuru. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Mheshimiwa Spika, haina Taarifa kama Mwenyekiti wa Wandengereko Duniani Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa kama amempa nafasi Mheshimiwa Mpembenwe. Kwa hiyo, ndiyo maana hajaruhusiwa kucheza hiyo ngoma, asije akachukua Uenyekiti wa Mheshimiwa Mchengerwa. Ila inabidi wafanye uchaguzi, maana unajua Mwenyekiti anaweza akawa wa kudumu.

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni ambao wameingia humu ndani, niwatangaze ili kama wanaweza kutoka, basi wataweza kuondoka.

Kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Oran Njeza niliyokuwa nimewatangaza asubuhi hawakupata fursa ya

kuingia. Hawa ni wanafunzi wanatoka Jijini Dar es Salaam, wamekuja kwa ajili ya mafunzo, kuangalia namna Bunge linavyofanya kazi. Sijui wako wapi? Wanafunzi wageni wa Mheshimiwa Oran Njeza; haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wageni wengine na hawa ni wageni wangu 44. Hawa ni UKWATA kutoka Jijini Mbeya wakiongozwa na Mratibu wa UKWATA Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Siwiti Whisper. Sijui wako upande gani hawa? Nimeambiwa wameingia. Haya, naona wataingia baadaye kidogo. Wapi? Wako wapi na hawasimami jamani? Eeh, haya karibuni sana. Sasa nafikiri wameingia kwa uwakilishi, kwa sababu hapa idadi yao ni 44. Karibuni sana. *(Makofi)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei na Mheshimiwa Joseph George Kakunda, ajiandae. *(Makofi)*

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa nami nijumuike katika kuchangia hii hotuba ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwa Watanzania. Jana tumeona alivyoenda kuzindua kile Kiwanda cha Kusafisha Madini kule Mwanza. Tumeona jinsi anavyoenda kuweka jiwe la msingi kwa ajili ya kile kipande cha Mwanza – Isaka.

Kwa hiyo, hii ni kazi nzuri sana ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameendelea kuifanya na kuendelea kufuata nyayo vizuri sana za mtangulizi wake *bulldozer,* Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri pia kwa kutuwasilishia hotuba hii nzuri ya bajeti ambayo tutaendelea kuijadili hapa na kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na neo la mapato. Mapato unaweza kuyaongeza kwa njia tatu au zaidi ya hizo. Moja, kwa kutumia ukuaji wa uchumi wa Taifa mapato yanaweza kuongezeka; pili, kwa kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato pamoja na kuimarisha zile njia zako unazotumia kukusanya mapato; na tatu, kutunga vyanzo vipya vya mapato. Hivi vyote kwa pamoja vinaweza kuongeza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hili moja ambalo nadhani Mheshimiwa Mwakagenda alilizungumza hapa kwamba, kwa nini tunajiuliza kuhusu ile Mahakama ya Rufaa pamoja na Baraza la Rufaa la Kodi pamoja na Bodi ya Rufaa za Kodi, hizi zote zimeshikilia kesi zaidi ya 1,097 ambazo zinaendelea kule na zina hiyo shilingi trilioni 360 na Dola za Marekani milioni 181.4. Mheshimiwa Waziri, kuna shida gani kuimarisha Mahakama zetu za Rufaa, kuimarisha Bodi ya Rufaa ya Kodi, kuimarisha Baraza la Kodi la Rufaa ili hizi kesi zote ziende zikaamuliwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwenye bajeti yako umesema kwamba kuna kesi mpya zilizoingia 653 zenye thamani ya shilingi trilioni 2.7. Kwa nini tusiimarishe hizi kesi zikawa zinaamuliwa kwa wakati tukapata mapato? Hapa tunaweza tukakusanya mapato mengi sana ya Serikali. Hatuhitaji kwenda hata kwenye kodi mpya, hizi tu zenyewe katika hili eneo Mheshimiwa Waziri kama tunaweza tukawezesha haya Mabaraza na hizi Bodi kuamua hizi kesi kwa wakati. Kwa sababu yawezekana tu tukawa na upungufu wa Majaji, upungufu wa watendaji, upungufu wa rasilimali fedha. Kwa nini tusipeleke fedha nyingi pale ili hizi kesi zikaamuliwa kwa wakati na mapato haya yaweze kupatikana Mheshimiwa Waziri?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni ukaguzi dhaifu unaofanywa kwenye miamala ya *transfer pricing.* Miamala hii ya *transfer pricing* katika nchi yetu tuna kampuni kubwa za Kimataifa 504. *MNCE's* ziko 504. Katika 504 tunakagua makampuni matano tu kwa mwaka *average* ya makampuni matano na miamala sita na haya makampuni yana fedha

nyingi sana ambapo nyingine zinapopitia katika utaratibu wa miamala ya *transfer pricing,* Serikali yetu inapoteza mapato mengi sana. Kwa mfano, katika makampuni 20 tu yaliyokaguliwa yalikuwa na mzunguko wa fedha wa shilingi trilioni 4.2 na kodi iliyokaguliwa ni shilingi bilioni 152 katika lile eneo. *Just* makampuni 20 yaliyofanyiwa ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukienda namna hiyo, kwa mantiki hiyo hiyo, maana yake sasa, kama tutayakagua makampuni yote 504 kwa mwaka, tunategemea kwamba tutapata mzunguko wa fedha zaidi ya shilingi trilioni 105 na tunategemea kodi zaidi ya shilingi trilioni nne katika lile eneo. Tatizo ni kwamba watu wetu wa *TRA* na hicho kitengo chetu cha *ITU, (International Tax Unit)* hakijawezeshwa kikamilifu kufanya haya majukumu na matokeo yake hili eneo la *transfer pricing* tunaendelea kupigwa katika hili eneo. Taifa linaendelea kupoteza mabilioni ya fedha katika hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, akiwekeza nguvu zake katika hili eneo, tutakusanya matrilioni ya fedha. Hapa tunaweza kukusanya shilingi trilioni nne na zaidi katika hili eneo, lakini ni fedha ambazo hatuzikusanyi na tunapigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tunaweza kukusanya mapato ni maeneo tu hayo mengine kama kuziba mianya hiyo kama ya Bandari bubu, ukokotoaji sahihi wa kodi tunaoweza kuufanya katika maeneo; na katika eneo hili peke yake kama tunaweza kufanya vizuri sana, tunaweza kuongeza mapato mpaka shilingi trilioni 4.71.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mkataba wa *ETS* ambao unatumika kukusanya kodi za ushuru wa bidhaa. Mkataba huu umeingiwa tofauti na mikataba mingine. Kwanza, ni mkataba wenye bei kubwa sana, una gharama kubwa sana. Wananchi wanaingia gharama kubwa sana lakini hautoi gawio lolote lile kwa Serikali. Huyu anakusanya fedha zake anakwenda; na sasa hivi haijaelezwa uwekezaji wake ni shilingi ngapi? Haijaelezwa pia hata yeye analipwa

shilingi ngapi kwa mwaka? Sasa kutokana na utata huu, kwanza mkataba huu ni lazima uchunguzwe vizuri ili kuona na kuweka uwazi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili mapato yanayopatikana tugawane kama tunavyogawana kwenye mtambo wa *TTMS,* kwa nini *TTMS,* kule *TCRA* tunagawana asilimia 50 kwa 50? Mwekezaji anapata 50 na Serikali inapata 50. Katika huu mtambo wa *ETS* ambao ni ubia kati ya *TRA* na kampuni ya *CISPA* hatupati chochote kama Serikali; na tukigawana hapa tunaweza kupata mapato ya karibia shilingi bilioni 150 kwa fedha anazozipata sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Msajili wa Hazina tunaweza kufanya maboresho madogo tu tukapata fedha nyingi sana. Tuna kampuni nyingi na mashirika mengi sasa hivi ambayo yamekuwa *parasite* kwenye Taifa ambayo tunalazimika kuyawezesha fedha kila leo badala ya yenyewe kutoa fedha kwa Serikali. Mashirika haya, yanahitaji mtaji tu. Yakipewa mtaji na Serikali yanaweza kutoa gawio kubwa sana kwa Serikali. Sasa hivi tunakusanya mapato kidogo sana na mwaka huu yameshuka kwa zaidi ya shilingi bilioni 81. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa ardhi hivyo hivyo. Ardhi tuna fedha nyingi kule. Sasa hivi kwa mujibu wa Taarifa ya *CAG* ana malimbikizo ya shilingi bilioni 61, hatujajua tatizo ni nini kule kwenye ukusanyaji? Huyu naye akiwezeshwa fedha, tunaweza kuongeza mapato. Haya maeneo tunaweza kuongeza mapato hata tukafikia mpaka shilingi bilioni mpya kutoka kwenye kiwango Mheshimiwa Waziri alivyokisia, shilingi bilioni 260 tunaweza tukafikia mpaka hata kwenye shilingi bilioni 300 na zaidi kwenye hili eneo tu la ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye madini na kwenyewe kuna shida kwa sababu masoko yale 39 tuliyoyafungua na vituo vya kuuzia madini 50 vinafanya kazi siku za kazi tu, lakini siku za *weekend* hazifanyi kazi na kutusababishia kupoteza mapato mengi. Hili eneo pia tunaweza kuongeza mapato mengi. Katika hili eneo tu kwa

hesabu zangu nimepata shilingi trilioni 7.1 ambazo zinaweza zikapatikana nje ya bajeti ya Serikali iliyotengwa. Shilingi trilioni 7.1 tunaweza kuzipata tukienda kuimarisha haya maeneo ambayo nimejaribu kuyataja katika huu muda mfupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la kufanya marekebisho ya Kanuni Na. 15 ya ukokotoaji wa kodi za Kimataifa *(transfer pricing)* ambapo Waziri anapendekeza kuondoa faini ya asilimia 100 katika miamala ya *transfer pricing.* Mheshimiwa Waziri, ukifanya hili kosa la kuondoa hiyo faini, nchi yetu utakuwa umeiingiza kwenye mtego wa kupigwa kila siku. Ni bora ukasema unataka upunguze adhabu ili kuongeza *compliance,* lakini ukisema hawa ma-*tycoon* hawa ambao wanafanya biashara kubwa na ziko *organized* na wanahamisha faida kutoka nchini na kuzihamisha kupeleka nchini kwao, unasema wakifanya miamala yao hiyo ya wizi halafu *then fine* yao ikaondolewa, tutapigwa na hakuna duniani kote ambako sasa hivi wanaweza kuikubali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata *best practice* duniani kote, kwa sababu upigaji mkubwa na wizi mkubwa wa kodi sasa hivi uko kwenye eneo la *transfer pricing.* Ni lazima tukawekeza vizuri kuhakikisha kwamba tunawabana ili kila mtu alipe katika hii miamala. Tuhakikishe kwamba ukaguzi wa kampuni zote 504 unafanyika ili Serikali yetu iendelee kupata fedha zinazostahili. Tukifanya hivyo, mapato ya Serikali tutakuwa tumeyaongeza kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan ajiandae.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa nafasi hii. Mimi pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuja na bajeti yake ya kwanza nzuri sana. Nampongeze Mheshimiwa

Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu wake na uongozi wa Wizara kwa ujumla kwa bajeti hii ambayo kusema kweli imezingatia maoni ya Wabunge pamoja na maoni ya wadau wengi na ninaamini kwamba imewafurahisha wananchi kwa ujumla katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu makubwa ambayo siyo sana ya kutaka kuingia ndani *in detail,* lakini niseme mambo matatu makubwa ya kisera. Kwanza, nikiangalia bejeti hii, kusema ukweli ni *contractionary budget.* Yaani ni bajeti ambayo haitaweza kukuza uchumi kwa kiwango kile ambacho tungetarajia. Kwenye wasilisho la hali ya uchumi wa sasa hivi tumeambiwa kwamba tumekua kwa asilimia 4.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kwamba tutakua kwa asilimia 5.6 mwaka ujao, 2022. Kwa nini tufikie asilimia 5.6 badala ya kurudi asilimia saba ambapo ndiyo *long term trajectory* yetu kwa miaka mingi? Wakati tumeshashuka mwaka huu tukapunguza ile kasi, tutawaona kwamba kwenye nchi nyingine ambazo wametekeleza aina fulani ya sera, utaona kama Ulaya zinaanza kurudi na kuwa mara mbili ya ile waliyokuwa wamebajeti mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tatizo ni kwamba ukiangalia bajeti, sera zilizomo humu ndani za *fiscal* na *monetary* utakuta zote ni *contraction.* Kwa nini? Kwa mfano, ukisoma bajeti ya mwaka jana, 2020 na ukisoma *Monetary Policy Statement* ya mwaka 2020 na ya miaka mitabo iliyopita kwa ujumla hutaona tofauti. Wanabaki pale pale kwamba tutakua kwa asilimia saba. Naamini kwamba ndiyo sababu tumebakia tunakua kwa asilimia saba kwa sababu hatubadilishi zile sera za ujumla, zinabakia ni zile.

Kwa hiyo, kama hubadilishi ile sera uka-*promote growth,* ni kwamba hutaweza ku-*break through out of your long term* hiyo ambayo tumekuwa tunaiendeleza asilimia sita au saba kwa miaka zaidi ya 10 toka wakati wa awamu ya nne na ya tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini ukweli ni kwamba ukiangalia sekta ya fedha, utakuta kwamba tatizo ni kwamba kama unashikilia *inflation* kwenye tarakimu kati ya tatu na tano kwa miaka 10 au 20, umejenga *fiscal space* kubwa sana ya kuweza kukopa na kuongeza fedha za kuendesha miradi katika nchi yetu; ya Serikali *in this case,* lakini pia inafungua fedha zile zilizo benki ziweze kwenda kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba sera hii ya kushikilia *inflation* kwenye asilimia tatu, maana yake ni kwamba mikopo isikue. Kwa sababu *the only way* unavyoingiza fedha kwenye uchumi ni kwa mikopo au kwa kuuza fedha za kigeni. Sasa sisi mikopo yetu tumeishikilia, Serikali inakopa kidogo na sekta binafsi inakopa kidogo, kwa hiyo, kwenye uchumi kunakuwa na ukwasi mdogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua Marekani ni nchi ambayo *the rate of employment* kule Marekani ni 5% au 6% na wao *inflation* yao inakuwa ni tatu kwa sababu wakichochea kidogo uchumi tayari *inflation* mambo yatakuwa magumu, hawatapatikana watu wa kufanya kazi. Hapa kwetu tuna *unemployment* kubwa, kwa hiyo, tunaweza tukaweka mkopo kwa sekta binafsi, sekta binafsi ikaajiri na uchumi ukaanza kukua kwa 7%, 8%, 9% au 10%. Ni *very easy. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba utakuta kwamba riba ni zile zile miaka hii yote. Toka mimi nianze kusoma hii *serious,* riba zinazotokana na Sera ya Fedha ni zile zile za zaidi ya asilimia 10. Ukiangalia nakisi ya bajeti ambayo sasa ni *budgetary policy* ni nakisi ile. Ukiangalie, yaani kitu unapotaka kuangalia zaidi kwenye bajeti ni nakisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia nakisi ya bajeti ambayo sasa ni *Budgetary Policy,* yenyewe *Budgetary Policy* ni nakisi ile. Uiangalie yaani kitu unavyotaka kuangalia zaidi kwenye bajeti nakisi. Ukiweka nakisi ndogo maana yake Serikali inajinyima kwenda kukopa fedha kwa sababu,

maana yake ni kitu ambacho lazima ukipate nje ya mapato uweze kukiingiza kwenye uchumi wako. Na sasa hivi kwa sababu kuna *fiscal space* ya muda mrefu ya *low inflation* unaweza ukakopa hata kwenye Benki Kuu, tumeona sasa wameanza kukopa Benki Kuu kwa kasi kubwa kidogo na hiyo ni kitu kizuri kwa sababu, tunaingiza fedha kwenye uchumi, na watu wakishaleta bidhaa zao wanaweza wakaongezea mikopo yao wakazalisha. *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo nasema kwamba, bila kufanya marekebisho hapo na niwakumbushe wale waliosoma kidogo, kuna *trade off* kati ya *inflation* na *growth. Trade off kati* ya *inflation* na, unaongeza *inflation* unaongeza na *rate of wealth growth* mpaka *a certain level* hapo *inflation* inapokuwa kwamba, ina *cause employment* imeshafikia mwisho ndio unasema hapa sasa nikienda zaidi nitajikuta napata hasara kwa sababu hata *labor cost* inakuwa sasa ni *structural inflation* imejitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kusema kwamba, hii *issue* ya *contraction monetary policy* na *fiscal policy* tuiangalie, nakisi sasa imeshuka wameishusha kutoka asilimia 3 kwenda asilimia 1.5 maana yake Serikali isikope, isitafute fedha mahali pengine ikaingiza kwenye uchumi uchumi ukakua; uchumi hauwezi kukua bila kuwekeza, sasa hiyo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme pili,nasema kwamba, ukiangalia kwa upande wa mapato ijapokuwa wana-*protect* ifike kwenye 23 *plus,* lakini ukweli ukiangalia mapato ya mwaka huu hayatafikia trilioni 18. Mpaka sasa hivi ukichukua takwimu za mwezi Mei ziko itafikia, nimepiga hesabu haiwezi kuzidi trilioni 18, sasa trilioni tano utazipata wapi? Uongeze ufike *23 trillion?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo una *over estimate,* tumesha-*over estimate* kwenye hii bajeti, lazima tuangalie ni wapi tupate au tuongeze vipato wanavyoshauri wengine kwenye simu, *whatever.* Japokuwa wanawema ukiweka kwenye simu au ukiweka kwenye miamala hii watu watarudi

kule kwenye matawi ya benki, benki zitafurika watu. Watu watasema kwa nini nikachukue kwenye *M-Pesa?* Nitaenda kwenye benki kwenye matawi nichukue pesa yangu *cash* kwa kulekule hudai kwa hiyo, sasa tatizo utaongeza mpaka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vitu hivi ambavyo vina *alternative ways* tukivishika tutapata matatizo. Kwa hiyo, nasema kwamba, ukweli ni kwamba, hilo ni tatizo na niseme hivi kuna hii *issue* kwa mfano kwenye upande wa mapato *unpredictability, again* mambo ya *policy unpredictability* yamejiingiza hapo.

Kwamba, unaweka ushuru kwa mwaka mmoja, nasema tumeweka huu kwa mwaka mmoja, hii kwa mwaka mmoja, sasa wewe mtu utafanyaje maamuzi ya kuwekeza wakati wewe unajua kwamba, huu ushuru umepata unafuu wa mwaka mmoja tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka ushuru ukae kwa miaka mitatu, minne, kabla hujajigusa. Tatizo hapa tunasema *tax current* kuwe na *tax current* ya kwamba, nikipandisha mwaka huu nitakaa miaka mingine mitatu kabla sijapandisha. Kwa hiyo, mtu akitaka kutumia ile *opportunity* anawekeza kweli kama *unpredictability* tunazidi kuiongeza hapa haitasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu nasema hivi kodi hii ambayo wanakamati wa bajeti wameisema ya *LUKU; LUKU, eehee, LUKU* ni watumiaji wengi ni wapangaji. Sasa wewe ukaenda kutumia unamtoza mwenye *property* au unamtoza aliyepanga *property?*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie vizuri namna ya kukusanya. Ni kodi nzuri ni ubunifu, lakini tuiangalie namna ya kukusanya na kitu kama hicho. Lakini niseme hivi kwenye upande wa ku-*allocate resources* zetu tunaziweka sana kwenye miundombinu, sawa, lakini tujiulize ni kitu gani tunafanya ili watu waanze kuona *opportunities* kwenye *central corridor* kwa mfano kwa sababu sasa *SGR is coming,*

lakini hebu niambie toka tuanze kujenga *SGR* mpaka Morogoro ni watu wangapi wameenda kuanza kuwekeza au hata kuulizia nijenge kiwanda gani? Niweke kitu gani? Niweke shamba gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hamna watu wamekaa kimya tu kwa sababu, kuna vitu vingine ambavyo havijafanyika kuweza ku-*motivate production* na *investment* katika hii nchi. Mwisho, *but not the last* kwa sababu muda tu. Niseme *execution, execution* unakuja kuona mwisho wa mwaka, unaona hela nyingi zinaanza kutolewa *quarter* ya tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *issue* ninayoomba ni kwamba, fedha hasa hizi za maendeleo tujaribu kuzipangilia kwa mpango kwamba, zile ambazo tunakopa tuzikope mapema, ili zianze kutekeleza miradi ya maendeleo tusingojee mpaka *quarter* ya nne ndio tuanze kupata pesa kwa sababu hizi zinakusanywa kwenye kodi *mostly for the current purpose,* lakini hizi za maendeleo ni fedha ambazo zinatakiwa zipatikane *immediately.* Tutafute wale watu wanaotukopesha watukopeshe, tutafute *donors* wazilete mapema tuanze kuzitumia kwenye miradi ya maendeleo, tuanze kuzi-*disburse* mara moja hasa kule kwenye wananchi zifike mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha mwisho ni *issue* hii ya ahadi za viongozi. Tuliahidiwa na Wabunge hapa tulipokuja tuliahidiwa kwamba, zile ahadi za viongozi kwa wananchi wetu kule kwenye majimbo zitaorodheshwa ziwekwe kwenye vipaumbele tuambiwe kwamba, hii ya kule Vunjo itatekelezwa mwaka wa tatu. Nikitajiwa hivyo nitasema haleluya, lakini kama hatujajua kwamba, zile ahadi zimewekewa mchakato gani wa kutekeleza itakuwa kwamba, tunabakia tunaenda kule wataanza kutupa mawe wewe ulizungumza hivi, tupeni tuende na hicho kitu. Nimesema hapa kwa sababu najua ni kwenye mambo ya *execution. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unisamehe kwa kuzidisha kidogo, lakini nataka kusema naunga mkono hoja hii vizuri sana. Na haya niliyosema ni mambo tu ya kuboresha tunaenda mbele, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Nilikuwa najaribu kuangalia nifahamu Mheshimiwa Musukuma yuko wapi ili asikilize wachumi wakiongea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhani. Mheshimiwa Neema Kichiki Rugangira ajiandae.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nitoe mchango wangu kidogo kwenye Hotuba ya Bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwanza nimpongeze yeye Waziri wa Fedha na pia Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti kwa uwasilishaji mzuri, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nianze kuchangia maeneo ya uchumi machache, lakini mwishoni nitatoa pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze pale ambapo mwenzangu ameishia. Nimekuwa nikishangaa sana ninapoona Wachumi wa Benki Kuu, Wachumi wa Wizara ya Fedha na Wachumi wa Serikali wanatamba kwenye taarifa mbalimbali unajua Tanzania tuko imara, mfumuko wa bei uko asilimia 3 hadi 5 kwa miaka miwili mfululizo iliyopita na maoteo hivyohivyo mwaka ujao, halafu wanatamba kwamba, ni kitu kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hilo sio zuri kwa sababu tuna uchumi imara. Tuna *stable economy,* ilitakiwa wacheze na *buttons* za kuweza kuruhusu *inflations* angalau isogee kwenye viwango vya *SADC* kati ya asilimia 5, asilimia 6, asilimia 7, asilimia 8, ili kuweza kuufumua uchumi usisimke watu wawekeze wapate faida za muda mfupi na muda wa kati, ili uchumi uweze kuwa *stable* zaidi na kutozalisha ajira

kwa wingi na tuzalishe fedha kwa wingi ndani ya nchi, lakini iliyopo sasa hivi ni kwamba, uchumi ni kama vile uko-*dormant.*

Kwa hiyo, suala hili la *inflations* asilimia 3 nikizungumzia kwa upande wa wakulima, wameathirika vibaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uhamasishaji wa Serikali wakulima wamezalisha mazao ya chakula, wameongeza kwa zaidi ya tani milioni mbili katika kipindi cha miaka mitano iliyopita; mwaka 2015 walizalisha tani milioni 15 mpaka ilipofika 2019 tulikuwa na tani milioni 17 za chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu ya *inflation* iko asilimia 3 matokeo yake ni nini, debe ambalo lilikuwa linauzwa shilingi 6,000, 8,000 mwaka 2015 leo linauzwa shilingi 3,000 hadi 5,000, ni kilio kikubwa sana kwa wakulima. Lakini suluhisho ambalo lingeweza kuchukuliwa na Serikali ambalo sijaliona kwenye hotuba ni kuwa na *price stabilization fund* ambayo ungeweka *buffer stock* wakulima wakizalisha zaidi ya mahitaji ya soko la ndani Serikali inanunua kilichoongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mwaka jana ingenunua tani milioni tatu ina maana kwamba, leo debe la mahindi lingeuzwa shilingi 6,000 na kuendelea, bado wakulima wasingekuwa kwenye kilio. Kwenye bajeti hii sijaona ile *stabilization fund* ya Serikali kwa sababu, Serikali lazima iongeze matumizi katika kuokoa uchumi wa nchi, hasa uchumi wa wakulima, lakini vilevile suala hilo lingeweza kuwapa nafuu wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, mfano sera za fedha zinatwambia kwamba, mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi umekuwa ukishuka. Mwaka 2019/2020 ulikuwa asilimia 13.5, mwaka 2020/2021 ulikuwa asilimia 11.6, maoteo ya mwakani 2021/2022 itakuwa asilimia 10.6 maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba, wafanyabiashara wanapunguza kukopa kwenye benki. Maana yake nini? Maana yake benki zinaatamia fedha. Fedha zinakuwepo, lakini hakuna mkopaji. Kwa sababu, gani hawakopi? Kwa sababu kuna masgarti ambayo sio rafiki ya riba ambayo yanaathiri faida. Mtu huwezi kukopa kwa sababu huwezi kupata faida na huo mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania pekee ndio utakuta tofauti ya riba ya mkopo na tofauti ya riba ya amana iko kati ya asilimia 7 mpaka asilimia 10. Hii ni mbaya sana na upunguaji wake umekuwa unapungua chini ya asilimia 1, sasa *data* hizo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili inatakiwa Serikali ifanye utaratibu mzuri wa kwanza kutokutafiti sababu ni nini? Sababu ni hiyo tu riba au kuna sababu nyingine ambazo zinasababisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo ningependa kulichangia; leo nimemtoa mtoto nenda dukani kanunue lita moja ya mafuta ya kula ya alizeti, kaambiwa dukani kwenye duka la jirani shilingi 9,000. Chupa hiyo hiyo ya lita moja ya alizeti mwaka jana nilikuwa nainunua shilingi 4,500 maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake kuna shida kubwa ya mafuta hapa nchini. Na viwanda vyetu ambavyo vilikuwa vinazalisha mafuta vimepunguza kuzalisha mafuta, ukiwauliza wanakwambia hatuna malighafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali nimeona juzi Waziri Mkuu alikuwa Singida, hiyo mikakati ambayo wanaifanya kupitia mikutano ya wadau haitoshi. Inatakiwa ionekane kwenye *Government expenditure* wamechukua hatua gani za wazi za kuhakikisha kwamba, viwanda vyetu vinapata malighafi ya kuzalisha vitu ambavyo vinaumiza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ningependa nitoe pongezi. Natoa pongezi bajeti kwa kweli, bajeti kwa ujumla katika maeneo fulani, fulani bajeti imekuwa nzuri sana, hongera sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana kwa mikakati ya kuongeza fedha kwa *TARURA,* kimekuwa kilio kikubwa kwa wananchi. Barabara za vijijini ni ukombozi mkubwa sana wa wananchi kuweza kusafiri wao wenyewe na kusafirisha mazao yao kwenda katika masoko, hilo ni jambo moja zuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nime-*calculate* hapo mtaongeza karibu bilioni 400 kwa ajili ya *TARURA,* hicho ni kitu kimoja kizuri sana, lakini vilevile mtaongeza fedha kwa ajili ya maji, mtaongeza fedha kwa ajili ya umeme. Hiyo ni pongezi kubwa sana nawapa, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu utapata umaarufu mkubwa endapo masuala hayo matatu yatatekelezwa vizuri na kusimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pongezi kwangu kule mmeweka fedha shilingi bilioni 5 kwa ajili ya kuanza kujenga Barabara ya Ipole – Rungwa. Nawaombea mwakani muweke angalau bilioni 100 kwenye barabara hii kwa sababu, huwezi kuweka bilioni 5 kwenye barabara ya kilometa 172.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu pongezi nyingine maji Ziwa Viktoria yatafika Sikonge, karibu zaidi ya bilioni 25 hongera sana, lakini Barabara ya Sikonge – Mbono – Kipili itakamilika. Barabara ya Tutui – Zimbili itaendelea kuwekwa changarawe, lakini vilevile tutaendelea kujenga Barabara ya Tabora – Sikonge – Mpanda ambayo nadhani ndani ya miaka miwili ijayo itakamilika. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tuna mpango mzuri wa kumalizia vijiji kuvipa umeme, lakini kuna kufikisha umeme kwenye Bwawa la Igumula. Kuna kufanya sensa mwaka 2022; hiyo sensa naipa kipaumbele cha juu sana na nitashiriki

kwenye Jimbo langu la Sikonge siku zote za hiyo sensa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hongera sana kwa Serikali kupeleka mawasiliano ya simu kwenye kata zote za Jimbo la Sikonge ifikapo mwishoni mwa 2021/2022, lakini pongezi nyingine ni kwa Serikali kuanzisha *nature reserve* katika eneo la Sikonge ambayo itasaidia kupunguza eneo lililohifadhiwa na kuongeza eneo la wananchi kuishi na kufanya shughuli zao za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea utekelezaji wa mambo hayo uwe wa makini kwa sababu Serikali hii naiamini sana. Naamini hizi ahadi zote ambazo zimewekwa kwenye hotuba ya bajeti na hotuba za bajeti za kisekta naamini zitatekelezwa. Naomba sana niwashukuru sana Serikali, ahsanteni sana Serikali. Karibuni Sikonge tufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramdahan, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira. Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Hamanilo ajiandae.

MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa fursa hii ya kuchangia kwenye hoja ya bajeti iliyoko Mezani. Nichukue fursa hii kumpongeza na mimi kama wenzangu Waziri wa Fedha kutokana na uwasilishwaji wake mzuri wa bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitaalamu sio mchumi ni Mwanasheria. Kwenye sheria za uwakala kwa kitaalamu tunaziita *Law of Agency,* kuna usemi wa kilatini unaosema *kuifasi pa alyum fas perse.* Tunapompongeza Mheshimiwa Waziri tunampongeza yeye pamoja na timu yake yote walioandaa bajeti hii. Tunampongeza yeye pamoja na Baraza lote la Mawaziri kwa sababu, alichokileta ndani ya

Bunge hili sio mawazo yake peke yake, ni yake yaliyochangayika na Mawaziri wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapolipongeza Baraza la Mawaziri tunampongeza Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia. Kwa hiyo, kilicholetwa mbele yetu ni maamuzi ya Serikali n ani maamuzi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa tanznaia. Mnafanya kazi nzuri kama Serikali, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri ameleta mapendekezo 15 ya kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, kuanzia *page* ya 28 mpaka ya 31, mapendekezo 15. Moja ya mapendekezo hayo amekuja kuomba kufanyiwe marekebisho ya sheria ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyumba vya ubaridi, *cold rooms. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoitazama bajeti hii ni kwamba, kwa asilimia 90 imesikiliza vilio vya Wabunge. Haya ndio ambayo yalikuwa yakipigiwa kelele kila siku na Waheshimiwa Wabunge humu ndani kwa hiyo, ni bajeti ambayo imesikiliza na kuliheshimisha Bunge. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani hiki kilio kimeliliwa sana humu na Dada yangu Mheshimiwa Neema Kichiki, mama lishe. Kwamba, inaenda kuongeza thamani ya mazao yetu ya mbogamboga kwenye sekta yake ya lishe ambayo itaenda kusaidia wakulima wanaolima mbogamboga na mauwa kuongeza thamani ya mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ameleta mapendekezo ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye madini *precious metals* Wabunge wa kanda Mungu aliwajalia madini, hasa Kanda za Ziwa, Geita na kwingine, Mheshimiwa Musukuma, wamelia sana. Wakati wa uchangiaji wa jumla tuliyasema haya sana ambayo hiyo inaenda kuongeza thamani kwenye viwanda vyetu vya uchenjuaji wa madini

ambapo jana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua kiwanda kimoja, inaenda kuongeza fedha za kigeni, inaenda kuongeza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameleta mapendekezo ya kusamehe kodi kwenye ongezeko la thamani kwenye huduma ya bima ya mifugo. Wabunge Kaka yangu Mheshimiwa Nicholaus Ngasa, wamelia sana kuhusu hili, ndio ambalo Mheshimiwa Waziri kalichukua kalileta ndani ya bajeti kwa sababu, lilikuwa kilio cha Wabunge. Ameleta mapendekezo ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye nyasi bandia; rafiki yangu hapo Mheshimiwa Sanga amelipigia kelele hili, kwa hivyo limechukuliwa likaja likawekwa kwenye bajeti kwamba, linataka utekelezaji. Maana yake ukiiondoa hii inaenda kukuza yale mawazo ya Mheshimiwa Sanga ya kukuza mpira wetu na kuleta viwanja vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameleta mapendekezo ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye kadi za kutengenezea *National ID.* Haya yamepigiwa kelele sana, upatikanaji wa *National ID* umekuwa tatizo, labda kutokana na gharama za uzalishaji kwa hiyo, Waziri akaleta mapendekezo, ili tupunguze huko hizi *ID* zipatikane kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameleta mapendekezo ya kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye simu janja, haya aliyasema kaka yangu Mheshimiwa Jerry. Tunataka kutoka asilimia 40 ya matumizi ya mitandao tunaelekea asilimia 86, hatuwezi kufika kwenye hiyo *target* kama gharama za simu janja, *moderm* na vishkwambi viko juu. Ndio hayo ambayo Serikali wameyaleta kwetu kwa sababu, hicho ndio kimekuwa kilio chetu cha muda mrefu; dada yangu Mheshimiwa Judith Kapinga haya kayasema sana kwa hiyo, yamechukuliwa mawazo yake yameletwa kwenye bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kaleta mapendekezo ya kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye

mikebe inayotumika kuhifadhia maziwa. Hapa yamesemwa hatusafirishi maziwa nje ni kwa sababu, kulikuwa kuna gharama za uhifadhi wa maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Zanzibar ambalo ndiyo limenikuna kweli kweli Waziri ameleta mapendekezo ya kuondosha au kurudisha utaratibu wa *VAT* kwa bidhaa inazonunuliwa Tanzania Bara na zinazotumika Zanzibar. Wafanyabiashara katika Jimbo langu la Chakechake na Wazanzibar kwa ujumla wafanyabiashara wakubwa kama *hardware's* kwa asilimia 80 sasa hivi wanaagiza bidhaa kutoka Tanzania Bara hawaendi tena China, hawaendi tena India, hawaendi tena nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nondo tunanunua Tanzania Bara, saruji tunanunua Tanzania Bara, *wire* za umeme tunanunua Tanzania Bara, tunanunua Tanzania *Bara gypsum board, gypsum powders*, bodi za kujengea, misumari, *wires* na tumekuwa tukililia hili kwa muda mrefu jirani yangu haya Mheshimiwa Abdul-Hafar wakati wa mchango wake alilisemea hili kwa sana kwamba kumekuwa na ukiritimba wafanyabiashara wanaotoka Zanzibar wakija wakinunua bidhaa zao Bara na kuzirejesha Zanzibar na hiki ndiyo kilio ambacho Mheshimiwa Waziri amekileta na Serikali ya Mama Samia wamelisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lango ni kutaka kuondosha hiyo migongano, watu ambao walikuwa hawapendi muungano wetu walikuwa wanatumia mwaya wa kutubomoa sehemu hii, ya kuonesha hii ni nchi moja mbona mnanyanyaswa mkifika Bara. Sasa haya ndio yanakwenda kuondoka maana yake sasa unaondosha *VAT* kwa sababu *VAT* inalipwa na yule mtumiaji wa mwisho mlaji.

Kwa hiyo ukiweka *VAT* akija Bara analipa halafu akifika Zanzibar analipa mara mbili, anafanya *double* maana yake anaiongeza thamani bidhaa yake ili apate kufikia ile *VAT* aliyoitoa mara mbili na bidhaa inapanda bei kwa hivyo haya yanakuja kuondosha tatizo na kupunguza bei na kuwasaidiwa wananchi wetu walioko kwenye maeneo yetu

na wafanyabiashara kufanya biasahra bila kusumbuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tatizo lilikuwa linatokea pia kwenye umeme tumesema sana kwenye *TANESCO* walipokuwa wanatuuzia umeme *ZEC* kwenda Zanzibar walikuwa wanatutoza *VAT* na ndiyo hayo madeni ambayo yalikuwa yanalalamikiwa na ikishafika umeme Zanzibar kwenda kwa mlaji mimi ili uingie kwenye nyumba yangu nalipa tena *VAT,* kwa hiyo mapendekezo haya yakishafanyiwa kazi maana yake yanaenda kuondoa hizo *double VAT* kwa sisi watumiaji wa mwisho wa umeme maana yake hii inaenda kurahisisha maisha ya wananchi watu. Kwa hiyo, nilivyoisoma bajeti hii kuanzia *page* ya mwanzo mpaka ya mwisho ya 121 hakuna kitu ambacho kilikuwa kinanipa furaha wakati nasoma kama nikiona haya yamesemwa na Mheshimiwa Waziri. Maana yake ndiyo yalikuwa vilio vya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Chakechake, naunga mkono hoja bajeti hii imetuheshimisha sana Bunge, Mungu aibariki sana Tanzania na Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira atafuatiwa na Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda niungane na Wabunge wenzangu kuipongeza sana Serikali kwa bajeti nzuri na bajeti ya kimkakati ambayo inakwenda kuinua wananchi wote hususan wananchi wa chini. Kipekee kabisa napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kasi ambayo amekuja nayo na nia yake ya dhati ya kuhakikisha kwamba maendeleo yanawafikia Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi napenda nichangie kwenye eneo la vyanzo vipya vya mapato, hapa nitaanza na eneo langu la kwanza ambalo linahusu huduma ya sekta hii ya ki-*digital* kwa mujibu wa takwimu za *TCRA* Tanzania ina jumla wa watumiaji wa *Internet* Milioni 29 lakini vile vile ina jumla ya watumiaji wa huduma za kupokea fedha kwa njia za mtandao wa simu Milioni 32 hivyo hii sekta ya ki-*digital* ni sekta kubwa na ninaipongeza sana Serikali kwa kutambua hilo na hata kuunda Wizara mpya ambayo ina dhamana ya masuala mazima ya *TEHAMA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kumshauri Waziri na Serikali kwa ujumla ifanye mapitio ya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014 ili sheria hizi mbili ziweze kuwa na vifungu vitakavyowezesha utozwaji wa kodi kwenye biashara ya sekta hii, napendekeza Serikali ije na kodi ya huduma za ki-*digital* kwa maana ya *digital service tax* nasema hivi kwa sababu hivi sasa kuna huduma nyingi zinafanywa na sekta hii ambazo chanzo chake ni ardhi ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwakuwa chanzo chake ni ardhi ya Tanzania basi Serikali inayo fursa ya kutoza kodi aina ya *digital service tax* nitatoa mfano mdogo, matangazo ya biashara yanayofanywa kupitia *online platforms* yaani mitandao ya kijamii kama *Facebooks, Instagram, Twitter Google* nayo yanaweza kuwa ni fursa ya kutozwa kodi, vilevile yapo masoko ya kimtandao ambayo yanakutanisha wanunuzi na wateja kama *Amazon, E-bay, Alibaba, Kikuu* na kadhalika, nako kunaweza kukawa kuna fursa ya kutoza kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia zipo biashara za kukodi usafiri na hoteli kama vile wengi tunatumia *Uber, Boat, Airbnb booking.com* nayo ni fursa ya Serikali ya kutoza kodi, lakini pia lipo eneo hili la michezo ya kubahatisha yaani *online betting.* Nimeona Serikali imependekeza kushusha ile *gaming tax on winning* kutoka asilimia 20 kwenda asilimia 15 lakini kiuhalisia wengi wanapenda kutumia *online betting* kwa

sababu unapocheza *online betting* hakuna kodi ambayo unalipia kwa hiyo nayo hiyo ni fursa ya Serikali kutoza kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuikumbusha Serikali kwamba hivi sasa tunao kakribani Watanzania Millioni 5.9 ambao wanatumia mitandao hii ya kijamii. Hivyo kwa mantiki hiyo, ninaiomba sana Serikali iiangalie sekta hii kwa jicho la kipekee na ije na utaratibu wa kutoza kodi ambayo inaweza ikaenda kwa jina la *digital service tax* ili kuhakikisha kwamba Tanzania tunanufaika na sekta hii ambayo inakua, ambayo inaendana na *digital economy* na hata Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii ya masuala ya *TEHAMA* aliahidi kwamba ataandaa sera ya *digital economy,* kwa hiyo kwa ujumla wake nadhani tutapata fursa ya kupata vyanzo vipya vya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la pili napenda kuongelea nishati ya jua, nafahamu kwenye Bunge lililopita Bunge la 11 Bunge lako Tukufu mlipitisha kuweka msamaha wa kodi wa ongezeko la thamani kwenye vifaa vya nishati ya jua *(solar)* lakini kwenye mapendekezo ya Mheshimiwa Waziri, amependekezwa kwamba afute msamaha huu, na hii inaendana na ile *unpredictability* ya sera zetu, nasema hivi kwa sababu Serikali imefanya jitihada kubwa sana ya kuhakikisha kwamba umeme unafika mpaka vijijini, lakini mpaka sasa tunavyoongea kuna vijiji takribani 2000 bado havina umeme na hata vijiji ambavyo vina umeme, umeme umefika kwenye *centre* sio kaya zote zenye umeme na sio vitongoji vyote kwa hiyo bado wananchi wetu wanategemea kwa kiasi kikubwa umeme unaotokana na *solar* nishati hii ya jua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule vijijini ukienda wanategemea *solar* kwa ajili ya Zahanati, wanafunzi wanategemea *solar* kwa ajili ya kusomea, wananchi kule wanategemea *solar* kwa ajili ya kupata habari, wanategemea *solar* kwa ajili ya kuchaji simu zao. Mheshimiwa Waziri hili pendekezo la kuondoa ule msamaha wa kodi kitakachokuja kutokea ni kwamba gharama ya kupata vile vifaa vya *solar* itaongezeka kwa takribani asilimia 27 mpaka

asilimia 35 na ambaye atakwenda kuumia kwenye gharama hii ni yule mtumiaji mwananchi wa kijijini ambaye Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan Rais wetu anataka kuhakikisha kila mwananchi popote pale alipo aweze kupata maendeleo na maendeleo ya kiuchumi chachu mojawapo kubwa ni nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ninaiomba sana Serikali kwa unyenyekevu mkubwa wauache huu msamaha wa kodi kwenye eneo hili uendelee kubaki pale pale kwasababu kuiondoa kuifuta ni kumuumiza mwananchi wa chini ambaye Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ndiye anayemtetea na ndiye anaye mpigania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la mwisho ni eneo la lishe napenda tu kusema kwamba, nadhani wakati umefika sasa Serikali iweke jitihada kubwa zaidi na uwekezaji kwenye kinga badala ya tiba, nasema hivi kwasababu kwa taarifa za Serikali kama tutaendelea Tanzania kuwa na hali ya ukosefu wa lishe bora tuliyonayo kwa kipindi cha miaka 10 yaani tangu 2014 mpaka 2025 Taifa letu litapoteza mapato mengi sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka tutakuwa tunapoteza Trilioni mbili kwasababu ya kuwa na hali ya udumavu tuliyonayo, kila mwaka tutapoteza Bilioni 230 kwa sababu ya upungufu wa damu kwa wanawake wajawazito, kila mwaka tutapoteza Billioni 15 kwa sababu ya upungufu wa madini joto, lakini kama hiyo haitoshi napenda niongezee kwamba tutakapokuja kwenye yale magonjwa yasiyoambukiza, ambayo yanamahusiano na lishe kama kisukari, moyo, *pressure*, figo, Inni na aina mbalimbali za *cancer* kwa taarifa za Serikali inasema kwamba kila mwaka Tanzania inatumia bilioni 457 kugharamia magonjwa haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na magonjwa haya yanapelekea hata mfuko wetu wa Bima ya Taifa upo taabani sasa basi, na kama hiyo haitoshi hivi sasa Tanzania inakadiriwa kila mwaka asilimia 2.65 ya pato ghafi la taifa yaani *GDP*

linapotea tu kwasababu ya udumavu. Sasa kama kila mwaka udumavu tu unachangia pato ghafi letu la Taifa lipungue kwa asilimia 2.65, mimi nadhani wakati umefika na Mheshimiwa Waziri pamoja na wachumi wabobezi kabisa ambao tunao ndani ya Wizara watakubaliana nami kwamba wakati umefika Serikali iweke jitihada kwenye kinga badala ya tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningependa kupendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba sera ya chakula na lishe imeshakamilika imebaki tu kupitishwa na sera hii ipo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu naomba sera hii kwa heshima zote na unyenyekevu ifanyiwe kazi, lakini pia napenda kupendekeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ione namna ya kuja na kodi ndogo kwenye vyakula ambavyo vina sukari nyingi, mafuta mengi na chumvi nyingi, hii itamlinda mlaji lakini pia itaipatia Serikali pato zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono ....

NAIBU SPIKA: Hebu ngoja kwanza umesema kwenye chakula chenye sukari nyingi, mafuta mengi wachaji kodi ndogo.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za wenzetu walichofanya hasa nchi za Bara la Ulaya ili kupunguza kasi ya magonjwa yasiyo ambukiza wametambulisha kodi kwa mfano wenyewe wanaiita *sugar tax* kwa hiyo kama juisi ambazo zimewekwa kiwango kingi sana cha sukari basi inatozwa.

NAIBU SPIKA: Sasa umetumia neno kodi kidogo hapo ndiyo tumepata changamoto.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kodi kubwa.

NAIBU SPIKA: Haya ahsante.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo atafuatiwa na Mheshimiwa, Deo Kasenyenda Sanga tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii adhimu nipate kuchangia katika bajeti ya nchi yetu kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuunga hoja mkono hoja zote mbili zilizowasilishwa ya kwanza ya Waziri wa Fedha na ile yetu ya Kamati ya Bajeti. Nimpongeze sana sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti yenye maono makubwa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii imebeba mahitaji ya Watanzania, bajeti hii imebeba matumaini ya Watanzania, bajeti hii imebeba maoni ya Wabunge, bajeti hii imebeba llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi, lakini bajeti hii imebeba dira ya Taifa letu, bajeti hii imebeba maono ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan. Nasema hivyo kwa sababu bajeti hii inakwenda kutupelekea barabara zetu zote mijiji na vijijini Mheshimiwa Rais kupitia bajeti iliyowasilishwa hapa anatengua Sheria ya Usalama barabarani ili tuweze kupata Bilioni 322 kwa ajili ya barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amebeba maono makubwa kwa Taifa letu kwasababu kupitia bajeti hii tunapeleka maji safi na salama kwa nchi nzima, kupitia hiyo ameamua kutengua Sheria ya Posta na Mawasiliano Sura Na. 306 ili tuweze kukusanya Trilioni 1.3 kwa ajili ya kuyafanya haya. Mama yetu amebeba maono makubwa kupitia bajeti hii kwa sababu anakwenda kufanya jambo ambalo limeshindikana kwa miaka mingi bima ya afya kwa

kila Mtanzania, Mheshimiwa Rais anakwenda kutekeleza miradi yote ya kimkakati ikiwemo mradi maarufu ambao mimi huwa ninasimama hapa kuuongelea kila mara mradi wa *SGR* unakwenda kutekelezwa kupitia bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii inakwenda kututengenezea miundombinu ya elimu, kwenye hili upande wa elimu ya juu kupitia bajeti hii watoto wote wa Kitanzania ambao walikuwa wameshapata udahili kwenye vyuo na wakakosa nafasi ya kusoma kwa sababu ya fedha, bajeti hii inakwenda kuwarudisha katika vyuo. Kwa hiyo, bajeti hii ni ya Watanzania na bajeti hii ni ya kwetu na tunakwenda kuijenga nchi yetu kwa kujifunga mikanda wenyewe kama ambavyo Waziri wa Fedha alituambia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali ukiacha maeneo haya mapya ambayo yametengua sheria nne na yakatupatia Trilioni mbili, *TRA* ina *department* Nne ukiangalia hizi *department* kuna moja ya muhimu sana inaitwa *department* ya *customs* na *excise* hii inakusanya asilimia 38 ya mapato yote ambayo *TRA* inakusanya yanatoka kwenye hii *department* hii inatafsiri kwamba kwa lengo tulilojiwekea la kukusanya mapato ya ndani Trilioni 26 ina maana kwamba Trilioni 8.4 zitakusanywa na *department* ya *customs* na *exercise duty*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaitaja hii *department* kwa sababu ndiyo inayohudumia bandari yetu, na ndio inayohudumia viwanja vyetu vya ndege lakini ndio inayohudumia mipaka yetu, Mheshimiwa Waziri wa Fedha twendeni tukafanya mapinduzi kwenye Bandari yetu. Haiwezekani eti bandari yetu ya nchi haina vifaa vya kisasa vya kupakua mizigo na kupakia mizigo. Twendeni tukanunue vifaa hivyo ili mizigo mingi ipite kwenye bandari yetu. Hali ilivyo hivi sasa Bandari yetu inapitisha tani Milioni 17 kwa mwaka, kiwango hiki ni kidogo sana ukilinganisha na bandari ambazo tunashindana nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukafanya mapinduzi kwenye bandari kwa kununua vifaa vilevile tutafanya

mapinduzi kwenye bandari kwa kuziangalia vizuri sheria tunazozitunga kwenye Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge sikilizeni niwaambie Sheria hizi za Afrika Mashariki Tanzania *trading* yetu kubwa ya kibiashara tunafanya na *SADC* tuna *trade* kidogo sana na *East Africa,* wenzetu wamekuwa wajanja sana wana tu-*fix* kwenye sheria hizi hasa hasa zile zinazohusu usafirishaji wa mizigo kutoka bandarini kwenda kwenye nchi tunazozihudumia. Kwa hiyo, tujipange vizuri kwenda kusimamia eneo hilo ili bandari yetu ipitishe mizigo mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile baada ya kupitisha bajeti hapa wenzetu wa Serikali tunawapa kazi ya kwenda kuitekeleza bajeti, siku zote hapa tumekuwa tukitaja suala la *monitoring and evaluation, budget circle* yetu ilivyo, ina sheria hapa Bungeni kupitia Sheria yetu ya Bajeti, inaangazia *draft* ya *budget*, inaangazia *approval* ya bajeti ndiyo tunachokifanya hapa sasa hivi tupo kwenye hiyo *stage* ya *approval,* vilevile inapoingia *stage ya execution kwenye stage* ya bajeti ndipo ambapo Sheria yetu inakosa nguvu, inakosa nguvu. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ikalete *policy* ya *monitoring and evaluation* ili tutunge sheria na hili hapa limekuwa likizungumzwa na kukosewa kosewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuhitaji kutengeneza *independent board* yeyote hapa, Bunge ndiyo jukumu lake hili yaani tunachotakiwa sasa sisi ni kuendelea kusimamia Serikali kwa maana ya *monitoring and evaluation* kipindi tutakapokuwa tumeitunga sheria hiyo ya *monitoring and evaluation* ili tuweze kuisimamia Serikali vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho niipongeze sana Serikali, nimpongeze sana Mama yangu Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu mimi ni shahidi tosha kwamba bajeti aliyoileta hapa imezingatia maoni yote ya Wabunge yakiwemo maoni ambayo tumeshauri hapa ya ku-*finance* miradi mikubwa kwa kutumia *infrastructure bond*, ipo hapa imetajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali nimpongeze sana mama yangu Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano, kwa sababu mimi ni shahidi tosha kwamba bajeti aliyoileta hapa imezingatia maoni yote ya Wabunge yakiwemo maoni ambayo tumeyashauri hapa yaku-*finance* miradi mikubwa kwa kutumia *infrastructure bond,* ipo hapa imetajwa. Bajeti pia imechukua maoni yetu Wabunge ya kufanya *credit rating* ya nchi yetu, ipo hapa imekaa. Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana, ondoa mashaka hautakuwa *unpopular,* utakuwa ni *popular finance Minister* kwa sababu umeyabeba maono ya Mheshimiwa Rais ukatuletea hapa kwa kadri ambavyo alielekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo nikushukuru sana ahsante sana kwa fursa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Deo Kasenyenda Sanga tutamalizia na Mheshimiwa Dkt Hamis Kigwangala.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu. Kwanza nianze sana kwa kumshukuru Rais wetu mpendwa wa Awamu ya Sita Mama Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti ambayo imegusa na imetii mahitaji ya Watanzania walio wengi, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili nimpongeze sana ndugu yangu Waziri Mwigulu kwa bajeti hii nzuri pamoja na Naibu Waziri *Engineer* wetu na Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii. Kwa kweli Mwigulu tembea kifua mbele na wasaidizi wako bajeti hii imewagusa sana Watanzania, tunakupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nilipenda niliseme; Waheshimiwa Wabunge wengi tupo hapa, tupo mchanganyiko; wapo vijana na kandalika. Ombi langu, mna mipango mingi mbele ya safari. Katika mipango mliyonayo sasa tumuache mama Rais wetu, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wafanye kazi yao, ninyi subirini mpaka 2029

ndipo muendelee na mipango mingine ambayo mnayo huko mbele nadhani mmenielewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumuombe Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwamba fedha hizi ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezijadili hapa tuombe ziende kwa wakati ili zikafanye shughuli ya maendeleo katika maeneo yetu na katika majimbo yetu. Kwa mfano Wabunge walisema hapa, na mimi nalisema, kwamba yapo madeni ya wazabuni ziende zikalipe. Zipo *return* za VAT za muda mrefu za wafanyabiashara, mwende mkalipe ili nao walipe madeni ambayo wanadaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile iko miradi ya maji ambayo Rais wetu na Wizara hii mmedhamiria kumtua mama ndoo kichwani. Sasa kuna miradi ile ya miji 28, na katika miji 28 na Makambaku ipo; mradi ambao fedha inatokana na mkopo nafuu kutoka Serikali ya India; sijajua tumekwamba wapi kwa sababu imechukua muda mrefu. Tuombe, wananchi wana mategemeo makubwa, mkalitatue hili ili kandarasi wawe *site* waweze kufanyakazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ziko fidia ambazo wananchi wamekuwa wakidai. wakiwemo na wa Jimbo langu la Makambaku. Niombe, maana wewe ndiwe bwana kihenge; nikuombe Waziri na timu yako mtoe hizi za fidia ili wananchi waweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la afya na barabara nakadhalika. Kwanza kuna kile wanasema kishika uchumba; nikushukuru Mheshimiwa Waziri kupitia Rais wetu, tumeshapata kwenye majimbo zaidi ya milioni tayari 500 ziko kule, tunakupongeza sana. Kwamba hivi sasa tukirudi au kabla; kwamba *TARURA,* ukiacha bajeti waliyokuwa nayo tayari milioni 500 wameongezewa. Kwamba pamoja na hili la shilingi mia za mafuta nakadhalika tuna imani zitaongeza maendeleo makubwa upande wa barabara na zitatatua changamoto ambazo zinakumba katika maeneo yetu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko fedha nyingi ambazo tayari hivi sasa zimeenda. Fedha hizi za maendeleo ambazo ziko kwenye *force account;* fedha hizi Wameshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wabunge kama mlikuwa hamjui, hawaruhusiwi kujua au kushiriki kwa sababu mwongozo unasema anayetakiwa kuwepo kwenye ile *force account* ni mwananchi mmoja katika kijiji au katika mtaa kwa mradi ule ambao unafanywa katika sehemu ile, na *engineer* na watu wachache, Diwani haruhusiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Diwani huyu ndiye badala yetu, ndio Wabunge wa eneo. Sasa Diwani huyu akiulizwa na wananchi hajui, akiulizwa anaambiwa wewe haumo kwenye kamati hii. Niombe sana Mheshimiwa Waziri, ili fedha hizi ziwe salama ni lazima Diwani aingizwe kwenye Mpango huu wa kusimamia shughuli za maendeleo katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilipenda kwa leo niliseme, *TANROAD* wanafanyakazi nzuri sana, lakini kuna kipengele kimoja ambacho kimekuwa kandamizi kwa wafanyabiashara, nacho ni hiki; gari likiharibika barabarani au likapata ajali likadondosha *oil* au mafuta ya *diesel* au *petrol* barabarani adhabu yake ni kuanzia milioni 15 mpaka 40 na ushee. Adhabu hii ni kandamizi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba, kwa sababu tunasema tuwawezeshe wafanyabiashara ili waweze kufanya vizuri, ombi langu ni kwamba adhabu hii ikaangaliwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna watu wa *EWURA* wanafanyakazi nzuri kudhibiti mfumuko wa bei za mafuta nakadhalika, lakini nayo iko changamoto ambayo inatakiwa iangaliwe, ni kandamizi kwa wafanyabiashara. Kwa mfano basi linapoingia kujaza mafuta kwenye kituo anatakiwa ashushe abiria, kwamba asijaze mafuta akiwa na abiria. Akipatikana mwenye kituo anamjazia mafuta basi la abiria faini yake ya papo kwa papo ni milioni tatu. Hii ni sheria

inayowakandamiza wafanyabiashara, niombe sana iweze kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo Mheshimiwa Mbunge wa Njombe Mjini, ndugu yangu Mwanyika amelizungumza sana hapa; kuhusu Mkoa wetu wa Njombe na kuhusu uwanja wa ndege. Uwanja ule ni uwanja ambao umekuwa kwenye llani kwa muda mrefu. tangu mwaka 2005 mpaka leo. Tunaomba; na sisi Njombe, kama alivyosema Mbunge, ni mkoa unaozalisha sana na ni mkoa tunaolima parachichi ambazo zimepata soko la dunia kwenye kilimo hiki cha parachichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna Liganga na Mchuchuma; na nimpongeze sana Mheshimiwa Rais jana alivyozungumza nyoyo za sisi wana Njombe na Watanzania yaani tumezuuzika sana. Kwamba Liganga na Mchuchuma imezungumzwa kwa miaka mingi, tatizo ni nini? Tutafute namna ya kulitatua tatizo hili la Liganga na Mchuchuma. Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mbunge wa eneo husika amelizungumzia sana. Tatizo ni kulipa fidia za wale watu na kadhalika. Kwa hiyo tunaomba sana, Mheshimiwa Mwigulu tunakuamini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu suala la hizi benki...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, sekunde. Hizi benki zinatukopesha lakini riba zao ni kubwa Mheshimiwa Mwigulu. Mimi mwenyewe nimekopa juzi, kama mwezi mmoja hivi nimekopa milioni 600. Katika milioni 600 riba ni asilimia 19, hivi tunalipaje? Kipindi kilichopita nilikopa bilioni moja, milioni mia tano thelathini na mbili kwa ajili biashara zangu. Nimemaliza kulipa wamenipa barua ya kunishukuru riba peke yake wameandika kunishukuru pale milioni 918; nitawaonyesheni barua...

NAIBU SPIKA: Ahsante sana mheshimiwa...

MHE. DEO K. SANGA:...milioni 918 ni bilioni nyingine. Kwa hiyo tunaomba benki waweze kupunguza riba kama ambavyo mama jana amesema ili tuweze kukopa na tuweze kufanyabiashara vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami nitoe mchango wangu kwenye Bajeti Kuu ya Serikali kufuatia hotuba ya hoja ya bajeti ambayo iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu wiki iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ameendelea kutoa uongozi uliotukuka katika taifa letu kwa muda huu mchache ambao ameanza kufanyakazi kama Rais. Kama ingekuwa kwenye mchezo wa mpira tungesema mama anaupiga mwingi sana kwa jinsi ambavyo anachukua hatua nyingi mbalimbali ambazo ni sahihi kwa nyakati sahihi. Nasema hivyo, kwa mfano hili ambalo amelizungumza Mheshimiwa Sanga *(Jah People);* kwamba mama jana tu ametoka kuzungumza kwamba riba kwenye mabenki ishuke na isiwe zaidi ya asilimia 10, hilo tu peke yake ni jambo kubwa sana kwenye kuchochea ukuaji wa uchumi katika taifa letu, hilo tu na mengine mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia hatua mbalimbali ambazo zimewekwa kwenye bajeti ya mwaka huu zinaonesha wazi kwamba mama ana dhamira ya dhati kabisa ya kutaka kukuza uchumi, kuchochea ukuaji wa uchumi, kutoa ajira nyingi pamoja na kuboresha huduma za kijamii kwa watu wetu; na kwa hili nina kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Mama yetu Samia Suluhu Hassan.

Lile alilolisema Mheshimiwa Sanga kwamba watu waache kufikiria mambo mbalimbali nadhani halipo. Mama anafanyakazi nzuri na sidhani kama kuna mtu ambaye atajaribu kukiuka utaratibu ambao tumejiwekea kwenye chama chetu, kuvuta fomu ya kuomba nafasi yoyote ile ya juu mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo kwa wale Wabunge wenzangu tuendelee kupambana majimboni, kwa wale ambao ni Mawaziri wapo kwenye *front bench* waendelee kupambana majimboni, waendelee kuchapa kazi wamuache mama afanyekazi kwa sababu anafanyakazi nzuri, na hakuna sababu ya kutikisa Taifa kwa uchaguzi ama kwa fununufununu zisizo na maana katika kipindi hiki ambacho mama anafanya mabadiliko makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya kwanza baada ya utangulizi ni kwamba, taifa ili liendelee linahitaji mambo mengi, lakini katika mambo makubwa ambayo taifa linapaswa kuyatumia kama chachu ya kuleta maendeleo ni pamoja na maliasili zake (*natural resources). Natural resources* zinapaswa kuwa chanzo cha taifa lolote lile kuendelea. Sisi tumejaaliwa gesi lakini pia tumejaaliwa dhahabu. Pia taifa ili liendelee linapaswa kutumia nguvu kazi yake, kwa maana ya watu wake. Sasa haya mambo mawili ninayaona katika uchumi wetu bado hatujaya-*exploit fully,* hatujayatumia ipasavyo kuweza kuturusha kwenda mbele kwa kasi zaidi katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na nasema hivyo kwa sababu bado hatujaweza kutumia uchumi unaotokana na maliasili zetu kama dhahabu, kwa maana ya kuongeza thamani; jana tumefurahi kuona mama amezindua kiwanda kikubwa kule Kanda ya Ziwa cha kufanya *refinery* ya dhahabu, ni uelekeo sahihi; lakini tunaweza tukafanya vizuri zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunapaswa tuongeze *speed* ya uwekezaji kwenye sekta ya gesi ili maliasili

ya gesi ambayo tumejaaliwa tuweze kuitumia kwa faida, kwa maana ya kuongeza thamani ili kutengeneza mbolea na baada ya kutengeneza mbolea hiyo gesi itaenda kuwa chachu ya kukua kwa uchumi wa mkulima ambaye atatumia ile mbolea. Kwa hiyo tuna haja pia ya kuwekeza kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbali na hivyo jambo lingine kubwa ambalo linakosekana katika uchumi wetu ni mfungamanisho *(linkage)* kati ya sekta ya kilimo na sekta ya viwanda; hapa tuna changamoto kubwa, na changamoto hii inasababishwa kwanza na viwango viwango vikubwa vya kodi, lakini pili kuwepo kwa *regulation* ya hali ya juu na Serikali kuingilia kwa kiasi kikubwa sana kwenye utendaji wa sekta ya kilimo, kitu ambacho kinasababisha biashara iwe ina *imbalances* nyingi kutokana na kanuni nyingi ambazo zinatungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo ili tuweze kuendelea na kuendeleza watu wetu ambao ni zaidi ya asilimia 65 na ambapo zaidi ya milioni 40 wanategemea sekta ya kilimo ni lazima tufanye *value addition,* tuongeze thamani kwenye mazao yanayolimwa na wakulima wetu. Sasa tukiweza kuongeza thamani ya mazao maana yake tutakuwa tumeongeza vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi ilivyo uchumi wetu Pato la Taifa linachangiwa kwa kiasi cha asilimia 25 mpaka 27 na watu zaidi ya milioni 40. Kwamba wale asilimia 65 ambao wanategemea shughuli za kilimo wanaokaribia milioni 40 ya Watanzania wote wanachangia kwenye Pato la Taifa kwa asilimia takriban kati ya 25 mpaka 27 tu. Sasa hawa ni watu ambao kwanza hatuwatozi kodi, kwa sababu hakuna mchungaji anayetozwa kodi ya mifugo zaidi ya milioni 30 ambayo tunajivunia kuwa nayo, lakini pia wakulima hawatozwi kodi. Sasa ili tuweze kupata kipato kutokana na hawa watu zaidi ya milioni 40 ni lazima kuwe kuna namna ambavyo kuna *value addition* kwenye ile shughuli kubwa ya kiuchumi wanayoifanya ili sasa kule ndiko tukapate kodi, kwa sababu kwenye mazao hatutozi kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ushauri wangu ni kwamba, tunakoelekea huko itafutwe namna ya hawa watu zaidi ya milioni 40 kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye Pato la Taifa. Tutaweka kodi gani, maswali hayo wataalam wanaweza wakayatazama, lakini kwamba tutafanya nini kuna uwezekano mkubwa, kama tutafanya *value addition* kwa kuwezesha ujenzi wa viwanda ambavyo vinafungamanisho la moja kwa moja na shughuli ya kilimo, mifugo na uvuvi, basi kule kwenye viwanda tutapata kodi ambayo itasaidia kuchangia kwenye uchumi wa taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye fungamanisho napenda kutoa mfano, amezungumza Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa wakati anachangia, kwamba kulikuwa kuna kongamano jana la alizeti pale Singida; na nina-*declare interest,* mimi nina kiwanda cha kusindika mafuta ya alizeti. Nilikijenga mwaka 2009 huko kabla sijaingia kwenye siasa. Tangu nimekijenga kiwanda hicho mpaka leo hatujawahi kufikisha uzalishaji wa mafuta kwa zaidi ya tani walau elfu 10, na kiwanda kikubwa ambacho kwa mwaka mmoja kinaweza kikafanya *volume* ya tani elfu 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa, ya kwanza tunafeli kwa sababu hakuna *raw materials* hakuna malighafi ya kuingiza kiwandani. Kwa hiyo tunaendelea kuhamasisha watu wawekeze kwenye uchumi wa viwanda, lakini watu wakiwekeza kwenye uchumi wa viwanda hakuna malighafi ya kupeleka kwenye viwanda. Sasa kwanini inakosekana malighafi ilhali Watanzania zaidi ya milioni 40 ni wakulima? Maana yake hapo kuna *miss match,* hapo kuna *gap* kubwa ambalo sisi kama Serikali tunapaswa kuliziba, tunapaswa kulifanyia kazi. Kwamba ni namna gani wakulima wetu watazalisha na hatimaye wanachokizalisha kiingie kwenye viwanda ambavyo vinajengwa? Kwa hivyo tunahitaji kufanyia kazi jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu kubwa nyingine ya pili ni kwamba, kwenye uchumi wa viwanda ukishakuwa tu mfanyabiashara kwenye nchi yetu unakuwa *labeled* kwamba huyu anataka kuwaibia wakulima, ana

lengo baya na wakulima, anawaminya wakulima. Dhana hiyo inasababisha kwa kiasi kikubwa sana kutokushamiri kwa uwekezaji kwenye eneo la viwanda, lakini pia mahusiano hasi kati ya Serikali wakulima na wafanyabiashara; jambo ambalo kama lingerekebishwa, na ni jambo tu la *mindset,* basi tungeweza ku-*unlock potential* kubwa sana ambayo ipo kwenye uchumi ambao unategemea zaidi kilimo, kwa maana ya kufanya *backward linkage* kati ya kilimo na viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine kikubwa ambacho ningependa kukisema ni kwamba *tax rate,* kiwango cha kodi kama Mheshimiwa Mwigulu ataenda ku-*review* mchumi mmoja anaitwa Arthur Laffer akasoma ile *Laffer Carve* ataweza kutusaidia sana kama taifa kutunga viwango vya kodi ambavyo ni rafiki kwenye kukua kwa uchumi pamoja pia kwenye kuongeza kipato cha Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimalizie tu kwanza kwa kumpongeza kwa hotuba nzuri ambayo aliiwasilisha hapa; kiukweli hotuba yake ilikuwa kama muziki kwenye masikio ya Waheshimiwa Wabunge wakati akiiwasilisha na...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana...

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA: ...ana-*deserve credit* zote japo kuwa Mheshimiwa Mwigulu ni Yanga hilo ndilo tatizo alilonalo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru na ninaunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu yetu ya kwanza kwa siku ya leo, niwataje Wabunge wachache watakaoanza uchangiaji wa mchana. Mheshimiwa Aloyce Kwezi, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve,

Mheshimiwa Neema William Mgaya, Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, Mheshimiwa Ally Hassan Omar King; ataanza yeyote kati ya hao mchana tutakapofika. Nimesikia Wabunge wengi wakisema kuhusu Mheshimiwa Mwigulu kuwa Yanga, Yanga nayo ni timu jamani. Yanga nayo ni timu inahitaji watu wazito kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naongezewa huku, ni timu kubwa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge kuna wageni ambao walitangazwa wakiwa hawajaingia hapa ndani. Wageni 44 kutoka Ukwata Mbeya; haya, walitangazwa lakini hawapo, hawa ni wageni wangu 44 kutoka Jijini Mbeya wakiongozwa na Mratibu wa Ukwata Mkoa wa Mbeya, na huyu ni mchungaji Siwiti Wispa; karibuni sana. Ninaamini mmepata fursa ya kujifunza namna Bunge linavyofanyakazi kama lilivyokuwa kusudio lenu.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 kamili jioni leo.

(Saa 07.20 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Majadiliano yanaendelea, tutaanza na Mheshimiwa Aloyce Kwezi, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma na Mheshimiwa Rose Tweve ajiandae.

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia, lakini kwa nafasi ya pekee naomba tu nianze kwa kuwapongeza sana Wizara ya Fedha kwa maana ya uratibu mzuri wa bajeti kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nafasi ya pekee mama huyu kwa kweli ni msikivu sana na usikivu huo utauona kabisa, kwa mfano mimi katika bajeti iliyopita nilichangia sana kwenye masuala ya

Utumishi nikaongelea stahili za Watendaji wa Kata pamoja na Wabunge wenzangu, tukaongelea stahili za Maafisa Tarafa na tukaongelea masuala ya promotion kwa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyokwambia karibu halmashauri zote wapo *busy* kuendelea na upandishaji wa vyeo kwa watumishi. Sio hilo peke yake utekelezaji tumeuona kwa ile laki moja moja ambayo inakwenda sasa kwa Maafisa Tarafa na pia kwa Watendaji wa Kata. Siyo hilo peke yake bado kwa wale wastaafu tulilalamika hapa, tumeona mkakati ambao amekuja nao, Mheshimiwa Waziri na usikivu wa Serikali unaonekana moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nisimame nitembee kifua mbele na niwaombe wenzangu tutembee kifua mbele kwa kuamini kwamba, ushauri tunaoutoa ni shauri ambao unasikilizwa na unatekelezwa. Maana yake hakuna kitu kizuri unaposhauri halafu kikafanyiwa kazi na ndiyo maana ya Ubunge, tungekuwa tunashauri halafu msifanyie kazi, kwa kweli tungekuwa tunasema mbona ili tulilisema hakuna ambacho kimefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwaweli nimejisikia faraja sana, ndiyo maana narudia kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa usikivu wake. Kwa namna hii naamini kabisa Watanzania wengi hata ukipita vijiweni wanajisikia furaha na amani kwa Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ni Serikali sikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze kwa miradi ambayo inaendelea, ukifuatilia bajeti kuu miradi mikubwa yote ya kimkakati bado inaendelea na mama mpaka tunavyoongea yuko Mwanza ametoka kuzindua reli, lakini jana nimeona anazindua masoko ya dhahabu. Pakubwa zaidi ambapo amepalenga na ambapo ndiyo kilikuwa kilio kikubwa cha Wabunge ni suala kubwa la *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba sitaki nimpongeze kwa namna ya kuuma ulimi,

nampongeza hapa akiwa ananiangalia kwamba kazi aliyoifanya na ushauri aliofikisha Mwenyezi Mungu ambariki sana, kwa sababu kwenye *TARURA* mazao ya wananchi wote wanafahamu yanauzwa bei ya chini kutokana na barabara. Mwananchi anatoka na mzigo wake kule wa mahindi, vitunguu, nyanya na alizeti, anakutana na barabara hakuna daraja, hakuna karavati na maji yapo kiunoni. Kwa hiyo matokeo yake yananunuliwa mazao yao kwa bei ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa *alternative* hii ambayo waekuja nayo, naomba niwapongeze sana na wasimamie hilo. Wasimamie hilo ili waturahisishie sisi kujibu maswali, maana yake tukimaliza Bunge hapa tutakuwa kwenye majimbo yetu, tutakuwa kwenye mikoa yetu, kwa hiyo itakuwa ni fursa nzuri ya kuwaambia nini ambacho tumekisema na nini ambacho Serikali sikivu imetekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa lingine ambalo nimeliona hapa na ni lazima niliseme kwenye Kamati yetu ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Pale kwenye utalii nimefurahishwa sana kwasababu tulikuwa tunapata wasiwasi kwenye Kamati kwamba utalii ni sekta ambayo inatuingizia fedha za kigeni, lakini baada ya kuondoa yale mapato yanaenda moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu ule, tukawa na wasiwasi watatuzoroteshea maendeleo ya utalii. Sasa niwaombe kwasababu wanatoa *in advance* labda miezi miwili, wamefanya akili ya ziada sana, kwa hilo nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nawaomba jambo kubwa kwenye mapato yetu ya ndani, ni lazima zaidi ya hapa tuimarishe sehemu gani kwenye utalii. Kwenye utalii, katika hifadhi zetu kuna maeneo au hifadhi wakati wa masika hazifikiki kabisa. Sasa tunahamasisha Watanzania waende kwenye maeneo ya hifadhi, naomba nitoe mfano wa Kitulo *National Park*, tulitaka kwenda pale Kitulo tukaambiwa kwa muda huu wa mvua, Kitulo barabara haifikiki. Pia tukataka kwenda kuna Ziwa moja linaitwa Ngosi ikashindikana, sasa hizo ni *sample* mbili, lakini nilikanyaga Biharamulo kuingia kule Burigi ikawa na yenyewe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba hapa tushauriane vizuri, tunahitaji fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu na kwa ajili ya miradi, nashauri tu-*inject* fedha nyingi kwenye kuboresha miundombinu ile ya kwenye hifadhi zetu ili hata kama ni masika watu wanataka kwenda *Christmas* kupumzika mwezi wa Tatu wanataka kwenda mle, pamoja na sikukuu zetu hizi za kuchinja, wawe na uwezo wa kwenda kule kula vitu vyao vizuri wakati wa masika na wakati wa kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningeweza kuwashauri, kwenye sekta ya afya nafahamu kabisa ziko kata hatujakamilisha shule na zipo tarafa ambazo hatuna vituo vya afya, hebu tujaribu kwenye hizi fedha ambazo wameangalia, nafikiria tuwabane kidogo, unajua unapoenda kutoa fedha kwenye *M-pesa*, kwenye *Halopesa*, kwenye *Tigo pesa* na kwenye *Airtel Money*, kama unatoa milioni moja au unatuma milioni moja unakatwa labda 3,500 au 4,000. Unapokwenda kutoa unakatwa tena 8,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomb tujaribu kuangalia hapo je, hatuwezi kuongea na makampuni yetu, yalipe kodi kama kawaida maana yake tusichezee kodi, lakini bado tuangalie ile fedha ambayo ilikuwa inapotea pale kwenye zile *transactions,* naona ile fedha ni kubwa. Yaani muamala nimekutumia hapo Mheshimiwa unaupokea, mimi niliyetuma nakatwa, wewe ukinyanyuka kwenda kutoa unakatwa karibu 8,000 mpaka elfu 10,000 na zaidi. Sasa ile fedha ni nyingi, kwa nini tusiongee, kwa sababu ni suala la uzalendo na wana-*exist* nchini kwetu na tunafanya nao kazi, tuwashawishi kwamba *if possible,* basi angalau na wenyewe wajaribu kuachia shilingi elfu moja moja ziende kwenye *TARURA,* kwa sababu barabara za vijijini ndiyo mishipa ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukitaka tuyapunguze maneno mengi ni hapo ambapo tumelenga kwenye *TARURA*, afya, elimu na maji. Haya maeneo tukibana vizuri, naamini kabisa mwelekeo wetu utaendelea kuwa vizuri na kama nchi tutaendelea kutembea kifua mbele kwa kuhakikisha tunawasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kubwa naendelea kupongeza ni la Madiwani wetu, nawaambia kabisa *by professional* mimi ni Afisa Utumishi, kwa hiyo nimekaa halmashauri karibia miaka 15 ninachokiona...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo ya kwanza?

NAIBU SPIKA: Malizia sentensi yako unachokiona...

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiona ambacho ningekishauri, inawezekana kuna halmashauri ambazo wakawa na wasiwasi kuwalipa moja kwa moja, naomba kupitia ule Mfuko Mkuu wajaribu kuziangalia zenye uwezo mkubwa sana, ndiyo iwe hivyo kwa maana yale majiji makubwa yenye fedha, lakini hizi halmashauri zingine zote zinasuasua, wahakikishe wanawalipa kupitia hii Serikali Kuu moja kwa moja, kusiwepo kwamba hiki na hiki, zile za daraja A, zile halmashauri kama Kinondoni hapo sawa.

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. ALOYCE A. KWEZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze sana na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve na Mheshimiwa Neema William Mgaya, ajiandae.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipende kuipongeza Serikali yake kwa kuja na bajeti nzuri ambayo ina mguso kwa Watanzania wote. Katika bajeti ya kwanza kabisa ya Rais Samia Suluhu Hassain imefanikiwa kugusa makundi yote katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na kundi la wakulima; zipo tozo pamoja na ushuru ambazo zimeondolewa katika mapendekezo haya ya bajeti. Nia, lengo na kusudi ni kuwawezesha wakulima wetu waweze kulima kilimo chenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ukisoma mapendekezo ya bajeti, unakuta kuna lengo ama dhamira ya kuongeza tija kwa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Sambamba na hilo pia wanakusudia kutafuta masoko kwa ajili ya mazao hayo ya wakulima yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalizia kundi lingine ambalo ni kundi muhimu sana, ni kundi la wafanyakazi ama watumishi. Tutakubaliana sote hapa Serikali inapata kodi yake ya uhakika katika vyanzo vyake vyote vya kodi, kodi ya uhakika inatoka kwenye kundi la wafanyakazi. Ni kodi ambayo haina kuvutana mashati, ni kodi ambayo haina kuifukuzia, yaani ipo inapatikana kiurahisi kabisa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia kwa kuona umuhimu wa kupunguza kodi ya *pay as you earn* kwa watumishi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa muda mrefu sana takribani miaka mitano ama miaka sita, watumishi wa Taifa hili wamekuwa wakinungunika juu ya masuala mazima ya kupanda daraja ama ya kupanda vyeo. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia katika bajeti yake ya kwanza kabisa kukusudia kutenga bilioni 449 kwa ajili ya kupandisha vyeo watumishi 92,619.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakubaliana ni haki ya msingi ya watumishi kupanda madaraja ama kupanda vyeo

na unapokuwa unawapandisha vyeo watumishi tafsiri yake ni kwamba ...

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Getere natumaini unataka kutoa taarifa na siyo kuchangia, Mheshimiwa Getere.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nataka kutoa taarifa kumpa mzungumzaji anayeongea. Alipozungumza ile malipo ya *pay as you earn*, nataka kujua tu anapoendelea kwenye mchango wake majibu yake yaje yapatikane kwamba asilimia iliyotolewa ni ipi, kuna watu wa kundi la kwanza ambao wanamshahara wa 270 mpaka 540 ambao wana asilimia 9.0, wanakwenda mpaka asilimia 10...

NAIBU SPIKA: Sasa hebu ngoja tuelewane hiyo ni taarifa au unamuuliza swali? Kwa sababu yeye hana uwezo wa kukujibu wewe.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia tu, watakavyompa majibu watuambie kwamba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Mchafu, endelea na mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, Mbunge akiwa anaenda na mchango wake hivi, ukimkatisha njia yaani ile namna anavyoenda unamchelewesha.

Kwa hiyo usimame kutoa taarifa kama hasa unataka kuongeza kwenye jambo ambalo unaona yeye hajamaliza vizuri pengine hoja yake. Sasa yuko katikati ya jambo, wewe umeingia hapo hata *point* yake hajamaliza bado.

Mheshimiwa Hawa Mchafu.

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naendelea kwa kusema kwamba tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutenga hizo bilioni 449 kwa ajili ya kupandisha vyeo watumishi wa Taifa hili. Nilikuwa nasisitiza kwa kusema kwamba mtumishi yoyote ambaye ana haki anastahili kupanda cheo, unapompandisha cheo unampa *moraly* na ari ya kufanya kazi kwa ufanisi, jambo ambalo litaenda kuchochea na kuchagiza kodi iweze kupatikana zaidi kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ambalo Rais Mheshimiwa Samia amelifanya na limenigusa kwa namna moja ama nyingine nilikuwa mtumishi wa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwenye Bunge lililopita nilikuwa nikiwakilisha wafanyakazi. Rais, Mheshimiwa Samia amefanya jambo kubwa sana kudhamiria kulipa madeni ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki alichokuja nacho hapa ni mwarobaini wa kuhakikisha tunatenga fedha za bajeti na zinaenda kutumika katika utaratibu wa hati fungani ili kwenda kulipa madeni ya hifadhi ya jamii. Hii nini maana yake? Ni kwamba hifadhi ya jamii ilikuwa na madeni ya muda mrefu sana na madeni ambayo yalikuwa yakienda yakikua katika mifuko yetu ile mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Serikali imeamua na kudhamiria kufanya hivyo, wakitenga fedha kwenye bajeti na kupeleka kwenye hati fungani na baadaye kulipa kulipa madeni kwa Mfuko tuliokuwa nao sasa wa *PSSSF*, tafsiri yake ule Mfuko unaenda kukuwa, Mfuko ule unaenda kuwa na ukomavu, sasa kile kilio cha wastaafu kinaenda kumaliza na mapendekezo haya. Ile kauli mbiu ya Mfuko wa LAPF iliyokuwa ikisema mstaafu wa leo analipwa kesho, kwa huu mwarobaini aliokuja nao mama Samia ndiyo inaenda kutekelezeka kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lilikuwa likipigiwa kelele sana na ndugu yangu Ester Bulaya pamoja na

Mheshimiwa Halima Mdee kwenye Bunge lililoisha na Bunge hili. Hivyo nitawaomba sana mapendekezo haya yakipita tutakapofika kupiga kura siyo dhambi wakapiga kura ya ndiyo kumpongeza Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassain kwa sababu ametii kiu yao ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba sana Mheshimiwa Mwigulu akija atufafanulie jambo moja, kulikuwa na watumishi waliokuwa wanafanya kazi Serikali Kuu ambao kimsingi walistaafu kabla ya mwaka 1999, watumishi wale Serikali ilisema walipwe mafao yao na Mfuko wa *PSSSF.* Sasa wale walilipwa lakini lile deni halikulipwa ambalo linajulikana kama *pre-1999* na muda wote ulikuwa tukijadili madeni ya hifadhi ya jamii *pre-1999* tulikuwa tunaijadili *separate*. Kwa hiyo nataka kujua kwenye hii dhamira waliyoileta ya kutaka kutenga hii hati fungani kulipa madeni ya hifadhi ya jamii na *pre- 1999* iko *included.* Kama watakuwa wamefanya hivyo Mheshimiwa mama Samia atakuwa amemaliza kabisa kilio cha *Trade Union*, cha wafanyakazi, cha watumishi, pamoja na wastaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi lingine ambalo linaguswa katika bajeti hii ni kundi la vijana na akinamama. Bajeti inakusudia kwenda kuboresha uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Tunaposema kuwawezesha wananchi kiuchumi ni kundi linalokusudiwa hapa ni akinamama pamoja na vijana na juzi alivyotuita wanawake wa Taifa hili alizungumza ana dhamira ya kuhakikisha anataka kuhakikisha haya majukwaa ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa maana hiyo hapa wanawake watanufaika na vijana watanufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi lingine ambalo linanufaika kwenye bajeti hii ni kundi la wafanyabiashara, kundi la wawekezaji hususani wenye viwanda, ukiangalia bajeti kwamba Mheshimiwa Waziri anakusudia kuondoa sharti la kuweka dhamana la asilimia 15 ya ziada ya ushuru wa forodha iliyorejeshwa kwenye sukari ya matumizi ya viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa sana, wakati tupo hapa Bunge lako linaendelea walikuja wadau wa viwanda chini ya mwavuli wa *CTI.* Katika mambo waliyokuwa wanayalalamikia, liko hili la kuondoa hii tozo asilimia 15, lakini lipo lile la kuondoa ama kupunguza tozo ya mabango ambayo kimsingi nadhani imependekezwa ishuke kutoka asilimia 15 mpaka asilimia 10, *if I am not mistaken*. Napenda sana kuipongeza Serikali na kama hivyo ndivyo basi kazi imebaki kwao wenzetu wenye viwanda kuhakikisha wanaongeza uzalishaji, wanaongeza ajira, lakini pia wanalipa kodi stahiki kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nimwonyeshe Mheshimiwa Waziri Sehemu ambayo kimsingi hajatolea jicho, pale tunaweza tukapata mapato ama tukapata kodi. Tukizungumzia uvuvi wa wa Bahari Kuu, tukizungumzia kule *deep sea*, sisi kama nchi hatuna meli itakayoweza kwenda kuvua kule, lakini sisi kama nchi hatuna bandari ya uvuvi kwa utaratibu meli kubwa kutoka nje zinalipa tozo kidogo kwa Wizara wanapewa kibali wanaenda wanavua. Wanavua *tones and tones* za samaki ambazo zinapatikana katika eneo la Jamhuri ya Muungano, ambayo ni bidhaa ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi bidhaa ile inayopatikana katika mipaka ya bahari ya Jamhuri ya Muungano haikatwi kodi. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, *TRA* waone namna bora ya kufanya makadirio ili tuweze kutoza kodi zile tozo tunazotoza ili kuwapa kibali wakavue, ni maduhuli tu yale madogo madogo, lakini tuweke utaratibu wa kisheria ili tuweze kutoza kodi hao samaki wanaoweza kwenda kuuzwa huko duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ukiangalia katika ukurasa wa 41(e) cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema anakusudia kuongeza ushuru wa forodha kutoka asilimia 25 mpaka 35 kwenye bidhaa ya marumaru. Bidhaa za marumaru...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. HAWA M. CHAKOMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kidogo. Kwa bidhaa hizo za marumaru zinazotoka nje, Mheshimiwa Waziri kuongeza tozo ni sahihi kabisa, kwa sababu anakusudia kulinda viwanda vyetu vya ndani. Tunapozungumzia suala zima la viwanda, mkoa unaoongoza kwa viwanda ni Mkoa wa Pwani; na ukizungumzia masuala mazima ya viwanda vya *tyles,* unavikuta Mkuranga, Mkiu, Chalinze, Bagamoyo na Kisarawe. Kwa kufanya hivyo, atavilinda viwanda hivi, watawaweza kuzalisha, kulipa kodi na kutoa ajira kwa Watanzania.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. HAWA M. CHAKOMA Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, ajiandae.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nakushukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu kwa namna ambavyo amewasilisha bajeti hii hapa Bungeni ili nasi sasa tuweze kutoa mapendekezo na maoni yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Rais wetu, mama yetu Mheshimiwa Samia Suhulu Hassan kwa namna ambavyo amesisimama imara kuendelea kuliongoza na kulisimamia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache ambazo zilifanikiwa kupiga hatua kubwa ya

kupanda kiuchumi ingawa tulipitia changamoto kubwa sana kidunia, lakini tuliweza kufika uchumi wa kati. Sasa ni jambo jema na hii haina *guarantee* kuwa tutaendelea kuwepo hapo, tunaweza kushuka au kupanda zaidi. Ni matamanio yangu na Watanzania wengine kuwa tutaweza kupiga hatua kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tuna jukumu kubwa la kuhakikisha tunawekeza ili uchumi wowote uweze kupiga hatua, lazima tuwekeze na eneo kubwa ambalo ningependa kuweka msisitizo ni kuhakikisha tunawekeza kwenye rasilimali watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais yetu Samia Suluhu Hassan alipokuwa akiongea hapa tarehe 8 mwezi wa Sita alisisitiza sana umuhimu wa kuhakikisha tunaendelea kuwekeza kwenye rasilimali watu na akaenda mbali zaidi kuisihi sekta binafsi kuhakikisha wanaendelea kuchangia ile 4% ya *gross pay* kuendelea kuboresha na kukuza ujuzi hasa wa vijana wetu. Hii hiko kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006 Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria ya Mafunzo ya Elimu ya Ufundi Stadi kuhakikisha hawa wenzetu sekta binafsi waendelee kuchangia vipaji vya vijana wetu hapa nchini. Hapa ndipo ambapo kidogo pana changamoto. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha twende sasa na mahitaji na mabadiliko ambayo nchi hii inataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii kile Kifungu cha 15 kinasema *two third* ya yale makusanyo yaende Serikali Kuu na *one third* ilikuwa inaelekeza kuwa iende kuboresha miundombinu tu ya hivi vyuo vya ufundi na siyo kufadhili elimu yetu. Hapa ndipo ambapo pamekuja na changamoto. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu hii pesa ambayo inakusanywa ililenga kuhakikisha inaendeleza ufundi na ujuzi wa vijana wetu. Tuje na mapendekezo kama ambavyo amefanya marekebisho ya sheria na tozo mbalimbali, *it is a high time* tupitie sheria hii, tulete hapa

tufanye mabadiliko ili tuendane na uhitaji na kuendelea kukuza uchumi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *as of today* tuna vijana zaidi ya 357 ambao wako vyuo na kama 201,000 ni vijana wa elimu ya vyuo vikuu na vijana 157,000 wako kwenye vyuo vya ufundi, sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ulipokuja kuwasilisha bajeti hapa, tumeonyesha kabisa nia njema ya kuhakikisha kupeleka *fund* kwenye vyuo vikuu. Tulipopitisha bajeti iliyopita tumeongeza kutoka shilingi bilioni 464 mpaka shilingi bilioni 500 ambayo itaenda kwenye vyuo vikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa na sheria hii ilivyo hapa sasa hivi, ambayo hiyo *two third* bado inakwenda Serikali Kuu, nilikuwa nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha tulete mabadiliko ya sheria hapa ili tutengeneze mfuko maalum kwa sababu Tanzania ya Viwanda sasa hivi inahitaji vijana ambao watakuwa na ujuzi na ubunifu ili tuweze kupiga hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili sasa kwa sababu hawa wenzetu wa vyuo vikuu wana mfuko huu wa bodi ambao unawasaidia. Hawa vijana wafundi nao tuwatengenezee mfuko wa mikopo wa vyuo vya ufundi kwa sababu kianzio kipo. Kutoka kwenye hii ongezeko ambalo wenzetu wanalilipa, tuanzishe huu mkopo ili hawa vijana waweze kuutumia. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, wenzetu Rwanda wamepiga hatua kubwa sana. Vyuo vyao vya Ufundi wamevi-*brand.* Mtoto anapotoka pale, kama anajifunza ufundi, anatoka na cherehani; kama anataka kwenda makenika anakuwa na *tool box* yake ambayo tayari itamwezesha yeye kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kama wenzetu wameweza kufanikiwa, nina uhakika tukiwekeza huko sisi Tanzania tutakuwa na uwezo wa kupiga hatua kubwa sana. Siyo tu kukua kwa asilimia sita au saba, tunaweza tukaenda hata

double digit kama tukiweka nguvu kuhakikisha hawa vijana wetu wa Kitanzania wanaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa ninukuu maneno ya mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alipokuwa anahitimisha hotuba yake ambayo aliifanya hapa Dodoma ile tarehe 8 mwezi wa sita. Aliongea kwa kusisitiza sana kuwa kwa heshima zote anaomba sisi kama Watanzania tumuunge mkono na tumsaidie. Kwa bajeti hii ambayo umeileta Mheshimiwa Waziri wa Fedha inaonyesha nia njema ya Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu Samia Suluhu Hassan kutaka Watanzania tufikie yale malengo ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania twende tukamuunge mkono Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha tunalifikisha Taifa letu pale tunapotakiwa lifike.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Neema William Mgaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha upendo mkubwa kwa Watanzania, ukisoma mapendekezo ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha upendo kwa makundi mbalimbali ya wananchi wa Tanzania kwa kupunguza tozo

kandamizi mbalimbali katika makundi mbalimbali wakiwemo wakulima, wafanyabiashara, kama bodaboda, kwa kupunguza tozo ya faini kutoka shilingi 30,000 mpaka shilingi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipee kabisa nampongeza Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya jana kwa maelekezo mazuri na maamuzi mazuri aliyoyatoa kuhusiana na mradi mkubwa wa Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Liganga na Mchuchuma kuna takribani tani milioni 128 za chuma pamoja na madini mengine. Mradi huu ukianza kutekelezwa utakwenda kutupatia malighafi ya chuma ambayo itatumika kutengezea nondo kwenye viwanda vyetu vya nondo, mabati, viwanda vya vifaa vya kutengeneza madaraja na viwanda vya vifaa vya kutengeneza reli. Kwa mradi huu, utatachochea uanzishwaji wa viwanda vingi vinavyotumia malighafi ya chuma. Sina shaka *SGR* aliyokwenda kuifungua kuanzia Mwanza huenda ikatumia malighafi ya chuma inayotokana na Liganga na Mchuchuma kama tutatekeleza vizuri kufuatana na Mheshimiwa Raisi alivyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu kwa sababu ameona kwamba mradi huu wa Liganga na Mchuchuma tutakwenda kuokoa takribani shilingi bilioni 640 ndani ya mwaka mmoja kwa muda wa miaka 30 ya uhai wa mradi huu wa Liganga na Mchuchuma. Hivyo natoa pongezi nyingi sana kwa mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hiyo ni sambamba na kuzalisha ajira 35,000. Hii pesa tutakayoenda kuokoa ni shilingi bilioni 640 kila mwaka ndani ya miaka 30. Itasaidia miradi ya maendeleo ndani ya nchi yetu. Wale watakaokwenda kuajiriwa, hao watu 35,000 watatusaidia pia katika kulipa kodi na kuendelea kupata mapato na kuweza kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yao nzuri ya Wizara ya Fedha. Naunga mkono pendekezo waliloleta la kutatua changamoto ya fedha ambazo zilikuwa zikirudi Hazina kila mwisho wa mwezi wa Sita na kuzifanya fedha zile sasa ziwe zinaenda kwenye akaunti ya amana ili ziweze kuendelea kutekeleza miradi ambayo ilikuwa haijamalizika. Hii itasaidia kuchochea kumalizika kwa miradi mapema na vilevile kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikuzungumza mara kwa mara umuhimu wa zao la parachichi ndani ya Bunge hili la Tanzania. Kwa sababu Parachichi sasa hivi ni *green gold,* ni zao ambalo linakua kwa haraka. Takribani mikoa 12 ikiwemo na Mkoa wangu wa Njombe tunalima zao hili la parachichi. Tunawashukuru sisi wakulima wa *hot culture*, wa mbogamboga, kwa pamoja na maua.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya mbogamboga tunakuta hili zao la parachichi. Tunawashukuru kwa kutoa kodi ya vyumba vya ubaridi *(cold room).* Tunawashukuru sana, kwani hii itatusaidia sisi wakulima wa mazao ya mbogamboga pamoja na maua hususan wakulima wetu sisi ambao wanalima parachichi kuhifadhi mazao yale, kwa sababu mazao haya ya mbogamboga pamoja na maua, biashara yake kubwa ni kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kutoa kodi ina maana sasa wakulima wataenda kutengeneza vyumba hivi vya ubaridi kwa wingi na kuweza kuhifadhi mazao hay ana kuweza kuyasafirisha nje ya nchi yakiwa na ubora na itasababisha kuongeza pato la Tanzania. Kwa sababu bidhaa zetu zitakuwa zinafika kwa mlaji zikiwa bora. Vilevile itawajengea imani kwa mazao ya mbogamboga na maua yanayotoka Tanzania na kuweza kuongeza wateja wengi ambao watakuwa wananunua mazao kutoka nchini kwetu Tanzania na kuweza kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema, hakuna kitu kilichokuwa kinaniudhi na kilichokuwa

kinanikosesha raha na kilikuwa kinaniuma sana kama kutoza kodi mara mbili *(double taxation).* Wale wafanyabiashara wa Zanzibar ambao walikuwa wanakuja kununua bidhaa huku Tanzania Bara kwa kweli tulikuwa hatuwatendei haki. Isitoshe sisi Watanzania Bara na Tanzania Zanzibar, tuna mahusiano, tumeoleana, kwa hiyo, tuna undugu. Unaweza ukaenda kwa mkwe wako; kwa mfano, kama mimi, naweza nikafika Tunguu kule Zanzibar kwa wakwe zangu wakaniambia tunakupa *TV* hii umpelekee mjukuu wetu. Nafika pale *custom* tena nalipishwa ushuru kweli! Hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono asilimia mia moja, tozo hii ya kulipa mara mbili mbili kwa kweli mmewatendea haki Wazanzibar. Wazanzibar ni ndugu zetu, ni jamaa zetu, ni marafiki zetu, ni wakwe zetu; Zanzibar na Tanzania Bara ni Tanzania moja. Kwa hiyo, kwa kuondoa tozo hizi mbili mbili itatusaidia kuendelea kuujenga Muungano wetu wa Tanzania. na

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na Mheshimwa Cecil David Mwambe ajiandae.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali iliyoko mbele yetu. Tukitambua hii ni bajeti ya kwanza ya Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia, niseme tu kwamba nampongeza kwa sababu kuna mambo mazuri ambayo yapo kwenye bajeti yanayoleta matumaini na mengine pia nitayashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza jambo zuri ambalo nimeliona hapa na kwa nini nasema nalipongeza? Kuweka bajeti kwa ajili ya kupandisha madaraja watumishi wetu wa Umma. Hili ni jambo zuri kwa sababu watumishi wetu wa Umma ndio injini ya nchi hii. Hawa Watumishi wa Umma

walisahaulika muda mrefu, hawakupanda madaraja, hawakuongezewa mishahara. Kwa hatua hii ya awali ya kuweka bajeti kwa ajili ya kupandisha madaraja, tunampogeza sana Mheshimiwa Mama Samia. Tunaomba aendelee hivyo ili huko mbele ya safari aweze kuongeza na mishahara ambayo Watumishi wa Umma muda mrefu hawajapata Nyongeza hii ya mishahara lakini hawajapanda madaraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwa nini nasema nampongeza? Imekuwa ni matamanio ya Madiwani muda mrefu kwa nchi nzima, nami nilikuwa Diwani. Nililvyoingia mara ya kwanza katika Bunge hili ilikuwa pia ni hoja yangu ya kuona namna bora ya kuboresha utendaji kazi wa Madiwani hapa nchini. Mama Samia ameliona tunampongeza kwa kuchukua hatua hii, kwamba sasa Madiwani walipwe na Serikali Kuu badala ya Halmashauri zetu za Wilaya ni hatua nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende mbali zaidi sasa, tuwajengee uwezo Madiwani, tuwape semina mbalimbali kwa sababu sasa watakuwa wametoka kwenye vile vifungo vya kuwatumikia Wakurugenzi ili wasikose posho zao, watakuwa *independent,* wataweza kujisimamia, kusimamia fedha zinazoenda, kusimamia miradi. Basi tujikite pia kuona namna bora ya kuwapa mafunzo ili fedha tunazopeleka katika *Local Government* kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo isimamiwe vizuri kwa uwezo na tuliowajengea Madiwani wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine muhimu, kuna masharti, kanuni, taratibu mbalimbali ambazo zimeondolewa, ambayo ni hatua nzuri ya kupunguza urasimu wa nchi hii. Nimeona kuna baadhi ya vitu vimeondolewa, siyo lazima vipite kwenye *GN,* siyo lazima sasa vikae Baraza la Mawaziri, vimempa mamlaka Waziri. Ziko tozo na adhabu na faini na misamaha mingine ambayo pia amepewa Kamishna wa *TRA.* Ni hatua nzuri ya kwenda kupunguza urasimu ili yale matokeo tunayoyatarajia yaweze kufikiwa. Hongera sana kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba mama alishajipambanua kwa kusema kwamba hataki kodi ambazo ni za dhuluma. Sasa tunaomba haya ambayo ameyatenda mama, watendaji wake na wasaidizi wake mkayafanye kweli kweli. Tunataka wafanyabiashara wetu ili waweze kulipa kodi, wawe na mazingira mazuri, rafiki yanayofikika, ambapo kweli watafanya biashara na watalipa kodi na uchumi wa nchi utakua na uchumi wa mtu mmoja mmoja utakua na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haya ambayo anayasema mama na kuyasimamia, ninyi kama wasaidizi wake kwa maana ya Waziri na watendaji wote myasimamie kwa vitendo, ndiyo tutapata matokeo ambayo tunayakusudia. Sasa ushauri wangu uko katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuhusu Kodi ya Majengo, tumekuwa na maelekezo na taratibu nyingi sana kuhusiana na Kodi ya Majengo. Huko nyuma, Halmashauri za Wilaya zilikuwa zinakusanya Kodi ya Jajengo, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani ikachukua tozo hizi ikaipa *TRA. TRA* wakapambana nayo ikawashinda kwa sababu hawakuwa na uwezo lakini pia ilikuwa ni ngumu kuikusanya. Sasa leo mapendekezo yanakuja, tozo hii ya Kodi ya Majengo, ikatwe kutokana na *Luku* za nyumba. Unaponunua umeme, unakatwa kodi. Niwaambie kwamba, nadhani hili siyo jambo jema, linahitaji kutazamwa tena kwa upya. Kwa sababu tunajua watu wenye majengo huwa ni wachache na wanaolipa kodi mara nyingi ni wapangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wamepanga. Akipanga anamlipa mwenye nyumba kodi yake, lakini suala la umeme linabaki kwake yeye mpangaji. Kwa hiyo, mwisho wa siku utekelezaji wa tozo hii inaenda kumfikia mpangaji na sio yule mwenye nyumba. Wenye nyumba ni wachache; ndiyo wapo, lakini anayenunua *Luku* ni yule mpangaji. Kwa hiyo, ni jambo la kutazama kwa upya ili kuhakikisha tozo hii iwafikie kweli wenye nyumba na sio wapangaji. Kwa sababu

tunaelewa miji mikubwa watu wengi ni wapangaji. Miji kama Dar es Salaam watu wengi ni wapangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nyumba moja siku hizi ni utaratibu hata nyumba za biashara, kila mtu ana mita *Luku* yake, anajaza umeme wake mwenyewe. Sasa unaweza kukuta nyumba moja ina *Luku* karibia 10. Ina maana hawa wote wanatakiwa walipe kodi ya majengo, wakati wao ni wapangaji tu, mwenye nyumba yupo, anapokea kodi yake ya pango, halipi kodi nyingine yoyote. Kwa hiyo, ni vyema sana hili jambo likatazamwa kwa upya tukaondoa huu utaratibu kwa sababu unaenda kumkandamiza yule mpangaji na sio yule mwenye nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la pili; mnaweka ongezeko la shilingi 100 kwenye tozo za mafuta. Tunafahamu *impact* ya kuongeza tozo kwenye mafuta. Umeshakuwa ni utamaduni; ukiongeza tozo kwenye mafuta, kila kitu nchini kinapanda. Hii shilingi 100 tunayoongeza hapa mwezi Julai kila kitu tutakachokishika dukani kitakuwa kimepanda bei; *impact* yake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *impact* ya hii lazima itazamwe, naelewa lengo ni zuri, kwamba hizi fedha zipelekwe *TARURA* kwa ajili ya ujenzi wa barabara zetu kule vijijini; jambo jema kabisa, kwa sababu tunajua mwisho wa siku matokeo ya kuwa na barabara nzuri. Wakulima watapeleka mazao yao sokoni, barabara zitapitika, wanaotaka huduma za afya watapita kwenye barabara zinazopitika. Lakini hii *impact* ya pili ya kuongeza kodi ambayo itasababisha mfumuko wa bei ni lazima itazamwe kwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, kama utatuhakikishia *you can control* mfumuko wa bei, *it's okay,* ni sawasawa. Kama hilo litawezekana, basi hizi fedha ambazo zitatozwa kwa ajili ya *TARURA,* kwa ajili ya ujenzi wa barabara zetu vijijini ziwe *ring fenced* kama zilivyo fedha za *REA.* Hapo ndiyo tutaona matokeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri kwamba hizi fedha za *TARURA* ziwe *ring fenced* zitumike kwa makusudio hayo yaliyokusudiwa ili matokeo yake tuweze kuyaona kwa barabara zetu kupitika kwa kadri inavyotokea kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine la mwisho; umuhimu wa sekta binafsi katika kujenga uchumi. Tunatambua uchumi wa nchi sekta binafsi nayo ni muhimu sana, lazima iwekewe mazingira mazuri, mazingira wezeshi, itazamwe ili iweze kuchangia katika uchumi wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mmoja; kulikuwa kuna viwanda mbalimbali hapa nchini ambavyo vimeanzishwa na ama ni wawekezaji au ni wazawa, lakini viwanda vingine vimekufa kwa sababu ya mambo mengi ambayo yanasababisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, kulikuwa kuna viwanda vya matrela. Miaka 12 iliyopita tulikuwa tuna viwanda visivyozidi 12, lakini hivi viwanda leo vimekufa, havipo tena. Kwanza, ajira imepotea, lakini hivi viwanda havijaweza kuwa endelevu kwa sababu ya mazingira mengi na mbalimbali, na moja wapo ni kwamba haya matrela yanaagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vyema Serikali ikatazama namna gani ya kutengeneza mazuri, kwanza kwa kuhakikisha kwamba hivi vifaa vinavyokuja kutoka nje, vinavyoagizwa, kwa maana ya matrela, na yenyewe iwekewe kodi kubwa ili ku-*discourage* zinazotoka nje na kuweza ku-*encourage* viwanda vya ndani vinavyotengeneza matrela na kuhakikisha kwamba kwa kufanya hivyo maana yake tutaongeza ajira, tutachangia kwenye pato la nchi kwa maana ya uchumi, lakini kuona namna gani kwamba tunaongeza ujuzi kwa Watanzania wetu, waweze kuwa na ujuzi ambao utatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye suala hili la viwanda vya matrela; ukiagiza gari dogo unatozwa

ushuru wa asilimia 25, haya matrela yakiagizwa ushuru asilimia 10. Sasa lazima tuone namna ya ku-*balance.* Kama zote zinakwenda asilimia 25 ili ku-*discourage* ili kusaidia viwanda vyetu vya ndani, na hata wakati mwingine tufikirie namna ya kutoa ruzuku kwa viwanda vya ndani kwa sababu itachangia uchumi wa nchi, ajira na kukuza pato la mtu mmojammoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo ajiandae.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupa uhai leo kuwa wazima tukaja tukajadili mambo yenye maslahi na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nikushukuru kunipa hii nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Katika Ushahidi ambao ninao kwenye Bunge lako hili Tukufu, bajeti hii ya mwaka huu ni bajeti ambayo imeongoza kuwa na maoni ya Wabunge wengi. Tumepitisha bajeti nyingi sana, na kila tukipitisha tulikuwa tuna maombi kama Wabunge, lakini safari hii maombi mengi yamesikilizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yamesikilizwa maombi ya Wabunge wa Bunge lililopita na Wabunge wa Bunge hili la Kumi na Mbili. Kwa hiyo tunaipongeza sana hii bajeti na tunamuombea mama yetu azidi kupiga kazi ili kazi hii aifanye iende kwa wepesi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli bajeti hii imetaja wajibu lakini pia imetaja haki za wananchi. Kuna msemo mmoja unasema kwamba paka kama huli panya Samaki hupewi. Sasa humu ndani ametakiwa paka akamate panya kwanza, ndiyo hizi tozo ambazo zipo kwa ajili ya kuja kufanyia haya maendeleo. Sasa tusilalamike sana kwa sababu hizi tozo ni lazima ziwepo ili mambo yetu yaende vizuri. Kwa hiyo, hilo,

kwamba paka asiyekula panya Samaki hapewi, tuendelee kuunga mkono jitihada ambazo zimefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni bajeti ya wananchi. Yameguswa makundi ya watu wengi; wameguswa wafanyabiashara, wameguswa wafanyakazi, wameguswa kwenye hii bajeti hata watu wetu wa bodaboda, wameguswa wanafunzi. Kila mmoja unaona kwamba amepata unafuu ndani ya hii bajeti. Kwa hiyo, hii ni bajeti ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo, kwamba hii bajeti imetokana na maoni ya Wabunge wengi sana. Sasa niende kuchangia katika jambo ambalo amelisema Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 31 alipotaja *VAT* ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara zikaenda Zanzibar na bidhaa zinazozalishwa Zanzibar zikaja Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze sana Serikali kwa hatua hii. Ni jambo ambalo tumelipigia kelele kwa siku nyingi sana, na tulilizungumza, lakini bado haukuonekana umuhimu. Sasa nini inakwenda kutokea; zile biashara za wafanyabiashara wadogowadogo wenye mitaji yao ambao wanakuja kuchukua bidhaa Tanzania Bara, sasa biashara zile zitafunguka na mambo yatakwenda yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na taasisi za kijamii zinakuja kufanya *shopping* Tanzania Bara, pengine vifaa vya ujenzi; misikiti, makanisa, shule na *NGOs* nyingine tofautitofauti. Hizo zote zilikuwa zinapata hiyo kero kwa sababu walikuwa wakipigwa *double VAT.* Sasa imeondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu katika hili; ni kweli tunarudi katika mfumo wa marejesho. Lakini kama tunarudi katika mfumo wa marejesho tufanye utaratibu upi; warejesheane *TRA* na *ZRB,* isiingie Hazina katikati. Ikiingia

Hazina katikati ucheleweshaji wa marejesho utatokea. Sasa hapo ndipo kwenye ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo nikuombe urudi ule utaratibu wa kurejesheana *TRA* na *ZRB.* Tukisema tunapitisha Hazina hapo kikwazo kinaweza kikaja kikatokea tena na baadaye tunaweza tukasema turudi tena katika mfumo wa *zero rate.* Kwa hiyo hilo nitoe ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii tumesema ni nchi ya viwanda. Mheshimiwa Waziri, hili naomba ulisikilize vizuri; ni nchi ya viwanda. Kuna viwanda vya dawa ambavyo vinatengeneza dawa ndani ya hii nchi yetu. Na sisi tuna-*import* dawa, tuki-*import VAT* ni *zero.* Sasa viwanda vyetu vinanunua *material* (malighafi), wananunua malighafi nje, lakini ile malighafi tunaipiga kodi. Ina maana hawa hatuwaweki katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vifaa mfano vifungashio vya kwenye dawa sisi tuna-*import,* lakini mle mna kodi Mheshimiwa Waziri. Na kodi inasababishwa kwa hila moja tu; kwamba eti ukileta hicho kitu kiwe kimeshachapishwa huko nje jina la dawa. Sasa ukifika hapa ukitaka kuviosha vile vitu unaviosha vipi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, hili tunalizungumza hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *material* ya kutengenezea dripu, nayo pia yanapigwa kodi. Na kiwanda chetu kitakuwa hakiwezi kushindana, na tujue kwamba tumepewa fursa ya soko la *SADC* kuuza dawa, *SMD.* Sasa hii fursa tutaipoteza kwa sababu ya hizi kodi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kifuniko kile cha *rubber* cha kufungia dawa, nacho pia kinatakiwa kiwe kina jina ndiyo kiwe *zero,* ukikileta hakika jina ina maana kwamba tayari kinapigwa kodi. Kwa hiyo, viwanda vyetu vitashindwa kuja kushindana na dawa za nje. Ijapokuwa kwamba hatutengenezi dawa zote, lakini tuna lengo la viwanda, kwa

kuwa tuna lengo la viwanda hiki kitu tukifanye. Vinginevyo tunaweza tukaja tukashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze hii bajeti, ni bajeti kweli kwamba kazi iendelee. Ni kweli bajeti kazi iendelee; imegusa miradi yote iliyokuwepo mwanzo na imechukua miradi mingine mipya. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali kwa kufanya bajeti ya aina kama hii ambayo ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, na sisi tunasema kazi itaendelea, na sisi tutaendelea kuiunga mkono. Hii ni bajeti ambayo imetokana na llani ya Chama Cha Mapinduzi. Yale yaliyosemwa katika ilani tumetakuta leo humu ndani ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo maana nikasema katika historia yangu ya kuwa Mbunge, hii ni bajeti ya kwanza ambayo imebeba maoni mengi ya Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil David Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa ajiandae.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa nishukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mchana huu kwa lengo mahususi kabisa la kutaka kuishauri Wizara na Serikali katika maboresho ya bajeti zilizowasilishwa pamoja na bajeti hii tunayoijadili wakati huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee pia nipongeze maamuzi mbalimbali yanayofanywa na mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu, kwa ajili ya manufaa ya Taifa hili. Na moja kubwa kabisa ni hili suala la Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara kwa muda mrefu sasa. Awamu iliyopita, kipindi changu cha mwisho, nilikuwa Mjumbe hapo na sasa hivi pia nimeendelea kuwa Mjumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Liganga na Mchuchuma limekuwa likirudi mara nyingi sana, lakini hata hivyo, tulivyojaribu kuwashauri Serikali na wenyewe tulijitahidi sana kuongea humu ndani tukionesha kwamba Liganga na Mchuchuma ni sehemu ambayo inaweza ikatuletea mapato makubwa sana kama nchi. Lakini mama sasa ameamua kuwa jasiri na anataka mradi huu utekelezwe, na tunaomba sana ukatekelezwe kadri ya alivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe pia kwamba machimbo haya na miradi hii ya madini mikubwa ndiyo yenye uwezo mkubwa sana wa kuleta mapato mazuri kwenye nchi yetu. Nikumbushe pia kwamba mama kafanya maamuzi mengine magumu sana kwenye Mradi wa Mbunyu uliopo kwenye Jimbo la Ndanda, kwenye Kata ya Chiwata, kwa sababu utekelezaji wake nao umekuwa wa kusuasua lakini utanufaisha Mkoa wa Mtwara, Wilaya ya Newala Vijijini, Wilaya ya Ruangwa pamoja na Wilaya ya Masasi. Kwa hiyo tunaomba kabisa na wenyewe wakauangalie waone namna ya kutaka kwenda kuutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu pia wakati wa utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma kutakuwa na reli pale inayotoka Liganga kuelekea Mtwara kwa maana ya bandarini. Kwa hiyo, matumizi ya bandari yatakwenda kufanyika. Lakini sasa madini hayo ya mbunyu *(graphite)* yatakayokuwa yanatoka Chiwata, ni rahisi kuyashusha pale Kata ya Chigugu nayo yakapakiwa kwenye reli hii yakaenda bandarini Mtwara na kuweza kusafirishwa kwa ajili ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kufanikiwa kutokana na namna ambavyo Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ameleta hii bajeti yetu, na nimuombe Mheshimiwa hapa

asiingie kwenye mtego ambao Mawaziri wengine labda waliopita walikuwa wanaingia. Mara nyingi tumekuwa na utaratibu wa kupunguza ama kuongeza kodi, lakini ni mara chache sana tumekuwa tuna utaratibu wa kufikiria kuhusu vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja nilikuwa nalifikiria tu peke yangu, kwamba tuna haja ya kuishauri Serikali ili iweze kupata vyanzo vipya vya mapato, sasa sijui kama Mheshimiwa Waziri ameshawahi kufikiria. Ukiwa bandarini Dar es Salaam na maeneo mengine, utaona magari mengi sana yanakwenda nje ya nchi yamewekwa zile *label* za *IT,* zimeandikwa tu kwa *marker pen.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sijui kama wasaidizi wako wameshawahi kujiuliza siku moja wakiamua vile vibao viandikwe kwa kutumia vibao halali vya *number plates* tutakusanya *VAT* shilingi ngapi na kiasi gani kingekwenda kusaidia kwenye maendeleo ya wananchi wetu. Kwa sababu watu hawa pia wamekuwa wanaharibu barabara. Lakini ukiandika kwa ile *marker pen* pale unachajiwa shilingi 10,000 tu ambayo inakwenda moja kwa moja kwa mwandikaji na Serikali pale haipati kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hapa tunaongeza kwenye kodi ya mafuta kwa maana ya *road toll* ili wananchi wakalipe. Na mpaka sasa Mheshimiwa Waziri ukumbuke Watanzania karibia milioni 2.5 ndio wanaolipa kodi, katika milioni 60. Na tumekuwa na taratibu sasa za kuwabana sana wafanyakazi pamoja na wafanyabiashara. Kwa hiyo, tunawakamua kwa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tujaribu kuangalia vyanzo vipya vya mapato ili viweze kuwasaidia hawa watu kupokea. Kwa hiyo niombe kabisa hili jambo la *number plates* mkaliangalie, mkaangalie pia hili wazo la mama kwamba Liganga na Mchuchuma sasa ianze kufanya kazi vizuri. Nia yetu na nia yako kama Waziri iwe ni uboreshwaji wa sera za

mapato na matumizi na kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili iweze kusaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, umeongea vizuri sana suala la *ETS.* Lakini pia umeongea kuhusu suala la *industrial sugar,* na Jirani yangu hapa, dada yangu Mheshimiwa Hawa naye amelisema, na Waheshimiwa wengine huku nao nimesikia wakiwa wanalisema. Sasa ni vizuri na wewe mwenyewe kwenye taarifa yako umesema umeamua kuondoa kabisa hii tozo ya asilimia 15 kwenye *industrial sugar* ili iweze kuwasaidia wafanyabiashara kuweza kupata *an extra working capital. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukumbuke kwamba Serikali sasa inadaiwa. Ile ambayo mliishikilia zamani mnasema nini kuhusu hii? Kuanza kuwapatia kuanzia sasa na kuendelea wakati huko nyuma zaidi ya miaka kumi hamjawahi kuwa-*refund* na yenyewe ni ngumu. Na pale umeonesha kidogo kwamba inapunguza mapato ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikukumbushe tena ile ilikuwa ni tozo ambayo mwisho wa siku ilitakiwa iwarudie wenyewe. Haikuwa mapato ya Serikali, Serikali mlikuwa mnaitunza. Sasa mfikirie namna ya kuwarudishia ili waongeze mitaji kwenye uzalishaji wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sawasawa na *VAT.* Sijasikia hapo vizuri mkakati wako mahususi wa kuona *VAT refunds* zinarudi kwa hawa wawekezaji, zinarudi kwa hawa wafanyabiashara ili waweze kukuza mitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kuongeza mapato ni suala la *ETS. ETS* Waheshimiwa Wabunge ni *Electronic Tax Stamp* ambayo imekuwa inawekwa kwenye vinywaji. Na sisi kwenye Kamati tumeongea mara nyingi. Tunaishauri Serikali kwa mara nyingine, mkataba huu haukuwa bora sana, unasimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, sasa hatuna uhakika hili jambo linawahusu ninyi moja kwa moja, linawahusu watu wa Viwanda na Biashara, lakini mkakae na kujadiliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ya kuhesabu chupa moja kwa shilingi 10 wakati Serikali inakwenda kukusanya kodi ya shilingi tatu kwa kuhesabiwa kwa shilingi kumi; tunamnufaisha nani? Kama tunaona kuna uhalali wa kufanya hilo jambo basi niishauri Wizara yako kimkakati kabisa sasa kazi hii ikafanywe na *TRA,* iwe sehemu ya kuongeza mapato. Kwa sababu hakuna haja ya kutumia gharama kubwa kutayarisha utaratibu wa kukusanya kodi halafu unakwenda kukusanya kodi ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, ukipata muda nitakuelewesha kwenye hili kwa sababu wafanyabiashara walikuja kulilalamikia. Kuna kampuni inaitwa *SIPA* ndiyo inayofanya kazi ya kuhesabu vinywaji tuseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano chupa moja ya Coca-Cola inatakiwa ilipiwe kodi ya shilingi tano, anayekwenda kuhesabu chupa na kumwambia *TRA* kwamba Coca-Cola wamezalisha chupa 20 katika chupa moja analipwa shilingi 10; hii siyo sawa. Muone namna sasa ya kuondoa ili kama inawezekana na kuna ulazima wa kufanya hivyo basi *TRA* wakafanye hii kazi ili iweze kuwanufaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ni nzuri kama walivyosema wengi, lakini tuombe sana sasa – na Wabunge wengi hapa wamesema ni kazi nzuri – basi ile shilingi mia iliyotengwa kwenye mafuta lazima tuhakikishe inakwenda kuwa *ring fenced* na iende huko *TARURA* kwenda kufanya kazi kwa wakati. Utaratibu wa kupeleka baada ya miezi sita, baada ya mwaka mmoja na wakati mwingine unaambiwa wanapeleka kwa Zimamoto siku za mwisho kabisa za kumalizia bajeti, siyo mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wana shida kubwa sana ya barabara huko vijijini, wananchi wana shida kubwa ya madaraja pamoja na vivuko. Sasa hela hii ikikusanywa na ukija hapa utueleze kwamba pesa iliyokusanywa kwa ajili ya miradi ya maji na miradi ya

barabara awamu iliyopita, kwa maana ya bajeti iliyopita, imekwenda mpaka sasa kiasi gani. Hiyo chenji iliyobakia itapatikana lini ili mkakamilishe... kwa sababu hii ndiyo miradi...

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shabiby.

T A A R I F A

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba haohao *SIPA* wanaotafuna sasa hivi upande huu ndiyo haohao walikuwa wana tenda ya vinasaba. Kwa hiyo bado wanaendelea kutafuna. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Cecil Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaikubali taarifa hiyo. Na nataka nimuongezee tena hapa Mheshimiwa Waziri kwamba watakapokwenda kufanya *review* ya hizi kodi mbalimbali wanazoziingiza kwenye mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo dada yangu pale, Mheshimiwa Paresso, amesema, wakaangalie sasa kwamba mpaka sasa kwenye mafuta kuna kodi zisizopungua 16. Zinakaribia sasa hivi kufikia shilingi 900, tunakaribia kwenda shilingi 1,000. Kwa hiyo kwenye bei ya mafuta ya shilingi 2,5000, shilingi zaidi ya 700 inakwenda kama kodi Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa mkafanye *review* tuangalie vyanzo vipya vya mapato, tupunguze hizi kodi mbalimbali ambazo mwisho wa siku zinakwenda kumgandamiza mwananchi. Kwa sababu kwa namna yoyote ile, unapoongeza shilingi 100 kwenye mafuta wasafirishaji nao karibuni utasikia wameongeza gharama za usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nauli kwa mfano kutoka Ndanda kwenda mpaka Masasi badala ya kuwa shilingi 2,500 au 1,500 tuliyoizoea sasa hivi, tunaweza tukaanza kuchajiwa shilingi 3,000 kwa sababu gharama ya mafuta imeongezeka. Na lazima hapa ukumbuke kwamba tunapoongeza hizi gharama za mafuta lazima tuone namna ya ku-*balance* tutafute sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze sana bajeti yako, na nikushauri tena kwamba weka malengo katika miaka mitano hii mama ikimpendeza na Mungu ikimpendeza, ukiendelea kuwa hapohapo basi twende kwenye utekelezaji wa *budget deficit* iwe *single digit.* Badala ya sasa ambapo tumetekeleza bajeti kwa asilimia 75 mpaka 80, tunatamani siku moja tuambiwe bajeti yetu imetekelezwa kwa asilimia 95 na kuendelea, ili tuwe tuna *single digit,* ndiyo tutakuja kuona manufaa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii tunapanga hapa tunaomba ikatekelezwe kama tunavyosema. Wakati mwingine inatokea ama mnachelewesha kupeleka pesa, mnataka tena watu kule chini waanze tena kuleta taarifa juu; hili siyo jambo jema. Utakapokuja kwenye *mid-year review* au *quarterly review* basi tuone Waziri unapeleka pesa kadri zilivyopangwa hapa na Wabunge ili zikafanye kazi inayokusudiwa na tuone matokeo chanya kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kwa nafasi uliyonipatia. Ahsante kwa muda wako. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo atafuatiwa na Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mheshimiwa Injinia Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, ajiandae.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nami namshukuru Mungu kwa kupata nafasi niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na kazi nzuri sana aliyoifanya hasa kuchukua maoni mengi ya Wabunge na kuyaingiza kwenye Mpango wa Serikali, nampongeza pia Waziri wa Fedha kaka yangu Mwigulu Nchemba pamoja na Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Injinia Masauni kwa kazi kubwa na nzuri sana ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitajikita kwenye mambo mawili la kwanza ni kuhusu utalii. Sekta ya Utalii imesahaulika sana. Bajeti hii imeangalia mambo mengi sana, lakini nataka nikuhakikishie haijatoa ahueni yeyote kabisa kwenye sekta ya utalii. Wizara ya Maliasili na Utalii ni kana kwamba vile haijui dunia imetoka wapi, ipo wapi na inakwenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia taarifa zilizopo kutokana na changamoto za *Corona* duniani tunaambiwa kwamba uchumi umekuwa na mdororo hadi kufikia asilimia 3.3 ambayo ni hasi kutoka asilimia 2.8 ya mwaka 2019. Lakini tunaambiwa kwamba Pato la Taifa limeshuka kutoka asilimia 7 mpaka asilimia 4.8 mwaka 2019/2020. Tunaambiwa pia mchango wa utalii umeshuka kutoka asilimia tuliyoizoea 17.5 mpaka asilimia 10.7 kwenye Pato la Taifa. Tunaambiwa pia mapato yamepungua na taarifa imetolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii kutoka bilioni 584 mpaka bilioni 89 ambayo ni sawasawa na asilimia 15 ya malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mapato ya mwaka 2019/2020 yalikuwa bilioni 252 kipindi kama hiki leo bilioni 44.8 kwa taarifa zao wenyewe Wizara ya Maliasili na Utalii. Tunaambiwa pia idadi ya utalii imepungua kutoka mwaka 2019/2020 walikuwa milioni moja elfu hamsini na mbili mia tisa arobaini na tatu (1,529,443) na sasa hivi ni watalii laki nne na kumi na nne na thelathini (414,030).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba changamoto kubwa zimejitokeza hasa kwenye ajira, ukienda

Arusha hoteli nyingi zimeathirika, *Tour Operators* wameathirika, waongoza utalii wameathirika, karibu sekta zote madereva, wahudumu wa hoteli, wapagazi wale, wapiga mahema, wapishi, *staff* wa maofisini wapo hoi kwa sababu hakuna wageni. Tunajua, Waziri anajua, Waziri wa Fedha anajua, Waziri wa Utalii anajua, lakini mambo yanavyokwenda kana kwamba wapo dunia nyingine tofauti na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonishangaza pamoja na matatizo yote haya *solution* waliyokuja nayo Wizara ya Maliasili na Utalii na Serikali yetu hii ni kuongeza tozo. Utaona tumeongeza dola 10 kipindi cha *high season* kwenye hifadhi ya Serengeti na hifadhi ya Nyerere, lakini tumeleta tozo nyingine mpya inaitwa *land base rent* kwa watu ambao wanakuwa na *seasonal camp* dola 2,000, ukiwa na *permanent tented camp* dola 20,000, ukiwa na *lodge* dola 50,000 ndani ya hifadhi, Serengeti mle ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mtalii anapokuja Tanzania akifika *airport* pale analipa *VISA,* akitoka pale anapanda gari ya utalii anachangia mafuta pamoja na masuala mengine, akienda kwenye hoteli akilala analipa ambapo Serikali inapata fedha, akienda kwenye *park* analipa *park fee,* akitoka pale akilala ndani ya hifadhi analipa kitu kinaitwa *concession fee* ambayo kila siku anayolala ndani ya hifadhi analipa dola 50 bila *VAT.*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wamekuja wenzetu maliasili na utalii na tozo nyingine, eti ukitengeneza *seasonal camp* umechukua hema lako umeliweka mle ndani ya hifadhi dola 2000, ukichukua hema lako kama ni kwa muda fulani, *permanent* dola 20,000, umejenga *lodge* ume-*invest* wanakupiga dola 50 hasa ile *concession fee* ni ya nini? kwa hiyo, unaona kabisa Wizara ya Maliasili na Utalii wasipoangaliwa hawa wanakwenda kuiua kabisa sekta hii wanakuwa ni *Corona* namba mbili katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri kwenye jambo hili Serikali ikaliangalie jambo hili vizuri hizi tozo zisitishwe, kwa

sababu kwanza hazijaanza kutozwa, zitaanza kutozwa kuanzia tarehe Moja mwezi wa Saba mwaka huu inamaana bajeti hii ikipita. Tunavyozungumza leo hata wakisitisha Serikali haijapata hasara yoyote kwa sababu mambo haya ni mapendekezo yote wamekuja nayo Wizara ya Maliasili na Utalii. Ndiyo maana nilisema kwenye mchango wangu uliopita tunazo hifadhi 22, hifadhi ambazo zinazalisha ni tano peke yake, hifadhi 17 hazina uwezo wa kuzalisha kiasi cha kujiendesha, badala ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuja na mpango mbadala kila siku wanafikiria kuongeza tozo Serengeti, kuongeza Nyerere na masuala mengine, ukiwauliza ni kwa sababu gani wanasema tunataka tuzuie *congestion!* eti tukiongeza tozo watalii wataogopa kwenda hifadhini kwa hiyo hifadhi zitabaki salama, halafu leo wanakuja na maelezo hapa tunataka tuongeze watalii kutoka idadi ya sasa mpaka milioni tano, unashindwa kujua hata haya mambo wanayo yazungumza wanayatoa wapi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo ni *very serious* naiomba sana Serikali kwa sababu tunaye Rais msikivu, Rais ambaye ameamua kuleta ahueni kwenye sekta binafsi, Rais ambaye anafahamu hawa sekta binafsi, kuna *hotel* pale Karatu, walikuwa zamani kabla ya utalii *hotel* ya dola 200 leo mtu ameshusha mpaka dola 100 ili kuweza kuvutia wageni waje, Serikali hii inakwenda kuongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hili jambo ni vizuri Bunge lako Tukufu na Serikali yetu waende wakaliangalie watu wa Maliasili na Utalii wakumbushwe kwamba kazi yao wao ni kuangalia *interest* za Serikali pia kuangalia na *interest* za wawekezaji kwa maana ya sekta binafsi, lakini siyo kuangalia Serikali peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu wenzetu hawa wa *bureau de change,* tumepata shida kubwa sana Mkoa wa Arusha, tumeteseka na ma-*task force* kila siku yanashindana kuja tu pale, baadaye wamekuja na mambo haya ya *bureau,* na watu wa *bureau* hawa kuna mchezo wanaucheza ambao sijui hawa watu wa Serikali kuna watu wao wanataka wafanye hii biashara? Maana

ukiangalia mwaka 2015 mtaji wa mtu wa *bureau* ulikuwa milioni 40, wakaja mwaka 2015 hadi kufika mwaka 2017 wakaongeza ikaja milioni 100, kufika 2018 Mei wakapeleka milioni 300, baadaye wakaona sasa kila wakiongeza wale wanafanya biashara, kila wakiongeza wanafanya biashara, baadaye wakaamua kuvamia na kwenda kuwapora! Wakapora pesa zao, wakapora magari yao, wakapora hati zao za nyumba, wakapora viwanja wamewaacha hoi taabani.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hii changamoto ni kubwa sana. Mambo ya msingi yakiongelewa acheni mambo ya taarifa sikilizeni hili Bunge ni *very serious* mmefanya taarifa ni *fashion*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mrisho Gambo kengele imegonga hapa ya pili na ...

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wameniingilia kwenye taarifa naomba angalau nimalizie tu, kwa heshima yako.

NAIBU SPIKA: Nikikupa nafasi ya kumalizia inabidi nimpe nafasi akupe taarifa.

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, sawa basi apewe taarifa nimalizie.

NAIBU SPIKA: Hapana ni muda wa watu wengine, ahsante sana Mheshimiwa Gambo. *(Makofi)*

MHE. MRISHO M. GAMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana lakini ombi letu kwamba warudishiwe leseni, warudishiwe fedha zao, gharama zipungue na *assessment* za kienyeji zile zifutwe ili watu wafanye biashara Serikali ipate kodi na fedha zake.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mjue tu kwamba hapa mbele huwa kuna kitufe cha kuzima *microphone* zote humu ndani. Kwa hiyo nawaheshimu sana mkiendelea kuzungumza baada ya mimi kusema ahsante sana, kwa sababu hapa mbele ninao uwezo wa kuzuia mtu kutokuzungumza.

Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Nusrat Hanje ajiandae.

MHE. NICHOLAUS G. NGASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami pia kunipatia nafasi ya kuongea na kutoa mchango wangu kwenye bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2021/2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama yetu Rais Samia Suluhu Hassan kwa *consistency* nzuri waliyoanza nayo katika ukusanyaji wa mapato, ukijaribu kuangalia taarifa ya Msemaji Mkuu wa Serikali mwezi wa nne tulikusanya trilioni 1.34, mwezi wa tano tumekusanya trilioni 1.3 naamini na mwezi wa sita mtakwenda vizuri, hongereni sana Serikali katika ukusanyaji wa mapato. Ni mwanzo mzuri, Wizara ina vijana wawili mahiri yupo Mheshimiwa Daktari Mwigulu Nchemba yupo na Injinia Masauni ambao kwa nyakati tofauti wameshakuwa mabosi wangu wakati nipo Serikalini nawajua umahiri wao naamini watakwenda vizuri, hongereni sana pia kwa kuaminiwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu itakuwa ina pande mbili, upande wa kwanza utakuwa ni wa kitaalam na upande wa pili nitaelezea uhalisia katika yale nitakayoyachangia. Upande wa kitaalam ambao utakuwa ni upande wa nadharia *reference* nitafanya kwa kutumia sheria mbalimbali na miongozo mbalimbali, sasa naanza na jambo la kwanza ambalo nataka nilichangie jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni udhibiti na usimamizi wa fedha za serikali, makusanyo ni mazuri

tumepanga bajeti ya trilioni 36 kwenda kukusanya na kutumia katika mwaka huu wa fedha, tunayo Sheria ya Fedha Namba 6 ya mwaka 2001 inaitwa *Public Finance Act* ilipofanyiwa maboresho mwaka 2010 ilizaa baadhi ya taasisi, moja ya taasisi ambazo zilizaliwa inaitwa taasisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani wa Serikali - *Internal Auditor General Office* ndiyo taasisi ambayo kwenye Halmashauri inaleta watu wanaitwa *Internal Auditors* au Wakaguzi wa Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakaguzi wa Ndani pamoja na majukumu yao mengine yote wana majukumu makubwa matatu ambalo la kwanza ni kuangalia michakato inayoendelea kwenye Taasisi za Serikali tunasema kuangalia zile *process.* Jukumu la pili ni kuangalia ile *assurance* udhabiti wa Serikali kwamba tunakokwenda ni uhakika na jukumu la tatu ni kuangalia *quality* tunasema *quality control.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kinachoendelea katika uhalisia katika halmashauri zetu Wakaguzi wa Ndani wamegeuka kuwa Menejimenti za Halmashauri na wenyewe badala ya kuwa wakaguzi. Ukienda kwenye SMT ambayo Mkurugenzi wa Halmashauri au kwenye Taasisi Mjumbe mmojawapo ni Mkaguzi wa Ndani ambaye anatakiwa amkague huyo Mkurugenzi wa Taasisi au Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye ni bosi wake, hivi unaweza ukamkagua bosi wako na ukatoa taarifa ya kumkaanga ni jambo gumu sana, matokeo yake ni nini? ndiyo maana tunapokuwa kwenye vikao vya Kamati ya Fedha au Mabaraza ya Halmashauri anapotuhumiwa *DT* unashangaa *Internal Auditor* anasimama kumtetea *DT,* kwa utaratibu huu itakuwa ngumu kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara hawa watu muwakumbushe majukumu yao, kutumia vyuo mbalimbali mlivyonavyo chini ya Wizara yenu muwajengee uwezo kama ambavyo la wiki iliyopita Mheshimiwa Hasunga alichangia mvitumie hivi vyuo, wakumbushwe majukumu yao, wao ni waangalizi wa Serikali wanawasaidia kuangalia wale ni *watchdogs,* lakini siyo sehemu ya *operations* katika Halmashauri zetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine kuhusu Wakaguzi wa Ndani, sasa hivi tunasema tuna *e-government* tunaendesha mfumo wa Serikali kimtandao, unakuta una Mkaguzi wa Ndani mmoja ambaye *basically* ni *accountant* namna gani ataenda kukagua hii mifumo ya Halmashauri ya kukusanya fedha ya kieletroniki? Sasa niwaombe Wizara kama mtaomba kibali cha kuajiri tuna halmashauri 185 kuna watu wanaitwa *Information System Auditors* hiyo Idara ipo pale katika Ofisi ya *CAG*. Katika Ofisi ya *AG* pia muiweke muajiri watu ambao wanajua mifumo waende kukaa na kukagua mifumo ili kuwarahisishia wale *Accountants* katika suala la Ukaguzi wa Mapato ya Serikali na Matumizi ya Serikali, hiyo ni sehemu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili baada ya sheria kufanyiwa maboresho kuna kitengo kilianzishwa kinaitwa vitengo vya usimamizi vihatarishi *(Risk Management Unit),* hivi ni vitengo ambavyo vimetengenezwa kwa ajili ya kuangalia viashiria vya viahatarishi Serikalini katika utekelezaji wa mipango yetu kwa kila robo mwaka, naomba pia mviimarishe mwajiri watu au waliopo wapewe mafunzo wajengewe uwezo waweze kuisaidia. Vitengo hivi vinaenda sambamba na vitengo vya Ukaguzi wa Ndani na kila robo mwaka wanaandaa taarifa inapitiwa na Kamati za Uongozi na kuangalia vihatarishi vitakavyokwamisha *operations* za Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni Halmashauri au Idara zinazojitegemea wanatoa maelekezo na kusema kwamba safari hii tuna *Corona* tutakwamisha kwa namna moja, mbili, tatu. Safari hii tuna mvua nyingi kwenye ujenzi wa barabara tutakwamishwa na moja, mbili, tatu. Mviangalie hivi vitengo mviimarishe mvijengee uwezo vitaweza kutusaidia sana katika kufikia malengo ya bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakwenda kitengo cha tatu au taasisi ya tatu ni Ofisi ya *CAG,* Ofisi ya *CAG* ipo chini yenu Wizara ya Fedha, sasa unapoongea Ofisi ya *CAG* ndiyo inaleta watu wanaitwa *External Auditors* wanapoenda kufanya ukaguzi kwenye taasisi nyingine. Hawa watu

wanapofika wanafanya mnasema zile *entrance meeting* na ukitaka kuondoka unafanya *exit meeting,* lakini ukifanya uchunguzi kwa kiwango kikubwa wana - *collide* na Wakuu wa Taasisi katika suala la uandaaji wa hizi hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta taasisi imepewa hati safi lakini ukifuatilia matumizi yake siyo mazuri, wanaenda wanakaa mezani wanajadiliana kabla hawajafanya *exit meeting* wanaacha kitu kidogo wanaongezewa pale mlungula wanaondoka ripoti inatoka safi, fanyeni uchunguzi mjiridhishe katika hili wizara. Kwa hiyo, katika upande wa udhimabiti wa fedha za Serikali na Usimamizi wa Fedha itawasaidia sana mkitumia haya maeneo matatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango namba mbili, eneo namba mbili nataka kuchangia Utumishi wa Umma. Wakati nachangia Mpango wa Maendeleo ya Taifa nilisema Utumishi wa Umma ni nyenzo muhimu sana katika kufanikisha mipango hii. Niwapongeze Serikali, niwapongeze Wizara ya Utumishi, TAMISEMI na nyinyi Wizara ya Fedha kwa kuja na motisha mbalimbali mlizotoa kwa watumishi wetu wa umma, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ambayo ninatamani niichangie kuna eneo la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma. Tunayo Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, Kanuni za 2013 na Kanuni za Kudumu za 2019 hapa changamoto ipo wapi, wanapoandaa mafunzo kuna mipango ya mafunzo ya muda mrefu na mafunzo ya muda mfupi ni kichaka kingine ambacho Maafisa Utumishi wanakitumia kunyima haki za Watumishi wa Umma. Wakati mwingine mtumishi anahitaji kujisomesha, kujiendeleza na kujijengea uwezo lakini unaambiwa haupo kwenye mpango wa mafunzo, sasa huyu mtu anajisomesha kwa hela yake sasa kwa nini unamzuia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie tuweke utaratibu kama ambavyo inasema Sera ya Mafunzo ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2013 watu hawa wanapohitaji kujiendeleza kwa sababu ni lengo ni kuboresha na kuongeza ufanisi katika

kazi, wapewe nafasi ya kwenda kusoma wakirudi waendelee. Kwa sababu Serikali ina fedha ndogo na uwezo wa kusomesha kila mtumishi kadri ya muda wake wa kusoma haiwezi, mtu anapotaka kwenda kujisomesha apewe ruhusa akasome kwa sababu atakaposoma ni faida kwa Serikali yetu, tuepukane na haya matusi wanayotukanwa watalaam wetu kwamba hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu amekaa miaka kumi na tano hajawahi hata kupata hata *refresher course* unadhani atakuwa na uwezo mzuri wa kufikiria? Ndiyo maana hata huko kwenye vyombo vya ulinzi na usalama ukikaa miaka mitatu, minne unapigwa *refresher course* maana yake ni kwamba kuna vitu vipya hata *computer* zina *software,* unasikia tunatoka *Window 7* tunaenda *Window 8,* tunaenda *Window 9.* Kwa hiyo Serikali hili mliangalie katika kuboresha hili eneo, watumishi wakiongezewa ujuzi litatusaidia sana katika kufikia haya malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanaisha Ng'azi Ulenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, ajiandae.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya kuchangia, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi hii ya uhai, kipekee kabisa niwashukuru sana Mawaziri wetu wa Wizara hii ya Mipango na Fedha kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti yetu, lakini pia kwa kujibu kwa umakini na uweledi mkubwa Hoja za Wabunge, Mwenyezi Mungu aendelee kuwasimamia katika majukumu yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na vilevile nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati Mzee wangu Sillo kwa kazi nzuri aliyofanya ya kuitengeneza bajeti hii mpaka hapo ilipofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee kabisa na kwa dhati ya nafsi yangu nimpongeze Mwanamama jasiri, Mwanamama hodari Rais wetu Samia Suluhu Hassan kwa usikivu mkubwa alionao kuhakikisha kwamba anakwenda kuondoa shida na taabu kwa Watanzania. Kama jina lake linavyoitwa Samia kwamba ni msikivu, Mama yetu ameitendea haki Watanzania kwa kusikiliza vizuri kabisa hoja za Wabunge na kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuchangia suala zima la kupunguza urasimu katika kodi za viwanja na mapango hili linakwenda kutekelezwa kwa kuhakikisha kwamba kodi za mapango yatalipwa kwa kupitia *LUKU,* niipongeze sana Wizara kwa usikivu huo nami nimeipokea kwa mikono miwili sana. Tahadhali moja ambayo naomba kuitoa wizara tafadhalini tujaribu kuangalia kwa wale ndugu zetu wanaofanya kazi ya biashara ya *real estate* isije kulipiwa kodi katika yale majengo ambayo kuna *LUKU* zaidi ya moja ndani lakini akaenda kulipa kodi moja kwa moja tutakuwa tumewabana wafanyabiashara wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niipongeze sana kwa suala zima la kuhakikisha tunakwenda kuziboresha barabara za *TARURA,* hili ni jambo kubwa sana kwa uchumi wa Tanzania na kuhakikisha kwamba sekta ya ujenzi inakwenda kuongeza na kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye Pato la Taifa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii ya kuongeza fedha katika mafuta ili tuweze kujenga barabara za *TARURA*, mimi naomba nichukue nafasi hii pia kuwatoa Watanzania wasiwasi. Watanzania wanafahamu kwamba unapoongeza fedha katika mafuta basi tunakwenda kuongeza mfumuko wa bei, kwa mujibu wa *data* za *National Bureau of Statistics*. Lakini Watanzania nawaomba tuwahakikishie kwamba, mama yetu mweledi mwenye upeo wa mbali ameangalia vizuri sana, kwa sababu *factor* muhimu katika kuhakikisha mfumuko wa bei ni suala zima la gharama za usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotoa nyanya zetu kutoka Iringa zinapokuja Dar es Salaam, msimu wa mvua barabara hazipitiki, hakika mfumuko wa bei utakuwa juu. Lakini tunapokwenda kuiangalia *GDP* ya taifa letu tunakwenda kuangalia uzalishwaji wote wa makampuni na watu binafsi. Kwa kilichofanyika hapa, *in a long run* tutaongeza *per capital income* ya Mtanzania na nchi yetu inakwenda kukua katika uchumi wa mbele wa taifa hili. Hongera sana mama yetu Samia Suluhu Hassan, hongera sana Mawaziri mliofanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya Watanzania wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba nichangie kuhusu suala la uchukuzi. Sisi Watanzania tuko kwenye umoja wa *East Africa* na tuko kwenye umoja wa *SADC* lakini hatuko kwenye umoja wa *COMESA*. Sasa, kwa kuangalia *Overload Control Act* ya *East Africa* na *Overload Control Act* ya *SADC* tunapata *confusion* kidogo hapa. Wafanyabiashara wetu wanapolipa *transit charge* kwa kila kilomita 100 ndani ya Tanzania analipa dola 16,000. Lakini huyu huyu Mtanzania anapokwenda Kenya kwa mujibu wa *East Africa* anatakiwa alipe dola 10, lakini wanaotoka *SADC* na wanaotoka Uganda ndani ya ukanda ule wa *East Africa* wanalipa dola 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iende ikaliangalie hili ili kuhakikisha wafanyabiashara wetu nao wanakwenda kufanya biashara katika *harmonizing way* ili wanaokuja Tanzania nao waweze kufanya biashara kwa kutumia *transit charge* ya dola 10 badala ya 16. Kwa sababu wenzetu ambao wapo kwenye *COMESA wana-take advantage* ile ya kutukandamiza sisi. Wale wa *SADC* wanapokwenda Kenya wanalipa 10 lakini wanapokuja Tanzania wanalipa 16. *It is obvious wata-run away from* Tanzania na wataenda kukimbilia Kenya na Uganda. Kwa hiyo naomba hili uliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba sana kuishauri Serikali. Tumepata mwarobaini wa barabara za vijijini kwa kutumia *TARURA*; lakini naomba niishauri Serikali kwa unyenyekevu mkubwa. Ni kwamba, barabara zetu kuu *(trunk*

roads) na barabara zetu za *regional roads* pamoja na *district roads* thamani yake ni trilioni 21 za Tanzania. Thamani hii tusipoilea ipasavyo tutakuja kurudi nyuma na tutaanza kuzijenga barabara hizi upya. Naomba tuangalie namna nzuri ya kuhakikisha kwamba barabara hizi, *trunk roads*, *regional roads* na *district roads* zinafanyiwa *periodic maintenance* ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwasababu gani, ukiangalia *corridor* ya *TANZAM* ambayo ni muhimu sana kwa sababu ndiyo inatuvutia wateja kutoka Malawi, Zambia pamoja na Lubumbashi – *DRC*. *Corridor* hii ni chakavu na imechoka sana, tunataka kuwaambia nini wafanyabiashara wanaopita katika njia hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukulieni mfano tu, kile kipande cha Chalinze – Mlandizi *it is almost collapsed,* lakini tukiangalia kutoka Dodoma mpaka Iyozi *it is almost collapsed*, ukiangalia Tunduma mpaka Igawa *it is almost collapse.* Sasa hii *TANZAM corridor,* ambayo ndiyo inatuletea wateja kwenda bandari ya Dar es Salaam, tunaiambiaje? Kwa hiyo, niishauri sana Serikali, kwa heshima na taadhima, *despite* ya njia nzuri tuliyoifanya upande wa *TARURA*, tuangalie namna ya kulea trillion 21 ya mtandao wa barabara za mikoa na barabara kuu pamoja na barabara za wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa data zilizopo, kwa mwaka wa fedha uliopita, barabara kuu na barabara za mikoa na barabara za wilaya zimefanyiwa *periodic maintenance* kwa asilimia 42 tu. Na ukienda barabara za wilaya ambazo zipo chini ya *TARURA*, zimefanyiwa *maintenance* kwa asilimia 28 tu, na asilimia 52 hazijafanyiwa *periodic maintenance,* kilichofanyika ni *just sports improvement*s na wala hakuna *over laying.* Nini tunakwenda kufanya? Maana yake tutakuja kuanza *afresh* kama tusipoamua kutenga fedha kwa ajili ya *maintenance* ya barabara kuu, barabara za mikoa na barabara za wilaya. Ukiangalia hata barabara ya Kibiti-Lindi-Mtwara ambapo kuna mfanyakazi mkubwa kule Dangote; Dangote anatoa mizigo yake kuleta huku mjini, anakwendaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuone namna ya kuhakikisha wafanyabiashara wetu wanapokuja Tanzania wanakuwa *in a good way* ya kufanya biashara na *kuwa-attract* zaidi ili waje kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba kuunga mkono hoja asilimia 100, nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, ninakusudia kumshauri Spika, inabidi aweke utaratibu hapa mbele wa kutoa tafsiri ya maneno mazito yanayozungumzwa kwa lugha ambazo wengine zinatuacha nyuma. Huwa najiuliza siku zote wakati wa kuomba sijui huwa kiswahili kinatoka wapi? *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Nusrat Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Mheshimiwa Joseph Zacharious Kamonga, ajiandae. *(Kicheko)*

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili na mimi nichangie kwenye Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi bajeti hii ni bajeti ya kwanza katika Awamu ya Tatu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, na ni bajeti ya kwanza kwenye Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. Kwa utaratibu huo maana yake tukiangalia, Mheshimiwa rafiki yangu, kaka yangu, ndugu yangu Mwigulu, Mheshimiwa Waziri mwenyewe ameiita bajeti ya kimkakati. Hata hivyo naomba nimbadilishie kidogo, hii bajeti pamoja na kwamba unasema ni ya kimkakati lakini ni bajeti ambayo mimi naiita bajeti ya tamu-chungu; yaani tunang'atwa halafu tunapulizwa, yaani tunatekenywa huku tunafinywa. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *yes*, bajeti hii kimsingi kuna mambo makubwa ambayo hayajawahi kuzungumzwa katika bajeti za miaka kadhaa mitano tukirudi nyuma. Kuna vitu ambavyo vimekuwa vikilalamikiwa mara kwa mara na

Waheshimiwa Wabunge mpaka na wananchi wetu huko, ambavyo vilikuwa havijaingizwa lakini kipindi hiki tunaviona. Pia, *at the same time* kuna vitu ambavyo kimsingi, vimewekwa kwenye lugha za kiuchumi sana, unaweza kuona havikuumizi, lakini kimsingi vinaumiza Watanzania kwa kiasi Fulani, nitaelezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa tunazungumzia Bajeti Kuu ya Serikali mwaka 2021/2022 ni muendelezo wa mipango ile ya miaka mitano mitano ambayo imeshapita, na sasa hivi tuko watatu, maana yake tumetoka wa pili. Hatuwezi tukazungumza leo bila kuangalia tulipotoka, tulipo na tunapotaka kwenda. Kwa hiyo ni lazima tujifanyie *evaluation* kama nchi, kwamba tumetoka wapi, tupo wapi na tunataka kwenda wapi. Kwa sababu ni muendelezo, ndiyo maana tukasema ni awamu kwa awamu, awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu. Hivyo tumekuwa tuna tatizo kubwa sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapanga mipango ya maendeleo ya miaka mitano mitano, tunatengeneza bajeti/*tuna-formulate* bajeti za kutusaidia *ku-implement* mipango; lakini kumekuwa kuna tatizo sugu la kutopeleka fedha za miradi ya maendeleo kama zinavyopitishwa na Bunge hili. Hili nalisema kwa nia njema ya taifa langu na ninalipenda sana taifa langu. Kimsingi Watanzania ukiangalia *comments* zao baada ya bajeti kusomwa kuna vitu wanavifurahia. Ninachosikitika mimi ni kwasababu, ninajua kuna mahala itafika tutakwama na tutarudi mwakani kusoma bajeti ya mwaka 2022/2023 tukiwa kuna sehemu hatujatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivyo kwa sababu, mathalani, zipo Wizara ambazo zinachangia Pato la Taifa kwa kiasi kikubwa na zinagusa maisha ya Watanzania kwa kiasi kikubwa sana, ambazo utekelezaji wake wa bajeti ni chini ya asilimia 30 kwa miaka mitano *consecutively,* tangu mwaka 2016, mpaka mwaka huu tunaozungumza sasa hivi, 2020/2021. Kwa hiyo, unaona ni namna gani tunavyozungumza kwamba kuna shida sehemu. Tunapanga

bajeti, tunapitisha vizuri, tunashangilia, tunafurahi lakini tukitoka hapo utekelezaji wake ni chini ya asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa miaka mitano mfululizo, *consecutively,* tangu 2016 *average* ya bajeti yake ya miradi ya maendeleo imepelekwa asilimia 19.3 tu. Sasa tunategemea Watanzania wengi wameajiriwa na sekta hii, pia tunategemea ndiyo sekta inayolisha Watanzania asilimia 100, na vilevile Wizara hii inachangia Pato la Taifa asilimia 27.7 na sasa tunapeleka fedha katika kiwango hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na tumekuwa tukilalamika kwamba bajeti iongezwe, lakini hata ile ndogo inayotengwa haipelekwi pia kwa wakati nabadala yakeinapelekwa mwishoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo *ina-good faith* kwa ajili ya taifa letu ni lazima tuone kwamba ni namna gani hizi Wizara ambazo tunasema zinaajiri asilimia kubwa ya Watanzania na kwamba zinachangia Pato la Taifa kiasi kikubwa, tunapeleka fedha kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya pili ambayo ina tatizo kwenye kupelekewa fedha ni Wizara ambayo kimsingi imebeba dhima kuu ya kauli mbiu ya Chama cha Mapinduzi, na hapa nipo na Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Tanzania ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda na biashara, kutoka ukurasa wa 56 - 60 kwenye hii Ilani ya Chama Cha Mapinduzi wamezungumza kwa undani na kufafanua masuala ya viwanda na ya biashara; lakini utekelezaji huu wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara *consecutively* in *years* ni asilimia 20. Kwa hiyo maana yake Serikali ya Viwanda, Tanzania ya Viwanda asilimia 80 ya bajeti haijatekelezwa kwenye miradi ya maendeleo na tunazungumzia kauli mbiu ambayo tunaenda nayo; kwa hiyo kuna changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ya tatu ni kuhusu mifugo na uvuvi ambayo inachangia asilimia tisa ya Pato la Taifa; bjeti yake yaani imetekelezwa kwa asilimia 21 *consecutively* kwa miaka mitano ambao ndio Mpango wa Pili wa Maendeleo; sasa ni changamoto kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Wizara ya Afya ambayo ndiyo inayotoa nguvu kazi ya taifa bajeti yake imetekelezwa kwa asilimia 18.1 tu. Watanzania wakiwa wagonjwa hatutaweza kuzalisha. Bajeti ya mwaka 2020/2021 ya afya Wizara iliomba shilingi bilioni 360 lakini mpaka Machi mwaka huu 2021 walipelekewa shilingi bilioni 83 tu za kutibu Watanzania ili Watanzania wawe wazima wazalishe; ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi ninajua kabisa, nikiwaangalia Mawaziri ninaona nia yao ni njema, changamoto ni tuna kasungura kadogo tunagawana hako hako, ndiyo shida. Kwa sababu ili tupate fedha za bajeti tupeleke kwenye miradi ya maendeleo ni lazima tukusanye kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na Mwalimu Nyerere alishawahi kusema, kwamba, Serikali ambayo haikusanyi kodi kimsingi haiwezi kwenda kokote. Mimi ninajua kuna changamoto, na najua nia ni njema; tunatenga fedha zinatakiwa zije ziende zote, lakini tunashindwa kupeleka kwa sababu hatuna fedha. Sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania kimsingi inatufelisha kwa kiasi kikubwa. Mpaka leo Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* wana matatizo yao mengi kule ndani, na inawezekana kuna mianya ya rushwa pengine ndiyo maana tunashindwa hata kufanya *evaluation* ya kodi. Kwa sababu wanaolipa kodi, wewe unafahamu, ni asilimia tano tu ya Watanzania milioni 60, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu wale ambao wanalipa kodi ambao ndio mnajua *system* zao, ni walimu, ni wafanyakazi wa Serikali, mnajua *system* zao za mishahara, ndio wanakatwa. Kwa hiyo ni Watanzania wachache wanaoendelea kunyonywa kwa kulipa kodi, kuna wengine

wengi ambao hawalipi kodi kwa sababu hamna utaratibu mzuri wa kuwafuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeshindwa kufanya ukaguzi wa walipa kodi. Mimi leo ninaweza nikatoa taarifa za uongo za biashara yangu, nikalipa mara ya kwanza na nikaendelea kufanya biashara miaka mitano, bado nitaendelea kulipa kiwango kile kile, niwe nimekua, niwe sijakua hakuna nia njema. Tulisikiliza wote hotuba ya Mheshimiwa Rais, nia yake, na kwa sababu alizungumza. Kwamba wigo wa ulipaji kodi ni mdogo sana, tunahitaji kupanua wigo, kwa sababu lengo ni kupata fedha tukapeleka kwenye miradi ya maendeleo, kwa hiyo ni changamoto kimsingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri, kwamba, kuna wale wawekezaji ambao tunategemea kuwa ni sehemu ya sisi kupata kupata mapato ili tuweke kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wana kesi na kuna kesi ziko mahakamani. Mpaka sasa tuna mashauri ya rufaa mahakamani, yanayosubiri kuamuliwa ya muda mrefu, tunadai takriban trilioni 360 na dola za kimarekani milioni 181. Hizi fedha ni za muda mrefu sana, na tumekuwa tukiimba kwamba zikipatikana zote zitasaidia kuendesha nchi miaka 10, na nini *story* zinanoga. Lakini kimsingi inawezekana mkatafuta mazingira ya kuongea na hao watu, *either* wasamehewe hizi kodi, waendelee kufanya biashara katika mazingira mazuri, au mtafute namna bora ya kuangalia. Lakini kwa sababu ya muda nashukuru, sitaunga mkono.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, ajiandae.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyopo mezani, ya Bajeti yetu Kuu

ya Serikali. Nitumie fursa hii kuipongeza sana Wizara hii chini ya uongozi wa ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba na Naibu wake Mheshimiwa Hamad Masauni na watendaji wote, kwa sababu kazi mliyofanya kutuletea bajeti hii iliyofurahisha taifa hili lote, na inawezekana hata mataifa ya jirani sio kazi ndogo, hongereni sana. Lakini pia nimpongeze Rais wangu, Mheshimiwa mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa sababu bajeti hii imeakisi maono yake; na nadhani ndiyo maana Mheshimiwa Waziri kila wakati ulisema mama amesikia kilio chenu akafanya hiki, amesikia kilio chenu akafanya kile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana kwa sababu amesikia kilio cha Watanzania ambao tunawawakilisha hapa Bungeni na amefanya mambo makuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina haja ya kuangalia mambo mazuri yaliyofanywa kwenye bajeti hii kwa sababu mengi yameshasemwa. Mimi nadhani kazi yangu hapa ni kutoa tu ushauri katika maeneo madogo madogo ambayo nadhani yangeweza kuboreshwa ili Watanzania waendelee kuneemeka na bajeti hii ambayo miongoni mwa vipaumbele katika miradi ya maendeleo ni kuwawezesha wananchi kiuchumi. Kuna mambo ambayo tusipoyazingatia tukayaweka sawa tutakuwa hatujawatendea haki baadhi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika eneo la mifugo kuna changamoto kubwa kwa sababu, kwanza bajeti yao ni ndogo, bilioni 16, kwa sekta ambayo ina rasilimali ya mifugo ambayo ni ya pili katika Bara la Afrika na malengo waliyojiwekea?

Ninaunga mkono kabisa maoni ya Kamati wamesema kwamba miongoni mwa malengo makuu ambayo wamependekeza Wizara ya Mifugo ifanye ni kuwezesha upatikanaji wa maeneo ya malisho, kuwezesha upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo, kutenga na kupima maeneo ya malisho, kusimamia suala la utafiti wa mifugo,

kutatua migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi, kuimarisha vikundi, kuboresha mbegu na mambo kama hayo. Sasa, kwa bilioni 16 utafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa napenda tu kuwashauri basi wasimamiaji wa utekelezaji wa bajeti hii katika sekta husika na Wizara yenyewe kwa ujumla, Wizara ya Fedha, kwamba tuangalie maeneo mahususi ya kipaumbele ili basi tuone kama na mfugaji naye atakwamuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, hili suala la migogoro ya ardhi kati ya watumiaji wengine wa ardhi ni suala nyeti sana. Napenda kuishauri Serikali kwamba, Wizara ambazo zinaguswa moja kwa moja na migogoro inayozuka zikae pamoja, zipitie sheria na kanuni na taratibu, zije na mfumo sahihi ambao utasaidia kutatua migogoro hiyo ili upatikanaji wa ardhi ya malisho iweze kubainishwa na maeneo ya watumiaji wengine yaweze kuwekwa wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Wizara ya Ardhi ambao ndio wapimaji wa ardhi, Wizara ya *TAMISEMI* ambayo ndiyo wenye vijiji, Wizara ya Maliasili ambao ndio wananyakua nyakua hati za watu bila hata kuwashirikisha wengine, wakae pamoja na Wizara ya Mifugo, ili kumaliza migogoro ya ardhi ambayo inajitokeza kila wakati na kupunguzia wafugaji maeneo yao. Na *nina-reference* nzuri kwa sababu kumbukumbu tuliyonayo sisi watu wa Longido kuna eneo linalotaka kutwaliwa la malisho. Eneo mahususi la malisho wakati wa kiangazi, eneo la *Lake Natron* na milima yote inayozunguka huo uwanda wa Longido. Haiwezekani Wizara moja ikachomoka ikaenda kutangaza eneo kwamba wanataka kulifanya pori la akiba, na ni la wafugaji na Wizara ipo, *TAMISEMI* waliotambua vijiji wenye hiyo ardhi wapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni masuala ya msingi ambayo lazima tuishauri Wizara ya Fedha na Mipango, waangalie wanapotenga fedha ielekezwe kwenye yale masuala ya msingi ambayo yatatusaidia kusonga mbele na

kupata maendeleo ya Watanzania wote kama yalivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia, ningependa kushauri Serikali katika maeneo mengine mahususi; kama kwenye hii sekta ya maliasili ambayo Mbunge mwenzangu wa Arusha ameshasemea na kutoa takwimu. Mimi napenda tu kuiomba Serikali, kwamba itoe kitu kinachoitwa *incentive package* ya kuchochea utalii ili uweze kurudi; kwenye sekta zote, utalii wa kuona wanyama, utalii wa uwindaji, wapunguze bei ili watalii warudi. Maana sasa hivi pamoja na *corona South Africa* wao wanapata watalii kwenye maeneo yao ya kiwindaji mpaka milioni tisa kwa mwaka. Namibia wanapata mpaka milioni nane, na hata Zambia ambao wote kwa pamoja hawana maeneo mengi ya uhifadhi kama sisi na ya uwindaji lakini kwa sababu, sisi bei zetu tumeziweka juu na hatuna mpango wa kupunguza bei ili kuvutia tumeendelea kuathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchochee utalii wa ndani. Utalii wa ndani utaimarika pale ambapo *packages* zitatangazwa, ziwekwe bayana kabisa kwamba watoto wa shule, watu wazima, ma-*group* yanapoungana wakienda kutalii kwa bei ndogo kabisa, hapo kila mtu atataka kuona hifadhi zetu na mapato yatapanda kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya madini. Napenda kuishauri Serikali kwa sababu watu waliposikiliza hii bajeti wakaanza na wao wananchi ambao tunawakaribisha kurusha kero zao. Kwa mfano, Ninalo andiko hapa watu wa madini wanasema kuna kitu kinaitwa kodi ya *pay as you earn* na kuna kodi inayoitwa *SDL* ambayo nadhani hiyo inahusika na masuala ya *Skills Development Levy,* sijajua Kiswahili chake. Wanasema kwamba *TRA* hasa kwenye migodi ya madini haya ya *Tanzanite,* wanawalazimisha wale wachimbaji wawalipe watu mishahara, wakaweka na viwango na kumbe makubaliano yao huwa ni kwamba wanalipana baada ya mali kupatikana na ni mfumo ambao ulishakubalika. Kwa hiyo ingebidi *TRA* wasiwalazimishe watu hawa wa madini kulipa fedha ambayo wenzao

wanaochimba bado hawajapata na watambue kwamba kuna utaratibu waliokwishajiwekea tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni tozo la huu Wakala wa Meli Tanzania inaitwa *TASAC*. Wao huwa wana-*charge* fedha tu lakini hawa-*track* ule mzigo, wao wakishapokea tu wakishalipwa basi hawana taarifa ya ku-*track* huo mzigo mpaka umfikie mnunuzi katika nchi aliyopo. Watu wa sekta ya madini hawa nao wanaotuma madini nje, wanaomba kwamba hilo Shirika la *TASAC* halina msaada wowote kwao, *charge* hizo wanazo-*charge* hazina maana kwa hiyo ziachwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu eneo la ongezeko la thamani kwenye biashara kati ya wafanyabiashara wa ndani, kwenye soko lile kuna watu wanaouuza na kununua mlemle. Wenzao wale wanaowauzia wanatoza *VAT* na *VAT* ilishaondolewa, kwa hiyo nalo pia liondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, kuna kitu napenda kuongeza kabla ya muda wangu haujakwisha, kwamba Madiwani walivyowaongozea maslahi yao na Watendaji wa Kata imekuwa ni nderemo, vifijo na furaha kwa nchi nzima. Hata hivyo, kuna watu ambao ndio wako kwenye *ground,* kule ambako ndio *tyre* inagusa lami. Watendaji wa Vijiji hawajafikiriwa katika kuwawezesha. *(Makofi)*

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kiruswa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Francis. Karibu.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Madiwani hawajaongezewa fedha bali wamewekewa kulipwa na Serikali Kuu kwenye Akaunti zao. Posho zao sio kwamba wameongezwa, ili taarifa zikae vizuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kiruswa unapokea taarifa hiyo.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hiyo taarifa, nashukuru kwa sahihisho lakini kile kitendo cha wao kulipwa moja kwa moja kimewaondolea adha na kero kubwa sana. Kile kitendo cha Watendaji wa Kata kupewa dhana, vitendea kazi, mafuta pia imewaongezea ari ya kufanya kazi kwa bidii sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kundi ambalo limesahaulika, Watendaji wa Vijiji na wao wanafanya kazi kubwa, ingefaa katika bajeti hii na wao wafikiriwe. Kwanza katika vijiji vingi katika nchi hii likiwemo Jimbo la Longido, sisi asilimia 75 hawajaajiriwa wana kaimu kwa miaka mingi sana, sijajua bajeti wanawaweka wapi na kama shida ilikuwa ni fedha itafanyika nini ili Watendaji wa Vijiji waajiriwe katika nchi nzima ambapo kuna Makaimu wasiohesabika na kwa miaka na muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchangia hoja yangu ya mwisho kwamba katika kupanga haya maendeleo ambayo hii bajeti inakwenda kutekelezwa, wananchi wanaoishi katika maeneo ya uhifadhi jumuishi kama Ngorongoro kuna haja kubwa ya Wizara ya Maliasili hata Wizara ya Fedha wasaidie ili fedha inayotolewa kwa ajili ya miradi kama shule, hospitali, barabara, wakati wa mchakato wa kutafuta namna sahihi ya kufanya uhifadhi jumuishi au wa mseto zikiendelea, wale wananchi nao waangaliwe maendeleo yao yasirudi nyuma. Nasema hivyo kwa sababu kuna vikwazo vikubwa na watu Ngorongoro hawapati maendeleo kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo basi, ili kuleta umoja kati ya wahifadhi na wafugaji kuna haja sasa ya kusahau sera za zamani za kuona kwamba mifugo na wanyamapori ni maadui. Sio maadui ni kuweka tu mpango wa matumizi bora ya ardhi ili wanyamapori na mifugo kwa utaratibu wa matumizi bora ya ardhi ambayo yanaweza yakapangwa wakashirikiana nyanda za malisho katika

maeneo mahsusi kama Ngorongoro ama katika maeneo ya uwindaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile hizi tozo ambazo watu wanatoza watu wa maliasili ile Sh.100,000; ningeomba hata sasa leo wakati baadaye hii hoja inajumuisha, tuambiwe ni sheria gani hiyo ilipitishwa na Bunge gani linaloruhusu mfugaji atozwe 100,000 kwa kila ng'ombe anapokutwa ameingia katika eneo la hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna pia kero kubwa kwa sababu bajeti haijazingatia matakwa ya wafanyabiashara wa mifugo. Kodi yao haijaguswa popote kupunguzwa. Naomba kodi yao iangaliwe hasa kupeleka mifugo nje maana bado soko la ndani ni hafifu, ni duni ili na wao wapate punguzo, wapate ahueni na maisha yao yaboreke kutokana na bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, atafuatiwa na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Ahmed Shabiby ajiandae.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan hasa kwa kauli yake aliyoitoa akiwa Mwanza kuhusu madini ya Mchuchuma na Liganga. Jana nilikwenda Ludewa Jimboni na kauli ile ilivyotoka nimepokea meseji nyingi sana kutoka kwa wananchi wa Ludewa kwamba sasa Mama yetu kweli ameikumbuka Ludewa kwa kuanzisha miradi hii na wanaomba sana viwanda vijengwe eneo lile lile la Ludewa, ili kuweza kufanya kitu ambacho wachumi wanaita *diversification of economy* na hizo *decentration of industries.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia sana kupunguza wale vijana wa Mkoa wa Njombe ambao wanahama sana

kwenda maeneo ya mbali kutafuta ajira. Kwa hiyo kukiwa na viwanda kule tutapunguza msongamano wa watu kwenye Jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Miji mingine mikubwa kama Mwanza na maeneo mengine. Vijana wengine wabaki kule ili na mimi niwe Mbunge ambaye nina nguvu kazi ya kutosha, sio vijana wakishakua wanakwenda kutafuta ajira maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wameomba sana katika miradi hiyo kuwe na maandalizi ya wale wananchi waweze kupewa elimu waone namna ya kunufaika na hizo fursa; kwa sababu miradi hii inakwenda kunufaisha kwa kiasi kikubwa Taifa letu kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wameeleza. Vile vile tukiwaandaa wananchi na ile *local content* na ile *community base* inayozunguka mradi ikaweza kupata manufaa na wakati na Taifa nalo linapata manufaa kutokana na miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo wananchi wa Ludewa licha ya kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu, wameomba vilevile wasaidizi wake waiangalie Ludewa kwa macho ya karibu. Kwa sababu imeonekana kuna miradi yake mingi ambayo inakwama; kuna daraja la Ruhuhu limekwama kwa takriban miaka sita. Jana nilikwenda kule Mwenyekiti wa Kijiji alinipeleka pale, wamelima sana mpunga bonde la Ruhuhu, soko lipo Ruvuma kwa sababu Kyela ni mbali, lakini wale wachuuzi wanashindwa kwenda kwa sababu kuna kivuko pale toka mwezi Septemba, 2020 hakifanyi kazi na daraja hilo ndio toka mwaka 2016 limekwama. Kwa hiyo haya yanaweza kusaidia kuleta tafsiri nzuri ya uchumi jumuishi, uchumi shindani iwapo na wananchi wote wanaweza kupata manufaa. Kwa hiyo naomba hilo liweze kuangaliwa kwa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulisema hapa pia mradi mwingine ambao umekwama kwa muda mrefu ule wa *VETA*. Miaka karibu 10, ulichimbwa msingi, wamezungusha mabati, kwa hiyo wananchi wa Ludewa wanajiona wao ni *losers* wakati wote. Kwa hiyo hili la Mama kuweza kutaja jana kwamba Serikali sasa imepania kuanza kushughulikia Mradi

wa Mchuchuma na Liganga limeleta faraja kubwa sana kwa wananchi wa Ludewa na wamekuwa na Imani kubwa sana na Serikali hii na kimsingi mimi sina sababu za kutounga mkono bajeti hii. Kwa hiyo naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa sababu nimeangalia vile vile kuna maeneo kama ya sekta ya afya, kuna changamoto ile ya watu kwenda kupata dawa. Mtu anakuwa na bima ya afya, anakwenda hospitali lakini walikuwa wanachelewa kupata dawa. Kwa hiyo sasa naona kwa bajeti hii inakwenda kumwangalia mwananchi wa chini ili aweze kupata matibabu ambayo ni ya uhakika. Ila tu niiombe Wizara ya Afya waangalie pia baadhi ya sheria ambazo wamezitoa kwenye Vituo vya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sheria inazuia Kituo cha Afya kumwandikia mgonjwa baadhi ya dawa. Sasa sisi ambao tupo maeneo ya pembezoni, kuna mwananchi anatakiwa kutembea kilometa 140 kutoka Mavanga mpaka Ludewa kwenda kufuata matibabu. Kwa hiyo kama kuna Kituo cha Afya pale Jirani, Daktari aliyopo Kituo cha Afya sasa hivi tunashukuru Serikali imetuletea *qualified Doctors,* kwa hiyo wangeruhusiwa, lazima tuangalie *intension of* ile *legislation*, ile dhamira ya kuweka ile sheria ya kuzuia. Miaka hiyo kulikuwa hakuna wataalam kwenye Vituo vya Afya, sasa hivi tunao. Kwa hiyo miongozo ya aina hiyo kwa kweli tuweze kui-*review* na kuweza kuruhusu Vituo vya Afya kuandika dawa kwa sababu kuna wataalam wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshiwa Naibu Spika, nipongeze pia agizo moja liliwahi kutolewa na Mheshimiwa Ardhi, Mheshimiwa William Lukuvi kwamba kwenye maeno ya hii miradi mikubwa ya mikakati kama kwenye *SGR* kufanyiwe mipango ya matumizi bora ya ardhi ili sasa *mindset* zetu ziweze kubadilika. Zibadilike kwa sababu watu wengi wanavyoona kwamba reli imetoka bandarini na kwenda maeneo mbalimbali, wanadhani iko maalum kwa ajili ya kusafirisha mizigo inayotoka viwandani peke yake au inayotoka nje ya nchi, kumbe maeneo yale ya ardhi ya pembezoni kufanyiwa mipango ya matumizi bora

ya ardhi kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007, wananchi wanaweza kutenga maeneo kwa ajili ya kilimo, mifugo na vile vile kuzalisha mazao yakasafiri kupitia reli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itasaidia sana kuinua kipato cha wananchi na wanaoishi kandokando ya Reli. Wataweza kuzalisha mazao ya kutosha, kunaweza kukawa hakuna mwingiliano wa matumizi ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, matokeo yake hii reli itapata mzigo wa kutosha, kwa sababu kilimo nacho kinatoa mazao kwa ajili ya viwanda vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuangalia lile eneo la malipo ya mbele wakati mwananchi anamiliki ardhi *premium*. Eneo hili lilikuwa linawasababisha wananchi wengi sana wanashindwa kuchukua hati miliki za ardhi kwa kushindwa gharama. Kwa hiyo kitendo cha kupunguza ada hii ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi hasa wa hali ya chini. Kwangu kule Lugarawa wananchi wale wameanza kufanya mambo ya urasimishaji na Mlangali na maeneo mengine. Naamini nao watamudu kupata hati miliki bila kikwazo. Kwa kweli hii nipende kuipongeza sana Serikali na tuangalie pia maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameendelea kuyalalamikia na kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi baadhi ya Wabunge wamezungumzia kwenye ile kodi ya Majengo. Ni vema sana tukaziangalia halmashauri zetu ambazo vyanzo vingi vya mapato vilichukuliwa. Kwa hiyo tujitahidi sana kuwaajiri wale vijana waliosoma *GIS* ile *Geographical Information System.* Wale wanaweza kukusanya taarifa za majengo yote wakayaweka kwenye mifumo ya kompyuta, ukiwa pale ofisini unaweza ukaona kila jengo na kuweza kujua kirahisi uweze kutoza kodi kiasi gani. Vijana hawa wanasoma katika Vyuo vya Ardhi, kuna Chuo cha Ardhi Tabora na Chuo cha Ardhi Morogoro na vyuo vingine ambavyo vinatoa mafunzo kama hayo wanaweza kusaidia sana kuboresha ukusanyaji wa kodi ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile nilichokuwa namwomba Mheshimiwa Waziri waangalie hiyo asilimia 15 kupeleka kwenye halmashauri ni changamoto haitoshi, wangefikiria kuongeza ongeza kidogo, kwa sababu Wakurugenzi wengi ukiwaangalia ukiwakuta kama hana ugonjwa wa moyo, basi ana presha au ana kisukari au tatizo lingine. Inakuwa hivyo kwa sababu wana matatizo mengi sana lakini hawana fedha. Kwa hiyo eneo hili tungeliangalia, hata halmashauri zingeachiwa asilimia 50, ingesaidia hata kujenga madarasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetembelea baadhi ya madarasa kwenye jimbo langu, yana hali duni sana. Unakuta darasa ni la vumbi. Nilikwenda Shule ya Msingi Liunji, nashukuru Serikali ilipeleka fedha pale, lakini ndio maana naomba sasa halmashauri zifikiriwe kuongezewa mapato. Wakurugenzi wataweza kumudu changamoto ndogo ndogo za madarasa na vituo vya afya. Nitatoa mfano kwenye jimbo langu, kuna kata saba ambazo zimejenga vituo vya afya lakini wanashindwa kumalizia. Wakurugenzi wangekuwa na fedha mambo yangekuwa mepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nirudie kumpongeza sana na kumshukuru Rais mpendwa kwa hoja yake ya jana ya Mchuchuma na Liganga. Wananchi wa Ludewa wanampenda, wanamwombea na wanamkaribisha sana Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji jioni hii ya leo. Napenda kutumia fursa hii kuipongeza sana Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuja na bajeti ambayo Watanzania waliokuwa wakiililia kwa muda wa miaka mingi

sana. Sambamba na hilo napenda kutuma pongezi za pekee kwa Waziri wa Fedha kwa kuja na bajeti iliyokusanya mawazo ya wananchi. Hiki kinadhihirisha wazi kwamba yeye mwenyewe ni mshabiki na mpenzi namba moja wa wananchi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo, ningependa sana nijikite sana katika masuala ya kilimo. Kwa mujibu wa wasilisho la Waziri wa Fedha, ukiliangalia kwa undani kabisa utabaini kwamba sekta ya kilimo ndio sekta ambayo inaendesha uchumi wa nchi hii. Sekta hii ya kilimo ndio sekta pekee inayowaajiri Watanzania wa kila aina. Hata hivyo, cha kusikitisha licha kwamba sekta hii ya kilimo kuwa ni *driving* sekta ya uchumi wa nchi bado haijawa na mchango mzuri katika pato Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siri ya mafanikio ya uchumi unaotokana na kilimo ni kuwepo kwa viwanda. Kuwepo kwa viwanda ambavyo vitakuwa vinasindika na ku-*process* mazao ya kilimo vitatusababishia sisi kuweza ku-*control* uchumi na mazao yetu yatakuwa na thamani ndani na nje ya Taifa hili. Kwa sababu tukiwa na viwanda vingi ambavyo vina uwezo wa ku-*process* mazao yetu tutaepuka ile biashara ya kupeleka mazao, malighafi nchi za nje na badala yake tutakuwa tunapeleka *products* zinazotokana na mazao yale ya mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tukubali kwa miaka mingi sana, kilimo hakikuwa kikiwekwa kipaumbele kinachostahiki. Ndio maana hakikuwa kikichangia kwa asilimia kubwa katika uchumi wa Taifa hili. Labda niseme kuna mtaalam mmoja Profesa wa Chuo Kikuu cha Mzumbe pale, Profesa Aida alisema kwamba mchango wa Serikali katika sekta ya kilimo bado ni mdogo sana, tena ni wa maneno matupu kuliko vitendo. Kwa sababu kasi ya kupunguza umaskini bado haijatekelezwa kwa mujibu wa vile tunavyotarajia.

Mheshimwia Naibu Spika, katika suala zima la kilimo kuna masoko mengi mno duniani. Kuna masoko Nchi za Asia,

kuna masoko ya mahindi Nchi za jirani zetu kama Kenya. Bunge hili lina nafasi ya kipekee katika kujadili hotuba na bajeti pamoja na sera za uchumi wa Taifa hili. Katika majadiliano hayo ni lazima tujadili kwa kuangalia vizuri sana faida na hasara zilizokuwemo katika kila bajeti na mpango. Isipokuwa bajeti na mpango iliyowasilishwa juzi na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kiuhalisia kabisa vinakwenda sambamba na uhalisia na wananchi wa nchi hii na vinakwenda kujibu matarajio ya wananchi wa kipato cha chini ambao ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masoko mengi mno duniani, bado hatujaweza kuyatangaza mazao yetu ndani ya nchi na nje ya nchi Kimataifa. Tukiweza kuzitumia vizuri balozi zetu, ukiangalia takwimu za balozi zetu tulizokuwa nazo na ukiangalia matunda na mazao tunayozalisha katika nchi hii, basi utaona bado balozi hazijafanya kazi tunayoitarajia kufanywa. Lazima imefikia hatua Serikali ikae na wakulima, ikae na mabalozi wajue namna gani wana uwezo wa kuyatangaza mazao yetu katika nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia takwimu za Balozi zetu tulizkuwa nazo, na ukiangalia matunda na mazao tunayozalisha katika nchi hii, bado utaona bado Balozi hazijafanya kazi tunayoitarajia kufanya. Lazima ifikie hatua Serikali ikae na mabalozi wajue namna gani wana uwezo wa kuyatangaza mazao yetu katika nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke katika mazao ya kilimo, niende katika sekta ya ufugaji. Tanzania hii ni nchi ya pili kujaaliwa kuwa na mifugo mingi Barani Afrika ikitanguliwa na Ethiopia. Ingawa Ethiopia wana mifugo mingi kutushinda sisi, lakini ardhi yao ni ya jangwa, ni kame. Hawana maeneo safi ya ulishia mifugo ukilinganisha na sisi. Tanzania hii kila unapopita ni ardhi ya kijani. Tuna sehemu nyingi za kulishia mifugo, ardhi yetu imejaaliwa kila aina ya neema, rutuba na baraka lakini bado tunashindwa na nchi kama Ethiopia na Sudan kusafirisha mazao yanayotokana na wanyama. Kuna soko kubwa sana katika nchi za Asia, hususan

Arabic Countries, kuna soko la ng'ombe mbuzi na kondoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia kitakwimu, Ethiopia na Sudan ambao ardhi yao ni jangwa, wao wanasafirisha sana mazao ya nyama kuliko sisi. Sasa kitu kama hiki kusema kweli inakuwa inaaibisha sana Taifa hili la Tanzania. Ni kitendo cha ajabu mno, mbuzi au ng'ombe anayetoka Sudan kwenda katika soko la Kimataifa ashinde bei kuliko mbuzi anayetoka Tanzania ambaye kuna kila aina ya neema ya malisho ya wanyama. Ni kitendo cha aibu sana kwamba Tanzania hadi hii leo tunaagiza nyama, tunakula *sausage* za ng'ombe au mbuzi na kuku wanaotoka Brazil wakati sisi ndiyo ambao tulitakiwa tu-*process* nyama hizi kusafirisha, lakini sisi tunapokea kutoka nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Wizara ya Fedha mkae na sekta ya ufugaji mwangalie hili tatizo. Tutumie hizi fursa, tusitarajie kwamba kuna neema nyingine zaidi ambazo za kutunufaisha kama hizi. Kwa sababu kilimo na ufugaji ndizo zinazowagusa moja kwa moja maisha ya masikini wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoke hapo niende nikazungumzie suala zima la mabadiliko ya tabianchi. Juzi katika wasilisho la Mheshimiwa Waziri wa Fedha alizungumza kitu ambacho kilituvutia sana sisi Watanzania hususan Watanzania Visiwani. Nafasi ya Zanzibar na mgawanyo wa Zanzibar katika masuala yanayokuja, pesa zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi. Mheshimiwa Waziri alisema kwamba wametenga fedha kwa ajili ya kwenda ku-*support* kingo za mito Wilaya ya Kaskazini A. Ni wazo zuri sana kwa sababu Zanzibar kwa kiasi kikubwa sasa hivi kuna mabadiliko na kuna athari kubwa zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Hata hivyo tungependa Mheshimiwa Waziri aende mbele zaidi, kwa sababu sisi Zanzibar hasa huko Kaskazini A hatuna hata mto unaosafiria hata kwa mtumbwi. Sisi ukiangalia bahari inatulea zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda maeneo ya Nungwi, mwanzo wa kisiwa, ukienda Kaskazi bahari inakula kisiwa, ukienda Magharibi bahari inakula kisiwa, ukienda Mashariki bahari inakula kisiwa. Tulitarajia zaidi kwamba Mheshimiwa Waziri ataacha hiyo *process,* maana inaonekana kwamba tafiti iliyofanyika labda haikuzingatia wapi iende. Bahari ina athari kubwa zaidi kuliko hiyo mito. Mito ya Zanzibar ni mito ambayo ikinyesha mvua dakika mbili, ikikata hakuna tena mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hili lifanyiwe kazi kwa sababu mabadiliko ya tabianchi, kule Kaskazini A visima vingi sana mwanzo vilikuwa vinatoa maji safi, lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi maji yanapatikana katika visima vile ni maji ya bahari. Sasa hayo ndiyo mambo ya kwenda kuyashughulikia kuliko hizo kingo za mito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazo zuri na kwa mujibu wa haya ambayo kayaelezea Mheshimiwa Waziri naona iko haja ya kukutana na hawa Wabunge wa Kaskazini kuweza kumpa ile picha halisi ya yale malalamiko yetu yanayotukabili kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa kabla sijasahau, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naunga mkono kwa sababu yale ambayo niliyazungumza sana siku za nyuma ambayo yalikuwa hayafanyiwi kazi, namshukuru mama yetu pamoja na Waziri wake wa Fedha kwa kuyashughulikia. Kwa mfano, mimi sio mpenzi wa kuweka majina kwenye magari, lakini mlipoweka shilingi milioni 10 mlikuwa mnapoteza sana mapato kwa *plate number* za binafsi. Tulitoa ushauri,

tunashukuru safari hii mmeufanyia kazi. Mabango yote ya matangazo iwe ya kwenye magari, iwe kwenye maduka na hili nalo mmelifanyia kazi. Kwa hiyo, nakuunga mkono Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kazi nzuri uliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima nizungumze, kwenye hii Wabunge wengi walizungumzia habari ya pesa kuongezwa kwenye mafuta kwa ajili ya kwenda *TARURA.* Mimi ni msafirishaji wa mizigo na abiria. Shilingi 100 haiwezi ikaleta madhara ya kuongeza nauli wala kuongeza kitu chochote.

Nimejaribu kuongea na wamiliki wa vyombo mbalimbali vya usafiri hasa *TABOA* nao wakaniahidi kabisa, wakasema hilo ni jambo zuri sana kwa sababu hiyo pesa inapelekwa sehemu ambayo ni muhimu, sehemu ya *TARURA.* Kwa sababu huwezi ukaikwepa ile shilingi 100/=. Utakwepa shilingi 100/= lakini ile gari ikitembea kwenye njia mbovu itavunja vitu zaidi ya ile shilingi 100/=. Kwa hiyo, utakwepa shilingi 100/= lakini gari inaweza ikavunja vitu mara 20 ya ile shilingi 100/=. Kwa hiyo, barabara zikiwa safi, gharama nyingi sana zitapungua. Nataka nikuhakikishie kwamba hii haitaongeza gharama ya aina yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishawahi kusema hapa katika Bunge hili kwamba Wachina hawakupata maendeleo hivi hivi kama mnavyofikiria. Miaka ya nyuma kidogo tu hapo walikuwa sawasawa na Watanzania, lakini wale hata walipokuwa wanaamua kuvaa suti, siku moja wote wanavaa *chew and lie* zote za rangi moja. Ilikuwa agizo la nchi yao. Wakiamua kuvaa suti moja wiki, ni wote. Masharti hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni lazima tufunge mkanda. Hili narudia, wewe unalikumbuka. Kama tunataka kweli maendeleo kwenye hii nchi, ni lazima kufunga mkanda, siyo kuzungumza. Maana Wabunge wote sisi kazi yetu ni kuishauri Serikali. Kuna watu wengine wanaitwa wachambuzi wako huko nje; na kuna watu wengine wanatoa mawazo. Sasa unatoa mawazo, mbadala wake nini? Unazungumza kodi hii, wananchi hapa watateseka, nini na nini; na nchi

inataka pesa. Nini unaleta mbadala wake? Kama hutaki kodi hii iende kwenye simu, iende kwenye mafuta, mbadala wake unaochangia ni upi? Ukilalamikia kitu, lazima ulete na mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta kuna mchambuzi hajawahi kufanya kitu cha aina yoyote. Mtu anachambua hapa, anasema wananchi kwenye simu watapata shida; wakati hajasoma hata hiyo yenyewe inazungumza nini? Imeshasema, kuanzia shilingi 10 mpaka shilingi 200. Mimi na-*recharge* kwenye simu yangu shilingi 50,000 sasa nikikatwa shilingi 200 kuna ubaya gani? Mtu anaweka shilingi 2,000, shilingi 1,000 anakatwa shilingi 10, kuna ubaya gani kuchangia maendeleo ya nchi yake? Hata hivyo, watu hawaelewi, wanapotosha. Utakuta kwenye vyombo vingine vinaandika tu, yaani hata haelewi, shilingi 200, kila siku shilingi 200/=. Kama kitu huelewi, acha kuzungumza. Kama unataka kupinga, lete mbadala wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ndani ya bajeti hii nakumbuka mama ameahidi kule Mwanza siku ya Mei Mosi kwamba mwakani ataongeza mshahara. Hatuna walimu, tunalalamikia walimu; tunalalamikia maji kama Mheshimiwa Mbunge pale alizungumza vizuri sana; tunalalamikia vitu vingi; na bajeti hii tunatakiwa tupate shilingi trilioni 36 kwa ajili ya kuleta hivyo vitu. Sasa kama huna mbadala wa kuleta hiyo pesa, wewe unalaumu tu, sasa tufanyaje? Nchi isimame! Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii bajeti ni nzuri sana, wala haina shida ya aina yoyote. Hata ile kuweka kodi ya viwanja ni vizuri, tena hata baadaye tuje tuangalie na kodi ya ardhi, ije iingie huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tu, *TRA* wanafanya kazi nzuri sana. Namjua Kidata, ni mlokole na ni mtu mzuri sana pamoja na Makamishna wake, lakini huku chini kuna matatu; na siyo tena kwa mameneja wa mikoa. Hawa watu wengine tu wako *TRA* lakini wamesumbua sumbua na nafikiri sasa hivi kidogo kumetulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililopo, *TRA* kulazimishwa kutumia na vyombo vingine ambao hawana utaalam wa kodi; unamshauri *TRA* akachukue TAKUKURU, TAKUKURU anaelewa nini kuhusu mambo ya kodi? Unamchukua *TRA* unamshauri, unamwambia atakula rushwa, yuko na watu wengine wa vyombo vya usalama, wanajua nini katika masuala ya kukusanya kodi? Kodi ni elimu na ndiyo maana kuna Chuo cha Kodi. Unapoleta mtu mwingine kwa wafanyabiashara, kwanza sura yake peke yake inatisha. Unaweza ukamuua yule mfanyabishara hata kabla ya kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuangalie hii. Mambo ya *task force* ambazo hazina mpango ni za kutisha. Mfanyabishara na *TRA* wanatakiwa wawe pamoja kueleza kwa lugha nzuri, mtu atalipa kodi. Kwa wafanyabishara nao, Mheshimiwa Waziri nimeona ulianza kuzungumza pale kwamba sasa hivi watu kwenye *account* wasiingiliwe, wasikamatiwe vitu vyao, lakini kuna mfanyabiashara mwingine anaenda *TRA,* anapigwa kodi shilingi milioni 200, anapeleka mahesabu yake, inakuja kodi labda mpaka shilingi milioni 80, anapewa miezi sita ya kulipa, anaomba mwenyewe au mwaka, lakini unaisha mwaka hajalipa hata shilingi 100/=. Sasa unategemea hiyo pesa itapatikana vipi? Kwa *style* gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kubembeleza mtu ambaye amekubali mwenyewe, kasaini mwenyewe halafu kodi yake mwenyewe halipi. Halafu unasema asichukuliwe kitu wala asikamatiwe mali au asichukuliwe hela yake benki. Hivyo vitu viwili tofauti. Lazima hilo tuliweke sana Mheshimiwa, usije ukaanza kuwa mpole mpole sana ukataka kufurahisha watu kwenye sheria. Sheria ing'ate huku na huku, pande zote mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme na Serikali nayo isiwe na fitina na wananchi wake. Sekta Binafsi ndiyo Sekta ambayo inaajiri watu wengi. Sasa kama ninyi Serikali mnataka kufanya kila kitu, basi sameheni na kodi. Punguzeni kodi. Maana sasa hivi ukitaka, ukienda sijui matangazo;

vyombo vya binafsi havipewi matangazo. Wanapewa vyombo vya Serikali, halafu vyombo vya Serikalini hatusomi, maana wanajisifia wenyewe kwa wenyewe tu. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utakuta matangazo. Halmashauri inaweza ikatoa tangazo inataka Mkandarasi kwenye magazeti sita, hajapatikana Mkandarasi, lakini ikienda kutolewa kwenye gazeti binafsi au kwenye *media* yoyote binafsi, tayari utakuta Wakandarasi 80 au 40. Kwa hiyo, mnakula hela zetu za Halmashauri bila sababu kwa kutulazimisha taasisi zetu za Serikali zifanye matangazo kwenye sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye Wakandarasi, mnataka nini? Kwa mfano, pale kwangu Gairo hakuna *Engineer* wa Wilaya. Kuna *technicians.* Unamwambia ajenge hospitali ya wilaya, ikibomoka! Ooh, tunatumia *force account,* hatuna wataalam. Pelekeni basi kwanza wataalam. Yote hiyo ni Mkandarasi asipate pesa wakati anaajiri watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwa hawa wenzangu kama akina Mheshimiwa Vita Kawawa wenye kumbi nakadhalika; aah, hatutaki kumbi, tunataka sisi tufanyie maofisini. Ofisi zote za Serikali sasa hivi zinanukia chapati tu kwa sababu ya haya mambo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani sasa kama ninyi mnataka kodi kwa watu binafsi na ndiyo wanaajiri watu wengi, lakini hamtaki wapewe kazi, sasa watafanya kazi gani? Ukienda kule bandarini, kuna *TASAC,* hawataki wale *clearing and forwarding* wafanye kazi; anaingilia sheria hata siyo zake. Iliundwa ifanye kazi ya sheria, mizigo ya Serikali shehena za dawa na vitu vingine, lakini sasa wanaingia wanataka wafanye kazi wao. Sasa watu watafanya kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuangalie na hizi kazi. Ujenzi ni JKT, halafu mafundi wenyewe ni hawa hawa. TEMESA

wanataka kazi za Serikali. Kwa mfano, Gairo, *generator* imeungua, nimeenda kwa fundi anataka shilingi 700,000/=, wamekuja *TEMESA* wanataka shilingi 4,000,000/= halafu fundi ni yule yule niliyekubaliana naye mimi shilingi 700,000/=. Sasa Serikali sehemu nyingine mnapigwa kwa ajili ya kukunja roho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nataka nikwambie kwenye mambo ya *VAT* ya maduka na sehemu nyingine. Utakuta hapa pana mtu amesajiliwa *VAT,* kuna mtu hajasajiliwa *VAT.* Kwa hiyo, akinunua huyu biashara kwa sabbau hana *VAT* anauza kitu shilingi 10,000, duka la pili anauza shilingi 11,800 maana yake ameshaweka ile shilingi 1,800. Sasa ni nani atakwenda kununua kwa huyu aliyezidisha bei kwa shilingi 1,800?

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu wanayonunua hii ni moja labda kule kwenye kiwanda, lakini kwa sababu huyu amesajiliwa *VAT* atauza shilingi 11,800 na kwa sababu huyu hana usajili wa *VAT,* anauza kwenye duka hilo hilo kwa shilingi 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jaribu kutafuta kwa hawa wanaoleta vitu kwa jumla kwenye viwanda; kama *VAT,* basi waangalie *technique* yake wanafanyaje kiutaalamu? Kwamba *VAT* ipigwe kule kule, ikija huku watu wote wameshalipa *VAT.* Uangalie tu utafanyaje asilimia zile kwamba hii akiuza ile *VAT* ya kwanza itatoka kiwandani na ya pili itakuwaje ili ilipishwe kule kule moja kwa moja? Ikija huku kila mtu na kila kitu kiwe kwa *VAT* ili *competition* ya maduka iwe iko sawa. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Bado au tayari?

NAIBU SPIKA: Tayari**.**

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Naibu Spika, haya ahsante. *(Makofi)*

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji wetu kwa siku ya leo, lakini nimesikia Wabunge mbalimbali wakichangia kuhusu hizi tozo hasa za kwenye simu. Napata picha kwamba wengine hawajasoma vizuri Mheshimiwa Waziri kasema nini? Ukurasa wa 115, kwa sababu tunaendelea na huu uchangiaji kwa siku saba, ni muhimu Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kuishauri vizuri Serikali tupitie haya maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

Maana kwenye marekebisho ya hii Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kieletroniki Sura 306, kuna tozo katika kila muamala wa kutuma au kutoa pesa, unaanzia shilingi 10/= hadi shilingi 10,000/= na kuna kutoza kiasi cha shilingi 10/= hadi shilingi 200/= kwa siku kwa kila *line* ya simu ya mtumiaji. Hizi ni tozo mbili tofauti. Sasa lazima tuwe tumesoma vizuri haya yanamaanisha nini ili tuishauri vizuri Serikali. Maana nimeona watu wanachangia lakini wanafikiri hizi tozo mbili zinafanana. Ni tozo mbili tofauti na zinamaanisha vitu tofauti japokuwa mtozwaji ni yule yule mmoja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia mmezungumzia alilolisema Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kule Mwanza alipokuwa anaweka jiwe la msingi kwenye Kiwanda cha Uchenjuaji. Ukurasa wa 45 Mheshimiwa Waziri katika kitabu chake cha bajeti; natoa hii mifano ili tuwe tumepitia hiki kitabu. Maana yake ni kwamba Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan haya mabadiliko anayoyasema amejipanga sawasawa. Alishatoa maelekezo kwa Wizara na wameshasoma yako humu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alipokuwa anasema kule, nikawa nawaza kabla sijapitia vizuri hata mimi, kwamba hivi Mheshimiwa Waziri sijui atawahi kuleta yale marekebisho ili yapite kipindi hiki! Kumbe yamo humu tayari. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Rais alishatoa hayo maelekezo na sasa alivyolisema pale maana yake amewekea uzito kuhusu haya maelekezo ambayo ameyatoa kwa Mheshimiwa Waziri aliyekuwa anamwita mama yetu humu ndani, nasi tukafurahi kabisa. Kwa hiyo, mama yetu amejipanga vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tusome vizuri hii hotuba tusije sisi ndiyo tukawa tumeenda kule, baada ya kupiga kura ya ndiyo, vizuri kabisa, halafu tukaenda kule tumeshindwa kuwaelewesha wananchi, tunarudi na maswali humu ndani na ya nyongeza yanakuwa mengi.

Mheshimiwa Massare, mwongozo.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 76. Mimi nimekuwa Mbunge kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na nimekuwa napita barabarani nikipeperusha Bendera ya Bunge kwa sababu nimechaguliwa katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, bendera iliyoko nyuma yako ndiyo inafanana na bendera ambazo tunazo kwenye magari yetu. Bendera ambazo tumegawiwa leo, bahati mbaya mimi sikuchukua mapema, nimekuja kuchukua *session* hii ya jioni. Bendera zile hazifanani na bendera uliyonayo hapo nyuma yako inayopeperuka. Bendera tuliyopewa leo pamoja na vigezo vyote kuwepo Bendera ya Taifa, Siwa ipo, jina la Bunge la Tanzania lipo, lakini rangi yake ambayo ndiyo iliyokolea kwa asilimia kubwa siyo rangi ambayo imezoeleka katika Bunge hili Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rangi ya bluu iliyokolea ndiyo rangi ya kwenye bendera yetu ya Jamhuri ya Muungano. Rangi ambayo ipo katika bendera ambayo tumegawiwa leo haifanani kabisa. Naomba Mwongozo wako: Je, Bunge limebadili mwonekano wa bendera yake?

Siyo kama hiyo iliyoko nyuma yako au ni ile tuliyopewa leo ndiyo bendera halisi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Massare kabla sijatoa huo Mwongozo, hiyo bendera unayo hapo?

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo hapa.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kuomba tu dakika moja zikafika hapa...

NAIBU SPIKA: Nani anayo hapa?

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, iko hapa.

NAIBU SPIKA: Hebu naomba hiyo bendera inisogelee hapa. *(Hapa Baadhi ya Wabunge walipaza sauti)*

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, hii hapa ndiyo ile ya zamani, lakini mpya ni hii hapa. Kwa nyongeza, pia hata katika ushonaji wake haziingii kwenye mikonga.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Naibu Spika, bendera aliyoishika dada wa hapa kwenye Bunge, ndiyo bendera ambayo nimepewa mimi na ndiyo niliyotolea hoja. Naomba uziangalie wewe mwenyewe kwa macho yako, utaona.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Zimechakachuliwa hizo!

WABUNGE FULANI: Zimechakachuliwa.

NAIBU SPIKA: Haya Waheshimiwa Wabunge, ngoja zinifikie hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Amar, hii bendera ambayo umesema ndiyo rangi yake sijaelewa kama hii imejaa vumbi au ndiyo rangi yenyewe ya bendera. *(Kicheko)*

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, niliifungua hiyo makusudi ili nije nayo. Kwa sababu Mwongozo kauomba Mheshimiwa Massare, hakuna tatizo. Bendera ambayo tumeizoea ni kama alivyosema Mheshimiwa Massare, lakini bendera hiyo ya pili, rangi yake siyo sahihi.

MBUNGE FULANI: Hiyo rangi ni ya *East Africa.*

MBUNGE FULANI: Ya China hiyo! CHADEMA...

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Yahaya Massare hapa akiomba Mwongozo kwa Kanuni yetu ya 76 na ameeleza kwamba bendera zilizogawiwa leo kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, bendera hii inayo Siwa kama ambavyo bendera ile nyingine inayo, pia na jina la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na bendera ile ya Taifa, lakini anajiuliza kama hii rangi iko sawa sawa?

Waheshimiwa Wabunge, sasa wakati mwingine mazoea yanaleta changamoto. Nawaomba tuzipokee hizi bendera, kwa sababu kwa taarifa niliyonayo ni kwamba hizi bendera ndizo zilizopitishwa na Shirika letu la Viwango nchini. Hizi bendera ndizo zilizopitishwa kabla hazijaenda kuchapwa kwa kiasi kile kinachotosheleza idadi ya Wabunge. Zimepitishwa na Shirika letu la Viwango. *(Makofi/Kelele)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ngoja, tuelewane. Nakumbuka kuna wakati kulikuwa na mjadala mzito, Waziri wa Elimu yuko hapa; kuhusu ile mistari miwili ya

kwenye Bendera ya Taifa. Kulikuwa na hoja kwamba hii mistari ni ya rangi ya dhahabu; kulikuwa na mjadala kwamba ni rangi ya njano; halafu kukatokea mvutano kabisa mkubwa, yaani kwamba kuna bendera zichomwe, nyingine zimekaa namna fulani, ndiyo maana nimeanza kwa kusema wakati mwingine mazoea yanaleta changamoto.

Sasa kwa hayo maelezo niliyoyatoa, Shirika letu la Viwango limepitisha rangi hizi. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi juu ya mazoea tuliyokuwa nayo, hizi ndiyo Bendera za Bunge sasa. Kwa hiyo, wewe peperusha hii bendera na utakuwa salama. *(Makofi)*

Kuhusu hiyo changamoto nyingine aliyoiongeza Mheshimiwa Amar ya kwamba haiingii kwenye mkonga, labda hilo ndiyo la kuweza kufanyia marekebisho. Kuhusu rangi ya bluu, msiwe na wasiwasi, kwa sababu *blue* hata iliyoko kwenye bendera yetu huwa tunasema ni *blue* ikiwakilisha maziwa; maji.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana.

MHE. ALLY M. JUMBE: Mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nikiwa nimeshasimama na ninyi mnasisitiza Mwongozo; ni kuhusu bendera au jambo lingine?

Haya, kama linahusu jambo lingine ngoja nimalize mafunzo. Mrejeshee mwenye bendera yake.

(Hapa Naibu Spika, Mhe. Dkt. Tulia Ackson alimkabidhi Mhudumu wa Bunge arudishe bendera kwa Mheshimiwa Mbunge aliyemkabidhi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Massare alisema Mwongozo wakati akimaliza Mheshimiwa Shabiby kabla sijasimama. Nikiwa nimesimama maana yake Wabunge wote mnatakiwa kuwa mmenyamaza ikiwa ni pamoja na wewe unayeomba Mwongozo, huwezi kusema unaomba nikiwa

nimesimama. Kwa hiyo, nikiwa nimesimama hakuna Mbunge anaruhusiwa kuzungumza, lakini kwa sababu tuko katika kujifunza, nitakupa fursa. Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe.

MHE. ALLY M. JUMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu Mwongozo wako kwamba sasa je, ni wakati sahihi kwa Bunge hili kubadilisha joho lako ulilolivaa pamoja na bendera iliyo nyuma yako? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na hii elimu. Elimu haina mwisho. Tutakapokuwa tumekamilisha mwaka mmoja wa kuwepo hapa Bungeni mwezi wa 11 nadhani watu wataelewa zaidi kanuni kwa sababu kutakuwa na kukalishwa chini sana.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zinaruhusu Mbunge ambaye hajaridhika na maamuzi ya Kiti kuweza kuchukua hatua, kwa sababu Kanuni zetu zinafahamu; hata kiti, yako mazingira ambayo kinaweza kufanya maamuzi ambayo Mbunge anaweza asiridhike nayo, kwa sababu sisi tunaokaa hapa mbele ni Wabunge wenzenu, lakini mmetutanguliza tu mbele kuwaongoza. Kwa hiyo, nasi ni binadamu.

Kanuni ya 5 inazungumzia Mamlaka ya Spika na fasili ya (4) inasema Mbunge yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza; ndani ya siku moja tangu uamuzi unaolalamikiwa kutolewa, kuwasilisha kwa maandishi malalamiko na sababu za kutokuridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika. Sababu ya kuweka Kanuni hii ni ili kuondoa mabishano kati ya Kiti na Mbunge. Kwa sababu Kiti kikifanya maamuzi huruhusiwi kuyahoji hapa ndani. Unaruhusiwa kuyahoji kwa maandishi kwa kupeleka kwa Katibu ili Bunge sasa lifanye maamuzi kupitia utaratibu wa kikanuni na utaratibu wetu wa Kikanuni ukishapeleka malalamiko kwa maandishi kwa Katibu, itaitishwa Kamati ya Kanuni.

Kwa mfano, sasa niliyeko hapa ni Naibu Spika. Kamati hiyo kwa kawaida Mwenyekiti ni Spika nami ni Makamu Mwenyekiti. Kwa maamuzi niliyofanya mimi, Spika anakuwa Mwenyekiti nami ni mlalamikiwa. Maamuzi akifanya Mheshimiwa Spika, mimi nakuwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika anakuwa mlalamikiwa. Kwa hiyo, Kiti kikifanya maamuzi, huruhusiwi kuyahoji hapa ndani. Nadhani hilo limeeleweka. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 01.30 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 15 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)